# PEO NA MIKAKATI YA KIMAZUNGUMZO KATIKA UUMBAJI WA UJINSIA MIONGONI MWA WAZULUFU NCHINI KENYA

**GACHEIYA, RAPHAEL MWAURA**

**Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu iliyowasilishwa katika Halmashauri ya Masomo ya Shahada za juu ili kutimiza baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamifu katika Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Egerton.**

**CHUO KIKUU CHA EGERTON**

**MEI, 2018**

# UNGAMO NA IDHINI

## UNGAMO

Tasnifu hii ya Shahada ya Uzamifu katika Kiswahili ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kutahiniwa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kikuu chochote.

Sahihi.................................................... Tarehe......................................

Gacheiya, Raphael Mwaura

**AD12/0301/11**

## IDHINI

Tasnifu hii ya Shahada ya Uzamifu katika Kiswahili imewasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na chuo kikuu cha Egerton.

Sahihi............................................. Tarehe..................................

**Prof. Furaha Chai**

Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi;

Chuo Kikuu Pwani

Sahihi............................................... Tarehe..................................

**Prof. Catherine Kitetu**

Idara ya Fasihi, Lugha na Isimu;

Chuo Kikuu cha Egerton

**HATILINZI**

© 2018, Raphael M. Gacheiya

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kamwe kuiga, kutafsiri, kunakili au kuhifadhi tasnifu hii kwa njia au mfumo wowote ule pasi idhini ya mwandishi au / na Chuo Kikuu cha Egerton.

## TABARUKU

Kwa wanangu:

Augustine Gacheiya, Adrian Mutwiri na Aiden Muchai

“Ninyi ni nyota ing’aayo maishani mwangu. Kazi hii iwe mfano bora wa kiusomi maishani mwenu. Muifaidi daima!

## SHUKRANI

Namshukuru Maulana kwa kunijalia siha nzuri wakati wote wa uzamifu na kuniwezesha kuikamilisha kazi hii.

Jifya moja haliinjiki chungu; bila shaka kuhitimisha tasnifu hii kunatokana na watu kadhaa ambao ninawawia shukrani. Nawashukuru sana wahadhiri wasimamizi wangu Prof. Furaha Chai na Prof. Catherine Kitetu. Kwa imani kuu walinipa motisha na shime ya usomi, kunielekeza na kuniongoza katika bahari ya uzamifu. Walisoma kazi yangu pasi kuchoka na kunipa mapendekezo ambayo yalinijenga kisomi. Bila mwongozo wao, tasnifu hii haingefikia ufanisi huu. Asanteni sana tangu mwanzo mmekuwa wanasihi wangu kiakademia. Maelekezo na ushauri mlionipa ni dira maishani mwangu daima.

Namshukuru Dkt. P. Bartoo mtiva wa Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii kwa imani yake kwangu. Prof. E. Ilieva ambaye kwa makini alifuatilia hatua za kisomi na kitafiti ili kuhitimisha kazi hii. Shukrani zangu pia zimfikie mwenyekiti wa Idara ya Fasihi, Lugha na Isimu Dkt. D. Kweya pamoja na wahadhiri wote idarani ambao kwa pamoja mawaidha yao yalinijenga kiasi si haba katika usomi na ufanisi wa kazi hii. Mhazili wa mtiva katika Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii Chuo Kikuu cha Egerton, Bi. Mary Maina kwa kuniauni matatizo yamkumbayo mwanafunzi. Prof. Benedict M. Mutua Makamu wa Naibu Chansela katika Chuo Kikuu cha Kibabii kwa kunipa moyo na kunishajiisha wakati wowote nilipotamauka. Wote nawaombea baraka zake Maulana.

Nawashukuru wazamili J. Gakii, M. Auma, V. Gatimu, M. Mueni, H. Omwoyo, na W. Oseko ambao walikuwa watafiti wasaidizi na kuhakikisha vikundi viini vilitekelezeka. Walikuwa msaada mkubwa katika kupata data kutoka kwa shule husika. Utaalamu wenu, umakini katika kunasa na kurekodi yaliyojiri kwenye vikundi viini yalizalisha kazi hii. Shule zote tatu ambazo zilihusika kupitia kwa walimu wakuu wa shule hizo nawatambua. Kutokana na kuajibikia usiri wa wahusika katika shule hizo imenilazimu kuzitambua pasi kuzitaja. Wanafuzi wote walioshiriki katika vikundi viini asanteni sana kwa muda, mijadala, mchango na uvumilivu wenu.

Nashukuru wasimamizi wa chuo Kikuu cha Egerton kwa kufadhili usomi wangu katika ngazi ya uzamifu na kunipa fursa ya kupata tajriba ya uhadhiri kama mhadhiri msaidizi. Pasi na mazingira ya usomi chuoni, ufanisi wa aina hii utakuwa nadra kwa wengi.

Namshukuru Bi. Janice Mutua na Bw. Duncan Kahiro Mwangi kwa kujitolea kuisoma na kuhariri tasnifu hii isiwe na dosari la kimuundo na kichapishaji. Asanteni sana.

Shukrani zangu ziwafikie wapenzi wazazi wangu Bw. Stephen Gacheiya Mwaura na Bi. Anne Njeri Gacheiya kwa kunilea, kunifunza amana na thamani ya jitihada maishani na kuwa na imani nami. Hakika hii ni hisani na mapenzi yasiyo na kifani, na bila shaka ni muhali kuyalipa kwa shukurani au mali. Aidha naishukuru familia yangu, mke wangu Bi. Janet Mugure pamoja na wanangu Augustine Gacheiya, Adrian Mutwiri na Aiden Muchai kwa uvumilivu wao.

Kwa wengine wengi ambao kwa namna moja au nyingine walichangia ufanisi wa uzamifu huu, Maulana aridhie kuwakirimia mahitaji yao yote.

**Asanteni Sana!**

# ABSTRACT

This thesis is based on an anlaysis of adolsecents' discursive construction of sexuality. Its main objective is to gain an understanding of the world of adolescents sexuality. Worldwide, studies on sexual behaviour among adolescents indicate that a significant number of adolescents are becoming sexually active at an early age. Whereas it is true that culture and language use fundamentally influence sexuality by creating and communicating values, norms, and expectations regarding sexual relationships and behaviour, it is also true that due to various socio-economic and political changes, these cultures are gradually being abandoned. How sexuality is linguistically defined and framed within adolescents groupings thereby influencing their sexual decision and actions inspired this research. Goffmans's Frame Analysis Theory and van Dijk's Critical Discourse Analysis framework were used to examine the lexical items, the different discursive frames and strategies employed in the discourse of sexuality among school going adolescents. The study randomly selected a sample of 104 students from three secondary schools purposefully chosen within Nakuru County. Data was collected through focus group discussions. The data was transcribed, coded and analysed using Frame Analysis as well as Critical Analysis methods. The study established that the words used by adolescents in the construction of their sexuality falls into three functional categories and within which there were subcategories. These words are largely euphemistic and metaphorical. In view of frames, it emerged that there are four distinct frames i.e urgency frame, abstinence frame, authority and characterization or categorization frames. These frames mirror adolescents' understanding and construction of sexuality and complement each other in the adolescent sexuality discourse. On strategies, seven strategies were used by the adolescents to naturalize and rationalize their sexual acts. These strategies are disclaimer, authority, categorization, euphemisim, metaphors, number game and hyperbole. It is hoped that these findings will not only add to the existing body of knowledge on sexuality discourse but will also inform stakeholders involved in designing youth sexuality programmes in different learning institutions. This may in turn contribute to solving issues such as unwanted pregnacies, school drop out and abortion among adolescents.

## IKISIRI

Tasnifu hii inatokana na utathmini wa uumbaji kimazungumzo wa ujinsia miongoni mwa wazulufu. Lengo kuu ni kupata uangavu wa ulimwengu wa wazulufu kuhusu uelewa na ufasiri wao wa ujinsia. Ulimwenguni, tafiti kuhusu tabia za wazulufu zimebainisha kuwa wazulufu hushiriki ngono za mapema licha ya ujamianaji kabla ya ndoa kukashifiwa. Ingawa utamaduni, matumizi ya lugha na miktadha ya kijamii imegunduliwa kuwa na nafasi muhimu katika kuelewa na kuthibiti mahusiano na ushiriki wa ngono, ni kweli kuwa kutokana na mabadiliko ya jamii kiuchumi, kisiasa na kijamii, tamaduni hizi zimeasiwa na kupelekea itikadi ya kujihini na ubikira kutozingatiwa na wazulufu. Wazulufu wanapofikia umri wa kuvunja ungo huanza kuunda kijitamaduni ambacho hutofautiana na watu wazima. Miongoni mwa jinsi ya kujitambulisha kama kundi la wazulufu ni lugha inayotumika kueleza ulimwengu wao. Uumbaji wa ujinsia kimazungumzo baina ya wazulufu ulimotisha utafiti huu. Utafiti huu, kupitia Nadharia ya Uchanganuzi wa Peo na muundo msingi wa van Djik wa Uchanganuzi Hakiki wa Usemi ulitathmini leksia, peo na mikakati mbali mbali katika uumbaji wa ujinsia miongoni mwa wazulufu. Wanafunzi 104 waliteuliwa kishelabela katika shule tatu za upili mjini Nakuru zilizoteuliwa kimakusudi. Mkabala wa kinyanja uliohusisha mijadala katika vikundi viini kumi na viwili ulitumika kupata data. Data ilirekodiwa, kutunukuliwa na kuchanganuliwa kwa kutumia uchanganuzi peo na uchanganuzi usemi. Ilitambuliwa kuwa maneno wanayoyatumia wazulufu katika uumbaji wa ujinsia yanaweza kugawika kiuamilifu katika makundi manne makuu yaliyo na vijikategoria vidogo vidogo. Maneno haya ni ya kitasfida na kistiari. Kwa mujibu wa peo za mazungumzo, peo za kimsingi za udharura, kujihini, mamlaka na uanishaji zilibainika. Peo hizi zinakuzwa na peo jenzi zinazotokana na utasfidi na ustiari wa maneno tumikizi. Peo hizi ni dira na kiambo cha uelewa wa ujinsia miongoni mwa wazulufu. Mikakati saba ya kimazungumzo imetambuliwa. Mikakati hii imegunduliwa kuwa hutumiwa na wazulufu kuhalalisha na kukawaidisha matendo yao ya kiujinsia. Inatarajiwa kuwa matokeo haya bali na kuongezea ujuzi uliopo katika uwanja wa lugha na uzungumzi, ujinsia, nadharia ya peo, utanufaisha washika dau katika taasisi mbali mbali za mafunzo wanaoratibu sera na vipindi kuhusu ujinsia na uadilishaji wa wazulufu. Inakisiwa huu ni mchango utakaoimarisha jitahada za kutatua tatizo la mimba za mapema na zisizopangwa na uachaji masomo miongoni mwa wazulufu.

# FAHARISI

**UNGAMO NA IDHINI** ........ ii
**HATILINZI** ........ iii
**TABARUKU** ........ iv
**SHUKRANI** ........ v
**ABSTRACT** ........ vii
**IKISIRI** ........ viii
**FAHARISI** ........ ix
**ORODHA YA MAJEDWALI** ........ xii
**ORODHA YA VIELELEZO** ........ xiii
**VIAMBATISHO** ........ xiv
**ORODHA YA VIFUPISHO** ........ xv
**SURA YA KWANZA:UTANGULIZI** ........ 1
1.1 Usuli wa Mada ........ 1
1.2 Mada ya Utafiti ........ 3
1.3 Madhumuni ya utafiti ........ 4
1.4 Maswali ya utafiti ........ 4
1.5 Umuhimu na sababu za kuchagua mada. ........ 4
1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti. ........ 4
1.7 Mdokezo wa Sura za Tasnifu ........ 5
1.9 Ufasili wa Dhana ........ 6
**SURA YA PILI:MAPITIO YA MAANDISHI NA MSINGI WA NADHARIA** ........ 7
2.1 Utangulizi ........ 7
2.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ........ 7
2.2.1 Ujinsia na Elimu ........ 7
2.2.2 Ujinsia na Utambulisho wa Wazulufu ........ 10
2.2.3 Ujinsia na Lugha ........ 14
2.2.4 Wazulufu na Ujinsia ........ 17
2.3 Msingi wa Nadharia ........ 19
2.3.1 Nadharia ya Uchanganuzi Peo ........ 19

2.3.2 Uchanganuzi Hakiki wa Usemi ........ 22
2.3.3 Muundo Msingi wa Kitambuzi ........ 23
**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI** ........ 24
3.1 Utangulizi ........ 24
3.2 Mufumo wa Utafiti, Mahali pa Utafiti na Jamii Kusudiwa ........ 24
3.3 Mfumo wa Uteuzi wa Sampuli ........ 24
3.4 Njia za Utafiti na Ukusanyaji Deta ........ 25
3.5 Data, Mfumo wa Uchanganuzi na Ufasiri wa Deta ........ 26
3.6 Maadili katika Utafiti ........ 28
3.7 Hitimisho ........ 28
**SURA YA NNE: KATEGORIA ZA LEKSIA ZA UUMBAJI WA UJINSIA** ........ 29
4.1 Utangulizi ........ 29
4.2 Uwasilishaji na Ufasiri wa Leksia ........ 29
4.2.1 Maneno yanaorejelea Ubikira ........ 30
4.2.2 Uwili wa Kuwa na Kutokuwa Bikira ........ 30
4.2.3 Maneno yanaorejelea Kujamiana ........ 43
4.3 Maneno yanayoashiria Maumbile ........ 52
4.3.1 Maneno yanayoashiria Sehemu za Mwili ........ 52
4.3.2 Maneno yanayoashiria Umbo ........ 66
4.3.3 Maneno yanayoashiria Urembo na Utanashati ........ 73
4.4 Maneno yanayorejelea Mpenzi ........ 77
4.5 Maneno yanaorejelea hali ya kuwa wapenzi/katika mapenzi ........ 86
4.6 Hitimisho ........ 88
**SURA YA TANO: PEO NA MIKAKATI YA KIMAZUNGUMZO** ........ 91
5.1 Utangulizi ........ 91
5.2 Peo za Kimazungumzo ........ 91
5.2.1 Upeo wa Udharura ........ 91
5.2.2 Upeo wa kujihini ........ 96
5.2.3 Upeo wa Mamlaka ........ 101
5.2.4 Upeo wa Uanishaji na Utambulisho ........ 107
5.3 Mikakati ya Kimazungumzo ........ 110

5.3.1 Mkakati wa Ukinai ........ 111
5.3.2 Mkakati wa Urejelezi ya Mamlaka ........ 112
5.3.3 Mkakati wa Uainishaji ........ 113
5.3.4 Mkakati wa kitasfida ........ 114
5.3.5 Mkakati wa Kisitiari ........ 116
5.3.6 Mkakati wa Kitakwimu ........ 121
5.3.7 Mkakati wa kupiga chuku ........ 122
5.4 Hitimisho ........ 122
**SURA YA SITA: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO** ........ 123
6.1 Utangulizi ........ 123
6.2 Muhtasari wa Matokeo Muhimu ........ 123
6.3 Hitimisho ........ 126
6.4 Mapendekezo ........ 128
**MAREJELEO** ........ 129
**VIAMBATISHO:** ........ 146

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 1:Uteuzi wa Washiriki katika Vikundi Viini ...................................................... 25
Jedwali 2:Kategoria za Maneno Kiuamilifu .................................................................... 29
Jedwali 3:Kategoria za Maneno yanayorejelea Kuwa na Kutokuwa Bikira..................... 30
Jedwali 4: Kategoria za Maneno ya Kujamiana .............................................................. 44
Jedwali 5:Makundi ya Maneno yanayorejelea Maumbile ................................................ 52
Jedwali 6: Kategoria za Maneno yanayoashiria Sehemu................................................. 53
Jedwali 7:Kategoria za Maneno yamayoashiria Umbo ................................................... 66
Jedwali 8:Kategoria na Wingi wa Maneno Yanayoashiria Urembo na Utanashati.......... 73
Jedwali 9: Kategoria na Wingi idadi wa Maneno yanayomrejelea Mpenzi ..................... 78
Jedwali 10:Kategoria za Maneno yanayoashiria kuwa na Mpenzi................................... 86

## ORODHA YA VIELELEZO

Kilelezo 1:Muundo Msingi wa Kitambuzi ........................................................................ 23
Kilelezo 2: Muundo wa Uchanganuzi Deta ...................................................................... 27

## VIAMBATISHO

Kiambatisho A: Fomu ya Kukubali Kushiriki Utafiti.................................................... 146
Kiambatisho B: Kielelezo cha Mahojiano ya Vikundi Viini ......................................... 147
Kiambatisho C: Makala Chochezi "A" ........................................................................... 148
Kiambatisho D: Makala Chochezi "B" ........................................................................... 149
Kiambatisho E: Makala Chochezi "C"............................................................................ 150
Kiambatisho F: Makala Chochezi "D"............................................................................ 151
Kiambatisho G: Kategoria na Jumla ya Leksia.............................................................. 152
Kiambatisho H: Unukuzi kutoka Kikundi kiini katika Shule C .................................... 155
Kiambatisho I: Tunukuzi kutokana na Vikundi Viini katika Shule B ............................ 163
Kiambatisho J: Unukuzi Kutokana na Vikiundi Viini Katika Shule A .......................... 178
Kiambatisho K: Leksia Rejelezi ..................................................................................... 196
Kiambatisho L: Leksia Rejelezi 2.................................................................................... 197
Kiambatisho M: Leksia Rejelezi 3.................................................................................. 198
Kiambatisho N: Leksia Rejelezi 4 ................................................................................... 199
Kiambatisho O: Kibali Kutoka NACOSTI .................................................................... 200
Kiambatisho P: Barua ya Idhini Kutoka NACOSTI...................................................... 201
Kiambatisho Q: Barua ya Idhini Kutoka Wizara ya Elimu ........................................... 202
Kiambatisho R: Barua ya Idhini Kutoka Wizara ya Usalama wa Ndani........................ 204
Kiambatisho S: Barua ya Idhini Kutoka Shule Shiriki .................................................. 205

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| WHO | World Health Organization |
| MOH | Ministry of Health |
| KNBS | Kenya National Bureau of Statistics |
| UKIMWI | Ukosefu wa Kinga Mwilini |
| UNESCO | The United Nations Educational, Scientific and Cultural Organisation |
| UNFPA | The United Nations Fund for Population Activities |
| Kdt | Kidato |
| Mv | Mvulana |
| Ms | Msichana |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Katika sura hii, usuli wa swala nzima la ujinsia miongoni mwa wazulufu limeangaziwa kwa kifupi kwa madhumuni ya kuwekea swala tafitiwa msingi. Maandishi kadhaa ambayo yalichochea ari ya kushughulikia mada hii pia yameangaziwa kwa muhtasari. Hatimaye kuna maelezo ya mada ya utafiti, madhumuni na maswali ya utafiti, umuhimu na upeo wa utafiti.

Dhana ya mzulufu na uzulufu ingali tatanishi na ni tu baada ya miaka tangulizi ya karne ya 20 ambapo uzulufu ulifasiriwa kama awamu bainifu katika ukuaji wa mtu kitambuzi na kimihemuko. Kulingana na Massoni (2006), ni katika miaka ya 1940 ambapo dhana ya mzulufu na uzulufu ilipata mashiko na kutumika zaidi. Kwa mujibu wa World Health Organization WHO (2005) na katiba ya Kenya (2010), mzulufu ni mtu yeyote aliye na umri wa miaka 10- 19. Awamu za uzulufu kwa mujibu wa maelezo ya WHO hugawika kimiaka katika makundi manne makuu. Awamu hizi ni kipindi tangulizi cha uzulufu kinachoanzia miaka 6-10. Awamu ya pili ni uzulufu wa mapema unaoanzia miaka 11-13. Awamu ya uzulufu wa kati inayoanzia miaka 14-16 na awamu ya mwisho ambayo ni hatua ya mwisho ya uzulufu inayoanzia miaka 17-19. Awamu mbili za mwisho za uzulufu (14-19) zilishirikishwa katika utafiti.

Uzulufu imedaiwa kuwa ni kipindi cha mpito katika maisha ya mwanadamu (WHO, 2005). Katika kipindi hiki, wazulufu hushuhudia mabadiliko ya kimwili, kihisia na ukuaji kijamii kwa ujumla. Watafiti wa maswala ya uzulufu wanadai kuwa kipindi hiki huambatana na uchujaji wa maadili ya mahusiano ya ngono na tabia tangulizi za majaribio ya mahusiano ya kingono (Kabiru na Ezeh, 2007; Gupta na Mahy, 2003). Aidha, katika kipindi hiki, wazulufu wanatarajiwa kutwaa kitamaduni majukumu ya kijinsia ambayo yataongoza na kuumba ujinsia wao siku za usoni. Kufuatana na maelezo haya, imetambuliwa kuwa, maamuzi yanayochukuliwa katika awamu hii yana uwezo wa kuathiri mhusika kwa namna chanya au hasi, kuathiri nafasi za mzulufu maishani, tabia na mienendo, pamoja na afya ya mzulufu (Lakshmi, Gupta na Kumar, 2007).

Uchanya na uhasi wa maamuzi ya wazulufu kuhusu ujinsia umelifanya swala nzima la ujinsia kushughulikiwa kwa kani katika karne ya 20 hususan kutokana na ongezeko la matukio ya wazulufu kushiriki ngono za mapema, mimba za mapema na zisizopangwa, magonjwa ya zinaa na athari nyingine hasi. Uhalisia huu unapata mashiko kulingana na Beguy, Kabiru, Nderu, na Ngware (2009); Cleland na Ali (2006); Dixon-Muller (2008; 2009) wanaodai kuwa maendeleo ya kimwili, kisaikolojia na kitabia yanayotokea wakati wa kipindi cha uzulufu yaweza kuchangia uwezekano wa maambukizi ya Virusi vinavyosababisha Upungufu wa Kinga Mwilini na maradhi mengine ya zinaa pamoja na uwepo wa mimba zisizopangwa, uavyaji wa mimba na kutokamilisha masomo (Kar, Choudhuryna Singh, 2015); (The National Campaign to Prevent Teen Pregnancy, 2002) na (Population Council, 2006).

Visa vya kushiriki ngono za mapema baina ya wazulufu vimeripotiwa kuongezeka ulimwenguni kote kwa zaidi ya asilimia 45 (WHO, 2011). Ugunduzi huu si swala geni nchini Kenya hususan miongoni mwa wazulufu walio shuleni. Kwa mujibu wa ripoti ya Ministry of Health (MOH, 2004), asilimia 12 ya wanaojifungua nchini Kenya ni wasichana wa kati ya miaka 15-19 na 42 % ya wasichana wamejamiana kabla ya kufikisha umri wa miaka 15. Kulingana na takwimu zilizoratibiwa, 74% ya wanaoavya mimba katika hospitali za Kenya ni wazulufu na hushirikisha 16.5% ya mimba zote zinazotunguliwa. Aidha wasichana 13,000 huacha shule kila mwaka kutokana na ujauzito na serikali hupoteza takriban milioni 60 kila mwaka Kenya National Bureau of Statisctics (KNBS, knbs.or.ke, 2011). Kulingana na ripoti ya Kenya Demographic Survey (KNBS, et al., 2014), asilimia kumi na nane ya wazulufu walio kati ya miaka 15-19 wamemejifungua au ni wajawazito. Asilimia 11 ya maambukizi yote yaliyoripotiwa mwaka wa 2013, yaliwashirikisha wazulufu wa kati ya miaka 10-19. Tafiti hizo na nyingine katika Afrika Kusini mwa Sahara zimethibitisha ongezeko la maingiliano ya kingono miongoni mwa wazulufu pamoja na athari zinazoambatana na mahusiano ya aina hiyo. Athari hizi kwa kiwango kikubwa imegunduliwa huhatarisha afya na maisha ya wazulufu.

Licha ya ukweli huo, kwa mujibu wa uanuwai wa kitamaduni uliopo katika Afrika Kusini mwa Sahara (SSA), jitihada zozote za kushughulikia na kuelezea dhana za kawaida za ujinsia wa wazulufu huwa zimekwazika mno. Kutokana na hali hii, ujinsia wa wazulufu ni swala kuu la kiafya na kijamii barani Afrika na nchini Kenya ambapo asilimia 26 ya jumuiya nzima ni wazulufu. Mbali na hayo, uhusiano wa karibu uliopo baina ya mimba zisizopangwa, kutokamilisha masomo na

umasikini unalazimu utafiti zamifu katika ulimwengu wa ujinsia wa wazulufu kwa lengo la kuelewa mitazamo yao kabla ya kuunda miundo msingi na mikakati ya kukabiliana na tatizo hili. Namna mmoja ya kupata mafanikio ni kuelewa ulimwengu na ufasiri wa ujinsia miongoni mwa wazulufu. Kulingana na Undie, Crichton, na Zulu (2007), kuna ushahidi kuwa iwapo programu za wazulufu kuhusu ujinsia zitawashirikisha wazulufu na lugha yao, zaweza kuwa kiingilio muhimu cha kuwarai wawajibikie maswala ya ujinsia kwani kama anavyodai Renne (2000), mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi na kijamii yameathiri pakubwa msimamo wa vijana kuhusu ujinsia wao. Zaidi ya hayo, licha ya lugha kuwa kiungo muhimu cha utamaduni na kiingilio muhimu katika maisha ya wanajamii, sifa za lugha waitumiayo wazulufu kuhusu ujinsia hazijazingatiwa.

Tolman (1996; 2005), anakiri kuwa lugha ni sehemu muhimu ya utamaduni wa jamii yoyote ile kwani hufanikisha upitishaji na udumishaji wa imani, itikadi, mila na tamaduni za jamii. Mojawapo wa itikadi na mila za kijamii ni ujinsia ambamo huwepo maswala mengine kama vile ubikira na kujihini. Kufanikiwa katika kukabiliana na janga la UKIMWI, washika dau hawana budi kuzingatia lugha ya walengwa (Ogechi, 2005). Ilikuwa mtazamo wa utafiti huu kuwa sharti kuzingatia na kuelewa sifa za lugha ya wazulufu kuhusu ujinsia ili kuelewa dhana ya matatizo ya kijamii yanayotokana na tabia za wazulufu zinazohusiana na ujinsia.

Utafiti huu ulitathmini lugha waitumiayo wazulufu walio katika shule za upili kuumba na kuelezea maswala yanayohusiana na ujinsia ili kupata upenyo wa ulimwengu wao; upenyo unaoweza kutumika kutatua tatizo hili na kukabiliana na mahitaji yao ya sasa na siku zijazo kuhusu ujinsia, afya na ustawi wao.

### 1.2 Mada ya Utafiti

Lugha katika jamii hutumika kutekeleza majukumu mbali mbali kama vile utambulisho wa jamii, kufanikisha mawasiliano baina ya wanajamii, kutekeleza jukumu la kiujumi, kuonya na kutahadharisha, kupitisha mila na tamaduni, kuumba na kudumisha ujinsia wa wanajamii miongoni mwa majukumu mengine. Wazulufu kama wanajamii hutumia lugha kuumba na kuelezea ulimwengu wao. Kufuatana na mabadiliko ya kijamii, jinsi wazulufu wanavyoumba ujinsia wao ili kujitambulisha kama kundi maalum ni swala linalohitaji kufanyiwa uchunguzi.

### 1.3 Madhumuni ya utafiti

Madhumini ya jumla ya utafiti huu ni kuweka wazi uumbaji wa ujinsia miongoni mwa wazulufu. Ili kuafikia haya, madhumuni haya mahususi yalilengwa:

i) Kubainisha kategoria za maneno yanayotumiwa na wazulufu katika kuumba ujinsia wao.
ii) Kubainisha na kueleza peo za kimazungumzo katika uumbaji wa ujinsia miongoni mwa wazulufu.
iii) Kufafanua mikakati ya uzungumzi katika uumbaji wa ujinsia miongoni mwa wazulufu.

### 1.4 Maswali ya utafiti

i) Maneno wanayoyatumia wazulufu kuumba ujinsia wao hugawika vipi kiuamilifu?
ii) Uumbaji wa ujinsia huakisi peo zipi za kimazungumzo?
iii) Mikakati ipi ya uzungumzi hutumika katika uumbaji wa ujinsia ?

### 1.5 Umuhimu na sababu za kuchagua mada.

Matokeo ya utafiti huu ni muhimu katika kumwezesha mtafiti kupata shahada ya uzamifu. Bali na hayo, matokeo ya utafiti huu katika mawanda ya nadharia, yameongezea maarifa na kukuza nadharia katika uwanja wa ujinsia na lugha. Ufafanuzi wa kategoria za maneno kiuamilifu katika kuwasilisha ujinsia miongoni mwa wazulufu, ufafanuzi wa peo na maelezo kuhusu mikakati ya kimazungumzo ni hali inayokuza uwanja wa Isimu. Matokeo ya utafiti huu aidha yatachangia katika utafiti wa lugha, ujinsia na vitengo mbali mbali vya elimu kuhusu maswala ya ujinsia wa wazulufu.

Katika muktadha wa taasisi za kijamii, lugha ni ala muhimu kwa walimu pamoja na wanasihi wa wazulufu ambao inatarajiwa watafaidi kazi hii. Aidha ni muhimu kwa taasisi zinazobuni mitaala katika shule hususan kwa kulenga mtaala wa mafunzo ya afya na ujinsia. Matokeo, yatachangia katika kuratibu ufasiri na usawiri wa maswala yanayohusiana na ujinsia. Hili litafanikisha upangaji na utekelezi wa sera madhubuti za mahusiano ya ngono katika taasisi za kijamii na serikali. Utafiti huu unachangia katika tafiti za awali kwa kuangazia na kutahmini uwasilishi wa ujinsia miongoni mwa wazulufu.

### 1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti.

Utafiti ulijikita katika kutathmini lugha waitumiayo wazulufu wa shule za upili katika jimbo la Nakuru pekee ili kubainisha kategoria amilifu za leksia, peo za kimazungumzo na mikakati ya

kimazungumzo kuhusu ujinsia. Data iliyokusanywa inatokana na wazulufu hawa na huenda isitumike kujumuisha na kushirikisha leksia zote zitumikazo na wazulufu wote nchini Kenya kwa vile lugha ni nyumbufu na hubadilika kutegemea muktadha.

**1.7 Mdokezo wa Sura za Tasnifu**

Tasnifu hii imegawika katika sura sita. Sura ya kwanza ni utangulizi ambapo kuna maelezo ya usuli wa mada ili kuweka msingi wa utafiti mintarafu ya maswali na madhumuni yaliyoazimiwa. Aidha kuna ufafanuzi wa umuhimu, upeo na mipaka ya utafiti. Sura ya pili, inaangazia mapitio ya maandiko na tafiti awali zilizo na uhusiano na mada tafitiwa. Sura hii pia inafafanua nadharia zilizoongoza utafiti na kuelekeza katika kujibiwa kwa maswali ya utafiti. Muundo msingi wa kitambuzi unaoweka wazi mahusiano yaliyopo baina ya kilichotafitiwa na kilichokusudiwa umeelezwa katika sura hii. Sura ya tatu inaangazia mbinu za utafiti zilizotumika ili kuafikia malengo ya utafiti. Sura hii imefafanua hatua baada ya nyingine mbinu za kiethnografia zilizotumika kuibua data, mfumo wa uchanganuzi wa data na maadili katika utafiti.

Sura ya nne inatanguliza matokeo ya utafiti kwa mujibu wa lengo la kwanza la utafiti. Maneno tumikizi katika uwasilishi wa ujinsia miongoni mwa wazulufu yamefasiriwa kiuamilifu na kuwekwa katika kategoria bainifu mintarafu ya mazungumzo ya wazulufu kuhusu ujinsia. Kategoria hizi ni kiingilio muhimu cha ubainishi wa peo za mazungumzo na basi sura hii ndio msingi wa sura ya tano ambayo imegawika kuwili. Sehemu ya kwanza ya sura ya tano inafafanua kwa kina peo za kimazungumzo. Peo hizi zinaweka wazi uelewa wa ujinsia miongoni mwa wazulufu na hapo kuzua mikakati ya kimazungumzo. Mikakati hii ya kimazungumzo ndiyo uti wa mgongo wa sehemu ya pili ya sura ya tano. Kila mkakati umefafanuliwa kwa kina. Tasnifu inatamatika katika sura ya sita ambapo muhtasari wa matokeo muhimu unadokezwa. Mapendekezo ya utafiti wa baaadaye ili kukuza na kuimarisha uwanja wa ujinsia, lugha ya wazulufu, uchanganuzi wa peo na mikakati ya uzungumzi yamefafanuliwa katika hitimisho.

**1.9 Ufasili wa Dhana.**

a) Mikakati ya Uzungumzi: Hizi ni mbinu za uzungumzi au usemi ambazo kwazo usemi huakisi na kufanyiza jambo au lengo.

b) Mzulufu : Mtu yeyote aliye na umri wa miaka 10- 19

c) Peo za Uzungumzi : Kundi la maoni na mali-gafi ya kijamii yanayoongoza, kumotisha na kuyapa maana matendo ya wanajamii.

d) Ufedheheshaji wa Mwanamke Mkoo: Ni aina ya unyanyapaa wa kijamii unaotumiwa kwa watu, hususan kwa kizazi cha jinsia ya kike ambao waaonekana kukiuka matarajio ya kitamaduni ya tabia za kiujinsia.

e) Ujinsia : Neno linalosimamia hali ya mtu kuwa mvulana au msichana pamoja na maelezo ya uchu na ashiki.

f) Uwili : hali ya leksia moja kuonyesha sifa mbili (chanya na hasi) kwa wakati mmoja

## SURA YA PILI

## MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA

### 2.1 Utangulizi

Sura hii inajihusisha na ufafanuzi na utathmini wa kazi za kisomi za awali zinazohusiana na ujinsia wa wazulufu. Katika kushughulikia malengo ya utafiti, sura hii imegawika kuwili ambapo katika sehemu ya kwanza mtafiti alijishughulisha na yaliyoandikwa na katika sehemu ya pili kuna maelezo ya msingi wa nadharia zilizotumika kama mwongozo wa utafiti.

### 2.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Kulingana na Izugbara (2005), ujinsia wa wazulufu na mikitadha ya kijamii ya usawiri na uumbaji wa ujinsia wao kimazungumzo na kitabia ni swala ambalo limepata kani miaka ya hivi karibuni. Katika Afrika Kusini mwa Sahara, imetambuliwa kuwa kama ilivyo katika bara nyingine, wazulufu wanajihusisha na vitendo vya ujinsia mapema. Kinaya hata hivyo ni ukweli kwamba, tafiti zilizopo na mjadala unaoendelezwa kuhusu mada hii huegemea kwa kiasi kikubwa watu wazima katika mataifa yanayaoendelea na bila ya kuzingatia kauli na mtazamo wa wazulufu wenyewe kwa misingi ya kujamiana, ujinsia na tajriba walizonazo. Izugbara (2004), anarai kuwa kazi za kisomi kuhusu ujinsia miongoni mwa wazulufu ni chache na zimeegemea maswala ya masomo ya ngono na hatari za maingiliano hayo. Watafiti Fergus, Zimmerman na Caldwel (2007); Kotchik, Shaffer, Forehand na Miller (2001); Resnick, *et al*. (1997) na Sandfort, Orr, Hirsch na Santelli (2008) wanadai kuwa huo ni mtazamo wa awali wa tafiti kuhusu ujinsia wa wazulufu. Aidha tafiti zinazoegemea mtazamo awali ni muhimu kutokana na athari za mahusiano ya kijinsia ulimwenguni (Wellings, *et al*., 2001); (Forhan, *et al*., 2009) na (Finer, 2010). Tafiti hizo zimezua maelezo muhimu kuhusu uimarishaji wa mikakati ya kukabiliana na matatizo hayo kupitia mfumo wa elimu (Nahom, *et al*., 2001); (Caron, Godin, Otis, na Lambert, 2004); (Boislard & Zimmer-Gembeck, 2012); (Salazar, *et al*., 2005); (Tolman na McClelland, 2011); (Kirby, 2008).

#### 2.2.1 Ujinsia na Elimu

McIlwaine na Datta (2004) katika utafiti wake anadai kuwa wazulufu hutazamwa kama kundi mahususi la jamii. Aidha taasisi za elimu ni mahali bora ambamo wazulufu kama wanafunzi husaka na kuafuatilia malengo yao ya kiakademia. Uhitimishi na maafikio ya elimu huathiri mafanikio maishani na huashiria hali ya mpito wa ukuaji hadi kwa utu uzima (Jekielek na Brown,

2005). Wanafunzi wengi kwa sasa imetambuliwa kuwa wana ari ya mafanikio zaidi ya ilivyokuwa awali na matarajio kutoka kwa wazazi kuhusu mafanikio ya kielimu yamekolea zaidi. Imetambuliwa kuwa wanafunzi wazulufu walio na maazimio fungamanifu, sio lazima wawe na umahiri mkuu katika masomo. Wanaelewa jinsi hali na dhana nyingine za maisha yao kama vile ujinsia na tabia zinazoambatana na ujinsia zaweza kuathiri mafanikio yao kielimu. Hata hivyo, wazulufu hawa wametengwa na kutambuliwa kama kundi sumbufu na ambalo linahitaji uongozi na ulinzi wa wazazi. Ingawa utafiti huu haukuingilia mafanikio ya wazulufu kielimu, hoja zinazoibuka kutokana na utafiti huo ni amali kwa utafiti huu. Kimsingi watafitiwa ni wanafunzi na hivyo basi ni muhimu kuangazia nafasi ya elimu katika maisha yao. Aidha, tafiti hizo zinaashiria mgao wa “sisi” na “wao” hali ambayo ni muhimu katika utathmini wa peo na mikakati ya kimazungumzo. Hata hivyo, tafiti hizo hazikulenga uamilifu wa leksia katika lugha waitumiayo wazulufu walio shuleni pengo lililoshughulikiwa na utafiti huu.

Licha ya mchango wa tafiti za Jekielek na Brown (2005), kama inavyodaiwa na ripoti za The United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization -UNESCO (UNESCO, 2012); The United Nations Population Fund-UNFPA (UNFPA, 2014), habari kamili na mafunzo kuhusu ujinsia ni haki ya kibinadamu. Haki hii ikizingatiwa ina nafasi muhimu katika kukuza na kuimarisha usawa na kuafikiwa kwa malengo ya milenia ikiwa ni pamoja na usawa wa kijinsia, elimu kwa wote pamoja na kukabiliana na athari za maambukizi ya Virusi vinavyosababisha Ukosefu wa Kinga Mwilini (UKIMWI) miongoni mwa wazulufu. Licha ya ripoti hizi kubainisha kuwa ufahamu wa maswala ya kijinsia ni haki ya kimsingi, tafiti za ripoti hizo hazikuzingatia jinsi elimu na habari hizo zinavyofaa kuwasilishwa kwa wazulufu. Aidha hazikuzingatia iwapo wazulufu hawa wana nafasi yoyote au mchango wowote katika mchakato mzima wa kushughulikia maswala yanayowahusu. Hili ni pengo ambalo utafiti ulinuia kujaza kwa kulenga sifa za lugha inayotumiwa na wazulufu kuuumba ujinsia. Watalamu kama vile Ogechi (2005) na Tolman (2005), walibainisha nafasi ya lugha katika kufanikisha juhudi zozote za kijamii. Ni muhimu kujazwa kwa pengo lililo wazi katika ripoti hizo za kimataifa kwa ambavyo bila matayarisho murwa kuhusu maisha ya kijinsia, wazulufu hawajidhibiti na wamo kwenye hatari ya athari kama vile dhuluma za kijinsia, maradhi ya zinaa na HIV/AIDS, mimba zisizopangwa na uavyaji wa mimba (Tolman, 1996; UNESCO, 2012; Tolman, Striepe, na Harmon, 2003).

Licha ya sababu wazi kama hizo za athari za wazulufu kujihusisha na ujinsia mapema, mafunzo kuhusu ujinsia ni swala tatanishi na hukabiliwa na changamoto nyingi katika tamaduni nyingi. Kulingana na Halstead na Reiss (2003), mafunzo yanayohusiana na ujinsia yana changamoto tele. Hali hii wanadai, husababishwa na mtindo wa kimaadili, uanuwai wa kisiasa, kitamaduni na kidini kuhusu maswala ya ujinsia na tabia za kingono miongoni mwa wazulufu. Katika Bara Afrika, kuna ithibati zinazoashiria uhalisia huu (Mbugua, 2007; Avusabo-Asere, Bankole, na Kumi-kyereme, 2008 na Mbonile na Kayombo, 2008). Hali ni iyo hiyo katika bara Asia (Pokharel, na Shakya, 2006; Sridawrung, Pfeil, &na Krozier, 2010). Hata katika tamaduni huru, mjadala kuhusu ujinsia umekumbwa na changamoto kuanzia kwa wazazi nyumbani hadi kwa walimu shuleni. Mijadala hii hukumbwa na changamoto za kimawasiliano miongoni mwa changamoto nyingine (DiCenso, *et al*., 2001; Turnbulla, Werscha na Schaika, 2008; Helleve, Flisher, Onya, Koma, na Klepp, 2011).

Hata kama tafiti hizo zimeweka wazi changamoto ya mawasiliano, hazikubainisha ni mawasiliano kwa namna gani na baina ya wahusika wepi. Aidha tafiti hizo zimeegemea changamoto za uwezekano wa wazulufu kujihusisha na ujinsia mapema na hivyo kuanza kushiriki ngono. Ingawa tabia hii ni kinyume na utamaduni na maadili ya kidini na kijamii, ni uhalisia uliopo kuwa wazulufu wanashiriki ngono. Kwa kufanya hivyo, tafiti hizo zinazua mjadala muhimu wa mtazamo wa jamii pana kwa ujinsia wa wazulufu lakini kwa kuacha nje nafasi ya wazulufu katika mchakato mzima pamoja na lile tatizo la kimawasiliano. Utafiti huu wa sasa ulichunguza leksia na uamilifu wazo, peo na mikakati ya kimazunguzmzo katika uumbaji wa ujinsia miongoni mwa wazulufu. Sifa hizi zaweza kubainika tu katika mjadala unaohusisha maswala ya ujinsia miongoni mwa wazulufu. Katika kafanya hivi, utafiti wa sasa utakuwa ukijenga na kujaliza matokeo ya tafiti hizo kuwa kuna ushahidi kwamba kwa kuwa na mafunzo yanayofaa na yanayozingatia lugha ya wazulufu, wazulufu watakuwa wanaimarishiwa usharifu na tafiti zimebainisha uhusiano wa karibu baina ya usharifu na mafanikio katika maisha ya muhusika (UNFPA, 2012).

Watu wazima kama wahifadhi na watoa habari na mafunzo yanayohusiana na ujinsia kwa wazulufu, huamua yaliyomo kwenye habari za ujinsia ambazo wazulufu watapokea. Hili hufanyika licha ya tofauti kubwa za wanachohitaji wazulufu ikilinganishwa na wanachofikiriwa kuhitaji (Avusabo-Asere, Bankole, & Kumi-kyereme, 2008). Watafiti hawa wamelenga tofauti za matarajio ya makundi hayo mawili-wazazi na wazulufu kama makundi mawili bainifu katika jamii. Ingawa ugunduzi wa uwepo wa tofauti hizo ni hatua ya kwanza katika kushughulikia mada ya

ujinsia miongoni mwa wazulufu, utafiti huo wa Avusabo-Asere, Bankole, & Kumi-kyereme (2008), haukulenga kimahususi ni tofauti zipi zilizopo. Katika kujaribu kujaza pengo hilo, utafiti huu unaangazia sifa za lugha ya wazulufu kama kundi bainifu lililo na mtindo wao mahususi wa matumizi ya lugha ambao ni tofauti na ule wa wazazi. Kwa kufanya hivyo, inatarajiwa utafiti wa sasa utakuwa umechangia tafiti za awali kwa kujaribu kushughulikia tofauti mojawapo iliopo baina ya makundi haya mawili.

### 2.2.2 Ujinsia na Utambulisho wa Wazulufu

Uzulufu hurejelea kipindi cha ukuaji au cha mpito kutoka kwa utoto hadi kwa utu uzima (Arnett, 2007; Albert na Steinberg, 2011). Kwa Mujibu wa Weinreich na Saunderson (2003), utambulisho ni ujumla wa ufasiri wa kibinafsi wa mtu, ambapo jinsi anavyojifasiri huashiria uendelevu uliopo baina ya jinsi mhusika anavyojifasiri, jinsi alivyokuwa na jinsi apendavyo kuwa siku za baadaye. Utambulisho waweza kuwa wa kibinafsi, wa kijinsia, wa kikundi, wa kijamii, wa ujinsia na kadhalika (Meyers, 2004; Brubaker na Cooper, 2000). Utambulisho huchukua sehemu kubwa ya utambulisho wa ujinsia wa faragha na utambulisho wa ujinsia wa hadharani. Dhana muhimu za utambulisho wa ujinsia miongoni mwa wazulufu hushirikisha: usharifu, maisha ya kifantasia, mwegemo wa ujinsia (ubasha, mwelekeo wa kawaida (hali ya kuvutiwa na jinsia tofauti), huntha) na ashiki, mitindo na tabia, pamoja na jinsi mzulufu anavyofanya maamuzi yanayoambatana na ujinsia, mahusiano, majukumu ya kijinsia (Lynn, 2009). Katika utafiti huu maswala ya maamuzi, ashiki na tabia yalikuwa amali muhimu ya uwasilishi wa ujinsia swala lililokuwa linatafitiwa.

Weinstein & Rosen (1991), wanadai kuwa swala moja kuu katika ukuaji na utambulisho wa wazulufu ni uumbaji wa ujinsia. Watafiti hao wanazidi kudai kuwa wakati wa uzulufu, ukomavu wa ujinsia huandamana na ashiki na hamu kubwa ya kujamiana. Kutokana na hilo, wazulufu hutumia muda wao kuzungumza kuhusu dhana mbali mbali zinazohusiana na ujinsia na kubadilishana mawazo (Rice, 2001). Ward (2004) anaunga kauli hizo mkono kwa kusema kuwa mazungumzo hayo ni namna ya wazulufu kuelewa na kuthibiti hisia zao zinazohusiana na ujinsia. Kwa mujibu huo, ripoti ya Planned Parenthood Federation of America (2001) inashikilia kuwa kudumisha mawasiliano wazi na wazulufu kwaweza kuwa namna moja ya wazulufu ya kukabiliana na haja ya kujieleza kwa misingi ya ujinsia wao.

Swala jingine muhimu katika ukuaji na utambulisho wa wazulufu ni uumbaji wa utambulisho wa kisaikolojia ambao ni ari ya kutafuta uelewa wa kibinafsi (Kroger, 2003). Mabadiliko yanayotokea wakati wa uzulufu huwa ni changamoto kwa mzulufu katika kutafuta utambulisho wake mahususi. Watafiti wameonyesha kuwa kazi ya mzulufu kwa misingi ya ukuaji kisaikolojia na kijamii ni kujiainisha, kujitambulisha na kukuza utambulisho wa kijinsia, kimaadili, kisiasa na kidini ulio thabiti na imara (Côté, 2006; Reis na Youniss, 2004). Namna bayana zaidi ya kuumba utambulisho huu na kuuelezea ni kupitia mwili (Greenfield, 2003; Merriwether, 2004). Kazi hizi zilirutubisha utafiti wa sasa na kukuzwa na kazi ya Herring (2000), kwa ambavyo, mawasiliano ya wazulufu kuhusu ujinsia wao kunaweka bayana vidokezo kuhusu utambulisho wao kwa misingi ya ujinsia, uana, na utumizi wa lugha "chafu" au ya matusi. Katika utafiti huu, maneno ibuka katika uwasilishaji wa ujinsia miongoni mwa wazulufu yalitathminiwa na kutambua utambulisho wao kama kundi mahususi katika jamii.

Watafiti wa maswala ya kimahusiano baina ya wazulufu wanadai kuwa masahibu wa wazulufu na wanaohusiana nao kwa karibu huchukua nafasi muhimu katika ukuaji wa kijinsia na utambulisho wa wazulufu (Berndt na Savin-Williams, 1993; Bouchey na Furman, 2003; Connolly, Furman, na Konarksi, 2000). Sifa moja kuu ya uzulufu ni uhitaji wa marafiki wa karibu (Pombeni, Kierchler, na Palmonari, 1990). Pia kuna uhitaji wa ukamilifu wa kimihemuko kutoka kwa marafiki (Larson, 1991). Kutokana na hili, wazulufu huzua makundi madogo ya marafiki yanayoshirikisha jinsia zote mbili na hushiriki nao muda wao na mazungumzo (Goff, 1990). Katika makundi haya huibuka mahusiano ya kirafiki baina ya wavulana na wasichana. Tafiti zimebainisha kuwa kuna utegemezi mkubwa kwa makundi haya kwa ajili ya utambulisho, urafiki na wandani (Connolly, Furman, na Konarksi, 2000). Tafiti hizo pamoja na utafiti wa Brown, Feiring, na Furman (1999), hutazama mahaba ya wazulufu kama muktadha wa ujinsia. Bali na hayo, ikizingatiwa kuwa mahusiano ya kimahaba ni mada muhimu katika mazungumzo ya wazulufu kama walivyotambua Furman na Shaffer (2003), uwasilishi wa ujinsia miongoni mwa wazulufu basi ni swala muhimu katika jamii pana kwa ambavyo kuna ukinzani wa mitazamo baina ya wazazi na wazulufu kuhusu ulimwengu wao wa ujinsia (Kundanis, 2003).

Tafiti hizo, zimeweka wazi mgao wa wazulufu katika makundi madogo madogo yaliyo na sifa anuwai. Hii ni hali muhimu katika utafiti wa sasa ili kuelewa dhana ya mgao wa "sisi" na "wao" katika uwasilishi wa ujinsia. Utafiti huu unapiga hatua na kutathmini sifa ya lugha inayotumika na

wazulufu katika makundi yao wanapozungumzia na kuumba ujinsia wao- mada moja ambayo tafiti zilibainisha hujitokeza katika mazungumzo ya wazulufu.

Kulingana na Epstein na Johnson (1998), uzungumzi wa ujinsia hufanyiza kwa kiasi kikubwa utambulisho, nafasi na tajiriba ya wazulufu. Aidha, uwepo shuleni huumba ujinsia wa wazulufu. Kutokana na hayo, wataalamu hawa wanadai kuwa kuwepo shuleni kwaweza kuchangia katika uzuaji wa ujinsia kandamizi. Hata hivyo, shule na walimu hutazama ujinsia kama swala linalokwamiza juhudi za usomi na ni bora lipuuzwe au lifungwe kwa programu kuhusu ujinsia (Rolon-Dow, 2004). Programu hizi hulenga zaidi habari za kibaolojia na kizahanati katika jitihada za kuafikia malengo ya kimanufaa, kama vile kupunguza mimba miongoni mwa vijana, maradhi ya zinaa na UKIMWI (Luttrell, 2004). Mtazamo kama huu unawasilisha ujinsia na ngono za mapema miongoni wa wazulufu kama "tatizo" la kutatuliwa. Na kulitatua, wazulufu hupewa faradhi kuhusu jinsi ya kukataa/kusema la au namna ya kushiriki ngono salama, lini na nani (Trudell, 1993). Bayana ni kwamba kuna uwasilisho wa aina fulani kuhusu kujamiana kwa wazulufu katika tafiti hizi. Inabainika kuwa kuna kusawiri ujinsia wa wazulufu kama 'tatizo' na hapo tafiti hizi zilichangia katika upanuzi wa mawazo ya mtafiti. Ubainifu wa uwasilishi wa aina hii ni muhimu kwani kwa mujibu wa nadharia ya uchanganuzi wa peo sharti kuwe na swala la kijamii na swala hilo liwekwe katika seti tangulizi za peo za kuongoza utafiti.

Sababu kuu ya wazulufu kunyimwa habari, huduma za afya kuhusiana na kujamiana na vifaa vya kujikinga (kama vile mipira) hutokana na namna kinzani ambazo kwazo wazulufu hutazamwa (Aggleton & Warwick, 1997; Forrest, 2000; French na Dishion, 2003). Aidha wazazi wengi hupata ugumu wa kuwatambua wazulufu kama watu wanaoweza kuthibiti ashiki zao, na basi, swala la ujinsia kwa wazulufu hutazamwa kama jambo ambalo sharti lidhibitiwe. Watalamu Aggleton na Warwick (1997) katika utafiti wao kule Zimbambwe kwa mfano waligundua kuwa inaaminika kwamba 'wahifadhi' wa tamaduni za Zimbambwe, wazazi na shule huwaona vijana wazulufu kama watu ambao ni wa kufanya mambo ya hatari na wapenda anasa wanaoishi kwa ajili ya wakati uliopo. Mitazamo kama hii imedaiwa kulemaza uelewekaji wa wazulufu na mahitaji yao. Aidha, hulazimu vijana kutazamwa kama watu walio na msururu wa upungufu wa maarifa, mielekeo na stadi. Kauli hizi zinakuza itakadi ya wazazi wa wazulufu kuwa wazulufu wanastahili kudhibitiwa kitabia. Hata hivyo, wazulufu wanajitambua kama kundi lililo na haki zao na lililofikia ukomavu fulani na basi wana uwezo wa kujiamulia mkondo wa maisha yao.

Inawia muhimu kulitafitia kundi hili la wazulufu kwa misingi ya lugha ili kubainikiwa na jinsi wanavyoumba ulimwengu wao wa ujinsia. Eaton, Flisher, na Aaro (2003), McFadden (2003) na Tamale (2003) wanadai kwamba UKIMWI, ambao kwa kiasi kikubwa ni tokeo la kushiriki ngono, kumezua mabadiliko katika ulimwengu wa ujinsia. Jamii hivyo basi imelazimika kutathmini na kuangalia upya swala la ngono. Wasomi hawa wanasisitiza kuwa tatizo la UKIMWI zaidi ya yote, limezua ari ya kuvumbua baadhi ya visaasili na mitholojia kuhusu ujinsia. Ari hii ndiyo iliyokuwa amali ya utafiti huu kwani imezua mazungumzo, elimu na nasaha kwa yanayozungukia swala tafitiwa. Ni muhali hata hivyo kutaja kwamba tafiti nyingi zimeratibu ukimya uliokithiri kuhusu uchu wa wanawake.

Licha ya wasichana kupewa maagizo ya mara kwa mara ya jinsi ya "kukataa" (kusema la); habari kuhusu nini cha kufanya wanapotaka "kukubali" (kusema ndio) ni finyu mno (Fine na McClelland, 2006). Ukosefu wa habari kama hizi unachangia ugavi wa wasichana kwa misingi ya "wabaya" na "wazuri" (Pichler, 2001). Cameron na Kulick (2003) wanatumia ugavi wa wasichana 'wazuri' na 'wabaya' kushadidia maoni ya Fine na McClelland pamoja na Pichler. Wanarai kuwa dhana ya wasichana 'wazuri' hutumika kuashiria tabia inayokubalika. Ugunduzi wa watafiti hawa kuhusu kundi 'baya' na 'zuri' kulirutubisha utafiti huu hususan kwa kuweka wazi baadhi ya peo za kimazungumzo. Hata hivyo, utafiti huu uliangazia peo za kimazungumzo zinavyojitokeza katika uwasilishi wa ujinsia miongoni mwa wazulufu walio katika shule za upili. Tofauti na Pichler, Cameron na Kulick, walioangazia jinsia moja pekee katika mazungumzo yao kuhusu ujinsia na ngono, utafiti huu uliwashirikisha wazulufu wavulana na wasichana kwa pamoja.

Uzungumzi wa kimahaba na ubikira unakuza mgao wa wasichana "wazuri" na "wabaya" (Holland na Eisenhart, 1990). Wataalamu hawa wanatanbihi kuwa wasichana wanaoruhusu ngono pasi na "fadhila" hufasiriwa kama wasichana "wabaya". Vivyo hivyo, uzungumzi kuhusu ubikira huwahakikishia usalama wa kifikra na tendo la ndoa wasichana "wazuri" wanaosubiri kuvunja ubikira wao kwa 'pendo' lao la kweli au angalau kwa mtu anayewajali. Aidha kauli za kushika mimba, kuambukizwa maradhi na kusutwa na mahirimu hujitokeza katika mazungumzo kuhusu ngono. Wavulana imetambuliwa huwa na shinikizo la kuthibitisha ubabedume wao kupitia kuwasaka wasichana. Kwa mujibu wa Sapon-Shevin na Goodman (1992), masimulizi kama haya huwasawiri wavulana na wasichana kama mahasimu katika mchezo wa ujinsia ambapo wavulana

wanausaka ubikira ilhali wasichana wanapigania kuuhifadhi. Tafiti hizi ziliunufaisha utafiti huu kwa kuweka wazi kuwa jamii imegawa tabia ya tendo la ndoa katika makundi ya: tabia inayokubalika na tabia isokubalika. Ili kuweza kukoleza mgao huo, je basi wazulufu wanazungumzia na kuumba vipi ujinsia ikizingatiwa kuwa wavulana wanakimbizana na ubikira huku wasichana waking'ang'ania kuuhifadhi?

Lichtenstein (2000) anakariri kuwa kuwepo UKIMWI kumezua usemi na uzungumzi unaozungukia mtazamo mpya kuhusu ubikira unaowasilisha ubikira kimazungumzo kama uadilifu wa kiafya kwa jinsia zote mbili. Hata hivyo, ingawa usawiri huu bado una mashiko kwa misingi ya dini na maadili, wataalamu wa afya wanausisitiza kama jambo la afya na tahadhari. Mbali na kuwasilisha ubikira kimazungumzo kama jambo linalofaa kwa jinsia zote, imegunduliwa kuwa wavulana wakati mwingi hawaonei fahari ubikira wao wakilinganishwa na wasichana. Aidha, kutokana na athari za mabadiliko ya kijamii na shinikizo la mahirimu, kuna wasichana wanaouona ubikira kama jambo linaloleta waa na hapo kuwa na mawazo sawa na wavulana. Ugunduzi huu unashadidia ule upeo wa udharura ulioasisiwa na Kelly (2007) ambapo mhusika hutaka kuupoteza ubikira wake haraka iwezekanavyo. Kwa kuchanganua peo na mikakati ya uzungumzi katika mazungumzo ya ujinsia miongoni mwa wazulufu, utafiti huu ulitofautiana na tafiti hizi kwani hazikuangazia peo na mikakati ya uzungumzi. Utafiti huu pia haukujihusisha na kutambulisha ni kina nani wanaoonea fahari ubikira mbali ni kung'amua peo za kimazungumzo na fasiri zinazojitokeza.

### 2.2.3 Ujinsia na Lugha

Kunazo tafiti kadhaa zinazohusiana na lugha, ujinsia na mikakati ya kimazungumzo baina ya wazulufu inayopatanisha uumbaji wao wa ujinsia na au ubunifu wao wa matumizi ya lugha kuuwasilisha ujinsia. Kuhusu athari ya mazungumzo yanayohusiana na mwanamke mkoo, imetambuliwa kuwa wasichana vijana hutumia unyanyapaa unaombatana na hali ya kuwa mwanamke mkoo kuunda mipaka ya kihadhi baina yao kama makundi yanayohusishwa na hadhi na wakati uo huo kuthibiti tabia za kiujinsia na utendaji wa kijinsia (Armstrong, Hamilton na Seeley, 2014). Utafiti huo unadai kuwa wanawake walio na hadhi ya juu hutumia usemi unaombatanishwa na mwanamke mkoo kujinufaisha ilhali wanawake wa hadhi ya chini huutumia kuashiria kero lao la kutengwa na ushiriki wao katika vitendo vya kiholela vya kujamiana. Kwa namna hii basi wanakuwa wanyonge na wepesi wa kusutwa na kupata fedheha.

Tafiti hizo zilizua maswala muhimu kama vile ya manufaa kwa kundi mahususi na kero linalotokana na tabia fulani maswala ambayo ni muhimu katika kuelewa udumishaji wa ubabedume na ugandamizi kilugha ambao wavulana huutumia kuwatawala wasichana. Licha ya kunufaisha utafiti huu kwa kauli hizo, utafiti wa Armstrong na wenzake hukubainisha sifa za lugha ya wazulufu pengo ambalo utafiti huu ulikusudia kulijaza. Aidha utafiti huo uliangazia matumizi ya lugha kwa mrengo wa jinsia ya kike tu. Utafiti huu uliangazia sifa za lugha inayotumika na jinsia zote mbili.

Watafiti na wataalamu wa ujinsia wanadai kuwa ujinsia ni tatizo la kiisimu (Okami, Olmstead, & Abramson, 1997). Basi swala la lugha sharti lizingatiwe katika tafiti zinazohusiana na ujinsia. Madai haya yanapata mashiko katika mjadala wa Leclerc-Madlala (2004) kuhusu ufinyu wa mkusanyiko wa kiisimu katika kushughulikia swala la ujinsia katika Afrika Kusini mwa Sahara. Mtafiti huyu anadai kuwa kuna ufinyu wa misamiati ambao ni zao la "Victorian-era sexology". Ingawa Manderson kwa upande wake anasisitiza umuhimu wa kuangazia ni kina nani hutumia dhana fulani za kileksia na jinsi wanavyotumia katika uchunguzi wa maana na athari za dhana hizi, Leclerc-Madlala (2004) anapendekeza kuwepo viunzi dhana vya kiwasilisho ili kufanikisha uelewaji wa ujinsia katika Afrika Kusini mwa Sahara. Wataalamu hao wanakubaliana kuwa licha ya tafiti kuonyesha jinsi "wengine" hutambulisha au kurejelea ujinsia katika Afrika Kusini mwa Sahara, jinsi wazulufu wenyewe huzungumzia swala hili hakujatiliwa maanani. Utafiti huu ulijaribu kujaza pengo hili kwa kuangazia maneno wayatumiayo wazulufu kuzungumzia na kujadiliana kuhusu ujinsia miongoni mwao. Utambulisho na uchanganuzi wa leksia hizo utakuwa ni upenyo katika lugha ya kizazi kilicho shuleni na kiingilio muhimu katika maisha yao.

Moto (2000) katika utafiti wake alidai kuwa Wamalawi hutegemea misemo ya mshabaha isiyo wazi, usafidi/tasfida na nahau kuzungumzia swala la ngono na UKIMWI. Machera (2004) alithibitisha hili katika utafiti wake wa urejelezi wa sehemu za uke na umme katika miji ya Kenya. Matokeo yake yanapiga hatua zaidi na kudai kuwa ingawa hisia za aibu zinahusishwa na urejeleo wa kimatamshi wa uke, hali ni tofauti ambapo dhakari inatajwa. Ugunduzi wa watafiti hawa ni muhimu kwani urejelezi na uzungumzi kuhusu ujinsia ni swala ambalo lingali mwiko na halizungumziwi tu; hulazimu uwepo wa namna fulani au lugha fulani ya kurejelea sehemu za ujinsia. Aidha kizazi cha wazulufu ni kizazi nyumbufu katika shughuli zake lugha ikiwemo. Mbali na hayo, utambuzi wa kuwepo aibu unaweza kuzua peo fulani za kimazungumzo. Je uchu

utawasilishwa vipi kimazungumzo na wazulufu ambapo Shefer & Foster (2001) wamesisitiza umuhimu wa kuwa na usemi chanya kuhusu uchu miongoni mwa wanajami?

Cense (2014) anabainisha jinsi vijana walio wachache kiukoo kule Uholanzi wanavyotathmini na kuweka peo tajiriba zao katika mazungumzo anuwai kuhusu ujinsia. Kulingana na utafiti huu, vijana hubadilishana na hushiriki maelezo ya tajiriba zao za matendo yanayohusiana na ujinsia miongoni mwao. Mazungumzo haya huumbwa upya kulingana na miktadha mahususi na mahitaji maalum. Utafiti huu aidha unatathmini jinsi vijana hawa wanavyozua mikakati kupatanisha usemi kinzani unaozuka kutokana na mgongano baina ya usemi wa nyumbani na usemi uliopo wa kawaida katika jamii ya Kiholanzi. Utafiti huo unahitimisha kwa madai kuwa uelewa bora wa mifumo mbali mbali ya uwakala wa ujinsia baina ya vijana unahitajika ili kuunga mkono uundaji wa mipango ya afya iliyo na misingi katika uhalisia wa ujinsia wa vijana na maisha yao (Bell, 2012). Matokeo ya utafiti huo yanabainisha kuwa uhitaji wa uwakala wa ujinsia wafaa kutazamwa kwa misingi ya uhitaji mwingine kama vile uhitaji wa kujitegemea na kupinga kaida za kijamii na kiisimu zilizoegemezwa kwa mawazo ganda.

Ogechi (2005) na Beck (2015) walitathmini lugha ya vijana na wanafunzi wa vyuo vikuu nchini Kenya kuhusu ngono na maradhi na au maambukizi ya UKIMWI. Katika tafiti zao wanaweka wazi ubunifu wa vijana katika urejelezi wa maswala hayo. Katika tafiti zao, wataalamu hawa wanarai kuwa wahudumu na waangalizi, wanakampeni na watekelezi wa sera za afya sharti wawepo na watumie lugha bunifu ya vijana hususan Sheng ili kufanikisha utoaji wa huduma za afya. Gonzalez na Anna-Brita (2011) pia wanatathmini ubunifu wa lugha baina ya vijana wanaosema lugha ya Kiingereza na Kihispania wakilenga zaidi utumizi wa lugha ya mtaani (slang). Utafiti huu unaweka wazi utaratibu wa kiisimu uliopo katika lugha ya mitaani kama mtindo wa kujieleza katika lugha ya vijana (Emanatian, 1996; Bucholtz na Skapoulli, 2009; Mensah, 2016 na Mensah, 2012). Utafiti wa Gonzalez na Anna-Brita unadai kuwa matineja wa Kihispania huzungumza kuhusu mihadarati ilhali matineja wa Uingereza huzungumza kuhusu ngono. Mbali na hayo wanabainisha kuwa vijana wa Kihispania hutumia kauli za mneni pamoja na usemi shadidi kwa kiwango kikubwa kuliko wenzao kutoka Uingereza ambao, hata hivyo ni watumizi wa kauli na maneno ya kushusha hadhi kwa wingi.

### 2.2.4 Wazulufu na Ujinsia

Kwa mujibu wa Centres for Disease Control and Prevention (2009), ujinsia na tabia hatarishi za ujinsia miongoni mwa wazulufu (hali inayofafanuliwa kama ushiriki wa ngono mapema, pamoja na kujamiana bila kinga na marafiki wengi), ni swala la kusikitisha ikizingatiwa athari hasi zinazotakana na hali kama hiyo. Hata hivyo, watafiti wameonyesha kuwa ulezi una mchango chanya katika kudhibiti ushiriki katika tabia hatarishi miongoni mwa wazulufu (Kotchik, Shaffer, Forehand, na Miller, 2001; Zimmer-Gembeck na Helfand, 2008). Tafiti hizi zinalenga zaidi uhusiano uliopo baina ya ulezi na tabia hatarishi za ujinsia miongoni mwa wazulufu.

Aidha tafiti nyingine nyingi (Brody, *et al.*, 2006; DiClemente, *et al.*, 2008; Dittus, Miller, Kotchick, na Forehand, 2004), zinalenga namna ya kuzuia matendo ya wazulufu ya ujinsia katika muktadha wa familia. Tafiti hizi hazijazingatia nafasi ya wazulufu wenyewe katika swala nzima hususan kwa kuangazia jinsi wao wenyewe wanavyouawasilisha ujinsia wao ilhali uelewa wa jukumu la wazulufu ni muhimu katika kubaini mwelekeo wa tabia zao zinazohusiana na ujinsia. Hili ni pengo ambalo utafiti ulikusudia kulijaza kwa kuweka wazi sifa za lugha wanayoitumia wazulufu katika kuumba na kuuwasilisha ujinsia wao.

Bearman na Brückner (2001), Dennison na Russell (2005) wanadai kuwa tafiti nyingi zimetathmini ungono wa wazulufu kwa mkabala wa tabia hatarishi kama ilivyo kwa utafiti wa (Zimmer-Gembeck & Helfand, 2008). Utafiti wa Centres for Disease Control and Prevention (2009) ni mfano bora. Utafiti huo ulibaini kuwa takriban asilimia 50 ya wazulufu walio katika kiwango cha gredi ya 9-12 kule Marekani wamejamiana. Kati ya hawa, asilimia 7.1 walishiriki ngono kabla ya kuhitimu miaka kumi na mitatu (awamu ya uzulufu wa mapema). Asilimia 14.9 walikuwa wamejamiana na zaidi ya wenzi wanne na thuluthi moja hawakuwa wametumia namna yoyote ya kujikinga. Tafiti hizi ni za wingi idadi na takwimu zinazotoa muhtasari wa kuenea kwa tabia za kingono za vijana. Aidha zinatoa maelezo ya visababishi vinavyoathiri tabia zao za ngono na kufafanua matokeo yanayohusiana na tabia ya ngono. Utafiti huu unanufaika na tafiti hizo kwa ambavyo swala la wazulufu kushiriki ngono mapema limefanyiwa utafiti na kuangaziwa. Hata hivyo, utafiti huu ulilenga jinsi wazulufu wenyewe wanavyoumba ujinsia wao kiisimu bila ya kujihusisha na idadi na asilimia za wazulufu wanaojihusisha na ngono za mapema. Mintarafu hii, utafiti huu ulitumia leksia zinazojitokeza kuafikia malengo yake.

Tolman (2005) akiwatafitia wazulufu wasichana anadai kuwa wasichana hukumbwa na mtanziko wa aidha kukubali au kukataa kutenda kulingana na hisia za uchu. Mtanziko huu unazuliwa na wasiwasi kuhusu matokeo ya (kibinafisi, kimwili, kijamii na kimahusiano) kushiriki ngono maoni yanayoshikiliwa na Tannen (2013) na Tolman, Striepe na Harmon (2003). Utafiti huu ulilenga tu jinsi ngono za mapema huwasilishwa kimazungumzo. Ugunduzi wa watafiti hawa unarutubisha na kushadidia ukweli kwamba mazungumzo kuhusu swala lolote lile ujinsia ukiwemo husheheni peo anuai za kimazungumzo. Kwa matilaba ya utafiti wao inabainika kwamba mijadala ya ujinsia huakisi peo za matokeo au peo za hatari. Ugunduzi wa uwepo wa aina fulani za peo katika mijadala inayohusu ujinsia ni swala la kati katika kutambua peo zilizopo katika uumbaji na uwasilishi wa ujinsia miongoni mwa wazulufu. Aidha, mchango wa tafiti hizo unaambatana na maelekezo ya nadharia ya uchanganuzi peo ambapo seti tangulizi za peo zafaa kuanishwa kabla ya kuanza kuchanganua peo za utafiti mwingine. Ifahamike kuwa, utafiti huu ni wa kimaelezo bali si wa kitakwimu au wingi idadi. Aidha, haikuzingatiwa kuonyesha kukithiri au kuenea kwa tabia za kingono miongoni mwa vijana.

Mazungumzo ya ngono baina ya wasichana wa asili ya British- Bangladesh husheheni peo mbili kuu za kimazungumzo: peo cheshi/tanifu na peo zisizo tanifu katika mijadala yao kuhusu ngono (Pichler, 2001). Kuna baadhi ya tabia za ngono miongoni mwa wanawake ambazo hufasiriwa kama zinazokubalika (Sprecher, Hatfield, Cortese, Potapova na Levitskaya, 1994). Muhimu katika ugunduzi huu ni ile hali ya kugawa tabia kuwili: tabia inayokubalika na tabia isokubalika. Aidha kutokana na utafiti wa Pichler, inabainika kuwa peo zinagawika kuwili. Dhana ya uwepo wa migao (iwe ni baina ya wazulufu au ni katika peo zinazojitokeza) ni swala muhimu katika utafiti huu kwa ambavyo inaboresha na kuchangia ufafanuzi wa “sisi” na “wao” kama inavyojitokeza baina ya wazulufu. Mintarafu hiyo, tafiti hizo zinakoleza hamu ya kutaka kugundua jinsi ujinsia unavyowasilishwa na wazulufu pamoja na kutaka kubaini mikakati ipi inajitokeza katika kuzungumzia swala hili ili kupinga au kukuza na kudumisha itikadi iliyopo.

Holland, Ramazazanoglu, Scott, Sharpe na Thomoson (1991) wanadai kuwa kwa wavulana, kuvunja ubikira wao huashiria kuwa ‘mwanamume’ kwa namna ambayo si sambamba na tajiriba ya wasichana. Wavulana kawaida huwa na shinikizo la kuthibitisha uwezo kiume wao kwa kuwasaka wasichana ilhali wasichana wanapigania kuuhifadhi ubikira wao. Licha ya kuwepo kwa madai hayo, ni bayana kuwa thamana ya wasichana ya kuhifadhi ubikira wao imedidimia hususan

ikizingatiwa usasa na mabadiliko ya kijamii ikilinganishwa na ukale. Ili basi kushadidia usuli wake je wazulufu huzungumzia vipi ujinsia ikizingatiwa kuwa wazulufu wameathiriwa na usasa?

Kunkel, *et al.* (2000 na 2007), Kunkel, Eyal, Finnerty, Biely, na Donnerstein (2005), Eyal na Kunkel (2008), waligundua kuwa 68% ya vipindi vyote katika runinga huhusisha mazungumzo kuhusu ngono na kwamba 35% ya vipindi vyote huhusisha tabia ya kingono. Inabainika kuwa wavulana huwathamini na kuwateua wasichana kwa mujibu wa umbo lao. Aidha kuwa ngono ni tendo la kuthibitisha ubabedume. Watafiti hawa aidha walilenga kuweka wazi kiwango cha usawiri wa hatari na uwajibikaji. Ilitambulishwa kuwa kwa kila vipindi kumi vilivyo na mada ya ngono kimoja hujadili vijimada vya hatari na uwajibikaji.

Aubrey (2004) anapiga hatua zaidi bali na kuangazia athari za wazi kama vile mimba zisizopangwa, kuambukizwa maradhi ya zinaa na kudhulumiwa, alizingatia pia athari za kimihemuko kama vile masikitiko, majisuto/wasiwasi, athari za kijamii kama vile kudhalilishwa au kukataliwa na adhabu kutoka kwa mzazi au mtu mwingine mwenye mamlaka. Aidha alikodi matokeo chanya: kuongezeka kwa kujistahi, kukaribiana, fahari katika kuzidisha sifa za mtu binafsi, kuridhika kimwili na mimba ilokusudiwa (Roberts, Henriksen, & Foehr, 2009). Haya ni mambo muhimu yaliyo na uwezo wa kuzua au kuzuliwa kwa peo na mikakati ya kimazungumzo, swala ambalo lilitafitiwa katika utafiti huu.

## 2.3 Msingi wa Nadharia

Nadharia ni taratibu, kanuni na misingi ambayo imefanyiwa utafiti na imejengwa katika muundo wa kimawazo kwa madhumuni ya kutumiwa kama kielelezo cha kuelezea jambo (Massamba, 2009). Hivyo basi, nadharia huchukuliwa kama dira au mwongozo wa kumuongoza mtafiti/mchambuzi ili kulielezea vema jambo fulani kwa mtazamo unaotarajiwa kuwa imara zaidi. Kwa msingi huu, utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili: Nadharia ya Uchanganuzi Peo iliyoasisiwa na Goffman (1974) na Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki wa Usemi hususan muundo msingi ulioasisiwa na van Djik (2005).

### 2.3.1 Nadharia ya Uchanganuzi Peo

Nadharia ya Uchanganuzi peo ipo katika uwanja mpana wa Isimu Maingiliano. Kimsingi, huangazia jinsi makisio ya pamoja huumba maana na ufasiri wa matukio. Nadharia hii iliasisiwa na Goffman mwaka wa 1974 na kukuzwa katika kazi ya kichanganuzi ya Tannen (1979).

Nadharia ya uchanganuzi peo hushikilia kuwa jinsi ujumbe huwasilishwa kwa watu huathiri uumbaji wa maoni kuhusiana na swala linaloangaziwa. Kwa mujibu wa nadharia hii, kuweka jambo katika peo ni ile hali ambayo kwayo watu hukuza namna fulani ya kutazama jambo fulani au kuongoza kufikiria kwao kuhusu jambo hilo. Nadharia hii inashikilia kuwa peo alizonazo mtu katika mawazo yake huathiri maoni yake. Aidha utaratibu wa kuweka jambo katika peo huhusisha:
(a) muktadha wa wasilisho,
(b) uhusiano na matukio ya awali,
(c) ufungamano na shughuli nyinginezo za sasa na
(d) muundo wa uwasilisho.

Kwa mujibu wa taratibu hizo, kina cha nadharia hii ni kwamba jambo fulani hutazamwa kwa mikabala mbali mbali na kufasiriwa kama lililo na vidokezo vya kidhamana na uzingatifu. Hali hii huafikiwa kwa kuangazia sifa/dhana fulani za jambo hilo kama vile madhara au athari zake au hata uhusiano na maswala muhimu. Kwa kufanya hivi mnenaji anakoleza peo katika mazungumzo. Kulingana na nadharia hii, kuna daraja nne katika uchanganuzi wa peo za kimazungumzo:

a) Jambo fulani hutambuliwa. Upeo wa kimazungumzo hufasirika tu kwa uhusiano na jambo mahususi (Entman, 2004). Katika utafiti huu swala ambalo lilitambuliwa ni ujinsia.
b) Kutambulisha lengo. Iwapo lengo ni kuelewa jinsi peo hizi za kimazungumzo huathiri maoni ya umma, kuna haja ya kutenga mwelekeo fulani. Katika utafiti huu mtazamo ni kwa mwelekeo wa jumla kuhusu kuwa na mpenzi shuleni ambapo hali hii hukashifiwa.
c) Kuteua amali kwa minajili ya uchanganuzi. Katika utafiti huu amali ya uchanganuzi ni data iliyorekodiwa kutokana na mazungumzo baina ya wazulufu kuhusu ujinsia katika vikundi viini.
d) Seti tangulizi za peo za kimazungumzo kuhusu jambo husika hutambulishwa kimantiki ili kuzua mfumo wa kukodi na kupata seti za peo zilizopo kitamaduni.

Kwa mujibu wa kauli hii, peo tano tangulizi zilitumika. Peo hizi ni mkusanyiko wa peo kutoka kwa watafiti Kelly (2007) aliyeainisha peo tatu (upeo wa udharura, upeo wa kujihini na upeo wa taratibu) na Kaufman, Michael, na Deborah (2003) walioanisha peo nne (upeo wa utambulisho na uainishaji, upeo wa mamlaka, upeo wa taratibu na upeo wa madhara dhidi ya manufaaa).

Kulingana na madhumuni ya utafiti huu, peo tano (upeo wa udharura, upeo wa kujihini, upeo wa utaratibu, upeo wa mamlaka na upeo wa utambulisho na uanishaji) zitatwaliwa na ambazo zimefafanuliwa ifutavyo:

i) *Upeo wa udharura*: Upeo huu huangazia swala husika kama jambo ambalo ni la kupendeza na lililo muhimu. Kutokana na mtazamo huu, swala husika huenda likatekelezwa ili kuweza kuafikia utambulisho chanya. Iwapo jambo husika halitatekelezwa, mhusika huwa usharifu wake umepata pigo kwani huainishwa na sifa hasi.

ii) *Upeo wa kujihini*: Upeo huu hutawaliwa, kujengwa na kukuzwa na maneno ya kitasfida kuhusu swala husika. Upeo huu huegemea uadilifu au ukosefu wa maadili (Kelly, 2007). Upeo huu umejengeka katika imani na mitazamo ya watu.

iii) *Peo za utambulisho na uainishaji:* Ambapo washiriki hujiona au hutazamwa kuwa na utambulisho fulani katika swala husika. Wanadai kuwa utambulisho huu hutokana na usawiri wa mtu binafsi na ujinasibishaji na kikundi au vikundi. Jinsi mtu anvyojihakiki ndivyo atakavyopinga tendo au kutekeleza tendo fulani. Kupuuza habari na mitazamo inayohatarisha utambulisho, kuimarisha ushirikishaji na kuwaainisha wengine kwa namna hasi ni baadhi ya namna za kutambulisha upeo huu. Katika uainishaji, wahusika huwaainisha wahusika wengine katika swala husika kwa sifa fulani. Peo hizi zina ukuruba mkubwa na uzuaji wa wazo-ganda, zaweza aidha kuwa hasi au chanya. Wahusika kawaida huumba peo ainishi kwa wengine kwa namna inayotofautiana na jinsi kundi hilo lingine hujiona. Mgao wa aina hii hudhoofisha uhalali wa wengine. Kwa mujibu huu peo hizi zitachangiana na ule mgao wa van Djik (2005) wa kujiwasilisha au kujiainisha kwa namna chanya na kuwawasilisha au kuwaainisha wengine kwa namna hasi. Upeo huu hutekeleza jukumu la kukoleza utambulisho wa muhusika na kutetea vitendo vyake.

**iv)** *Peo za Mamlaka:* Upeo huu humfaa mtu katika kuamua ni mamlaka yepi yaliyo halali na yale ambayo yanaweza kukuza nafasi yake kwa namna chanya miongoni mwa wanachama wa kundi na jamii pana. Aidha ni upeo muhimu katika uhalalishaji wa jambo au mtazamo wa mhusika.

Kwa mujibu wa nadharia hii, mtafiti ana hiari ya kuteua kati ya ukodi wa kiada na ukodi wa mashine. Licha ya kuwa kukodi kwa mashine huwa ni rahisi na haraka, hupungukiwa katika

kutambulisha peo/ mbadala/mpya za kimazungumzo ambazo labda hazikutambuliwa katika mfumo wa seti tangulizi. Kutokana na hilo, katika utafiti huu, ukodi wa kiada ulitwaliwa kutokana na unyumbufu wake.

### 2.3.2 Uchanganuzi Hakiki wa Usemi

Uchanganuzi Hakiki wa Usemi (UHU) ni mkabala wa kisasa katika utafiti wa lugha na usemi. Hufasiriwa kama utathmini wa jinsi jamii-lugha hutumia lugha. Hutambulisha dhana za kiisimu zinazobainisha tanzu tofauti na pia vipengele vya kijamii na kitamaduni vinavyosaidia katika ufasiri na uelewa wa matini mbali mbali na aina tofauti tofauti za mazungumzo. Msingi muhimu wa uchanganuzi hakiki wa usemi ni ukweli kwamba lugha ni zao la jamii. Pia, huzalisha imani na thamani za jamii ambamo lugha hutumika. Aidha wasomaji au wasikilizaji ni wapokezi hai (Wodak, 2007). Wananadharia hii wanashikilia kuwa raslimali kuu ya uchanganuzi katika UHU ni matini.

Halliday (1985) anasema kuwa sifa za kileksia na kisarufi za matini huwa na majukumu yafuatayo: kuuwakilisha na kuusawiri ulimwengu halisi na wa kijamii; kuumba na kuathiri mahusiano ya kijamii. Zaidi ya kufafanua makisio ya kijamii yanayoelezwa katika muundo pana wa matini, uchanganuzi waweza pia kufafanua chaguo fulani la kileksia kama vile maneno, majina na uwakilishaji wa kisarufi wa udharura na utendaji. UHU huchunguza na kuchanganua matini kutambulisha vyanzo vya kimazungumzo vya mamlaka, utawala, utabaka na upendelevu na jinsi vyanzo hivi huanzishwa, kudumishwa, kuzuliwa upya na kuumbuliwa katika miktadha ya kijamii, kisiasa na kihistoria (Van-Djik, 1993).

Fairclough, (2001 na 2003), aliorodhesha mihimili minane ya UHU. Kwa matilaba ya utafiti huu mhimili unaosisitiza kwamba UHU hushughulikia matatizo ya kijamii ni wa kati kwani swala lililoshughulikiwa ni tatizo la kijamii. Kwa kuangazia mhimili kuwa usemi hutekeleza kazi ya kiitikadi, katika utafiti huu inachukuliwa kuwa kujihini kushiriki au kutoshiriki ngono za awali ni swala la kiitikadi. Aidha ni bayana kuwa usemi katika mazungumzo ni tendo la kijamii. Kauli hii ni ya kati hususan kwa kuzingatia maoni ya Fairclough, kuhusu UHU kwamba UHU huonyesha kwa nini mzungumzaji au mwandishi, miongoni mwa miundo na mitindo ya lugha huchagua maumbo au mitindo fulani (Fairclough, 2003). Uchanganuzi utakaofanywa utakuwa wa kimaelezo na kifafanuzi kulingana na mhimili wa saba. van Djik (2006), anashikilia kuwa matini haitumiki

tu kufahamisha bali pia hutumika kuumba ukweli kutegemea itikadi na msimamo wa muhusika. Basi kulingana naye mhimili mmoja wa UHU ni kubainisha mikakati ya uzungumzi ambayo hutumika kuumba au kudumisha itikadi na upendelevu katika miktadha mbali mbali. Kwa mujibu wa van Djik (2011) itikadi ni mwelekeo ambao watu au kundi fulani hushikilia kuhusu maswala fulani. Kwa minajili ya madhumuni ya utafiti huu muundo msingi wa van Djik (2005) utatwaliwa.

### 2.3.3 Muundo Msingi wa Kitambuzi

Uumbaji wa ujinsia ni dafina ya utafiti unaohusisha matini semwa. Lugha si maneno tu bali hubeba maana na baadhi ya maana hizo hufasirika tu kwa watumizi lugha kwa misingi mbali mbali (Wodak 2007). Ni kutokana na maelezo hayo muundo msingi ufuatao wa kitambuzi ukabuniwa

***Kilelezo 1:Muundo Msingi wa Kitambuzi***




Uwasilishi wa ujinsia hubeba maneno na virai vya maneno ambavyo ni deta ya utafiti huu. Maneno hayo husitri peo na mikakati anuwai ya kimazungumzo ambayo imechanganuliwa kwa mujibu wa nadharia ya uchanganuzi wa peo na muundo msingi wa uchanganuzi usemi ulioasisiwa na van Djik. Kutokana na peo na mikakati hiyo, utafiti unaweka wazi uelewa na ufasiri wa ujinsia miongoni mwa wazulufu katika shule za upili nchini Kenya na hivyo kuathiri maamuzi yao na kuwapelekea kushiriki au kutoshiriki(matendo) ngono za mapema.

## SURA YA TATU

## MBINU ZA UTAFITI

### 3.1 Utangulizi

Sura hii inafafanua maswala muhimu katika mbinu za utafiti zilizomwezesha mtafiti kutekeleza utafiti uliodhamiriwa. Utafiti huu ulijikita katika uchanganuzi wa uwasilishi wa kimazungumzo wa ujinsia baina ya wazulufu. Masuala yanayoshughulikiwa katika sura hii ni pamoja na: mahali pa utafiti, mfumo wa uteuzi wa sampuli, njia ya utafiti na ukusanyaji deta, deta, mfumo wa uchanganuzi deta na ufasiri wa deta.

### 3.2 Mufumo wa Utafiti, Mahali pa Utafiti na Jamii Kusudiwa

Utafiti huu ulikuwa ni wa kithamano na ulifanyika nyanjani katika shule tatu katika jimbo la Nakuru. Jimbo hili liliteuliwa kwani ni jimbo wakilishi kitamaduni na kimila. Jamii husika ni wanafunzi wa shule za upili kuanzia kidato cha kwanza hadi kidato cha nne.




Ramani ya Jimbo la Nakuru

### 3.3 Mfumo wa Uteuzi wa Sampuli

Uteuzi wa kimaksudi ulitumika kuteua sampuli ya shule tatu: shule mbili za bweni (moja ya wanafunzi wa jinsia ya kiume na nyingine ya wanafunzi wa jinsia ya kike) na shule moja ya mseto na isiyo ya malazi. Jumla ya wanafunzi 104 waliteuliwa kushiriki katika utafiti na waliwekwa katika makundi mawili; kidato cha kwanza na cha pili ili kuunda kundi la wanafunzi wachanga na kidato cha tatu na nne ili kuunda kundi la wanafunzi komavu. Kwa ambavyo shule zilizoteuliwa

hazikuwa na idadi sawa ya wanafunzi na vidato, uteuzi ulifanyika kimahususi katika kila shule. Mtafiti alipata orodha ya wanafunzi kutoka kila shule ("A, B, C" - hizi ni kodi za shule zilizoshiriki) na kutumia mfumo wa kitarakilishi wa kuibuka na nambari za kinasibu.

Katika shule ya A- (ambayo ni shule ya wasichana) na shule B- (ambayo ni ya wavulana), kidato cha kwanza na pili kulikuwa na vijidato vitano ambapo wanafunzi wawili kutoka kila kijidato waliteuliwa hivyo kuwa na wanafunzi kumi katika kidato cha kwanza na wanafunzi kumi katika kidato cha pili jumla ikiwa ni wanafunzi ishirini. Katika kidato cha tatu na nne, kulikuwepo na vijidato vinne na wanafunzi wawili wawili waliteuliwa kutoka kwa kila kijidato. Wanafunzi 36 kutoka shule A na wanafunzi 36 kutoka shule B walishirikishwa. Katika shule C (ambayo ni ya mseto) kila kidato kilikuwa na vijidato viwili na wanafunzi wanne wanne (wasichana 2 na wavulana 2) waliteuliwa kushiriki jumla ikiwa ni wanafunzi 32 (taz jedwali 1 uk 25).

<table>
<tr><td>Aina ya Shule</td><td colspan="2"></td><td>Kdt 1</td><td>Kdt 2</td><td>Kdt 3</td><td>Kdt 4</td><td>JUMLA</td></tr>
<tr><td>Wavulana pekee</td><td colspan="2">Bweni</td><td>10</td><td>10</td><td>8</td><td>8</td><td>36</td></tr>
<tr><td>Wasichana pekee</td><td colspan="2">Bweni</td><td>10</td><td>10</td><td>8</td><td>8</td><td>36</td></tr>
<tr><td rowspan="2">Mseto</td><td rowspan="2">Mchana</td><td>MV</td><td>4</td><td>4</td><td>4</td><td>4</td><td>16</td></tr>
<tr><td>MS</td><td>4</td><td>4</td><td>4</td><td>4</td><td>16</td></tr>
<tr><td colspan="3">JUMLA</td><td>28</td><td>28</td><td>24</td><td>24</td><td>104</td></tr>
</table>

Jedwali 1:Uteuzi wa Washiriki katika Vikundi Viini

Kwa mujibu wa vikundi viini mwafaka hufaa kuwa na idadi washiriki kati ya 8-10. Katika utafiti huu kulikuwepo na vikundi viini kumi na viwili kwa jumla. Katika kila shule kuliandaliwa vikundi viini vinne vilivyowahusisha wanafunzi kati ya nane na kumi. Kila darasa la kidato liliwakilishwa na wanafunzi wawili ili kuibuka na jumla kama ilivyo katika jedwali la kwanza

### 3.4 Njia za Utafiti na Ukusanyaji Deta

Utafiti ulichukua mfumo wa kimaelezo na ulikuwa wa nyanjani. Data ilikuwa ni matini kutokana na mazungumzo yaliyorekodiwa kutoka kwa vikao vya mijadala katika vikundi viini. Katika vikundi viini, mazungumzo yalitawaliwa na vimada vilivyohusiana na urejeleaji wa ujinsia kwa kulenga maswala kama vile sehemu za ujinsia, urejeleaji kiumbo na kimo cha wapenzi, kujihini, mimba zisizopangwa, ubikira, kushiriki ngono na kutoshiriki ngono awali. Katika utafiti huu kulikuwa na vikundi viini kumi na viwili. Katika kila shule kuliendelezwa vikundi viini vinne.

### 3.5 Data, Mfumo wa Uchanganuzi na Ufasiri wa Deta

Mazungumzo ya wazulufu kuhusu ujinsia ndiyo yaliyokuwa data ya utafiti huu. Mazungumzo yaliendelezwa katika vikundi viini. Katika utafiti huu, ujinsia wa wazulufu ulifasirika kama tukio la kiisimu linalowakilisha hisia na tabia zinazohusiana na mvuto wa kiujinsia, ashiki, kujamiana na matokeo kama inavyojitokeza katika mazungumzo ya wazulufu. Ili kuzua data, kulikuwepo vikundi viini kumi na viwili; vikundi viini vinne kwa kila shule iliyoshiriki. Makala chochezi (taz. Viambatisho C, D, E, F uk. 148-151) yaliyo na uhusiano na mada tafitiwa yalitumika kuchochea mazungumzo. Mazungumzo yaliibua maneno yanayolenga mada  za maumbo na sehemu mbali mbali, mapenzi, urembo na utanashati, ubikira na kujihini, matokeo na fungu za maneno yanaoashiria mapenzi.

Ili kuchanganua mazungumzo ya wazulufu kuhusu ujinsia, utafiti huu ulitumia mfumo wa utathmini-changanuzi kama ulivyoasisiwa na Sauston & Kyratizis (2007). Mfumo huu ni namna ya kuchanganua na kuelezea lugha tathmini na una misingi yake katika muundo msingi wa mfumo amilifu. Mfumo wa utathmini-changanuzi hubainisha namna ambavyo mahusiano ya kijamii husimbwa na kutekelezwa kupitia lugha. Kwa mujibu wa Martin na White (2005), utathmini-changanuzi ni amali za kisemantiki zinazotumika kuzungumzia na kupatanisha mihemuko, maamuzi na ukadiriaji pamoja na amali za kukuza na kujihusisha na taathmini hizo. Kulingana na Martin amali hizi za kisemantiki huwa na viwango chanya na hasi.

- Hisia: kiwango kinachoshirikisha malighafi ya kiisimu inayotumika kuunda na kueleza mihemuko na itikio la mtu binafsi.
- Hukumu/maamuzi: kiwango kinachoshirikisha malighafi ya kiisimu inayotumika kuunda na kueleza tathmini adilifu au za kijamii za tabia.
- Utathmini: kiwango kinachoshirikisha malighafi ya kiisimu inayotumika kuunda na kueleza sifa za kiujumi za mfanyiko asilia wa jambo au dhana fulani.

Katika utafiti huu, amali za kisemantiki ni maneno yaliyonukuliwa ambayo yamekodiwa katika kategoria kulingana na mada zinazojitokeza katika mazungumzo ya ujinsia. Mfumo huu ulifaa utafiti huu kwa ambavyo ni mkakati unaomwezesha mtafiti kuzua mahusiano baina ya usemi, fasiri na mazungumzo katika mahusiano ya kijamii. Kulingana na mfumo huu, kigezo cha muundo wa kimazungumzo kilitwaaliwa. Kigezo hiki huhusisha mtindo wa uteuzi wa wazungumzaji kama vile uteuzi wa maneno, tasfida, sitiari  na kadhalika.

Kulingana na Martin na White (2005), kategoria hizi hutambuliwa kisemantiki na huafikiwa kupitia sarufi-leksia katika matini. Katika utafiti huu, mfumo huu ulifaidi uchanganuzi wa deta kwa ambavyo kategoria hizi zinahusiana na kusababishana. Aidha zinaelekeza katika uwepo wa peo za kimazungumzo na basi kuafikiana na ile nadharia ya uchanganuzi wa peo. Zaidi ya hayo, maamuzi humwezesha mzungumzaji au mwandishi kutathmini tabia ya mhusika kama inayokubaliana au kutokubaliana na kaida fulani za kijamii. Viashiria vya maamuzi hutoa habari za jinsi ujinsia wa mhusika hutazamwa, kufasirika na kuwasilishwa katika muktadha wa kijamii. Uchanganuzi ni wa kimaelezo na ulihusu mfumo wa kusoma na kupitia matini zote kwa makini kutambulisha na kunakili maneno na maelezo yote ya kiisimu yanayoeleza/kufafanua ulimwengu wa ujinsia wa wahusika. Matumizi ya lugha na maneno maalum ambayo yanaelekea kuonyesha peo za kimazungumzo na vile vile mikakati ya uzungumzaji yalilengwa. Mfumo wa uchanganuzi ni kama ilivyo katika kielelezo .

***Kilelezo 2: Muundo wa Uchanganuzi Deta***



### 3.6 Maadili katika Utafiti

Kanuni za kimaadili katika tafiti zinazowahusisha wanadamu kama wasailiwa zinafafanuliwa katika Declaration of Helsinki mwaka wa 1964 kama ilivyoratibiwa na World Medical Association WMA (2013), pamoja na Shaw, Brady, na Davey (2011), Schenk na Williamson (2005). Kuambatana na mapendekezo ya kazi hizo na ili kuhakikisha kuwa maadili yametimizwa katika utafiti huu, idhini ya utafiti ilitafutwa kutoka kwa Tume ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi (National Commission For Science, Technology and Innovation). Baada ya kupata idhini hii na kabla ya utafiti wenyewe, watafitiwa waliulizwa kujaza fomu ya idhini yao ya hiari ya kutaka kushiriki katika utafiti. Katika fomu hiyo, walikuwa wamepewa uhuru wa kutaka kushiriki, kujiondoa wakati wowote bila shuruti. Shule zilizohusika zilipewa kupitia kwa mwalimu mkuu na Idara ya Unasihi maelezo na ufafanuzi wa kimaandishi kuhusu malengo na mipaka ya utafiti. Maswala ya faragha yalifafanuliwa kimaandishi, kuzingatiwa na kudumishwa. Ili kutimiza hili, wasailiwa na washiriki katika vikundi viini pamoja na shule shiriki hazitatambulishwi kwa majina halisi, hali au maelezo yanayoweza kuwa vitambulisho kwa vyovyote vile. Shule zilipewa kodi ya siri kuzitambulisha. Washiriki wote walipewa kodi za kitafiti ambazo hazitakuwa na uhusiano wa moja kwa moja na shule au swala tafitiwa.

### 3.7 Hitimisho

Kwa kufuata kielezo cha mfumo wa uchanganuzi deta (kielelezo 2 uk 27) utafiti huu ulitathmini uumbaji wa ujinsia miongoni mwa wazulufu walio katika shule za upili nchini Kenya. Kuafikia hili, utafiti kupitia wazulufu 104 walioteuliwa kushiriki ulilenga: kutathmini maneno wanayoyatumia wazulufu kuwasilisha ujinsia ili kubaini yanavyogawika kiuamilifu, kutambulisha na kufafanua peo za kimazungumzo pamwe na kutambulisha mikakati ya kimazungumzo kuhusu ujinsia.

# SURA YA NNE

# KATEGORIA ZA LEKSIA ZA UUMBAJI WA UJINSIA MIONGONI MWA WAZULUFU

## 4.1 Utangulizi

Utafiti huu ulitathmini uumbaji wa ujinsia miongoni mwa wazulufu walio katika shule za upili nchini Kenya. Kuafikia hili, utafiti ulilenga: kuweka wazi maneno wanayoyatumia wazulufu katika mazungumzo yao kuhusu ujinsia, kutambulisha na kuchanganua peo za kimazungumzo na kutambulisha mikakati mbali mbali ya kimazungumzo kuhusu ujinsia. Sura hii imejikita katika uchanganuzi kiuamilifu wa leksia zilizoibuka katika mazungumzo ya wazulufu kuhusu ujinsia.

## 4.2 Uwasilishaji na Ufasiri wa Leksia

Kama alivyodai Rice (2001), wazulufu hutumia muda wao kuzungumza kuhusu dhana mbali mbali zinazohusiana na ujinsia na kubadilishana mawazo. Maneno yaliyoibuka katika utafiti huu yamegawika katika kategoria nne kuu kulingana na mada zilizojidhihirisha katika mazungumzo ya wazulufu kuhusu ujinsia kama inavyobainika katika jedwali lifuatalo:

| **Kategoria** | **Jinsia** | **Idadi** | **Jumla ( ∑ )** | **Asilimia (%)** | **Mifano** |
|---|---|---|---|---|---|
| Maumbile | MV | 26 | 86 | 23.12 | Fig 1, Pistol |
| | MS | 60 | | | Yana, Soft Pillow |
| Mpenzi | MV | 25 | 69 | 18.55 | Sponsor, hot stuff |
| | MS | 44 | | | Kipusa, ploti, flower |
| Ubikira na Matokeo | MV | 103 | 217 | 58.33 | Mtoto,mshamba |
| | MS | 114 | | | Poko, mtaro, taka taka Kuingizwa, tendewa wema, kutafunwa |
| **JUMLA** | | | **372** | **100 %** | |

Jedwali 2:Kategoria za Maneno Kiuamilifu

Kwa mujibu wa jedwali la pili, asilimia 58.33 ya maneno katika urejeleaji wa ujinsia miongoni mwa wazulufu huegemea swala la ubikira na matokeo. Swala la ubikira ni swala la kati katika utafiti huu kwa ambavyo huathiri na kuamua mahusiano baina ya wazulufu kuhusu ujinsia. Katika kipindi cha uzulufu, imedaiwa ndio wakati wazulufu wanatafuta utambulisho wao kuhusu ujinsia na pia ndipo wanapozua na kufanya majaribio ya tabia za kiujinisa. Katika sehemu ifuatayo kategoria hizi zinajadiliwa kwa kina.

### 4.2.1 Maneno yanaorejelea Ubikira

Maneno katika kategoria hii yamegawika katika kategoria tano kuu oanifu. Kategoria hizi zinazuana, kusababishana na kujengana. Maneno katika kategoria ibuka si maneno tu. Yana uwili wa kirejelezi. Yaani leksia moja inabeba sifa chanya na sifa hasi kwa wakati mmoja. Kategoria hizo ni pamoja na usafi, udhalilishaji, udokezi, weledi na ukarimu kama inavyobainika katika jedwali lifuatalo.

| **Kategoria** | | **Usafi** | **Udhalalishaji** | **Udokezi** | **Weledi** | **Ukarimu** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kuwa Bikira | MV | Priest | Mshamba, Fala, Outdated, Hustler, Mlalia masikio | Kuogopa sweet life, | - | Boy Mstinji |
| | MS | Nun | Hawes-Make, Mama Pima, Desparate | Fear of having fun, | - | Mchoyo, mkazia |
| Kutokuwa Bikira | MV | - | Poko, Fisi, Vulture Ako juu/ Sawa, Mtaka yote, Mtu kusema | Boy aliyeonja utamu | Player, Expert, striker | Cake eater, Mtenda wema, NYS, Mwanuaji |
| | MS | - | Coco, Whore, Door Mat, Used, Fala, Mpanuaji, Tasteless, Mama Huruma | Aliyefunguliwa Bonnet | Player | M-Pesa, ATM, Cake Supplier, Bamba, Bonga Point, soko huru |

Jedwali 3:Kategoria za Maneno yanayorejelea Kuwa na Kutokuwa Bikira

### 4.2.2 Uwili wa Kuwa na Kutokuwa Bikira

Kulingana na matokeo kama ilivyo katika jedwali, hali ya mzulufu kuwa bikira au kutokuwa bikira kimsingi huashiria ushiriki wa tendo la kujamiana. Kuwa bikira na kutokuwa bikira kwa mujibu wa kategoria ibuka kunafasirika kwa namna chanya na namna hasi hivi kwamba maneno husika yana uwili wa kisifa. Uwili huu wa kirejelezi ni utambuzi unaokubaliana na utafiti wa Jackson na Cram (2003). Kwa wazulufu wa kiume na kike, kuwa bikira kunahusishwa na usafi katika ile kategoria ya usafi tofauti na ilivyo kwa mzulufu ambaye si bikira. Hata hivyo, kwa misingi ya kategoria hizo nyingine, kuwa bikira kumerejelewa kwa maneno yaliyo na sifa hasi kwa jinsia zote mbili. Kutokuwa bikira kwa wazulufu wavulana kuna uwili wa kirejelezi kwani kuna maneno hasi

ingawa machache na maneno chanya. Wazulufu wasichana wanarejelewa kwa maneno hasi pekee. Uwili na ukinzani huu katika swala kuu la ubikira, kunaweka wazi ukweli wa kijamii kuwa kwa mvulana kutokuwa bikira ni sifa inayotambuliwa kichanya ilhali kwa mzulufu msichana ni sifa na tabia inayoashiria ukosefu wa maadili. Uwili na ikinzani huu unafafanuliwa kwa kina.

Kuwa bikira kumerejelewa kama usafi wa kutokuwa na doa. Ugunduzi huu unaambatana na ugunduzi wa Kelly (2007) aliyetambulisha peo tatu zinazotumika na wazulufu kuzungumzia swala la kuvunja ubikira. Kwa kurejelea upeo wa kujihini upeo huo huambatanishwa na maswala ya maadili na dini (Kelly, 2007). Mintarafu ya utafiti huu, hiki ni chanzo cha uwepo wa leksia zinazotumika kuwarejelea wazulufu mabikira. Kwa wazulufu, wasichana kwa wavulana, kuwa bikira ni kutokuwa na doa. Ni kuwa safi na kunaambatanishwa na utakatifu. Hii ndiyo taswira inayokuzwa na maneno kama vile *holy jo*, *holy boy*, *monk*, *mtoto* na kadhalika. Maneno haya kwa pamoja yanatosheleza ule mgao wa namna hasi na namna chanya.

Katika ule mgao wa uchanya, dhana na sifa za uzuri wa kiumbo, ukosefu wa doa na kutochafuliwa zinajitokeza katika urejeleaji wa ubikira sifa inayokolezwa na leksia ya mtoto. Dhana hii ya ubikira kama ukosefu wa doa, inashadidiwa na kukuzwa na kuwepo maneno ya kidini na nyadhifa za kidini kama vile *Mtakatifu*, *Bishop*, *Pastor*, *Father*, *Mary Mother of Jesus* pamoja na *Mama Kanisa*. Basi mzulufu bikira kurejelewa hivi ni ishara ya usafi wake. Kwa namna yake, dhana ya usafi na utumizi wa maneno yanayoambatana na nyadhifa za kidini huzua ushawishi na mamlaka. Usafi ni sifa chanya na kila mtu angependa kuhusishwa na mtu safi. Dhana ya usafi ina nafasi muhimu katika uvutiaji wa mtu na hukuza usharifu wa muhusika. Umuhimu wa leksia hizi ni kukuza na kuhimiza upeo wa kujihini kwa ambavyo jamii itamtambua mhusika kwa majina ya heshima. Leksia hizo zinakuza uadilifu ambapo iligunduliwa kuwa katika vikundi viini, wazulufu wanakuza hali hii kwa kutumia mkakati wa urejelezi wa mamlaka. Mbali na hayo, maneno hayo yanazua hali ya kukubalika kwa mhusika miongoni mwa wanajamii. Aidha kuna hali ya ukarimu inayoambatana na majina hayo. Ukarimu ni sifa chanya kwa mja katika jamii na kila mtu anashawishiwa kuwa mkarimu.

Hata hivyo kuna uhasi katika urejeleaji wa ubikira kwa misingi ya maneno yayo hayo. Hali hii ni bayana kwa kuzingatia sifa za baadhi ya maneno kama vile mtoto ambapo dhana ya mtoto hutumika kudunisha katika jamii nyingi za Kiafrika. Mtu akilinganishwa na mtoto katika vitendo

na maamuzi yake huwa amedhalalishwa. Huu ni ukinzani uliopo katika uelewa wa ubikira miongoni mwa wazulufu. Ukinzani huu unakuza utata unaozungukia ubikira ambapo hata kuwa bikira hakumhakikishii mzulufu amani na utulivu. Ukinzani huu unakuzwa na  uwepo wa dhana ya ukarimu na uchoyo.

Ukarimu na uchoyo ni pande mbili za sarafu moja. Katika muktadha wa uumbaji wa ujinsia wa ujinsia miongoni mwa wazulufu ukinzani wa sifa za ukarimu na uchoyo ni bayana . Mintarafu hii, ujinsia wa wazulufu kwa kuegemezwa kwa ubikira unakata kuwili. Kuwa mkarimu ni swala la maadili na hali inayoheshimika katika jamii nyingi. Basi katika ukuaji na uumbaji wa ujinsia miongoni mwa wazulufu huenda wakatatizika iwapo sharti wawe wakarimu na kuvunja ubikira wao ili wasiambatanishwe na unyimivu hali ambayo haionewi fahari. La muhimu katika taswira hii ni jinsi neno chanya linavyoweza kufasirika vitofauti. Hali hii inawasababishia wazulufu utata na mtanziko wa kiakili na kuwaacha katika njia panda. Hususan binti hajui awe mkarimu na akiwa mkarimu atakuwa mkarimu kwa kiasi kipi ikizingatiwa kuwa akiwa mkarimu atarejelewa kihasi na akiwa mnyimivu pia atarejelewa kihasi. Ni jambo bora na la utu kuwa mkarimu na hivyo basi mhusika ana sifa chanya za kutokuwa mchoyo. Hata hivyo mzulufu msichana akiwa mkarimu na kuvunja ubikira wake hata kama ni kwa mpenzi mmoja huenda akaonekana kihasi kwa ambavyo atakuwa amepoteza thamani yake. Ukweli huu unashadidwa na uwepo wa maneno hasi yanayomrejelea mzulufu msichana aliye bikira. Ukarimu inaelekea ni hali inayosababisha ukinzano wa kimatarajio na huenda wazulufu wakatumia hali hii kugandamizana wenyewe kwa wenyewe na au kuhalalisha matendo yao yanayohusiana na ujinsia.

Mbali na hayo, wazulufu wanafasiri ubikira kama uchoyo. Dhana hii inakuzwa na uwepo wa maneno kama vile *kuomba*, *kupewa* na *kupeana* kuashiria tendo la kujamiana. Katika fasiri hii, mvulana bikira anaitwa *boi mstinji* (stinginess) ilhali msichana anaitwa moja kwa moja *mchoyo* na kwa lugha ya mtaa *mkazia*. Uchoyo si sifa chanya na basi ili kuepuka kubandikwa hivi, wanavunja ubikira wao. Maneno hayo yanaongeza unyanyapaa unaoambatana na kuwa bikira. Unyanyapaa huu unajenga na kuimarisha udharura wa kvunja ubikira. Ikizingatiwa kuwa utumizi wa maneno katika kategoria hii unaegemea sifa hasi na chanya. Ni muhimu kutambua jinsi maneno ya kawaida yanavyotumiwa ili kukawaidisha vitendo vya wazulufu na kuweza kujitambulisha kama wadhulumiwa. Mtu aombapo jambo au kitu, iwapo anayeombwa anacho hana sababu za kumnyima mwenzake. Basi kwa vyovyote vile pasi kuzingatia ni nani anamuomba nani, wahusika

hawana budi kuonyesha ukarimu wao. Hapa ndipo mzulufu anajipata katika njia panda asijue ama anataka kujitambulisha na kundi la wachoyo au la wakarimu ikizingatiwa kuwa kutegemea uwanachama katika kundi, maneno haya yaweza kueleweka kichanya au kihasi. Utata huu huenda unawasababishia wazulufu kufanya maamuzi ya papo hapo pasi kutafakari matokeo ya matendo kama hayo na hivyo kusababisha athari za ngono za mapema.

Hata kama kuwa bikira kumepewa sifa ya usafi, kama inavyobainika katika maneno ya kategoria hii, kuna maneno yanayoashiria uhasi wa kuwa bikira kwa namna bayana. Mintarafu hii, maneno hayo yanatumika kukejeli hali ya mja kuwa bikira. Hii ni hali inayokuzwa na maneno ambayo yapo kwenye kategoria ya udhalalishaji, udokezi na ukarimu. Aidha ilibainika kuwa hata maneno chanya kutegemea utambulisho na uwanachama na mieleeko ya mzulufu yaweza kuwa na sifa hasi. Hii ndiyo hali inayozua ukinzani katika uelewekaji wa ujinsia miongoni mwa wazulufu. Ukinzani huu ni sababu moja ya wazulufu kuwa katika mahusiano ya mapema. Kulingana na maneno yanayotumika, inabainika kuwa wazulufu wengine hata hawaamini kuwa katika kizazi cha sasa yeyote aweza kuwa bikira. Wanadai kuwa ni unafiki na ndiposa maneno yenye sifa chanya yanatumika kihasi.

Wavulana bikira hurejelewa kama: *Mshamba, Outdated, Fala, Hustler, Mlalia masikio* ilhali wasichana hurejelewa kama: *Hawes-Make, Mama Pima, Desparate*. Majina haya kwa mapana ni uhalisi wa sura ya pili ya ubikira kama usafi. Huu ni urejelezi hasi na hauna lolote la kuvutia au kupendeza. Katika umri huu wa wazulufu, ni wakati ambapo wanataka sana kujitambua na kuwa na utambulisho wao. Utambulisho chanya. Wanatafuta uwanachama na kukubalika katika kundi la wenzao. Utambulisho wa wazuluufu haupo katika ulimwengu wa kuwa *mshamba*, *outdated*, *fala*, *mlalia masikio*, *desparate* na *hawes-make*. Utambulisho wao upo katika kuwa *Player, Expert*, *striker* na kadhalika maneno ambayo yanajitokeza katika kuupoteza ubikira.

Utambuzi huo unakuza upeo wa pili wa Kelly (2007) - upeo wa udharura ambapo mzulufu angependa kupoteza ubikira wake haraka iwezekanavyo ili kuepukana na unyanyapaa unaosababishwa na kuwa bikira. Kwa mtazamo huu mkakati wa kimazungumzo wa “Sisi na Wao” kama ulivyobainishwa na van Djik (2005) unabainika. Bayana ni kuwa walio bikira watakuwa na kundi lao ilhali waliovunja ubikira watakuwa na kundi lao na kutumia maneno ya aina fulani kuwarejelea wasio wanachama wa kundi husika. Inabainika kuwa urejelezi wa aina hii unausawiri

ubikira kama swala lisiloonewa fahari na linalozua aibu miongoni mwa wazulufu. Aidha ni swala la kizazi cha zamani na ndiposa kuna matumizi ya neno kama *outdated*.

Neno *outdated* linazua mkabala wa dhana ya wakati ambayo ni muhimu katika kuelewa ulimwengu wa wazulufu. Wazulufu ni kundi la wanajamii wanaodaiwa kuishi kwa wakati uliopo na dira ya maisha yao inatawaliwa zaidi na dhana za sasa au wakati uliopo. Kuna uhalisia wa ukongwe na usasa miongoni mwa wazulufu. Ukweli huu unaungwa mkono na uwepo wa leksia kama vile *on-point*, *in-thing* n.k zinazoashiria kuwa mrejelewa, unakwenda na majira yaliyopo. Hali hii inakolezwa na utumizi wa mkakati wa takwimu ambapo wazulufu wanadai kuwa kwa kuwa kila mwanachama anashiriki tabia fulani, hiyo ndiyo fashoni iliyopo na bila shaka " *its the in-thing*" kwao. Uhalisia huu unakinzana na kusababisha mgawanyiko miongoni mwa wazulufu.

Sifa na utumizi wa neno *hustler*, *hawes-make* na *desparate* ni utambulisho wa mtu hohehahe asiye na la mno maishani. Ni udhalilishaji. Kwa misingi ya sifa za maneno haya wazulufu wanachukulia kuwa kuwa bikira ni kuwa hohehahe. Mhusika ambaye hakufanya au hajafanya lolote la muhimu maishani. Hana lolote la kuweka wazi kwa wahusika. Aidha ni maneno ya kimsimu ambayo yamezuka kimatumizi miaka michache iliyopita na mwanzo yalitumika na naibu wa rais nchini Kenya. Licha ya kwamba ni maneno yaliyotumika na mhusika mashuhuri, ni maneno yaliyo na sifa ya usasa kimatumizi, wazulufu hawataki utambulisho kama huu. Sababu ni kwamba ni maneno yanayoibua sifa hasi. Ili kukuza utambulisho wao, wazulufu wanawarejelea wenzao mabikira kwa namna hasi. Hisia na urejelezi kama huu unakoleza uhitaji wa kuvunja ubikira ili kukubalika katika kundi la wazulufu. Hata hivyo ni dhana inayobainisha athari ya watu mashuhuri na matumizi yao ya lugha miongoni mwa wazulufu. Huu ni ugunduzi ulio muhimu hususan ikizingatiwa vibadiliki vya kijamii vinavyoathiri matumizi ya lugha huku ikitambuliwa kuwa lugha hupokezanwa kitamaduni.

Namna nyingine ya kuelewa ubikira miongoni mwa wazulufu ni uwepo dhana za uoga na utamu wa maisha zinazodokezwa na utumizi wa fungu la maneno "*Boy anayeogopa sweet life*". Fungu hili la maneno linaweka wazi uwili katika uelewa wa wazulufu kuhusu ujinsia kwa misingi ya kuwa na kutokuwa bikira. Kwanza kuna dhana ya kuogopa na pili ni dhana ya "*sweet life*". Utumizi wa fungu hili la maneno linakuza uhitaji wa wazulufu kuvunja ubikira wao kwa misingi ya dhana hizo mbili. Huu ni wakati wa kujitambua ambapo hamna mzulufu anayetaka kusawiriwa kama

mwoga. Wanataka kutambulikana kama majabali wasioogopa. Mtazamo huu unakuzwa na ugunduzi wa wataalamu waliotambulisha kuwa kizazi hiki ni kizazi kisichozingatia hatari au kinachojiingiza katika maswala ambayo yanafasirika kuwa hatari ili kuonyesha ushupavu wao (Reyna na Farley, 2006; Galvan, Hare, Voss, Glover, na Casey, 2007). Aidha inakuzwa na itikadi iliyopo miongoni mwa wazulufu ya kutojali.

Kwa misingi ya dhana ya "*sweet life*", inabainika kuwa wazulufu husawiri tendo la ngono kama utamu- utamu wa maisha/maisha matamu. Katika hali za kawaida vitamu vinashawishi. Wazulufu wanafasiri bikira kama mtu anayeogopa utamu wa maisha. Kwa misingi hii, wazulufu wanachukulia kuwa kuvunja ubikira ni kushiriki utamu wa maisha. Kwa kuambatanisha na dhana nzima ya maisha, ni mkakati bayana wa wazulufu wa kushadidia nafasi ya utamu katika maisha yao. Wanakuza umuhimu wa kutoogopa kushiriki utamu unaorejelewa. Fungu hili la maneno linakuza unyanyapaa miongoni mwa wazulufu mabikira. Kusawiriwa kama mja anayeogopa maisha matamu ni pigo kwa usharifu wa mhusika.

Usharifu una uhusiano wa karibu na maendeleo ya mtu (Steinberg, 2013). Usharifu waweza kuwa na athari kwa mahusiano baina ya wazulufu hali ambayo wazulufu wanaitambua katika uwasilishaji wa ujinsia miongoni mwao. Ambapo mzulufu anahisi vibaya kujihusu, ndivyo atakavyowatendea wengine mabaya na kuwaona kwa mtazamo hasi (Steinberg, 2013; Litwack, Aikins na Cillessen, 2012). Ni bayana basi kuwa jinsi mzulufu anavyojiona huathiri matendo na tabia yake. Huathiri jinsi anavyofikiri na kufanya maamuzi, mihemuko na hisia zake, ashiki, maadili na malengo yake maishani. Usharifu chanya humwezesha mzulufu kufikiri na akumbwapo na usharifu hasi, daima anaishi na shauku ya ufaafu wake. Kutokana na hilo, mzulufu atakuwa amenaswa na mtego ya shauku yake na hiyo kujihisi kama mtu asiyefaa na asiyejimudu. Utambuzi huu, unaweka wazi basi kwa nini wazulufu wengi wanapendelea kuonja utamu wa maisha.

Awamu ya pili ilikuwa ni kutathmini maneno yanayotumika kumrejelea mzulufu asiye bikira. Swala kuu lililojitokeza ni kuwa kuna mitazamo miwili mikuu. Kwanza kuna maneno yanayokuza mtazamo chanya hivi kwamba, mzulufu aliyevunja ubikira anarejelewa kwa sifa chanya. Pili kuna maneno yanayokuza mtazamo hasi. Mitazamo hii inakinzana yenyewe ikizingatiwa kuwa bikira pia hurejelewa kwa namna hasi. Ukinzani huu unawiana na utafiti wa Marks & Fraley (2006) kuhusu uwili wa urejelezi wa ujinsia. Utambuzi muhimu katika utathmini wa maneno haya ni jinsi

maneno hayo yanavyokuza mkakati wa kimazungumzo wa “sisi” na “wao” na hapo kuweka wazi umuhimu na nafasi ya utambulisho wa kila kundi katika maingiliano ya mwanadamu. Aidha uwili wa uwasilishi wa ujinsia kwa msingi wa ubikira unajitokeza bayana.

Mintarafu ya utafiti huu, wazulufu wana maneno yanayoashiria dhana ya kutokuwa bikira kuwili. Wavulana wazulufu wasio bikira hurejelewa kwa maneno kama vile: *Ako juu, ako sawa, mtu kusema*, *mwalimu* n.k. Aidha kuna maneno hasi kama vile: *Poko*, *fisi*, *mtaka yote* n.k. Ilitambuliwa kuwa wasichana hurejelewa kwa namna hasi pekee na ndiposa kuna maneno kama vile: *coco*, *whore*, *Door mat*, *used*, *tasteless* n.k. Utambuzi huu unaelekeza kwa uhalisi wa kijamii kuwa kwa mvulana kupoteza ubikira ni swala ambalo kwa kiwango fulani linakubalika katika jamii. Ni hali inayompa mvulana fahari ya aina yake katika jamii na miongoni mwa wenzake. Ukweli huu, unaweka wazi dhana mbili muhimu katika utafiti huu, uwili wa ujinsia na uwepo wa dhana ya ufedheheshaji wa mwanamke mkoo.

Wazulufu wavulana wanapowarejelea waliovunja ubikira kwa vifungu vya maneno kama *kuwa juu*, *kuwa sawa* na *mwalimu* ni urejelezi chanya na ambao kwa namna yake unahalalisha na kukuza mtazamo wa kizazi cha wazulufu kuwa mvulana bikira ni *mshamba* (sifa hasi). Mvulana aliyevunja ubikira amepewa sifa na hadhi ya kuweza kuwa mjuzi na mwenye maarifa (dhana ya ualimu/ukufunzi). Hii ni sifa inayoenziwa katika jamii. Amekwezwa katika jamii. Zaidi na maelezo hayo, ikizingatia walipo wazulufu na ngazi yao ya maisha, kimsingi ni wanafunzi katika shule mbali mbali. Inabainika basi kuwa huu ni utambulisho wa muktadha wa wazulufu- wenyewe ni wanafunzi walio shuleni ambapo wanasaka elimu na maarifa. Elimu hii na maarifa yanapatikana kupitia kwa mwalimu. Mwalimu ni dira ya wanafunzi wake na anaaminika sana. Ana mamlaka juu ya wanafunzi wake. Katika muktadha wa utafiti huu dhana ya ualimu inazua hali ya ujuzi fulani na uongozi na ndiposa hali hii inapata mashiko kupitia mafungu ya maneno kama vile *mtu kusema*. Ufasiri na uelewa wa wazulufu ni kuwa wavulana waweza kuvunja ubikira wao na kuwa walimu wa kuwafundisha wenzao na ndiposa tendo la kujamiana linatukia kwa wingi.

**Dondoo 1: FGD 4 shule C**

> MV001C: First of all mimi nikuwe na **background experience** na yeye asikuwe nayo ndio mimi tukiingia sex ni kama game kuna mwenye anachezeshaga mwingine **anamfundusha kunaendaga hivi na hivi** so..... **(Tzm Kiambatisho H UK 162)**

Kwa upande wa pili kuwa bikira ni hali iliyopitwa na wakati (*outdated*) na yeyote aliye katika hali hiyo ni *fala*. Huu ni mtazamo hasi kwa wavulana walio mabikira. Kwa dhana za kuwa amepitwa na wakati na hana ujuzi wowote basi hawezi kuwa mwalimu. Hii ni sababu tosha ya wengi kutaka kuupoteza ubikira wao ili kuweza kukubalika na kutambulika kwa wenzao. Utambuzi huu unakubaliana na utafiti wa wataalamu wengine kama vile Reid, Elliott na Webber (2011), Masters, Casey, Wells, na Morrison (2013); O'Sullivan, Brotto, Byers, Majerovich, na Wuest (2014). Ni dhahiri kuwa wavulana wangependa kuupoteza ubikira wao haraka iwezekanavyo ili kuweza kupata utambulisho chanya. Hii ni hali inayokuza upeo wa udharura. La mno katika ugunduzi huu ni kule kukoleza uwili wa mtazamo wa ubikira katika jamii na jinsi hali hii inatumika kuwagandamiza wazulufu wasichana na jinsia ya kike kwa jumla. Udharura wenyewe si ubaguzi lakini wanajamii wanautumia kuwabagua na kuwaweka watu katika makundu mintarafu ya jinsia yao. Wavulana wakitimiza wito wa upeo huu wa udharura, wanakuwa *wajuzi* ilhali wasichana wakiitikia wito wa upeo huo wanakuwa *mapoko*, *mitaro* na *tasteless*.

Kuliibuka maneno hasi ingawa machache yanayomrejelea mvulana aliyepoteza ubikira wake. Ni maneno ya kudhalilisha. Kuna utumizi wa sitiari ya wanyama wawili- *fisi* na *vulture*. Hawa ni wanyama walafi na hula nyama na mizoga. Maneno haya yanaungwa mkono na uwepo wa maneno kama vile *mtaka yote*. Ni muhimu kugundua taswira pana inayotokana na maneno haya. Kwanza kwa mzulufu kurejelewa kama *mtaka yote*, ni ishara ya kutojali na ulafi. Kutokana na kutojali huku pamoja na ulafi, yawezekana kwa kiwango kikubwa kukawa na matokeo hasi (maradhi au hata ujauzito, uavyaji wa mimba, kuacha masomo au hata kifo) ambayo yanazua fedheha na fadhaa. Sifa ya kutojali na ulafi ni sifa zinazoambatana na *fisi* na *vulture*. Kimsingi fisi ni myama ambaye kimaumbile hapendezi na havutii.

Kwa misingi ya wazulufu wanaoshikilia maadili, wenzao wazulufu waliovunja ubikira hawavutii, hawana lolote la kupendeza. Maneno haya yanaelezeka tu kwa misingi ya maadili katika jamii ambapo hata kama kizazi cha sasa cha wazulufu kinasutwa, kungali baadhi yao ambao wameshikilia maadili kwa misingi ya mafunzo ya kidini. Wanaambatanisha maelezo yao na mafunzo ya kidini na ndiposa waliovunja ubikira wanatambuliwa kama kundi tofauti lililo na sifa hasi. Kutokana na maelezo haya, inabainika kuwa bikira kungali kunathaminiwa na baadhi ya wazulufu na hivyo basi haiwezi kudaiwa kikamilifu kuwa licha ya usasa, tamaduni na itikadi ya ubikira imeasiwa asilimia mia kwa mia.

Wasichana waliovunja ubikira hurejelewa kwa namna hasi pekee. Urejelezi huu unakuza ukweli kuwa, ubikira wa msichana unathaminiwa sana katika jamii. Kuuvunja ni kama kuwa mtovu wa maadili. Maelezo haya yanaambatana na harakati za baadhi ya wanaong'ang'ana kuudumisha. Maneno yote yanayotumika yanamdhalalisha binti aliyevunja ubikira wake. Kuna utumizi wa maneno kama vile "*tasteless*".

**<u>Dondoo 2: Tunukuzi kutoka Kikundi Kiini Shule C</u>**

> MS001C: Eeee. Hapana sasa saa hii si kwa marriage. Obvious nikisema maybe nilikuwa na chali tukaachana nikapata mwingine tukaachana nikapata tena mwingine na maybe tuseme nikalala na hao wote by the time nikuwe marriage si nitakuwa kitu ingine mbaya
>
> *Mtf: Kitu kibaya kipi?*
>
> MS001C: Kitu **tasteless** **(Tzm Kiambatisho H Uk 157)**

"Tasteless" ni neno la Kiingereza, ambalo kisawe chake katika lugha ya Kiswahili ni ukosefu wa ladha. Msichana ambaye amevunja ubikira wake anachukuliwa kama mtu asiye na ladha. Hili ni neno linalomdunisha msichana. Ikikumbukwa kuwa kuna kategoria ya ladha inayoambatana na utamu, basi kisichokuwa na ladha hakionewi fahari. Hakithaminiwi. Katika ulimwengu wa kawaida, kisicho na ladha hakitamaniwi na yeyote. Kama ilivyo katika dondoo hilo la pili, neno hilo limetumiwa na msichana. Hali hii inakoleza ukweli kuwa wasichana wametekwa nyara na itikadi ya jamii inayoendelezwa na wavulana kuwa, ikiwa atakuwa amekwisha kuwa mkarimu basi hatakuwa na ladha. Wenyewe hawajaweza kujitanzua kutokana na ubabe dume wa wavulana wenzao. Wapo tu kwa ajili ya matumizi ya wavulana hao. Hapa ndipo itikadi ya wasichana kuwa chombo inapoanza kupata mashiko.

Utumizi wa maneno kama hayo katika urejeleaji wa swala nzima la ubikira kwa wasichana wazulufu unashadidia na kuunga mkono uwepo wa maneno hasi yanayomrejelea binti asiye mrembo. Ni ishara kuwa itikadi ya kitamaduni kuhusu ubikira ingalipo. Aidha kwa binti kusawiriwa kama mtu asiye na ladha kwa sababu amepoteza ubikira wake pasi kuwa na kisawe sawa kwa mvulana ni thibitisho tosha la tofauti za kijinsia baina ya wavulana na wasichana. Hali hii inaungwa mkono na maneno mengine kama vile *soko huru* na *mama huruma*.

Soko huru ni kirai cha maneno kinachoweza kutazamwa kuwili ili kuelewa fasiri ya wazulufu kuhusu ujinsia. Kwanza kwa misingi ya mahali ambapo ununuzi unafanywa. Iwapo mahali hapo ni huru, basi yeyote anaweza kuingia na kufanya ununuzi wake. Fasiri ni kuwa, binti huyu hana maadili yanayomwongoza na basi mvulana yeyote aweza kumpata. Pili, utumizi wa neno hili unaweka wazi sababu za wazulufu kuwa na "*sponsors*". Kutokana na ujio wa usasa na kuasiwa kwa tamaduni za Kiafrika, baadhi ya wazulufu wanaiona miili yao kama soko yaani daraja ya kufikia na kupata wasivyo navyo. Wanaweza kupigia biashara ujinsia wao. Katika soko nyingi zijulikananzo hususan barani Afrika, kuna sifa ya uchafu. Kwa uelewa wa wazulufu, binti aliyevunja ubikira tayari ni mchafu hali inayoweza kuambatanishwa na ukosefu wa ladha. Kwa upande mwingine, bidhaa zikiwa sokoni na mnunuzi ana fedha, hana kizuizi cha kutonunua. Fasiri hii inaweka wazi sababu za kuwepo wazulufu wengi wanaoanzisha mahusiano na wanajamii waliokomaa bora wana fedha na wanaweza kuwagharimia. Kinachojitokeza hapa ni ubiashara wa ujinsia swala lililo dhahiri katika ulimwemgu wa sasa.

Pili uelewekaji wa neno soko huru unatokana na ukopaji kutoka kwa muktadha wa usafiri. Nchini Kenya kuna kampuni ya usafiri ya ushirika inayojulikana kama "Soko Huru". Fasiri ya kuvunja ubikira kwa misingi ya mtazamo wa usafiri inatokana na uhalisia wa kuwa mja ana hiari ya kuabiri gari lolote lile. Wazulufu wamo safarini ya kujitambua na kutafuta mahali pao katika jamii. Katika safari hii, banati ana uhuru wa kushiriki na kuvunja ubikira na anayependa. Dhana hii inashadidia haki na uhuru wa wazulufu kujiamulia wapendavyo. Mteja anapofika katika kituo cha kuabiri gari (kwa maana ya kukomaa kwa wazulufu), hujiamulia gari atakaloabiri. Hii ni sawa na haki ambayo wazulufu wamekuwa wakiitafuta kwa muda mrefu. Uhiari wa kujiamulia na kutenda wapendavyo hususan baada ya wao kujihisi kuwa wamekuwa wa umri wa kujiamulia.

Swala lingine linalojitokeza ni kuwa, abiria ana hiari ya kushuka apendapo na ambapo fedha zake zimemwezesha kufika. Hali hii inamtanzua mhusika awe mvulana au msichana na hawajibikii na hafungwi na sheria za uhusiano. Mahusiano yao yanaelekezwa na uhitaji wa papo papo. Ni kana kwamba ni mahusiano ya kimkataba. Basi "*Sponsor*" ufadhili wake ukiisha anaweza kushukishwa na banati akaabiri gari jingine. Banati naye kwa upande wake, anaweza kukomesha uhusiano wakati wowote ule. Hajafungwa kuwa na yule mvulana daima. Maelezo haya yanafunua

ulimwengu wa wazulufu kuhusu ujinsia ambapo fedha ni muhimu na pia kuna uhiari wa kuamua jinsi mtu apendavyo.

Ikizingatiwa maneno kama *doormat* na *used paper*, ni bayana kiwango cha kudhalilishwa kwa wasichana. *Doormat* ni mkeka unaowekwa mlangoni ili kila aingiaye nyumba hiyo ajipangusie uchafu miguuni. Kwa taswira hii, inafasirika kuwa msichana aliyevunja ubikira wake ametumiwa tu. Wavulana wamejipagusia uchafu wao na kwa sababu kifaa hiki si mahususi kwa mtumizi mmoja, inabainika kuwa binti aliyevunja ubikira wake ni kama kifaa kilichotumiwa na wengi. Labda ndio maana anachukuliwa kama aliyechafuka kama ilivyo kwa mikitadha ya uchafu unaopatikana sokoni. Inabainika hapa kuwa kuna dhana ya kutumiwa ambapo binti anachukuliwa kuwa kama kifaa na pia kutumiwa. Dhana ya kutumiwa hapa ni dhana hasi na haimkwezi msichana kwa vyovyote vile. Hajafaidi kwa lolote lile. *Doormat* haina mtu mahususi atakayeitumia. Ni mkeka ambao kazi au jukumu lake ni muhimu lakini halienziwi. Kwa msingi huu mzulufu banati anatumika kuondoa uchafu hivi kwamba mvulana anapoingia katika kasiri yake ni msafi (ana weledi). Ufasiri huu unapata mashiko kwa kuwepo maneno kama vile *kuingia kasirini* yanayorejelea tendo la kujamiana na ili mfalme aingie pale sharti awe amejipangusa uchafu.

Kupoteza ubikira pia kunafasirika kihasi kwa kuwepo taswira inayotokana na uwepo na utumizi wa *karatasi iliyotumiwa*/(*ka*). Wazulufu wanamfasiri binti aliyevunja ubikira wake kama mtu ambaye utenda kazi wake ushakamilika na hana lingine la kutoa. Amekuwa "*tasteless*", "*formless*". Karatasi ikitumika kitabuni au kama karatasi sashi, hutupwa tu. Haina matumizi mengine. Basi baada ya msichana kupeana tunda lake, anatemwa tu. Mvulana anapiga hatua ya kutafuta karatasi nyingine ambayo ina manufaa. Uwepo wa neno *formless* ambalo kwa Kiswahili linamaanisha kitu kisicho na umbo/ si maridadi, ni ithibati tosha kuwa mzulufu akivunja ubikira wake amepoteza umbo lake miongoni mwa wanajamii. Umbo hili laweza kuwa la kimaumbile, nafasi na hadhi yake na hivyo basi hapendezi na havutii. Kutokana na shinikizo za maisha, uwili wa kuufasiri ubikira na kutokuwa bikira miongoni mwa wazulufu ni sababu tosha za kufafanua tabia za mara kwa mara za kujamiana baina ya wazulufu. Itambuliwe kuwa mvulana hatazamwi kama aliyetumiwa, yeye amefaidi na amepata ujuzi. Amekuwa mwalimu na basi hadhi yake imepanda.

Kuhitimisha, uwasilishi wa ubikira miongoni mwa wazulufu unakata kuwili. Wazulufu bikira licha ya kurejelewa kwa kutumia leksia zinazobeba uzuri na uadilifu wa aina fulani, leksia hizo zinaambatana na sifa ya kukejeli. Yaelekea basi kuwa ubikira ni hali nzuri kwa mzulufu kuwa nayo ikizingatiwa uchanya wa maneno husika. Ni hali inayompa mzulufu msichana hadhi zaidi lakini inayomfadhaisha na kumtatanisha mzulufu mvulana. Kategoria za maneno zilizoibuka, zimeweka wazi kuwa ubikira kwa wasichana una thamani katika jamii, lakini kwa wazulufu wavulana si swala la kuonewa fahari. Leksia ibuka zinabainisha uhalisia wa kijamii kuwa ni bora zaidi, kwa ajili ya hadhi ya mwanamume kijamii, kutokuwa bikira. Utambuzi huu unakubaliana na uhalisia wa uwili wa ujinsia kama ilivyo katika tafiti awali za Bordini na Sperb (2013), Carpenter (2005), England na Bearak (2014), Crawford na Popp (2003). Utafiti wa sasa unashadidia hali hii kupitia dondoo zifuatazo kutoka kikundi kiini katika mojawapo wa shule:

**<u>Dondoo 3: Tunukuzi kutoka Kikundi Kiini Shule C</u>**

**MV001C:** majority ya maboy vile huwa nasikia wakiongea wanasemaga experience makes the perfect. So ndio **in future boy asilet bibi yake down** lazima alale na madem wengi ndio akuwe perfect. Huwezi amka tu na uende kwa field kwa game. Kwa sababu hata wewe ni mwanaume kamili. So lazima udanganye madem uwaingize box wakishaingia kwa box yako **ujifunze na wao vile game itakuwa** inachezwa ndio sometimes in future ukiingia kwa game **bibi yako atakuwa anashindwa na huyu alifunzwa na nani unaona**?

**<u>(Tzm Kiambatisho H Uk 157)</u>**

MV002C: **Me nataka virgin. Me kama sio virgin** na **yeye ni virgin** game itakuwa poa **<u>(Tzm Kiambatisho H Uk 162)</u>**

MV001C: First of all **mimi nikuwe na background experience** na **yeye asikuwe nayo** ndio mimi tukiingia sex ni kama game kuna mwenye anachezeshaga mwingine anamfundusha kunaendaga hivi na hivi so **me naweza taka dem virgin** lakini **mimi nisikuwe** ndio lazima nikuwe nishapitia kile ninafanya.

MS001C: Me naweza taka yeyote tu **<u>(Tzm Kiambatisho H Uk 160)</u>**
*(Kicheko)*

MS001C: Yeah juu wakiwa virgo wawili hawataenda mahali juu yes of course hawawezi enda mahali na bado pia nikiweza pewa huyo virgin siwezi kataa so hapo me naona tu mwenye atakuja. **<u>(Tzm Kiambatisho H Uk 162)</u>**

**<u>Dondoo 4: Tunukuzi kutoka Kikundi Kiini Shule B:</u>**

**MV012**: Tunasemaga **kifunguo inayofungua vifuli mingi ni master key** lakini **padlock inafunguliwa na vifunguo mingi ni mbovu.** Mwanaume **amechew** madem wengi ako na **experience yeye ni master key** anajua hizi vitu halafu sasa **dem ndio padlock** anaweza **funguliwa** na **key** yoyote huyo ni **china.** Siwezi

taka vitu zangu za box ziibiwe so siwezi chukua padlock mbovu. **(Tzm Kiambatisho I Uk. 175)**

Kwa mujibu wa dhana hii ya uwili wa ubikira, wazulufu wasichana hufedheheka kutokana na kujamiana na kuupoteza ubikira wao (wote by the time nikuwe marriage si nitakuwa kitu ingine mbaya.... Kitu **tasteless)** ilhali wazulufu wavulana wanaenziwa na kutuzwa. Mintarafu hii basi, ubikira ni swala la kijamii linalotumika kwa minajili ya ubidhaaishaji wa jinsia ya kike. Uwasilishi wa ujinsia miongoni mwa wazulufu kwa kuzingatia kategoria za maneno tumikizi, ubikira wa wavulana upo lakini hauna thamani na hauna matokeo sawa kama ilivyo kwa wazulufu wasichana. Inabainika kuwa ubikira una thamani kwa wazulufu wasichana na wakiupoteza isivyotarajiwa au isivyofaa, jamii inawabandika kama wakosefu wa maadili hali inayoeleza chanzo cha maneno hasi.

Jamii kupitia wazulufu inawaona kama *"used goods"* or *"desperate."* Wazulufu wavulana kwa upande wao hawana haja ya kujali kuhusu lawama la jamii au kufedheheka. Fedheha yao inatokana na kuwa bikira. Wao wanatambuliwa kama magwiji na wajuzi kwa kuupoteza ubikira wao. Uwasilishi huu umebainisha kuwa dhana ya ubikira imeumbwa ili kuhukumu wazulufu wasichana na jamii pana ya jinsia ya kike kwa misingi ya jinsi na wakati walipovunja ubikira wao. Imebainika kuwa kuupoteza ubikira kwa wazulufu wasichana kuna tokeo hasi la kijamii ambalo kwa misingi ya utafiti huu ni unaibua na kukoleza uwepo wa dhana ya ufedhehesahji wa hali ya mwanamke mkoo.

Ithibati ya dhana ya ufedhehesahji wa mwanamke mkoo katika uwasilishi wa ujinsia miongoni mwa wazulufu inakubaliana na tafiti nyingine kama vile tafiti za (Tolman 2005; Schalet 2011; Ridgeway 2011; Ringrose na Renold 2012; na Hess 2014). Dhana hii hurejelea tukio la kuadhibu au kuhukumu wengine hususan jinsia ya kike kwa misingi ya matendo ya ujinsia wao (Tolman, Hirschman, na Impett, 2006). Ni aina ya unyanyapaa wa kijamii unaotumiwa kwa watu, hususan kwa kizazi cha jinsia ya kike ambao waaonekana kukiuka matarajio ya kitamaduni ya tabia za kiujinsia. Yaani wazulufu wasichana na kwa ujumla jinsia ya kike hushambuliwa kwa mbinu mbali mbali ikiwemo ile ya maneno ya matusi kwa kukiuka matarajio. Linalojitokeza hapa ni udumishaji wa utawala wa jinsia ya kiume na unyanyasaji kwa ambavyo hata "kaida" hizo zinazokiukwa na jinsia ya kike zimewekwa kwa ajili ya manufaa ya jinsia ya kiume kama

inavyobainika katika dondoo hili wazulufu wakitoa maoni ya kupendelea kuoa au kuolewa na bikira:

**Dondoo 5: Tunukuzi kutoka Kikundi Kiini Shule B**

> **MV003:** Hata me ningependa virgo. Reason ni unajua tuseme saa hizi hata we saa hizi huwezi penda tuseme kitu kama big yenye msee **ametafunatafuna** unaona. Unajua saa unapenda ile yenye we ndio **unatafuna lakini** pia kama **imeumwa mara moja** pia si mbaya sana. **(Tzm Kiambatisho I Uk. 177)**

> **MV005:** Mimi ningependelea msichana ambaye ni bikira hata sisi sote hapa saa hizi tukikaa hapa hakuna mtu anapenda **kitu imezeeka**, yenye **imechakaa** hivi **kitu mpya hii yenye inafunguliwa kwa karatasi ndio me naprefer.** Kwa hivyo hii inategemea na mtu tena juu saa hizi **ukieza kuja na kitu mpya itaweza kukupea service kwa muda….** **(Tzm Kiambatisho I Uk. 173)**

Uwasilishi wa ubikira miongoni mwa wazulufu basi ni dhana tata kwa ambavyo ni ya ubaguzi wa kijinsia na hukoleza fikra hasi. Ubikira na thamani yake haiwapi wazulufu wasichana uhuru wa ujinsia, bali hukwaza na kuzuia tabia zao na maamuzi kwa kuyaegemeza kwa namna wanavyostahili kuendeleza ujinisia wao. Yaani hawafai. Ni kana kwamba ujinsia una uhusiano wa moja kwa moja na usafi hivi kwamba mzulufu msichana akipoteza ubikira yeye si safi.

Kwa wazulufu wavulana, kuna uhusiano chanya kati ya kuvunja ubikira na hadhi katika jamii. Wao wanatambuliwa na kuenziwa tofauti na wazulufu wasichana ambao wanadhalalishwa. Mvulana ni gwiji ilhali msichana ni "*mtaro* au *karatasi sashi*. Basi ubikira unahusiana sana na muktadha wa kijamii kama alivyodai (McKelle, 2013). Yaelekea kuwa ubikira ni swala la kijamii linalotumiwa kuwabagua wazulufu wasichana na jinsia ya kike kwa jumla kwa misingi ya ujinsia. Utumizi wa maneno husika na kategoria zake, umeweka wazi hali ambayo kwayo ujinsia unatumika kuwathibiti na kuwatishia wazulufu wasichana. Kama ilivyo katika utamaduni, imebainika kuwa hata wazulufu wavulana wanatumia dhana ya ubikira kugandamiza. Inawapa wavulana namna ya kuthibiti wasichana na kuwafanya waaibikie miili na ujinsia wao. Uaibishaji huu ni utambuzi unaokubaliana na ugunduzi wa Chomba (2005) akizungumzia usawiri wa mwanamke katika methali za Kikuyu ambapo wanawake wamesawiriwa kihasi wakilinganishwa na wanaume.

### 4.2.3 Maneno yanaorejelea Kujamiana

Maneno yanayoashiria kujamiana yanaweza kugawika katika kategoria tano muhimu. Wazulufu hufasiri hali ya kujamiana kama bahati au bahati nasibu, spoti, ukulima, ukarimu upishi na ulaji.

| Kategoria | Bahati | Spoti | Ukulima | Ukarimu | Upishi na Ulaji |
|---|---|---|---|---|---|
| Kujamiana | Ku-jackpot | Kuride bike | Kupanda mbegu, Kuhatch, Kuzulu shamba la Mfalme | Kupeana, Kutenda(wa) wema, Ku310 | Kula halua Kuliwa, kutafunwa |

Jedwali 4: Kategoria za Maneno ya Kujamiana

Kategoria za maneno ya kujamiana zinaambatana na uanishi na maelezo ya meneno tangulizi. Aidha zenyewe zinakuzana. Kwa mfano kutokana na ketegoria ya ukarimu, kategoria ya upishi na ulaji inakuzwa. Kategoria ya bahati/bahati nasibu inaunga mkono maneno yanayomfasiri mvulana kama "sponsor" na pia kukuza kategoria ya spoti. Kategoria hizi zinafafanuliwa kwa kina moja baada ya nyingine katika sehemu ifuatayo.

Katika utafiti huu kuliibuka maneno sita, yanayosawiri, tendo la kujamiana kama bahati au bahati nasibu. Dhana kuu katika utumizi wa leksia hizi ni dhana ya anayefaidi na kule kuchukua thamana. Maneno hayo aidha yanaibua dhana ya raha na furaha inayoambatanishwa na kujamiana. Kutokana na utafiti ni wavulana wanaobahatika. Dhana hizi zinakuza ile hali ya kutendwa na kutenda baina ya wazulufu. Wazulufu wavulana ndio washiriki hai au watendaji ikizingatiwa mofolojia ya maneno ilhali wazulufu wasichana ni watendwa. Wavulana wanapojamiana hudai kuwa *wamegurumisha* na *kukwachua* kuashiria kuwa wamefaidi au wamefanikiwa katika swala husika kama inavyodhihirika katika dondoo lifuatalo kutokana na rekodi ya kikundi kiini.

**Dondoo 6. Tunukuzi kutoka Kikundi Kiini Shule B**

> MV I am having sex with my girlfriend for fun and to be popular in my friends' circle. 98% of all my close associates even the "**holy joes**" na **masavedees** **wamebamba, kukwachua** na **kugurumisha** dame fulani mtaani. Indeed it's a **shame** for a form IV boy if he has not had sex yet. It means that **he is not experienced** and did **nothing** in life." **(Tzm Kiambatisho I Uk. 166)**

Katika nukuu hiyo, kulikuwepo na maneno kama vile *kugurumisha* na *kukwachua* ambayo yamekopwa kutoka kwa mchezo wa bahati nasibu wa kampuni ya mawasiliano ya Safaricom. Mchezo wa kampuni hii mwaka wa 2016 "Shangwe Mtaani" umezua neno la "*shangwe kitandani*". Kwa kuzingatia kampuni ya mawasiliano ya Safaricom, ni bayana kuwa ni kampuni iliyo na ufuasi mkubwa zaidi nchini Kenya. Aidha mitandao yao ya kifedha ina umaarufu sana. Hii ndiyo sababu wazulufu wakawa wepesi wa kukopa maneno kutoka kwa michezo ya mauzo.

Bali na kuashiria utendaji na utendwaji, maneno haya *kubamba, kukwachua na kugurumisha* ambayo yametumika kwa pamoja yana sifa mahususi ambazo ni muhimu katika kuelewa ufasiri wa ujinsia miongoni mwa wazulufu. Neno kubamba miongoni mwa wazulufu huenda linafasirika kuwili; aidha kuashiria kushika au swala ambalo linavutia. Kukwachua ni neno linaloashiria kukwaruza. Wakati mtumizi simu anaongeza salio kwenye simu yake, akinunua kadi lazima aishike na kuikwaruza kwa uangalifu. Kugurumisha ni kutia moto au kuanzisha gari. Basi miongoni mwa wazulufu, kuingilia swala la kijamiana, ni kana kwamba mvulana amebamba (kuingiza box), kukwachua na kugurumisha kama inavyodokezwa katika dondoo hili ili kupata tajiriba.

**<u>Dondoo 7. Tunukuzi kutoka Kikundi Kiini Shule C</u>**

> So **lazima udanganye madem uwaingize box wakishaingia kwa box** yako ujifunze na wao vile game itakuwa........... **<u>(Tzm Kiambatisho H Uk. 157)</u>**

Taswira inayojitokeza ni kuwa mvulana amemtaka msichana urafiki na hivyo basi ni mpenziwe. Ikiwa hivi lazima amshike vizuri kwa makini na uangalifu na kukwachua ili kupata utamu wa maisha na hivyo kuwa amemgurumisha kama ilivyo kwenye dondoo la 7. Maneno haya yanaweka bayana hatua wanazozipitia wazulufu katika kujamiana ambapo kwanza wanatafutana urafiki, wanabembelezana na hatimaye kushiriki ngono. Mbali na hayo, maneno hayo yanaweka wazi jinsi hali ya kutafutana urafiki wa mapenzi na kujamiana inafasiriwa kama tukio la bahati nasibu miongoni mwa wazulufu. Mhusika aweza kupata au akakosa.

Kutokana na ubahatishaji katika mchezo wa kadanda kwenye sportpesa, neno *kujackpot/kuhit jackpot* limetwaliwa na wazulufu. Wazulufu wanazua taswira ya mchezo; dhana ambayo yaweza kufafanua sababu za wao kutomakinikia sana mahusiano yao. Kutokana na kuimarika kwa michezo ya bahati nasibu, wazulufu wanachukulia kuwa iwapo mtu atapata fursa ya kushiriki tendo la kujamiana ni kama aliyeshiriki katika mchezo fulani na ameshinda. Ikiwa hivi, wavulana wanawasaka wasichana ili waweze kushinda. Kumpata na kumfanya rafiki ni hatua moja tu inayochukuliwa kama ujisajilishaji ambapo atatumia hela au rasilimali zake kuwekeza. Iwapo atabahatika, basi *atahit the jackpot* ambayo ni taji kuu linalotafutwa, ndiposa atakuwa amegurumisha na kukwachua. Basi iwapo mvulana atakwachua au kukugurumisha, kuna shangwe na shangwe hii ipo kitandani. Wazulufu wametwaa maneno hayo na kuyafanya yakubaliane na muktadha wao wa kujamiana. Katika umri wao, wanajisaka katika safari ya kujitambua na kwa ambavyo jamii ina kaida fulani za mahusiano, shangwe ibuka ii miongoni mwao.

Wazulufu wanafasiri tendo la kujamiana kama mchezo wa spoti. Dhana hii kwanza inakuza uhalali wa kuwepo kwa wachezaji. Hawa ni wazulufu. Katika mchezo kuna mshindi na anyeshindwa. Wakati mwingine timu hutoka sare. Katika mazungumzo ya wazulufu kuhusu ujinsia, inaelekea ndiye hushinda na ndiposa kuna maneno kama vile *kuscore*. Neno hili huashiria kuwa mvulana amefanikiwa kula tunda na pia kuna uwezekano wa kurejelea tukio la kujamiana ambapo msichana amegurumishwa na basi amepata mimba. *Mbegu imepandwa*. Aidha kuna utumizi wa neno la *kulaunch* ambapo ni kama mwanzo wa jambo fulani. Kuna maneno mengine kama *kucheza mechi/ligi* ambayo yanachangia na kukuza dhana ya washiriki kama wachezaji walio na hiari ya kucheza mchezo huu. Si mchezo tu bali ni ligi au mechi kuashiria umuhimu wa mchezo huu. Wazulufu basi wanaona ujinsia wao kama nafasi ya wao kuingia katika mchezo wa kuonja utamu, kujitambua na kutafuta mahali pao katika jamii. Wanafanya hivi wakitambua kwamba katika mchezo huu mbali na kushinda na kushindwa, pia kuna uwezekano wa mchezaji kuumia.

Kujamiana pia kunaambatanishwa na dhana pana ya fedha. Dhana hii inakolezwa na uwepo wa meneno halisi *M-pesa, bonga point, kiotomotela* (*ATM)* kurejelea mpenzi mzulufu. Ikizingatiwa neno *M-pesa* na *kiotomotela*, inawezekana kupata uangavu wa jinsi wazulufu wanavyofasiri ujinsia wao. Maneno haya yanashirikisha dhana na sifa ya fedha pamoja na huduma zinazoandamana na hela. Dhana hizi mbili (fedha na huduma) ni muhimu katika uwasilishi wa ujinsia miongoni mwa wazulufu kwa ambavyo zinachangia uwepo wa huduma, mhudumu na mhudumiwa pamoja na gharama ibuka. Maswala hayo yanakoleza nani anafaidi na kivipi, nani mshiriki tendi, nani mwenye mamlaka na nani anatawaliwa baina ya wazulufu.

M-Pesa ni huduma ambapo mtumizi aweza kuweka au kutoa pesa kama ilivyo kwa kiotomotela. Hali hii inaweka wazi nafasi ya fedha miongoni mwa wazulufu katika mahusiano yao. Ambapo maneno haya yanatumika kuna tofauti za kijinsia. Msichana anaporejelewa kama M-Pesa ni kwamba yeye anatoa na hivyo si mmiliki wa fedha. Mvulana anafaidi. Msichana mzulufu yupo kwa ajili ya manufaa ya mzulufu mvulana. Yaani kwa mvulana kuna kile ambacho amewekewa na anaweza kukitumia wakati apendapo na kutumia kwa ajili ya manufaa yake. Kwa msingi huu, ile dhana ya binti kutumiwa inapata mashiko. Ni bayana kuwa binti anadhalalishwa. Iwapo atarejelewa kama kiotomotela, ni kwamba jukumu lake ni kutoa huduma mahususi. Kadi yenye nywila yaweza kutumbukizwa na hapo kiotomotela husika kikitekeleza huduma zinazostahili. Ambapo mvulana amerejelewa kama kiotomotela, ni kwamba thamana yake tu ni kutosheleza

mahitaji ya msichana. Iwapo kadi yake ina hela na nywila inayokubalika, basi atakubalika. Kwa msingi huu, inabainika kuwa hata mvulana aweza kufasirika kama kifaa na vile vile aweza kutumiwa.

Kuna taswira ya ufahari na makabiliano katika kuashiria tendo la kujamiana. Utumizi wa leksia *kuingia kasri* na *glad to glad combat* ni ithibati tosha. Kimsingi hivi ni virai vilivyo na vitenzi na nomino. Vitenzi ni maneno ya kutenda. Taswira pana katika matumizi ya maneno haya ni utendaji unaotokana nayo. Virejelezi hivi vinazua fasiri ya tendo la kujamiana kama swala muhimu na la kifahari. Kwanza kuingia kasri ni tukio muhimu na huenda ndio sababu hukumbukwa na wengi. Kutokana na taswira hii aidha, yawezekana kutambua mvulana kama mfalme na ndiye anayeingia kasrini. Hali hii inapata mashiko na kushadidia sababu za mvulana kurejelewa kama *king* na yeye ndiye mmiliki wa kasri. Msichana anafasiriwa kama malkia na yeye humfungulia mfalme milango ya kasiri. Katika utathmini wa maneno haya, swala la mamlaka linajitokeza. Mvulana anabainika kuwa na uwezo juu ya msichana. Licha ya kwamba msichana ndiye aliyebeba kasri, kasri hilo ni la mfalme na yeye si mfalme. Huu ni uhalisi wa ushiriki tendi na ushiriki uso hai unaojitokeza katika mahusiano ya kijinsia ambapo mvulana anasawiriwa kuwa mshiriki tendi ilhali msichana si mshiriki hai. Katika hali halisi za maisha wanaume hufunguliwa milango ya manyumbani mwao licha ya saa wanazorejea nyumbani.

Neno *combat* lililojitokeza katika mazungumzo ya wazulufu ni neno linaloelekeza katika vita. Neno hili linaaksi tendo la kujamiana kama tukio la kivita. Vita vya sehemu husika. Vita vya hisia katika kuonja utamu. Ndiposa wazulufu wanaambatanisha neno hili na maneno *glad to glad combat* yaliyojitokeza katika maneno yaliyoandikwa. Ni bayana kuwa hapa wazulufu hawajazingatia utumizi wa kinga. Utambuzi huu unathibitishwa na nukuu ifuatayo kutoka kundi kiini:

**Dondoo 8: Tunukuzi kutoka Kikundi Kiini Shule A**

> Huwezi kula sweet na karatasi so utatoa karatasi ndio ukule sweet so ndio maana wao. Yaani hawataki kuhave sex wakitumia condom sa wanataka tu kuhave ile direct contact ya mwili. Unasikiaga mabeshete wakisema sisi tulipoanza kuhave sex **we didn't use anything—not even pills**—ilikuwa like eeeeh (kicheko) you know, you don't eat a candy with the wrapping. B**ut** then a **disaste**r happened. **(Tzm Kiambatisho J Uk. 184)**

Utumizi wa maneno *".....we didn't use anything- not even pills"* ukiambatanishwa na kirai cha "*boi anaogopa sweet life*" ni bayana kwamba kuna hofu na wasiwasi unaoambatanishwa na tukio la kujamiana kama ilivyo katika vita. Vitani walinda usalama huwa wana hofu ya kuumizwa au hata kuangamizwa na mahasimu wao. Ingawa katika mahusiano ya wazulufu hakuna mahasimu, wasiwasi huu ni ishara ya kutokuwa na uhakika wa matokeo. Matokeo yaweza kuwa hasi na wazulufu wanaelewa.

Si kwamba wazulufu hawajui yanayoweza kutokea na ili kujiepusha na maswali yanayozuka kutokana na kutomakinikia matokeo, wanaumba taswira ya mchezo. Michezo ni swala muhimu katika kudumisha uimara wa kiafya. Aidha pia ni swala linalomshughulisha mzulufu hivi kwamba hajakaa bure au kutulia. Wazulufu wanatumia hali hii kukuza itikadi ya kuwa kujamiana ni swala la kawaida na lililo muhimu kwao. Mintarafu ya mkabala huu kuna utumizi wa kirai cha Kiingereza cha "*Dancing in between the sheets*" kwenye orodha ya leksia. Kirai hiki kinaumba taswira ya ngoma au densi. Kinakuza uwepo wa maneno ambayo kisarufi yapo kwenye kundi la vitenzi.

Kutokana na maneno ya kirai hiki, taswira ya kusakata densi inakuzwa. Fasiri yake kwa mujibu wa wazulufu ni kwamba tendo lenyewe linalinganishwa na kucheza densi pamoja na raha inayotokana na mshiriki kwenda kusakata ngoma. *In between the sheets* huenda ikafafanua mtazamo wa sehemu za mwili wa msichana. Wanalinganisha uke na *sheets* na basi mvulana anacheza ngoma yake kwenye sehemu zile. Tukio au tendo la kusakata ngoma ni tukio la kawaida sana. Kwa wanajamii, huwa ni namna moja ya kutuliza fadhaa inayosababishwa na wingi wa kazi. Wazulufu nao wanabuni namna fulani ya kujituliza.

Mbali na hayo, haya ni maneno ambayo yanaweza kuzungumzwa hadharani pasi na kuibua aibu na maneno haya yanabana na kudumisha usiri miongoni mwa wazulufu. Taswira hii inakuzwa na utumizi wa maneno kama *smashing the walls of Eden*. Maneno haya yanasawiri tendo la kujamiana kama tendo shughulishi. Kuta (walls) pia ni taswira ya labia na Eden ni shamba lenyewe ambapo ili mvulana afike kwenye shamba hilo sharti avunje kuta/nyua za shamba lenyewe. *Testing suspension* na *kucheck oil level*, ni maneno yanayotumika katika muktadha wa magari. Maneno haya yametumika ili kuimarisha ukawaida wa tendo la ngono miongoni mwa wazulufu.

**Dondoo 9: Tunukuzi kutoka Kikundi Kiini Shule C**

MV 002 Chali anatakaga kitu inaitwa road test(kicheko). **(Tzm Kiambatisho H Uk. 161)**

Ili gari liweze kushiriki kikamilifu katika mashindano, lazima viangiko vyake viwe imara. Huthibitishwa tu kuwa imara kupitia majaribio. Aidha lazima mwendeshaji ahakikishe *oil level* iko sawa. Katika kuthibitisha *oil level*, lazima kutumbukiza kipimio. Kipimio hiki ni taswira ya dhakari.

Uimara na uzuri wa gari hapa unarejelea uzuri wa binti. Dhana ya binti kuwa kama chombo inajibainisha tena ambapo katika maneno yanayomrejelea binti kulikuwa na dhana ya gari, kadri binti anavyoweza kustahimili na kumpa mvulana utamu pasi kulimbikia katika fadhaa inayosababishwa na tendo lenyewe basi atakuwa imara. Hata hivyo, kadri oili inavyoangaliwa ndivyo binti anavyozidi kuwa kama *doormat, formless na tasteless*. Hii ni hali inayowaacha wasichana pasi kujua la kufanya ili kupata mahali pao katika jamii. Aidha ni dhahiri kutokana na utumizi wa maneno haya kuwa mvulana ndiye mwenye gari, ndiye mwendeshaji. Anaamua mkondo na njia ambayo gari litafuata, kasi na kadhalika. Hii inampa nafasi na uwezo zaidi ya msichana na hapo kudumisha ubabedume uliopo katika jamii.

Kujamiana miongoni mwa wazulufu kunasawiriwa kama hali ya upanzi na uvunaji. Kilimo ni uti wa mataifa mengi ya Kiafrika. Umuhimu wa taswira hii katika urejeleaji wa ujinsia miongoni mwa wazulufu ni kuhalalisha vitendo vyao, kuvipa thamana katika jamii na kwa muktadha wa utafiti huu ni hali inayoonyesha mwingiliano na usababishano wa maneno katika swala la ijinsia. Utumizi wa leksia ambazo zinaashiria umuhimu wa tendo au shughuli ya kilimo, ni namna mojawapo ya wazulufu kuonyesha kuwa wanafaa kueleweka na wanajamii. Wao wanashiriki katika jukumu lililo muhimu. Ni jukumu linalofaa kuungwa mkono. Katika kuhalalisha vitendo vyao hivi, wanajaribu kujiepusha na kusutwa na kizazi tangulizi jinsi walivyopotoka kimaadili.

Mbali na hayo, maneno yanayotumika na wavulana au kwa wavulana yanaashiria uwezo wao. Huu ni mgawo ambao kwa miaka mingi umekuwepo katika jamii licha ya jitihada za wasichana na jinsia ya kike kwa ujumla. Wazulufu wavulana wamekuzwa kama washiriki hai na ndiposa kuna maneno kama *kupanda mbegu*, *kundunga mbegu*, *kutumia mbegu* na *kuzuru shamba la mfalme*. Mpanzi hapa ni mvulana na ndiye anayepanda mbegu (mshiriki hai) hali inayomfanya msichana

kuwa mpokezi na ndiposa kwa msichana dhana inakuwa ni *kudungwa mbegu*. Ufafanuzi huu unaungwa mkono na uwepo wa neno *kunyunyiziwa* ambapo ni binti ananyunyiziwa. Taswira ni ya kitasfida ambapo maneno yanayoweza kutamkika hadharani yametumika kuweka wazi maswala ambayo yangekuwa mwiko katika jamii za kiafrika kusemwa. Msichana anatazamwa kama shamba hivi kwamba mvulana (mfalme) anakwenda kuzuru shamba lake. Tendo la kujamiana linahalalishwa kwa ambavyo, mfalme ana hiari ya kuzuru shamba lake bila ya kizuizi chochote. Msichana anamilikiwa, ananyimwa mahali pake kama mshiriki na muamuzi wa mkondo wa mahusiano ya kiujinsia.

Utumizi wa leksia hizo unakuza sababu za msichana mpenzi kurejelewa kama *shamba* na *ploti*. Yeye ni mali ya mvulana. Itambulike kuwa haya si maneno tu. Shamba linahitaji kuwa na uwezo wa kukuza chakula hivi kwamba mbegu ikipandwa itaota, kumea na kukua. Zaidi ya hayo, ni kwamba mzulufu mvulana anaweza kuwa na mashamba mengi. Nchini Kenya, iwapo mtu anamiliki mashamba mengi ana sifa na hadhi ya juu. Vivyo hivyo mzulufu mvulana ambaye ana mashamba mengi anaenziwa na wenzake na kutambulika kama mjuzi na aliye na uwezo kwa ambavyo ameweza kuyamiliki na anaweza kuyazuru apendavyo na wakati apendao. Umiliki wa mashamba au ardhi ni alama ya utajiri na ushawishi miongoni mwa kundi husika. Mvulana hana budi kutafuta shamba, kulilima na kulitunza. Ni jukumu lake kupanda mbegu. Ni bayana kuwa kama ilivyo katika jamii, ugavi wa majukumu unajitokeza. Mvulana anapanda mbegu (kutenda wema) na kwenda zake. Hana lawama. Hana jukumu lolote baada ya hapo. Hii ni hali inayoweka wazi wazulufu wavulana kutowajibikia matokeo ya vitendo vyao hususan wanapowapa wasichana uja uzito. Wasichana nao wanatarajiwa kukabiliana na upadaji wa mbegu. Aidha kuitunza kumaanisha kuwa licha ya yote ataibeba mimba hadi ukamilifu wake au atatafuta namna ya kuiavya na pia kukabiliana na hatari zinazotokana na uavyaji wa mimba.

Kutokuwa bikira kunamithilishwa na uakarimu ambo ni maadili muhimu katika jamii. Kila mwanadamu angependa na yafaa awe mkarimu. Ukarimu unasisitizwa hata katika bibilia. Ukarimu huaashiria wepesi wa kumfaa mja wakati wa uhitaji wake. Kwa kutumia upeo huu, wazulufu wanasawiri ashiki na hamu yao ya kutaka kushiriki tendo la kujamiana kama uhitaji. Kama mzulufu ana uhitaji na mwenzake ana uwezo wa kumsaidia, basi na amsaidie kwa ambavyo atakuwa *ametenda wema*, *akatendewa wema* na kila mmoja wao akaenda zake (tenda wema nenda zako). Ufasiri wa ashiki na hamu kwa namna hii, ni namna moja tu ya kumfanya mshiriki

kutokuwa na lawama kwani yeye alitenda wema tu. Uelewa wa aina hii unakata kuwili: Iwapo binti atashika mimba, mvulana yeye alitenda wema na kwenda zake hivyo basi asilaumiwe. Kwa binti naye, hatalaumiwa na jamii kwa kuupoteza ubikira wake kwa ambavyo yeye alikuwa akitenda/ndewa wema. Ndiposa wazulufu wasichana wanarejelewa kama *mama huruma* ambapo yeye alimwonea mzulufu mwenzake huruma- alipewa bure na anatoa bure. Hata hivyo hali hii inabadilika miongoni mwa wazulufu ambapo imebainika kuwa kuna umuhimu wa fedha katika mahusiano. Aidha kuna wafadhili ambao wanawafadhili mabinti na kutendewa wema. Maneno haya ni namna ya kuhalalisha mahusiano yote iwe ni kwa misingi ya fedha au misingi ya mapenzi thabiti.

Katika jamii za Kiafrika, mgeni akibisha mlango, inatarajiwa atakaribishwa na zaidi huonyeshwa wema wa mwenyeji kwa kufunguliwa mlango. Binti ndiye anayemwonyesha mvulana wema huu kwa kumfungulia mlango wa kasri abishapo. Maelezo haya yanaunga/ngwa mkono na utumizi wa neno *mpanuaji* kuashiria binti aliyepoteza ubikira. Licha ya kuwa hilo ni neno hasi, ukali wa kupanua unapunguzwa na dhana ya wema wa kumfungulia mtu mlango anapobisha ikilinganishwa na kumfungia na kumyima ruhusa. Ndiposa binti bikira anarejelewa kihasi kama *mnyimi* au *mchoyo*. Hali hii inaweka wazi ulimwengu wa wazulufu kuhusu ujinsia ambapo mvulana anaomba, akiomba atapewa na kisha kwa pamoja watakuwa wamepeana na kutua muhuri wema wao kwa kutendeana wema. Ikiwa hivi wanadai kuwa wamehudumia taifa/jamii. Taifa na jamii hapa ni mvulana na msichana. Kila mmoja wao anahitaji huduma. Ashiki zao zinalinganishwa na huduma ambayo lazima itekelezwe. Ni wajibu wa wanataifa au wanajamii kulihudumia taifa au jamii.

Dhana ya huduma kwa taifa imekopwa kutoka kwa taasisi kama vile *NYS* (Huduma ya vijana kwa taifa) na NPS (Huduma ya kitaifa ya Polisi). Wazulufu wanakuza swala hili kwa kuzua swala la *ku310* neno linaloambatanishwa na kutoa sadaka katika kanisa. Nchini Kenya kanisa moja liliwarai wafuasi wake kupanda mbegu ya 310 ili kubarikiwa. Basi ni wajibu wa wafuasi kusaidia kanisa katika uhitaji wake na kulihudumia. "umepewa bure nawe utoe bure". Wazulufu hapa wanafasiri ushiriki wao wa tendo la kujamiana kama huduma ya kijamii na pia kama mwaliko wa kutokuwa mchoyo. Kijamii na kidini, wanadamu wanaalikwa kutoa. Kanisa ni dira ya maadili na basi wazulufu wanatumia kauli za kidini kuhalalisha vitendo vyao. Katika jamii kila mtu ana jukumu ambalo hana budi kulitekeleza. Wanapunguza makali ya tendo hilo kwa kulihalalisha kwa

kulionyesha kama jukumu ambalo wanafaa kulitekeleza. Hali hii ndiyo inayowafanya kuona tendo hili kama tendo la huruma na tendo la kufanya wema.

### 4.3 Maneno yanayoashiria Maumbile

Kwa mujibu wa deta, maneno katika mazungumzo ya wazulufu kuhusu ujinsia yalibainika kuwa ni ya kitasfida, kisitiari na yaliyopigwa chuku. Kutokana na matokeo ya utafiti, maneno ibuka yanagawika katika makundi matatu makuu kwa mujibu wa mada ya maumbile. Makundi haya ni pamoja na sehemu ya mwili, Umbo la nje na utanashati na urembo. Kategoria hizi hazijibainishi tu. Ilibainika kuwa makundi ya kategoria hizi yanawakilisha dhana kuu zilizo muhimu katika mvuto wa mtu binafsi. Uvutivu wa mzulufu ni dhana ya kati katika kuamua na kuathiri ujinsia wa mzulufu. Makundi haya yameorodheshwa katika jedwali la 5 hapa chini.

| **Kundi** | **Jinsia** | | **Jumla ( ∑ )** | **Asilimia (%)** | **Mifano** |
|---|---|---|---|---|---|
| Sehemu ya Mwili | MV | 14 | 30 | 35.7 | Pistol, Bazuka, Banana, Milango, Pumpkin, Nyanya, Katiba |
| | MS | 16 | | | |
| Umbo la nje | MV | 6 | 22 | 26.2 | 6 Pax, Fig 1, Fig 8, Size 8, Flat screen, “Momo”, Kaskonde |
| | MS | 16 | | | |
| Utanashati na Urembo | MV | 7 | 32 | 38.1 | Mhunk, Prince charming, On point, Hot stuff, Mxupa, Mtoto, Potential |
| | MS | 25 | | | |
| **JUMLA** | | | **84** | **100** | |

Jedwali 5:Makundi ya Maneno yanayorejelea Maumbile

Makundi haya matatu hujengana na kukamilishana katika uumbaji na urejeleaji wa ujinsia miongoni mwa wazulufu. Ugunduzi huu mbali na kulingana na tafiti za wataalamu wengine, inabainika huambatana na dhana mbali mbali katika ulimwengu wa wazulufu. Maneno haya yanachanganuliwa na kufafanuliwa kulingana na makundi yanayorejelea sehemu mbali mbali za mwili zinazohusiana na ujinsia, umbo, urembo na utanashati.

#### 4.3.1 Maneno yanayoashiria Sehemu za Mwili

Sehemu mbali mbali za mwili hutumika kutekeleza majukumu mbali mbali. Katika utafiti huu, sehemu za mwili wa mwanadamu zilizo na uhusiano wa karibu na ujinsia zilikuwa za kati. Katika kundi la maneno yanorejelea sehemu hizi, ilidhihirika kuwa leksia wanazozitumia wazulufu huegemea kategoria tano: uzani, kifaa, chakula, stakabadhi na taasisi. Katika jedwali la 6, kuna tofauti dhahiri kati ya jinsi jamii ya wazulufu hurejelea sehemu zinazoelekeza au zilizo na mvuto

kwa swala nzima la ujinsia kutegemea jinsia. Sehemu za mwili wa mzulufu zilizo na uhusiano wa karibu na ujinsia hurejelewa kitasfida kwa kuumba taswira inayoambatana na uzani, vifaa, chakula, stakabadhi na taasisi. Tasfida hizi zinakuzwa na kuimarishwa na mkakati wa kimazungumzo wa kistiari na upigaji chuku dhana ambayo ni ya kati katika kuelewa urejeleaji wa ujinsia wa wazulufu. Kwa misingi ya kijinsia, wavulana hawakuwa na maneno yoyote yanayoambatana na taswira ya stakabadhi na taasisi. Maelezo ni kuwa dhana ya tasfida ya stakabadhi na taasisi inaambatanishwa zaidi na wasichana hususan kwa kuangazia maumbile yao kama inavyobainika katika jedwali hili:

| **Kategoria** | **Kundi** | **Maneno** | **Idadi** | **Jumla (∑)** | **Asilimia (%)** |
|---|---|---|---|---|---|
| Uzani | MV | Zigo | 1 | 2 | 6.9 |
| | MS | Mizigo | 1 | | |
| Kifaa | MV | Pistol, Nyundo, booster, transformer, bazooka, ABS, Fimbo ya Nyayo, Chuma, Shaft, Kalamu/Marker | 12 | 16 | 55.2 |
| | MS | Soft Pillow, Milango, firestone, Yana | 4 | | |
| Chakula | MV | Muwa, Banana | 2 | 6 | 20.7 |
| | MS | Nyanya, Grapes Pumpkin, Matunda za round | 4 | | |
| Stakabadhi | MV | | 0 | 3 | 10.3 |
| | MS | Assets, Supporting Documents | 3 | | |
| Taasisi | MV | | 0 | 2 | 6.9 |
| | MS | KCC, State House | 2 | | |
| **JUMLA** | | | | **29** | **100%** |

Jedwali 6: Kategoria za Maneno yanayoashiria Sehemu

Utafiti ulibainisha kuwa kuna maneno mahususi yanayolenga sehemu za siri kwa misingi ya taswira ya kifaa. Imedhihirika kuwa maneno yanayoashiria sehemu za siri za wazulufu vijana huegemea sana vifaa amilifu. Asilimia kubwa (55.2%) ya maneno katika kundi hili yaliegemea kijikategoria cha kifaa (jedwali la 6 katika uk 52). Katika asilimia hiyo, maneno yanayotumika kwa wavulana ni asilimia 75% ilhali yale yanayotumika kwa wasichana ni asilimia 25% pekee. Hali hii yaweza kuelezwa kwa kurejelea uamilifu wa vifaa rejelewa ambapo kuna sifa tatu zinazobainikia: nguvu, mamlaka na uwezo wa kusababisha uharibifu na /au maafa. Kutokana na deta, maneno muhimu yaliyoibuka ni pamoja na *Pistol, Nyundo, Booster, Transformer, Bazuka, ABS, Fimbo ya Nyayo, Chuma, Shaft, Marker* (maneno haya yametumika kitasfida kuashiria dhakari). Kama inavyobainika, dhana ya vifaa katika urejelezi wa sehemu hizi ina sifa bainifu zinazoashiria uwezo wa wavulana ikilinganishwa na wasichana na kukuza ubabe- dume wa

wavulana. Vifaa vilivyotajwa vinazua taswira ya nguvu, mamlaka na umuhimu katika utimizi wa kazi maalum inayotekelezwa na vifaa hivyo kirasmi. Hali hii inaelekeza katika ukuzaji wa dhana ya mvulana kumtawala msichana katika maswala ya ujinsia.

Kwa kurejelea sifa ya uwezo wa kusababisha maafa dhakari imerejelewa kama bastola na *Bazoka*. Ingawa vifaa hivi kihalali hutumika katika ulinzi na kimsingi vina uwezo mkubwa, vyaweza pia kutumiwa kusababisha maafa. Sharti maneno haya kueleweka kwa misingi yote miwili. Ambapo kitatumika kusababisha maafa, wazulufu, wanajiondolea lawama kwa ambavyo anayemchezea aliye na kifaa hiki hana budi kutarajia matokeo ya aina fulani. Kwa upande wa pili ajaliwaye kuwa na kifaa hiki na kukitumia, ana mamlaka dhidi ya asiye nacho. Kulingana na (Mdee, Njogu, & Shafi, 2011), bastola ni aina ya bunduki ndogo inayobebwa mfukoni na hufyatuliwa kwa mkono mmoja tu. Bazoka kwa upande wake ni bunduki ndefu, nyepesi ambayo hushikiliwa begani inapofyatuliwa.

Kulingana na maelezo haya, kunazo sifa kadhaa andamizi zinazojitokeza ambazo ni muhimu katika ufafanuzi wa urejeleaji wa dhakari. Kwanza ni uwepo wa dhana ya "bunduki". Pili ni dhana ya ufyatuzi. Tatu ni udogo, ukubwa na wepesi wa aina hizo za bunduki. Dhana ya "bunduki" inaashiria uwezo wa mtu kujikinga na pia kuna uwezekano wa kutumia kifaa hicho isivyostahili. Kwa misingi ya utafiti huu, inadaiwa kuwa mvulana huonea fahari dhakari yake kama kitambulisho chake cha kuwa mwanamume kama ilivyo kwa walinda usalama ambao huionea bunduki yao fahari na kuilinda. Yaani, mbali na kuwa mvulana kimaumbile, lazima kuwe na sifa nyingine ambayo ni dhakari. Ili bunduki itimize wajibu wake lazima ifyatuke na kutoa risasi. Hii ndiyo hali inayozua dhana ya ufyatuzi. Dhana ya ufyatuzi hukuza ile hali ya mwenye bunduki kuitumia kujikinga au kujilinda au hata kuitumia isivyofaa. Kwa misingi ya utafiti huu, inachukuliwa kuwa swala la "kuitumia" linalenga kushiriki ngono kwa wahusika. Ni, kitasfida, kifaa kilicho muhimu katika utekelezaji wa jukumu la kujamiana. Wazo la kujikinga ni ambapo mvulana anajihisi akitakikana kudhihihirisha uume wake ana kifaa cha kujikinga kutokana na fedheha ya kutotimiza wajibu huo kutokana na ukosefu wa kifaa.

Katika kuitumia lazima kuwe na mfyatuko unaoambatana na tendo la kujamiana. Wazo la kuituma vibaya, ni ambapo mvulana hajali matokeo ya "kufyatua au hata kufyatua fyatua amali (risasi) za bunduki yake. Mwisho dhana ya udogo, ukubwa na wepesi wa kifaa hiki. Kama walivyotambua

wasomi wengine wanajamii wengi huwa na upendelevu wa aina fulani kuhusu urefu na ufupi wa dhakari (Veale, et al., 2014); (Stephens, 2007); (Schneider, Cockcroft, & Hook, 2008). Ingawa utafiti huu haukulenga moja kwa moja maswala hayo, ni bayana katika ulimwengu wa wazulufu ikizingatiwa uteuzi wa maneno haya mawili kuwa swala la ukubwa na udogo wa dhakari ni dhana muhimu. Popote alipo anacho na utumizi wacho ukihitajika basi chaweza kutumika. Hali hii inafafanua ni kwa nini basi miongoni mwa wazulufu wanafunzi, swala la kujamiana hutokea hata katika mazingira tatanishi (makala kwenye gazeti la The Standard 9- Agosti-2015 naye Kibata Kihu)

https://www.standardmedia.co.ke/article/2000171945/shock-as-35-secondary-school-students-nabbed-with-drinks-drugs-and-snuff

"Parents of 35 secondary school students are reeling in shock and disbelief after their children were reportedly caught red-handed smoking bhang and having sex inside a bus. In what sounds like a scene from a horror movie, the students from different schools in Central Province had each paid Sh600 to ride in the bus, whose conniving crew looked the other way as the students' proceeded with sex orgies and indulged in drugs. But the party for the students from Nairobi County was spoilt by some villagers in Kibirigwi, Kirinyaga County, who were alarmed by the noise coming from the vehicle. The matatu had made a stop-over in the village and when the villagers peeped, they were taken aback by what they saw—some of the students were busy having sex while others were smoking bhang. According to villagers who intercepted the bus at Kiangwachi Market between Sagana and Karatina on the main Nairobi-Nyeri highway, some students in the the bus named 'Cash Money Millionaire' were drinking alcohol, while others were kissing."

Uelewa wao wa ujinsia unaoambatana na urejelezi wa dhakari kwa taswira ya vifaa hivyo kwa misngi ya sifa ya nguvu, mamlaka na uwezo wa kusababisha maafa, unahalalisha ni kwa nini wanashiriki ngono za mapema. Mbali na hayo, inaibuka kuwa bunduki ni kifaa ambacho lazima kitunzwe na kufanyiwa majaribio. Namna ya kufanyia majaribo na kuthibitisha kuwa kinafanya kazi ni kwa kumimina risasi. Ili kukoleza mahali pao katika jamii, wazulufu katika harakati zao wanazua dhana ya kufanya majaribio ya uzulufu wao. Katika majaribio hayo, watapata tajiriba. Kutokana na maelezo mtazamo huu, inasadifu kuwa, mvulana ndiye mwenye bunduki na msichana ndiye mwenye kumiminiwa risasi. Mbali na maelezo haya kuonyesha umiliki na nai mwenye mamlaka, ni hali ambayo pia yaweza kufafanuliwa kimaumbile na kukoleza nani mshiriki hai (mtendi) na ni nani mtendwa. Msichana kwa misingi ya taswira hii yaelekea kuwa ni mhasiriwa wa maumbile tu na mvulana amejaaliwa nafasi ya kumtawala kijinsia. Hata hivyo, msichana ana uwezo wa kuamua aina ya "bunduki" aitakayo au hata mmiliki fulani.

(Transfoma) au kigeuzi ni kifaa cha usambazaji wa nguvu za umeme. Kina nafasi muhimu katika kuhakikisha nguvu za uumeme zipo na kwa iwango kinachostahili. Iwapo kifaa hiki kina hitilafu basi nguvu za umeme hutatizika. Aidha ndanimo huwepo mafuta yanayodaiwa kuwa na thamani ya juu. Ni wazi kutokana na sifa hizi kuwa wazulufu wanatumia kifaa hiki kitasfida kukoleza

umuhimu wa dhakari. Ukweli huu waweza kushadidiwa na uwepo wa ile sifa ya "mafuta" ambayo yanarejelea manii ambayo hubeba mbegu za kiume zanazosababisha ujauzito. Ujauzito ndio mwanga unaoshabihiana na mwanga unaotokana na nguvu za umeme (nguvu za kiume). Maelezo haya yanaambatana na habari zilizoenea sana nchini Kenya ambapo jinsia ya kike kutoka mkoa mahususi waliwavamia wenzao wa jinsia ya kiume kila kulipokuwa na ugomvi na kung'oa kigeuzi chao kama namna ya kulipiza kisasi. Ingawa utafiti huu haukuwa na nia ya kuingilia maswala hayo ya kijamii, inabainika kuwa maneno yanayotumika na jamii pana yanapenya hadi katika ulimwengu wa wazulufu. Hali hii inaweka wazi athari za jamii pana kwa wazulufu. Aidha inakuza uhalisia wa sifa ya lugha ya mwanadamu kuwa hupokezanwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Kwa mujibu wa utafiti huu, mbali na umuhimu unaopewa kifaa hichi, dhana ya kuwa kigeuzi ni muhimu katika kuelewa ulimwengu wa ujinsia wa wazulufu. Kwanza wameambatanisha dhakari na kifaa halisi na zaidi kuweka wazi kilichopo ndani ya kifaa hicho ambacho lazima kipitie mageuzi ya aina fulani ili kuzua matokeo fulani. Kulingana na utafiti huu, matokeo ni ujauzito ambao unaambatana na athari fulani miongoni mwa wazulufu hali inayosababisha maneno na peo mahususi za matokeo na taratibu za kushughulikia matokeo hayo.

Kwa kurejelea dhakari kama *fimbo ya Nyayo*, mbali na kuashiria kiumbile kama lile umbo la fimbo, kuna swala la kuihusisha na mtawala wa taifa la Kenya- raisi wa pili wa taifa. Ishara ya uongozi na utawala wake ilikuwa ni fimbo ambayo ilienziwa kiasi cha kubuniwa kwa wimbo- "Fimbo ya Nyayo yatuongoza kwenda mbele". Ilikuwa ni ishara ambayo kila alipokuwa alikuwa nayo. Kila wimbo wa taifa ukichezwa aliinyosha juu. Hali hii inaambatana na utumizi wa *pistol* na *bazoka* ambazo wamiliki wazo hawaziachi na vivyo hivyo dhakari haiachwi. Aidha lazima mtumizi ailekeze kwa mtu au kitu fulani. Aidha kule kunyoshwa kwa fimbo kunatumika kitasfida na wazulufu kuashiria uwima wa dhakari hisia za kujamiana zinapoamshwa. Mbali na fafanuzi hizo, ni bayana kuwa swala la ujinsia wa wazulufu ni swala linaloibusha hisia za kisiasa na labda ndiposa kuna chembe chembe za maneno yanayoambatana na siasa au utawala fulani. Nchini Kenya, swala hili limekuwa ni kiazi moto kilicho na kinachozidi kuibua mijadala katika bunge la kitaifa. Taswira hii ya fimbo, inakuzwa na uwepo wa urejelezi wa vifaa vingine kama vile *shaft*, *chuma*, *kalamu* na *marker*. Hivi ni vifaa ambavyo huwa wima. *Kalamu* na *Marker* hutumika katika muktadha wa kielimu hususan katika taasisi. Vifaa hivi huwa na wino (*manii*-kitasfida) na wino

huu hutumika kuandika kwenye vitabu (neno mojawapo ambalo hutumika kurejelea sehemu za wazulufu wasichana).

Muhimu zaidi katika sehemu hii ni dhana ya kuandika ambapo mja aweza kuandika kwa kutumia wino usiofutika na hivyo kuashiria kudumu kwa maandishi. Haya ni maelezo yanaoashiria tokeo la kujamiana ambapo mzulufu aidha amepata ujauzito hususan kwa wasichana au matokeo hasi kama vile kupatwa na maradhi au kusutwa na wakubwa au hata kufukuzwa shuleni. Hizi ni athari ambazo zinaambatanishwa na kushiriki ngono za mapema miongoni mwa wazulufu. Maneno haya yanakuza na kudumisha nafasi ya mvulana kama mhusika aliye na uwezo juu ya msichana. Aidha ni sababu tosha ya ni kwa nini utamaduni ungali unasisitiza kuwa kawaida ni mwanamume anayemsaka mwanamke na ndiye anayefaa kuzua mazungumzo yaani kumwendea msichana na kumrai. Pia ana wajibu wa kumlinda na ndiposa kimazungumzo amepewa uwezo.

Ugunduzi huu unapata mashiko kwa kuangazia urejelezi wa sehemu za msichana kwa kutumia vifaa kama vile *milango*, *yana*, *soft pillow* na kadhalika. Kwa *mlango*, kifaa hiki hutekeleza jukumu la kufunga na hadi ambapo umefunguliwa mja hawezi kuingia nyumbani. Hii ni taswira inayoashiria umbo la sehemu za siri za msichana. Aidha ni kwa hiari yake ambapo tu anaweza kufungua kuashiria ukubalifu wake wa kushiriki mapenzi. Hali hii ndiyo inayokuza uwepo wa maneno kama vile "*amefunguliwa*" na "*amefungua*" kuashiria binti asiye bikira. Taswira hii aidha inakuza na kufafanua uwepo wa maswala kama vile ubakaji ambapo mhusika mmoja hajatoa idhini na hajaridhia lakini amelazimishwa na hivyo kuingia kwa lazima. Binti hakutoa nafasi ya kufunguliwa mlango. Dhana hii pia inakolezwa na uwepo wa maneno kama vile "*hiting home stretch*" kuashiria tendo la ngono. La muhimu katika kirai hiki cha maneno ni dhana ya *nyumbani* ambapo ili mtu ahisi amefika nyumbani sharti afunguliwe mlango na kukaribishwa.

Kwa kulenga mamlaka aliyo nayo msichana, yaweza kudaiwa ana mamlaka kiasi lakini mamlaka hayo yangali ya kiwango cha chini. Inapoangaziwa wizi unaotekelezwa, wezi huja kwa bunduki ambazo huwababaisha walio ndani ya nyumba hata kama imefungwa. Vivyo hivyo hata kama binti amefunga anahofia kuhusu "nyumba" yake. Aidha wezi hao waweza kuvunja lango hilo na kuingia nyumbani ambapo wahusika kimsingi hawana la kufanya. Yaweza kudaiwa kuwa licha ya kuwa mlango humpa mamlaka mhusika, mamlaka hayo huwa ni kwa kiasi tu. Basi mvulana angali ana uwezo juu ya msichana ifikapo maswala ya ujinsia. Huenda akaomba kufunguliwa au akalazimisha

kufunguliwa iwe kwa nguvu au kwa kutumia misingi ya kitamaduni ambapo mvulana anafaa kuwa na weledi wa kimapenzi na hivyo kuenziwa akilinganishwa na msichana. Ugunduzi huu unashadidiwa na nukuu ya kikundi kiini

**<u>Dondoo 10: Tunukuzi kutoka Kikundi Kiini Shule C</u>**

> MV 001 Unaona unaanza kujimake perfect kwa game juu hata mtu footballers, athlete wote huwa **wanafanya mazoezi unaona**? Huwezi amka tu na uende kwa field kwa game. Ndio before uoe lazima utake ukuwe perfect unaona? Kwa sababu **hata wewe ni mwanaume kamili.** So lazima udanganye madem uwaingize box wakishaingia kwa box yako ujifunze na wao vile game itakuwa inachezwa ndio sometimes in future ukiingia kwa game bibi yako atakuwa anashindwa na huyu alifunzwa na nani unaona? **<u>(Tzm Kiambatisho H Uk. 157)</u>**

Neno *soft pillow*, limetumika kuashiria maziwa ya msichana. Utumizi wa neno hili unaibua dhana mbili zilizo muhimu katika kuelewa fasiri na uelewa wa ujinsia miongoni mwa wazulufu. Kwanza kuna dhana ya ulaini. Dhana hii inaasharia kwa kiwango kikubwa uzuri wa kirejelewa na pia starehe inayotokana na kulalia kifaa hicho. Kwa misingi ya utafiti huu, hii ni taswira halisi inayotokana na sifa za maumbile ya sehemu rejelewa. Wazulufu wanafasiri hali hii ya ulaini kama swala linalovutia na hivyo kuwapa hamu ya kutalii na kugundua ulaini huu. Kwa maelezo haya, hii ni sababu mojawapo ya wao kushiriki mapenzi mapema. Dhana ya pili ni utumizi wa neno *pillow*. Hiki ni kifaa kitumikacho kila mtu anapolala. Kimsingi ni kafaa ambacho sharti kiwepo kwenye malazi ili kuegemeza kichwa.

Kwa wazulufu wasichana, wanatambuliwa kwa wao kuwa na maziwa mawili na ambayo wazulufu wavulana wanayapa taswira ya *pillow*. Kifaa hiki iwapo ni kizuri, huyafanya malazi kuwa ya kuvutia na hivyo basi kutegemea mvulana anavutiwa na kimo kipi cha maziwa, wasichana tofauti watakuwa wamewavutia wavulana tofauti. Kutokana na maelezo ya ashiki na mapenzi, watafiti wa tabia za kutafutana urafiki wa kimapenzi wamedai kuwa hii ni sehemu ya mwili wa jinsia ya kike ambayo huwavutia wale wa jinsia ya kiume kwa kiwango kikubwa. Ingawa utafiti huu haukuangazia sababu za kuvutiwa na saizi tofauti, ni muhimu katika kuelewa utazamishaji wa wazulufu wavulana kwa sehemu hii. Aidha ni kiingilio cha ni kwa nini baadhi ya wasichana wanaingilia tabia mbali mbali za kubadili umbile la maziwa yao ili kukidhi hamu ya wavulana wawapendao au hata kuwa miongoni mwa wanaoenziwa zaidi na hivyo kupata ukabalifu katika kundi husika na kupata utambulisho. Utumizi wa neno hili unachangia ufafanuzi wa kuwepo kwa maneno yanayomrejelea msichana kwa misingi ya ukubwa na udogo wao hususan kimaumbile.

Aidha msichana anafasirika kama mhusika anayefaa kumpa raha na starehe mvulana. Mtazamo wa aina hii, unampa mvulana uwezo wa kimamlaka dhidi ya msichana. Aidha unahalalisha kwa kiwango fulani kwa nini wavulana wenyewe hawawajibikii matendo yao. Iwapo kifaa hakistareheshi, yawezekana mtumizi au mwenyewe akakitupa. Kwa mujibu wa utafiti huu, basi kama kirejelewa hakiibui starehe kwa mvulana hata baada ya kuwa amekitumia, anaweza kukitupa, kukiacha na kutafuta kingine ambacho kitampa starehe.

Kutokana na utafiti, ilibainika kuwa sehemu za mwili wa mwanadamu zilizo na mvuto fulani kwa ujinsia kitasfida hurejelewa kwa misingi ya uzani kwa kuwepo maneno kama vile *zigo* na *mizigo* kwa wazulufu wavulana na *mizigo* kwa wazulufu wasichana. Swala la uzani au uzito ni muhimu katika utambuzi wa mwili wa mwanadamu kumaumbile. Kwanza wazulufu wanaporejelea sehemu za wavulana kama *Zigo* ni kukuza ubabe dume wa wavulana ambapo wavulana hutazamwa kuwa na mamlaka dhidi ya wasichana katika maswala ya mapenzi. Aidha, kimofolojia, neno zigo ni ukubwa wa neno mzigo na kawaida kilicho kikubwa huwa na uwezo na nguvu zaidi. Ugunduzi huu unakuza imani kuhusu umuhimu wa swala tatanishi la ukubwa wa dhakari miongoni mwa wapenzi.

Kwa mujibu wa wazulufu na kutokana na athari za utamaduni, ni bayana kuwa lazima sehemu hii ingepewa jina la aina hii kimofolojia ili kusisitiza umuhimu wa ukubwa wa sehemu hii hususan miongoni mwa wavulana. Ukweli huu unafunua uwazi wa kipindi mahususi cha wazulufu ambapo wanatafuta utambuzi wao. Kusifiwa kuwa na zigo ni swala ambalo laweza kumuimarishia mzulufu usharifu. Ambapo neno *mizigo* linatumika linarejelea "*the balls"*. Kwa upande wa wazulufu wasichana, utumizi wa neno *mizigo* husimamia makalio na maziwa. Kwa wazulufu wengi hizi ni sehemu zinazoamsha hisia za kimapenzi na huenziwa na kupewa nafasi muhimu katika kuamua mkondo wa uhusiano wa kimapenzi. Hali hii inaambatana na mvuto wa wazulufu wavulana ambao iligunduliwa kwa kiasi kikubwa huvutiwa na ukubwa au unene wa sehemu hizi.

Aidha miongoni mwa wasichana, kunao wanaoonea fahari ukubwa wa sehemu hizi hali ambayo yaweza kueleza sababu za baadhi yao kutaka kuvaa nguo zinazobana au zinazowacha maziwa nje. Kwa kufanya hivi wanatumia vibaya uhalisia uliopo kuwa macho hayana pazia na kwamba wavulana kama ilivyo kwa wanaume huvutiwa zaidi na kinachoonekana. Hii ni mbinu ya wasichana kuwanasa wavulana. Maelezo ya ni kwa nini tofauti na wavulana kuna utumizi wa neno

mizigo na sio mzigo, ni kwa ambavyo sehemu rejelewa inajumuisha aina ya nomino ambayo kisintaksi ni nomino ya jamii. "Maziwa" ni mawili na kimaumbile huwa hivyo. Basi haina budi ya neno hilo kuwa katika wingi kama ilivyo pia kwa makalio.

Utumizi wa maneno hayo kitasfida kunatekeleza jukumu la unyenyekevu katika mawasiliano ambapo kwanza utumizi wa neneo halisi na ukali wa kimatamshi unaotokana na utumizi wa neno hilo kijamii umepunguzwa na kuepukwa. Kwa kufanya hivi, wazulufu wanahalalisha mazungumzo yao, wanabainisha wazi kuwa wanazingatia kaida za kimazungumzo na hivyo kitimiza masharti ya kiisimu jamii.

Sehemu za ujinsia pia hurejelewa kwa kutumia taswira ya chakula. Maneno yaliyojitokeza miongoni mwa wavulana ni *Muwa* na *Banana*. Miongoni mwa wasichana kulikuwepo na maneno kama vile *Nyanya*, *Grapes* na *Pumpkin*. La muhimu katika utumizi wa maneno haya ni kuwa sehemu hizi zimehusishwa na chakula. Aidha zimeoanishwa na aina fulani ya matunda. Inaelekea kuwa wazulufu wanafasiri ujinsia wao kitasfida kama chakula ili kushadidia umuhimu wa ujinsia katika maisha ya mwanadamu. Chakula ni mahitaji ya kimsingi ya mwanadamu hata kwa misingi ya maelezo ya ngazi za mahitaji ya mwanadamu kama ilivyopendekezwa na Maslow mwaka wa 1943 na 1954 katika (McLeod, 2017). Ingawa chakula kinatokea katika daraja la chini, Maslow alieleza kuwa ni baada tu ya mja kutimiza mahitaji hayo ambapo anaweza kuelekeza jitihada zake katika mahitaji ya juu zaidi na kuafikia ufanifu wa maisha. Kutokana na maelezo haya, dhana ya chakula inakuwa muhimu katika kuelewa ulimwengu wa jinsia miongoni mwa wazulufu. Hawajatumia dhana ya chakula tu, wanaweka bayana nafasi ya kati ya ujinsia maishani mwao kwa misingi ya utambulisho na pia uhalilishaji wa vitendo vyao vya kijinsia.

Mbali na hayo, siyo tu dhana ya chakula lakini pia umahususi wa chakula na aina ya chakula; matunda. Matunda yaliyotumika bali na kuwa kikawaida yana manufaa mengi katika kuongezea mwili madini na kuukinga na maradhi mbali mbali, yana vile vile sifa mahususi zinazojenga taswira kamilifu ya ufasiri wa ujinsia miongoni mwa wazulufu. Kwa mfano kwa wazulufu vijana, dhakari hurejelewa kama *muwa* na au *ndizi*. Muwa huwa na sifa ya uimara. Ndizi kwa upande wake huwa na umbo mahususi linalojenga taswira ya dhakari. Mbali na hayo, muwa ukitafunwa (tendo la kushiriki ngono) hutoa maji yalio na utamu wa sukari. Hali hii inachangia na kuipa mashiko kile kijikategoria cha maneno ya kiladha yanayorejelea utanashati na kuvunja ubikira.

Utumizi wa matunda haya aidha unaweza kufafanua ni kwa nini wazulufu wengi hawatumii kinga wanapojamiana na hivyo kuwa katika hatari ya maambukizi. Matunda yote mawili sharti yashushuliwe ili yaweze kuliwa. Yanaposhushuliwa, hubidi yaliwe mara moja kwa ambayo yaweza kushika uchafu haraka. Mintaarafu ya wazulufu, maelezo ni kuwa ndizi halitakuwa tamu likiwa na maganda yake. Basi kujamiana hakutafikia raha na ukamilifu wanaoutarajia iwapo watatumia kinga.

Kwa upande wa miwa, licha ya kuwa muwa waweza kuliwa pamoja na maganda yake, mlaji hutatizika kiasi kutokana na ugumu wa maganda hayo. Ugumu huu waweza kuambatanishwa na taratibu za utumizi wa kinga na madhara ambayo yanatokana na kinga mbali mbali. Aidha hueleweka kama hali inayopoteza wakati.

Kwa upande wa wasichana, matunda kama vile *nyanya* na *grapes* huwa na mvuto wa aina fulani. Iligunduliwa kuwa neno *nyanya* linatumika kurejelea matiti. Kimsingi, kwanza kuna lile umbo la mviringo la matiti. Umbo hili linabainishwa wazi wazi kwa kuwepo kirai cha maneno *matunda ya round*. Swala la umbo ni muhimu katika kufasiri mvuto na urembo wa mhusika bali na kuwa matiti kimaumbile huchukua umbo hilo la mviringo. Sehemu hii huwavutia wanaume sana na huathiri maamuzi yao kuhusu uvutivu Furnham na Swami, 2007; Gueguen, 2007). Wataalamu hawa wanadai kuwa hata sifa ya kimo ni muhimu na huvutia macho sana hususan katika tamaduni ambapo nguo husitiri matatiti (Dixson, *et al*., 2010; Lynn, 2009; Pawlowski na Jasienska 2008). Nyanya kama tunda ambalo limeiva, huvutia sana machoni hususan kutokana na rangi yake na uthabiti. Utumizi wa neno hili unaafikiana na tajriba iliyopo katika bara la Afrika ambapo kuna baadhi ya jamii zilizo na misemo inayotumia nyanya kitasfida kurejelea urembo na matiti. Pili kama nyanya imekua, ikaiva vizuri huwa inapendeza na hakuna budi kuichuma. Isipochumwa, uzuri wake utanyofoka. Zabibu (*Grapes)* kwa upande lake, ni aina ya matunda yaliyo adimu na ambayo yana thamani ya juu.

Kutokana na sifa hizo, taswira ya thamani ni muhimu kwa ambavyo, kwa wazulufu hii ni sehemu inayothaminiwa sana katika urembo wa binti, ashiki za mapenzi na pia katika hali ya ulezi na uendelezi wa kizazi. Kutokana na thamani hii, basi yaweza kudaiwa kuwa wazulufu wangependa kulinda na kwa upande mwingine wengine wanasaka kugundua thamani hiyo. Pamoja na maneno hayo, kuna maneno mengine kama vile *zabibu* na *pumpkin*. Haya ni matunda yaliyo na thamani

kubwa ya kimadini na huchangia katika afya ya mtumizi. Zabibu hazipatikani vivi hivi na huwa na gharama ya juu. Taswira inayoibuka hapa ni ambapo wazulufu wasichana wamepewa thamani na hususan inaporejelewa sehemu ya matiti. Kwanza ni kitambulisho muhimu cha msichana. Pili ina thamani kwa maisha ya mtoto kwani ndiyo sehemu inayomlisha katika siku tangulizi za maisha.

Kutokana na thamani na umuhimu huu, si sehemu ya kuchukuliwa vivi hivi au kupatikana vivi hivi. Maelezo haya yanaweka wazi sababu za wavulana kwa wasichana kuthamini sehemu hii na kuionea fahari. Wasichana hawaiachi kiholela hadharani na ambapo labda wameidhihirisha ni kutokana na sababu za uwezo wake wa kuvutia macho ya wavulana. Kwa mujibu wa utafiti huu, dhana ya umuhimu unaombatanishwa na sehemu hii ni muhimu katika kuelewa ulimwengu wa ujinsia wa wazulufu. Hii ni sehemu ya mwili ambayo inampa mhusika hadhi ya juu mbali na kumtofautisha na mhusika mwingine. Kwa uelewa wa wazulufu, uvutivu huu ni sababu yao kuu ya kutaka kuzua mahusiano ya kimapenzi.

Wazulufu pia hurejelea sehemu za mwili wao zinazohusiana na ujinsia kwa kutumia taswira ya stakabadhi. Hususan taswira hii ni kwa wazulufu wasichana. Hali hii yaweza kutokana na umbo lao. Kimsingi msichana hutarajiwa kuwa na umbo kubwa kiasi (lililo na nyama kiasi). Kwa misingi hii, yaweza kufafanuliwa sababu za wao kurejelea sehemu ya makalio kama "*supporting documents*". Dhana hii imekopwa kutoka kwa miktadha ya kuomba kazi ambapo mja huulizwa kuambatisha stakabadhi zitakazoimarisha nafasi yake ya kupata kazi. Kutegemea tajiriba ya mja, stakabadhi hizi huenda zikawa ni nyingi. Mintaarafu ya utafiti huu, inachukuliwa kuwa dhana ya tajiriba inaoanishwa na ukomavu wa msichana. Kadri anavyokuwa, ndivyo makalio yanavyozidi kuimarika na basi kutumika kama stakabadhi katika swala la mapenzi. Swala kuu linalojitokeza hapa ni kuwa mbali na kuashiria sehemu husika, ni ishara pia ya mja kuwa amefikia kiwango fulani cha ukomavu na hivyo basi kuweza kustahimili yanayotokana na ujinsia.

Zaidi ya hayo ni bayana kutokana na tafiti tangulizi kuwa sehemu hii ya mwili wa mwanamke huwa ni kivutio kwa wanaume wengi. Dhana ya kuvutia huku huibua fikra na hisia za kimapenzi miongoni mwa wahusika na hivyo basi taswira hii yaweza kufafanua wingi wa kushiriki mapenzi miongoni mwa wazulufu. Kwa misingi ya masomo ya kijamii, mvulana ni kiumbe anayevutiwa na kushawishika zaidi kutokana na kuona. Basi iwapo mhusika atakuwa na stakabadhi, macho ya

mvulana huenda yakavutiwa na hapo kuzua uhusiano wa kimapenzi. Utumizi wa neno hili miongoni mwa wazulufu ni ushahidi wa uwepo wa miiko na kanuni za namna ambavyo wanajamii wanapaswa kutumia lugha. Kwa mujibu wa miiko na kanuni kama hizo, ndiposa wazulufu wamebuni jina hilo ambalo laweza kutamkwa hadharani pasi kuibua hisia za aibu na kukiuka sheria za uzungumzaji.

Uhalisia huo unaweka wazi ufahamu wa kanuni hizi miongoni mwa wazulufu. Ili kuzungumzia maswala ambayo ni tata katika jamii, wazulufu hawa wameibua mtindo wa kitasfida na kutumia vitu ambavyo ni vya kawaida sana katika hali halisi maishani. Mbali na neno *stakabadhi*, kuna utumizi wa neno *kitabu*. Neno hili katika mkutadha wa wazulufu huashiria ngazi walipo. Wao ni wanafunzi na hivyo basi wanahusiana na vitabu kwa wakati mwingi. Utumizi na fasiri ya kitabu na kalamu unaungwa mkono na utumizi wa neno *katiba*. Katiba ni stakabadhi muhimu kwa taifa lolote lile. Katiba ndiyo dira ya taifa na hushikilia nafasi muhimu katika namna ambavyo taifa linaongozwa. Viongozi huapa kwa katiba na kuapa kuilinda na kuizingatia. Fasiri ni kwamba wazulufu hawa wanatumia maneno yaliyo katika mazingira yao ya kawaida kuzungumzia swala la ujinsia.

Utumizi wa maneno ya kawaida kunafanya swala la ujinsia na kujamiana kuwa kama swala la kawaida katika maisha ya wazulufu na hivyo basi kuepuka usiri na ubanifu unaozungukia ujinsia. Ukawaida huu, unahalalisha matendo ya kiujinsia ya wazulufu kama matendo ya kawaida. Ufafanuzi mwingine ni kwamba iwapo wanataka "*kula tunda*" lazima msichana afungue kitabu. Basi iwapo mvulana ana *kalamu* sharti kuwe na kitabu cha kuandikia. Kalamu lazima iwe na wino wa kuandika, kitabu kiwe na uwezo wa kuandikiwa na wamiliki wa kalamu na kitabu wawe na hiari ya kukubali utumizi wa vifaa hivyo. Inabainika kuwa mwanafunzi anapokuwa shuleni hana budi kuandika. Tendo la kuandika ni tarajio mojawapo la mwanafunzi. Mwanafunzi sharti awe pia na kitabu au mahali pa kuandikia. Kwa mujibu huu, ni bayana kuwa kitabu kipo kwa ajili ya manufaa ya kalamu. Mzulufu msichana yupo kwa ajili ya kumfaa mzulufu mvulana licha ya ukweli kwamba wote ni wamiliki wa "vifaa" muhimu katika utekelezaji wa uhusiano kijamii. Mintaarafu hiyo, mvulana anamtawala msichana hali inayoambatana na utumizi wa leksia kama vile kigeuzi na bastola. Mgao wa kimaumbile wa ni nani anamiliki nini unahalalishwa. Pili ni uwezo wa kutekeleza jukumu mahususi linalofaa kutekelezwa na kifaa husika. Tatu ni swala la mamlaka. Ikilinganishwa vifaa vyote vinavyorejelewa, mvulana ana mamlaka zaidi ya msichana. Kama

alivyobainisha Onyango (2007), mamlaka yaweza kuwa ya kisiasa, kiuchumi, kijamii, kitamaduni, kisaikolojia na hata kimaumbile. Kwa kurejelea leksia tumikizi, utafiti huu umeshadidia ukweli uliopo katika jamii kuwa mvulana anamtawala msichana kiujinsia kwa kutumia mamlaka yake kimaumbile na kijamii.

Dhana ya ni nani mwenye mamlaka zaidi ya mwingine miongoni mwa wazulufu ni swala muhimu kwa mujibu wa ujinsia miongoni mwa wazulufu. Umuhimu huu unaweka wazi sababu za wazulufu wavulana kuwasaka wasichana. Wavulana hata kwa misingi ya kitamaduni wanafaaa kuwasaka mabinti na kuzua mahusiano ya kimapenzi. Hata hivyo, kumekuwepo na mabadiliko ya kijamii ambapo hata kama ni kwa kiasi kidogo tu kunao wasichana wanaowasaka wavulana na kuzua uhusiano huu wa kimapenzi. Hali hii inatokana na usawa ambao umepigiwa upatu sana katika jamii. Kwa misingi ya usawa huu, wote wawili kwa pamoja wana nafasi sawa. Kila kifaa kinakihitaji kifaa mwenzake. Basi mvulana anamhitaji msichana na vivyo hivyo msichana anamhitaji mvulana. Dhana hii inazua dhana ya thamani hali ambayo inaweza kutumika kueleza ni kwa nini wavulana wanawalinda wapenzi wao kwa hali na mali. Aidha kutokana na picha pana ambapo watawala huapa kwa katiba na pia kuapa kuilinda ni taswira zilizo muhimu. Mvulana anampa msichana aliye mpenzi wake utambulisho. Anamtambua kama mpenziwe na hapo ndipo dhana za umilikaji huanzia na kuhodhiwa.

Kutokana na utafiti, ilibainika kuwa matiti hurejelewa kwa kutumia taswira ya taasisi inayohusiana na maziwa. Neno *KCC* lilibainika miongoni mwa maneno yanayotumiwa na wazulufu. Kuelewa neno hili, sharti kurejelea muundo na umuhimu wa taasisi hii kwa jamii. Kwanza hutoa ajira kwa wanajamii. Pili, maziwa ni muhimu kwa wanajamii kutokana na thamani yake kwa mwili wa mwanadamu. Kwa kutumia neno hili katika misingi ya wazulufu, matiti ni utambulisho wa msichana. Humpa nafasi na mahali pake katika jamii. Pili ni kivutio kikubwa kwa jinsia ya kiume. Inapozingatiwa jukumu la uzazi, matiti humfaidi mtoto kwa maziwa.

Kutokana na utafiti, fasiri na uelewa wa ujinsia wa wazulufu waweza kuegemezwa katika taswira pana zinazotokana na maneno mahususi. Swala la utambulisho imedhihirika ni muhimu kwa wazulufu. Katika awamu ya uzulufu, ndipo wazulufu wanapoanza kujitambua na kutafuta nafasi yao katika jamii. Uhalisia huu unaweka wazi ulimwengu wa wazulufu na mitindo yao pamoja na maswala ya upodozi. Labda hii ndiyo sababu wengi wanatafuta ushauri na namna ya kubadilisha

umbo lao iwe la mwili kwa ujumla au la sehemu mahususi ili kuafiki utambulisho wa kijamii. Swala la mvuto ni muhimu katika shughuli nyingi tu za mwanadamu likiwemo swala nzima la ujinsia. Huenda hii ndiyo sababu baadhi ya wazulufu wasichana wanavalia kwa mtindo fulani ili kuweka wazi baadhi ya sehemu za mwili wao kwa lengo la kuwavutia wazulufu wavulana. Kutokana na mvuto huu, hamu na hisia za mapenzi huamshwa na kama mzulufu hatoweza kudhibiti hamu hiyo, basi tendo la kujamiana huenda likatimizwa na hapo kupata ufafanuzi wa uwepo wa ngono za mapema miongoni mwao. Katika muktadha wa kuashiria mapenzi wazulufu wana virai kama vile " *touching awesome places*". Hiki ni kirai cha maneno ambacho wazulufu hutumia wanapopunga hewa na kustarehe na mpenzi. Kimsingi kinaibusha dhana ya kugusa na ukweli kuwa kuna sehemu za mwili zilizo za kati katika mapenzi.

Dhana ya kugusa ni muhimu kwa ambavyo yaweza kuashiria vitendo vya kimsingi katika mahusiano ya kimapenzi. Aidha lile fungu la "*awesome places*" linaelekeza kwa sehemu ambazo zinatambuliwa kwa sifa za uzuri fulani. Si ajabu basi kuwa wazulufu wanafasiri baadhi ya sehemu za mwili zilizo na uhusiano na ujinsia kama "*awesome places*". Kutokana na urejelezi wa aina hii, wazulufu wanazua hamu na hivyo kusababisha udharura. Pia wanaondoa fikra kwamba hizo ni sehemu zisizotajika katika jamii. Wanapunguza ukali wa mawazo ya sehemu hizo kwa urejelezi halisi kwa kusisitiza "*awesomeness*" wa sehemu hizo. Huu ni mkakati wa kimazungumzo wa kupiga chuku na una nafasi ya kati katika mazungumzo ya wazulufu. Inavyobainika hapa ni kwamba wanakweza uzuri na kudidimiza hisia hasi zinazoweza kutokana na utaji wa sehemu hizo. Inafasirika pia kuwa wazulufu wanaoanisha bidhaa na mahali ambapo bidhaa hiyo hutoka. Fasiri hii ni muhimu kwa ambavyo dhana ya utenda kazi wa sehemu husika unaeleweka.

Sehemu hii imeweka bayana kuwa sehemu za mwili zilizo na uhusiano wa karibu na ujinsia hufasirika miongoni mwa wazulufu kwa misingi ya: uzani, vifaa, chakula, stakabadhi na taasisi. Misingi hiyo imeweka wazi kuwa maneno yanayotumika kurejelea sehemu mbali mbali, ni ya kitasfida. Tasfida kama mbinu ya mawasiliano ni mbinu muhimu katika kuvunja ukali wa maneno yanaoyelekea kutokuwa na wepesi wa kusemwa hadharani kutokana na kaida za mawasiliano miongoni mwa wanajamii. Hii ni hali muhimu katika kufanikisha mazungumzo ya wazulufu kuhusu ujinsia. Pia inachangia usiri wa mazungumzo yao swala ambalo ni muhimu kwao katika kuumba utambulisho wao na kuwasiliana pasi kizazi cha wazazi kupata moja kwa moja wanachokisema.

Aidha maneno ibuka (fimbo, milango, *soft pillow*, chuma, kalamu na kitabu n.k.) yanaambatana na vitu halisi vinavyotumika katika shughuli za kawaida za wazulufu. Ufafanuzi unaelekeza kuwa ukawaida huu ni mbinu ya wazulufu ya kuzungumzia na kulifanya swala la ujinsia kufasirika kama swala la kawaida. Yaani haina haja kwa jamii pana kuliona tofauti na kutumia muda wao mwingi kwalo. Kwa kufanya hivi, wazulufu wanatafuta kibali cha kuhalalisha vitendo vyao vinavyoambatana na ujinsia. Uhalalishaji huu ni hali muhimu katika kuelewa tabia zao zinazohusiana na ujinsia kama vile kushiriki ngono za mapema, ongezeko la ujauzito miongoni mwa wazulufu, uavyaji mimba na kutokamilisha masomo.

### 4.3.2 Maneno yanayoashiria Umbo

Maneno yanaoashiria umbo katika utafiti huu yanafasirika kama mvuto wa maumbile. Yaani, ni kiwango ambacho kwacho, umbo la mzulufu huchukuliwa kuwa la kupendeza na kuvutia na basi kuzua dhana za urembo na utanashati. Katika kugawa maneno yanayorejelea umbo kiuamilifu, kategoria tatu ziliibuka kama ilivyo katika jedwali la 7 katika ukurasa wa 67. Kategoria hizi tatu huzuana na kuchangiana. Uzuri wa umbo la mzulufu yaelekea huathiri maendeleo, ukuaji, mahusiano na ujinsia wa mzulufu (Becker na Luthar, 2007; Boyatzis, Baloff, ma Durieux, 1998; Hargreaves na Tiggemann, 2003). Uvutivu imetambuliwa huegemezwa kwa misingi ya taratibu za kisaikolojia ambazo zimeibuka ili kuwatambulisha wenzi watarajiwa (Buss na Schmitt, 1993).

| **Kategoria** | **Kundi** | **Maneno** | **Idadi** | **Jumla (∑)** | **Asilimia (%)** |
|---|---|---|---|---|---|
| Umbo la nje | MV | Fig 1, Layout, Packs, Number 11, 6 Pax | 6 | 16 | 72.7 |
| | MS | Fig 8, curves, Figure ya chupa, mafigure, 8 GB, kiuno cha nyigu, momo, kaskonde, shapeless, formless | 10 | | |
| Umashuhuri | MV | | 0 | 2 | 9.1 |
| | MS | Size 8, Vera Sidika | 2 | | |
| Chombo | MV | | 0 | 4 | 18.2 |
| | MS | Flat Screen, Tablet, Transit goods, Gari kubwa | 4 | | |
| **JUMLA** | | | | **22** | **100%** |

Jedwali 7:Kategoria za Maneno yamayoashiria Umbo

Kwa misingi ya kategoria ibuka, wazulufu wavulana kwa wasichana, hurejelea maumbo kwa misingi mitatu: umbo la nje, umashuhuri na chombo. Kwa mujibu wa umbo la nje, ni bayana kuwa

hili ni umbo lililo dhahiri machoni mwa muhusika. Kutokana na vikategoria vinavyobainika, ilitambuliwa kuwa, kuna mengi yanayoathiri mvuto wa mtu mmoja kwa mwingine, na umbo la nje ni mojawapo. Mintarafu ya maneno husika, mvuto wa nje wa kiumbo hushirikisha mawazo ya kilimwengu yaliyo ya kawaida kwa tamaduni zote za wanadamu. Miongoni mwa wazulufu wavulana, kuna matumizi ya maneno kama vile *Fig 1, 6 pax* ilhali baina ya wazulufu wasichana kuna matumizi ya maneno kama vile *Fig 8*, *8GB* na *Size 8*. Maneno haya yanatokana na anachokiona muhusika na ndiposa  kuna urejelezi wa kutumia umbo (Figure). Maneno haya yanaashiria uimara na uvutiaji.

Kama ilivyo katika tafiti nyingine (Schick, Calabrese, Rima na Zucker, 2010; (Schooler na Ward, 2006; Woertman na van den Brink, 2012; Yamamiya, Cash, na Thompson, 2006; Saxton, *et al.*, 2010), jinsi umbo lilivyo ndivyo linavyovutia machoni mwa wahusika. Ufasiri wa uvutivu wa umbo ni ishara ya mwanamume kuweza kumshawishi mwanamke. Basi urembo wa nje baina ya wazulufu unahusishwa na ushawishi, kutawala na kutawaliwa na umashuhuri. Hii ni hali ambayo yaweza kufafanua ni kwa nini wazulufu wengi wanatumia muda wao kujiimarisha kiumbo na kiafya kupitia mazoezi. Hali hii inaungwa mkono na swala la kitamaduni kuwa wanaume wazito na walio na kitambi hawavutii. Aidha kwa kuzingatia muktadha wa washiriki katika utafiti huu, ni wanafunzi ambao wangali katika shule na hivyo basi hawatarajiwi kuwa wameota vitambi.

Neno *6 Pax* ni neno ambalo limekopwa kutoka kwa muktdha wa hoteli. *Pax* na *six pax* linatumika kitasfida kuashiria umbo la mwanaume hususan upande wa kifuani ambapo misuli inajidhihirisha na kuashiria uwezo wake wa kumlinda mpenziwe. Utambuzi huo unakubaliana na tafiti nyingine kuwa umbo la kiuno chembamba, mabega mapana na kifua chenye misuli (6 Pax) huvutia wazulufu wasichana kama ilivyodaiwa na (Braun na Bryan, 2006; Frederick na Haselton, 2007; Fan, Dai, Liu na Wu, 2005). Dhana ya uwezo wa kumlinda mpenziwe ni muhimu katika mzulufu kuilinda ngome yake.

Uwezo huu huonekana kama hali inayovutia na hukuza usharifu wa mzulufu mvulana. Kwa mujibu huu, utambuzi huu unaafikiana na tafiti nyingine za awali (Lippa, 2007; Luo na Zhang, 2009; Montoya, 2008; Shaffer, Crepaz, na Sun, 2000; Swami na Tovée, 2008) ambazo zimetambulisha kuwa wakati wa kuchagua mpenzi, umbo na sifa za umbo ambazo jinsia ya kike huangazia huelekeza kwa hadhi ya juu, mamlaka na nguvu, amali na uwezo wa kulinda. Kwa

misingi ya utafiti huu, inabainika hii ni namna mojawapo ya utambulisho. Aidha ni hali inayompa mhusika staha na ukamilifu wa kimawazo. Kwa kufanya hivi, mvulana anakoleza utambulisho na nafasi yake katika jamii. Ni bayana kuwa kuna umbo pendelewa la jinsi mvulana anvyofaa kuwa. Yaani wima na aliye na misuli. Hali hii inaambatana na mtazamo wa kitamaduni ambapo mhusika aliye na umbo kama hili hufasirika kuwa na uwezo wa kumridhisha mpenziwe.

Kwa wazulufu wasichana, umbo la nane (*Fig 8*) ni umbo maarufu na linaloambatanishwa na urembo. Ni umbo linalowavutia wavulana sana. Wasichana wengi huweka bidii za haja katika kudumisha umbo hili. Kiuno chembamba yaelekea chapendeza hali inayoungwa mkono na uwepo wa neno "*kiuno cha nyigu*". Hali hii inashadidiwa na uwepo wa maneno mengine kama vile *size 8, hour glass, chupa ya fanta* na kadhalika. Haya ni maneno ambayo kimsingi yanalenga umbo la nje la mhusika na yana sifa zinazofanana. Kuwa na umbo hili na utumizi wa dhana ya chupa ni namna mojawapo ya ubidhaaishaji wa mwili wa wazulufu wasichana aidha wao wenyewe au kutoka kwa wazulufu wavulana. Umbo hili laweza kumfanya mzulufu msichana yeyote kuwa mrembo sifa iliyo muhimu katika uzuaji wa uhusiano baina ya wazulufu. Umbo, kwa wazulufu ni muhimu kuliko kimo. Taswira bainifu ni kuwa umbo mwafaka la mzulufu msichana ni udogo kwenye sehemu ya juu ya mwili na ukubwa kwenye sehemu ya chini ya mwili (umbo la chupa).

Yaani umbo pendelevu na lililo kamilifu lafaa kuwa kubwa kiasi kwenye sehemu ya juu, nyembamba kiunoni (kiuno cha nyigu) na kuwa kubwa kwenye sehemu ya chini (size 8) taswira inayoingiliana na leksia tumikizi *hour glass*. Kutokana na umbo hili, uvutiwaji wa wazulufu wavulana na umbo la kiuno ni swala la kati katika kuzua mahusiano yanayoambatana na ujinisa. Utambuzi unaoafikiana na utafiti wa (Buss na Schmitt, 1993; Singh na Young, 1995; Barber, 1995), ambao waligundua kuwa wanaume huvutiwa na dhana na sifa kadhaa za umbo la mwanamke kama vile udokezo wa ujana, umbo la sura, kiuno na mengine.

Kwa wazulufu wavulana, imedaiwa kuwa umbo hili la chupa lina athari sawa na vileo. Huwateka kifikira na kuwapumbaza. Utambuzi huu waweza kutumika kufafanua sababu za wazulufu kujihusisha na kujishughulisha na picha au maandishi yenye kutia ashiki (ponografia). Umbo hili la nane/chupa huambatanishwa na urembo, utungishi na siha nzuri katika jinsia ya kike. Mintarafu hii, wazulufu wavulana wanaona umbo hili la chupa kama umbo linaloibua mvuto wa kimapenzi.

Basi, swala kuu la uvutiaji inabainika lina nafasi muhimu katika swala la ujinsia miongoni mwa wazulufu. Kwa mujibu huo, ni bayana ni kwa nini lazima umbo la kiuno chao lingerejelewa.

Maelezo ya utumizi wa maneno yanoashiria umbo la nje ni kutokana na umaridadi wa nje wa kitu husika. Kwa misingi ya Saikolojia, iwapo kitu kwa nje kinavutia machoni, hunata akili na razini za anayekitazama. Ukweli huu ni muhimu katika uzuaji wa mahusiano ya ujinsia miongoni mwa wazulufu. Inabainika kuwa sharti mzulufu avutiwe na anachokiona hali ambayo yaweza kufafanua ni kwa nini wengi wao wanatumia muda wao mwingi kuhakikisha wanasalia kuwa watanashati au warembo. Athari na umuhimu wa urembo wa nje unashadidiwa kuwa kilicho kizuri machoni kinavutia na kinapendeka na kukubaliana na tafiti za watafiti wengine kama vile Eagly, Ashmore, Makhijani na Longo (1991), Langlois, *et al.* (2000), Jackson, Hunter, na Hodge (1995), Riniolo, Johnson, Sherman na Misso (2006).

Jambo jingine linalotokana na fasiri ya maneno haya ni kuwa msichana anachukuliwa kama kifaa au chombo. Ugunduzi huu unaambatana na kauli ya Tolman (2012), kuwa ambapo jamii inaangazia zaidi umbo la mwili, mwili hautazamwi tena kwa unafsi wake au kwa udhanifu bali kama chombo. Chombo hichi kina sifa ya kuhitaji uangalifu mkubwa (Breines, Crocker, na Garcia, 2008; Harper na Tiggemann, 2008). Fasiri ya hili ni kuwa huyu mzulufu msichana ni kiumbe "dhaifu" anayehitaji kutunzwa na kulindwa. Wa kutoa ulinzi huu ni mvulana. Hali hii inakuza utawala wa mvulana dhidi ya msichana na kumpa nafasi ya mbele katika mkondo wa ujinsia na mahusiano ibuka.

Taswira hiyo inakuzwa na utumizi wa neno *ua* ambalo likishachunwa hunyauka. Licha ya kuwa ua linapendeza na lina thamani, hunyauka upesi likichunwa au hata likishakomaa. Uzuri wake haudumu. Basi mzulufu msichana akishakomaa hana budi kuchunwa na mzulufu mvulana (kujamiana) na hata akishachunwa ladha yake inapungua; uwili wa mtazamo na ufasiri wa ujinsia miongoni mwa wazulufu unajidhihirisha. Uwili huu haukolezi tu mgao wa majukumu ya kijinsia kwa misingi ya utamaduni, bali pia dhihirisho la ubaguzi unaompa mvulana mamlaka dhidi ya msichana pasi misingi thabiti.

Wazulufu pia hufasiri umbo kwa misingi ya watu mashuhuri. Hali hii ni bayana zaidi kwa wasichana. Kulingana na tafiti awali vyombo vya utangazaji vina ushawishi mkubwa katika maisha ya wazulufu. Wazulufu hutafuta habari za ujinsia kutoka kwa mahirimu, mitandaoni na

katika vyombo vya habari (Kunkel, *et al.*, 2007; Brown, 2002). Hali hii inalingana na utafiti huu ambapo ingawa haikulengwa kugunduliwa ushawishi huu, chembe chembe za ushawishi ni wazi. Wazulufu wasichana hufasiri umbo kwa kurejelea watu mashuhuri kama vile *Vera Sidika* na *Size 8*. Vera Sidika ni msoshiolaiti anayetambulika kutokana na kimo cha "*supporting documents*" zake pamoja na urembo kisiwa. Kutokana na umashuhuri wake na nafasi anayopewa na vyombo vya habari, anakuwa kigezo cha kufasiri urembo. Aidha kuna itikadi kuwa wanaopata nafasi katika vyombo vya habari kwa namna fulani huwa ni warembo. *Size 8* kwa upande wake ni muimbaji maarufu na anaenziwa sana. Umaarufu wake ulianza alipokuwa akiimba nyimbo za densi na alikuwa na umbo la nane (*fig 8*). Katika ulimwengu wa wanawake umbo na kimo cha nane huashiria urembo.

Kutokana na urejeleaji wa watu mashuhuri katika ujinsia, wazulufu kwanza wanajitambulisha kama watu mashuhuri katika jamii bali na kujilinganisha na watu hao mashuhuri. Inabainika kuwa ulinganishi huu si tu kwa misingi ya mafanikio ya wahusika bali pia kutokana na urembo wa nje wa wahusika. Huu ni ukweli halisi katika ulimwengu wa vijana ambapo urembo wa nje unachukua nafasi muhimu katika maisha yao. Swala jingine linaloweza kuambatanishwa na ufasiri wa utumizi wa watu mashuhuri ni nafasi waliyonayo ya kuamua mwelekeo wa jamii katika maswala muhimu. Wana ushawishi mkuu kuanzia swala la mitindo, mavazi hadi kwa tabia mahususi katika jamii. Wazulufu nao wanajifasiri kuwa na nafasi muhimu katika kuamua dira ya maswala muhimu katika jamii. Si watu wanaoweza kupuuziliwa mbali. Basi ni muhimu kwa jamii pana kama ingependa kutatua matatizo yanayotokana na ujinsia wa wazulufu kutambua nafasi yao katika jamii. Aidha watu hawa mashuhuri waweza kuwa kiingilio muhimu katika ulimwengu wa wazulufu hususan inapoangaziwa programu za mafunzo yanayoambatana na ujinsia miongoni mwa wazulufu.

Wazulufu aidha hurejelea umbo kwa misingi ya vifaa. Vifaa hivi vinaambatana na vyombo vya kiteknolojia (*Tablet na flat screen*) na vifaa vya usafiri (*Gari kubwa, Transist goods*). Kimsingi kinachodhihirika hapa ni kuwa kwanza kuna kule kumtazama mhusika kama chombo na pili ni uwepo wa umbo ndogo na umbo kubwa. Ikiangaziwa vyombo vya kiteknolojia, *tablet* ni kifaa kidogo kuliko kipakatalishi na hutekeleza majukumu tu kama yale ya kipakatalishi. Hata hivyo, kina wepesi wa kubeba. Kwa upande ule mwingine, *flat screen* inarejela kiwambo/kiambaza cha kisasa cha runinga. Kiambaza/ kiwambo hiki huwa bapa na chaweza kutundikwa hata ukutani na pia kwa wepesi. Mintarafu ya utafiti huu, vifaa hivi kwa pamoja vinarejelea umbo la wastani na

usasa. Fasiri ni kuwa hawa ni wazulufu wasichana wa kisasa walio na wepesi na wanapendeza na kuvutia. Aidha huambatanishwa na wazulufu wasichana wasio na maziwa makubwa hivi kwamba wakitazamwa ni kama walio bapa.

Wasichana wanene wanarejelewa kwa kutumia maneno gari kubwa na *transist goods*. Katika usafiri, haya ni magari ya safari ndefu. Yana sifa ya ukubwa na mengine hulemewa njiani. Aidha pia huheshimiwa na kuondokewa na magari madogo barabarani. Kwa mujibu wa utafiti huu, maneno haya yanasimamia wazulufu walio wanene. Utumizi wa maneno haya waweza kueleweka kuwili kutokana na sifa za vyombo hivi vya usafiri. Kwanza ikizingatiwa ukubwa wa magari haya, yana uwezo wa kubeba mizigo mikubwa. Neno zigo lina nafasi ya kati katika kuelewa ulimwengu wa ujinsia wa wazulufu. Zaidi ya hayo, madereva wanaoendesha magari haya huchukuliwa kuwa na uwezo wa aina yake. Wanaheshimiwa sana.

Mintarafu ya wazulufu, mvulana ambaye ana uwezo wa kuendesha gari kubwa au *transist goods*, ana umahiri mkubwa. Ni gwiji na anaenziwa na wenzake. Itambulike hapa kuwa wazulufu wamehalalisha tendo la kujamiana kwa kutumia neno la kawaida *kuendesha* na *gari*. Basi mvulana anastahili kuwa na ujuzi wa kuliendesha gari. Ni dereva (mvulana) anayedhibiti gari (msichana) husika. Namna ya pili ya kufasiri utumizi wa maneno haya ni kwa jinsi yanavyotumika kwa namna hasi kuashiria kuwa mhusika ameshindwa kudhibiti ukuaji wake. Umbo hilo halipendezi kwa wazulufu na pia linaogofya (laweza kuondokewa). Kuondokewa huku ni kwa kitasfida ambapo wasichana wanene kutokana na umbo lao hawapati wavulana wanaowapenda.

Hali hii inaelezea ni kwa nini kuna neno lililokopwa kutoka kwa lugha ya kikuyu "*Momo*" kutoka kwa wimbo maarufu "*Ino ni Momo*" kurejelea unene wa muhusika. Katika wimbo huo mwimbaji ni mwanamume na anamrejelea mwanamke mnene kwa namna hasi. Wazulufu wamekopa hali hii na kuiingiza katika muktadha wao wa mazungumzo kuhusu ujinsia. Maneno haya hasi yanaambatana na maneno mengine kama vile *shapeless* na *kaskonde*. Neno *shapeless* ni neno linaloibua hisia hasi kama ilivyo kaskonde. Licha ya kwamba wazulufu wanawaenzi wenzio walio na umbo la kadri, iwapo yeyote yule hususan msichana atakuwa amekondeana sana, basi atarejelewa kwa namna hasi (kaskonde). Uchanya na uhasi huu unazua dhana ya uwili katika maneno swala ambalo ni ugunduzi muhimu katika utafiti huu.

Kuhitimisha kuna ithibati tosha ya umuhimu wa mvuto wa umbo onekevu katika swala nzima la ujinsia. Uzuri wa kiumbo kama kitengo kimoja cha mahusiano na mvuto, una nafasi muhimu katika ujinsia wa wazulufu. Ni dhana moja kati ya nyingine nyingi ambayo mzulufu hutambua kwa mwenzi mtarajiwa (Eastwick, Eagly, Finkel na Johnson, 2011; Finkel na Eastwick, 2008; Luo na Zhang, 2009; Kurzban na Weeden, 2005; Sprecher, 1989; Thao, Overbeek, na Engels, 2010). Umuhimu wa uzuri huu huendelezwa hata baada ya urafiki tangulizi hadi kwa mahusiano ya baadaye maishani. Ingawa wazulufu wavulana na wasichana wanathamini urembo huu, kuna tofauti bayana. Utafiti huu kwa kuangazia kategoria na maneno yanayotumika, umethibitisha uwepo wa upendelevu wa uvutivu wa kiumbo katika uwasilishaji wa ujinsia miongoni mwa wazulufu utambuzi unaokubaliana na tafiti za (Becker na Luthar, 2007; Lippa, 2007).

Ni dhahiri kuwa wazulufu wavulana wanathamini zaidi uzuri wa nje ilhali wazulufu wasichana wanathamini zaidi uwezo wa mvulana kimaumbile na kifedha. Utambuzi huu unakubaliana na tafiti za awali zilizobaini nafasi ya fedha katika swala nzima la mahusiano baina ya jinsia ya kiume na ile ya kike (Buunk, Dijkstra, Fetchenhauer na Kenrick, 2002; Buss, Shackelford, Kirkpatrick, na Larsen, 2001; Cunningham na Russell, 2004). Wazulufu kama kundi mahususi wangependa vilivyo vizuri – wanataka na kuvutiwa na mwenzi pendelewa kwa misingi ya uvutivu wa nje (physical attractiveness). Kwa mujibu wa maelezo haya, utafiti huu unaweka wazi kuwa jinsi mzulufu anavyofasirika kuwa na uzuri wa kimaumbile ndivyo atakavyokuwa ameridhika katika mahusiano kwa misingi ya ujinsia. Hizi ni kauli zinazoafikiana na tafiti za watalamu wengine kama vile Galliher, Rostosky, Welsh na Kawaguchi (1999), Hong (1998) na Hatfield & Sprecher (1995).

Mintarafu hiyo, kuna uwezekano wa uvutivu wa kimaumbile kuathiri mahusiano na matendo ya ujinsia miongoni mwa wazulufu kama ilivyogunduliwa katika tafiti za (Prisbell, 1987; (Patzer, 2006; Stelzer, Desmond na Price, 1987; Levesque, 1993; Feingold, 1992b). Kwa wazulufu swala la uzuri na mvuto wa kiumbo ni muhimu na wazulufu wanatumia uzuri huo kama kizuizi kinachoathiri na kuamua mkondo wa mahusiano yao. Uhalisia huu ni sawa na ugunduzi wa watafiti wengine ambao walikiri kuwa wanadamu wanaporejelea mahusiano na maamuzi ya ujinsia, uzuri na mvuto wa kiumbo hutawala na watu huamua kufuatilia kwa makini na kuekeza katika mahusiano na watu wanaoamini (wao wenyewe) au wanaodaiwa kuwa wanavutia (Luo na Zhang, 2009); Kurzban na Weeden, 2005; Thao, Overbeek, na Engels, 2010).

### 4.3.3 Maneno yanayoashiria Urembo na Utanashati

Baada ya kuchanganua maneno yanayohusiana na urembo wa nje (umbo), ilikuwa ni muhimu kuchunguza maneno yanayorejelea urembo na utanashati. Kama inavyobainika katika jedwali la 8 hapa chini, urembo na utanashati ambao ni zao la umbo, hurejelewa kwa maneno yanayogawika katika kategoria nne kuu. Maneno yanayowarejelea wazulufu wavulana hata hivyo yalikuwa katika kategoria tatu pekee.

| **Kategoria** | **Kundi** | **Maneno** | **Idadi** | **Jumla (∑)** | **Asilimia (%)** |
|---|---|---|---|---|---|
| Mvuto/Bembelezi | MV | Hunk (M), On Point, Hot Stuff, Mdope, Msawa, mhandii | 6 | 21 | 60 |
| | MS | Kuiva, Mxupa, Kidosho, Mresh, Demu Mnoma, Mcool,hot/hottie, Sexy, Pretty, Kabeuty, Beautiful one, Cutey, Kidosho, Kipusa, Love bird | 15 | | |
| Utukufu | MV | Prince Charming, King | 2 | 8 | 22.9 |
| | MS | Malaika, Future, Potential, Past, Rose, Malaika | 6 | | |
| Ladha | MV | Honey | 1 | 4 | 11.4 |
| | MS | Honey Plum, German Juice | 3 | | |
| Utegemezi | MV | | 0 | 2 | 5.7 |
| | MS | Chick, Mtoto | 2 | | |
| **JUMLA** | | | | **35** | **100%** |

Jedwali 8:Kategoria na Wingi wa Maneno Yanayoashiria Urembo na Utanashati

Kila kategoria ya maneno kama ilivyo kwenye jedwali, inafafanuliwa ili kuweza kuzua fasiri na kuafiki peo za kimazungumzo zilizotambuliwa. Mvuto kulingana na (Mdee, Njogu, na Shafi, 2011), ni hali ya kuwafanya watu wapendezwe na uzuri wa kitu, mtu, wazo au tabia ya mtu. Kulingana na maelezo haya, wazulufu wavulana hurejelewa kitanashati kwa kutumia maneno: *(M)hunk*-neno la kimsimu lililo na asili ya Kiingereza. Aidha kuna maneno kama *Hot Stuff* na *On Point*. Haya ni maneno yanoyoibua hisia ya kupendeza. Basi mzulufu mvulana aliye na umbo la kupendeza anadaiwa kuwa mtanashati na kihisia anarejelewa kwa maneno kama hayo. Muhimu katika ugunduzi huu ni ile dhana ya kuwa lazima mhusika awe na hali fulani ya kuvutia au kupendeza ile aweze kuwavutia wanaokusudiwa. Katika muktadha wa mapenzi, na kama walivyogundua wataaalamu wengine, uvutiaji huwa daraja ya kwanza katika kutaka kuzua uhusiano. Aidha baadhi ya hisani maishani mwa mwanadamu huafikiwa kupitia jinsi mhusika anavyovutia (Lorenzo, Biesanz, na Human, 2010; Rhodes, Simmons na Peters, 2005; Flood, 2008).

Katika ulimwengu wa wazulufu, lazima mja avutie kwa mtazamo wa macho ili kuamsha hamu za kimapenzi. Hapa wazulufu wanalinganisha hali hii na ilivyo kwa mwanadamu katika ulaji. Sharti chakula kipendeze. Pia katika uuzaji, sharti bidhaa iwe ya kuvutia na kupendeza machoni mwa mnunuzi. Mintaarafu ya utafiti huu, dhana ya *(M)Hot Stuff* inatokana na muktadha wa ununuzi ambapo bidha inayouza sana hurejelewa kimsimu kama *hot stuff*. Kwa msingi huo, mvulana ambaye ni mtanshati na ni kivutio cha wengi anarejelewa kama *Mhot. On Point* ni neno la Kiingereza linaloashiria ushwari wa jambo husika. Katika rununu, kuna *Emoticons* zinazotumika hususan katika arafa ambapo kinachowasilishwa kimewasilishwa kishwari kwa kulenga ndipo basi ishara hii hutumika.

👍

Fasiri kadhaa zinaafikiwa kutokana na utumizi wa maneno bembelezi au ya mvuto. Kwanza ni kuvutia na kupendeza ambako kunachangiwa na umbo la nje. Pili ni ushwari unaotokana na kitu mahususi. Tatu ni dhana ya kihisia inayotokana na utumizi wa maneno haya. Kwa pamoja dhana hizi tatu ni muhimu katika ujinsia wa wazulufu. Zinachangiana na kukamilishana. Hisia ni muhimu katika kumrejelea mhusika kwa namna chanya au hasi. Maneno husika yanaibua hisia za aina fulani, hisia ambazo ni chanya na zinakuza na kuimarisha mazingira ya kuzua uhusiano wa kijinsia. Iwapo mzulufu anavutia na anapendeza machoni, na ni shwari, atakuwa mtu anayeng'ang'aniwa na wengi ugunduzi unaoweza kufafanua ni kwa nini mzulufu msichana au mvulana anasakwa na wavulana au wasichana wengi na kuishia kuwa na wapenzi wengi. Umuhimu wa ugunduzi huu ni kuweza kuweka wazi sababu za ushindani iwe hasi au chanya miongoni mwa wazulufu na ushindani ambao ikiwa ni hasi unasababisha maafa ambapo kutokana na wivu wanatekeleza vitendo viovu au hata kujitoa uhai kutokana na kulagaiwa.

Kwa upande wa wazulufu wasichana, urembo hurejelewa kwa misingi ya mvuto kwa kutumia maneno kama vile *kuiva*, *mxupa*, *kidosho*, *kipusa* na kadhalika. *Kuiva, Kipusa* na *Kidosho* ni maneno ya asili ya Kiswahili. *Kuiva* huenda kukawa ni kwa matunda dhana ambayo inawiana na maneno yanayotumika kurejelea sehemu za mwili zilizo na uhusiano wa karibu na ujinsia. *Kuiva* waidha kwaweza kuwa ni kwa chakula kuashiria chakula chaweza kuliwa. Kwa vyovyote vile, wazulufu wanatumia maneno haya kuhalalisha tendo lao la kujamiana. Yaweza kudaiwa kuwa iwapo tunda limeiva, lisipochunwa na lisipoliwa huoza na halina thamani tena. Aidha si vibaya

kula. Wazulufu vijana katika vikundi viini walitetea hali hii kwa kusema kuwa iwapo unataka kula tunda lazima pia kuligusa gusa ili kuthibitisha iwapo limeiva vyema.

Kulingana na utafiti huu, inabainika kuwa wazulufu hufasiri tendo la kujamiana kitasfida kama ulaji. Ulaji ni hitaji la kimsingi kwa mwanadamu. Neno hili linaambatana sana na utumizi wa kuiva kuashiria kukomaa. Kawaida, wazulufu wanachukuliwa kuwa wangali watu ambao hawajakomaa na hawafai kushiriki au kufanya baadhi ya maamuzi. Ni muhimu kutambua kuwa wenyewe wanajitambua kama kundi lililofikia ukomavu wa aina fulani na basi wana haki ya kuamua lini na vipi watachuna au kuchunwa kwa tunda lililoiva au lini na vipi watakula chakula kilichoiva. Dhana hizi zinaungwa mkono kwa kuwepo maneno ya "kula" kulejelea tendo la kujamiana, *Cake eater* (ambaye alitambuliwa na wazalufu kuwa mvulana na *cake supplier* ambaye alitambuliwa kuwa msichana) kurejelea wazuluvu waliovunja ubikira.

Katika utafiti huu kuliibuka maneno kadhaa yanayosawiri dhana ya utanashati na urembo kwa upeo wa utukufu. Wazulufu wavulana hurejelewa kama *"Prince Charming", "King"* ilhali wazulufu wasichana hurejelewa kama *"Malaika", Malkia, "Her Excellency"*. Wazulufu wamekopa dhana hii kutoka ulimwengu halisi ambapo walio katika falme tofauti tofauti au hata katika nyadhifa za uongozi na utawala huwa na ushawishi mkubwa miongoni mwa watu. Kila mwana wa ufalme huo anapotajwa, kuna hamu ya kujua mengi na kufuatilia yanayojiri. Katika baadhi ya tamaduni hata wana wanapozaliwa hupewa jina zlinaloambatana na falme mahususi.

Nchini Kenya jina la utukufu *H.E* (*His/Her Excellency*), awali ilikuwa ni hifadhi ya raisi. Serikali za jimbo zilipoanzishwa, magavana na wake wao kwa kuwa ndio viongozi wa jimbo walitwaa jina hilo. Kutokana na mamlaka aliyo nayo raisi, huwa ana mvuto sana na popote aendapo huwa kuna halaiki ya watu. Mzulufu aweza kutumia neno hili kuashiria nafasi ya mpenziwe katika maisha yake. Heshima na cheo chake maishani. Aidha laweza kutumika hivi ili kuibua hisia chanya na hivyo kuchangia uwezekano wa kudumu kwa uhusiano. Kwa misingi ya utanashati na urembo dhana ya utukufu inakoleza umuhimu wa ujinsia katika maisha ya wazulufu. Ni swala la kuenziwa. Urembo inabainika kuwa ni muhimu na kwa kiasi kikubwa huamua mkondo wa mahusiano yao kama wazulufu. Maelezo haya yanafafanua na pia kutumiwa na wazulufu kuhalalisha mahusiano yao katika ulimwengu wao.

Katika mazungumzo ya wazulufu kuhusu ujinsia, dhana ya utanashati na urembo hurejelewa kwa misingi ya ladha. Katika mazungumzo ya wazulufu maneno kama vile *"Honey"* kwa wavulana na *"Honey plum"* na "*German Juice"* kwa wasichana yalijitokeza kwa asilimia kubwa miongoni mwa wasailiwa. La muhimu zaidi ni jinsi mtazamo wa wazulufu kuhusu utanashati na urembo unavyozuana, kuingiliana na kukuzana. Wazulufu wanafasiri hali ya kuwa mrembo au mtanashati kama kuwa na ladha maishani. Ikiwa hivi, basi mhusika ana mvuto maalum na basi atakuwa na jina la kihadhi au la kiutukufu. Ingawa sio lazima kila kilicho na ladha nzuri kivutie au kiwe cha kupendeza, ufahamu wa kilimwengu unaelekeza fikra za wazulufu katika imani na tajriba za kuwa umbo nzuri hukuzwa na kuambatanishwa na ladha nzuri. Kwa mfano baadhi ya halua, huwa na umbo la roho. Mapenzi huashiriwa kwa umbo hilo. Kutokana na maelezo hayo, yaweza kufafanuliwa ni kwa nini urembo na utanashati unarejelewa kwa upeo wa utamu kwa kutumia vionjo vilivyo vitamu (*Honey* na *Honey Plum*). Zaidi ni kwamba iwapo urembo huo una ladha tamu basi haina budi kwa wahusika kuonja au kuchovya kama walivyosema. Mtazamo huu, unazua mtazamo wa utanashati na urembo kwa misingi ya thamani.

Kawaida vitu vilivyo na ladha tamu huwa na thamani ya juu. Tofauti ni kuwa katika mazungumzo ya wazulufu, mtazamo wa kithamani ni dhahiri kwa wasichana pekee. Kulikuwa na maneno kama vile "*Future*", "*Potential*", "*Rose*" na "*Past*". Maneno haya yanaweza kuwekwa katika kundi chanya (*future, potential* na *rose*) na kundi hasi (*past*). Hali hii inaelekeza kwa uhalisi kwamba, urembo unatazamwa kuwili. Kimsingi wazulufu wangependa kuoanisha urembo na sifa chanya na ndiposa kuna maneno mengi chanya. Sifa hii inakuza dhana ya kupendeza au mvuto wa mtu kwa mtu au watu wengine. Inazua matumaini. Wazulufu wanaporejelea urembo kama *future* au *potential*, wanaashiria matarajio, thamani na uzuri wa walichokiona kwa macho. Hii ndio sababu kuna maneno kama vile *chick* na *mtoto* yanayotumika kurejelea urembo.

*Chick* ni kifaranga. Kabla ya kuota manyoya ya kumwezesha kustahimili hali ya anga, manyoa yake huwa laini, yanayovutia hata hisi za mguso. Huwa laini. Hivyo ndivyo ilivyo hata kwa mtoto. Katika uchanga wake ngozi yake huwa laini inayovutia na kupendeza. Mbali na sifa hizi ni kuwa viumbe hawa huwa na utegemezi mkubwa. Kwa misingi ya utafiti huu, inafafanuliwa kuwa, urembo ni swala safi na nzuri ambalo wasichana wamejaaliwa. Hutegemea jitihada zao za kudumisha urembo huo. Hata hivyo katika harakati hizo, wengine huishia kutumia vipodozi vinavyoathiri urembo na basi kuwa na neno hasi kwa urembo.

Mzulufu msichana anapopendeza na kuvutia machoni, anafasirika kama mtu aliye na "*future* au *potential*". Yaani ana matarajio, kuna imani kumhusu. Matarajio haya ni kwamba atapata mpenzi sasa na katika maisha ya usoni. Hali hii inachangia katika kukuza usharifu wa kibinafsi wa mhusika. Usharifu na staha ya kibinafsi ni muhimu katika utambulisho wa mzulufu. Ni hatua muhimu katika kujitambua kwa mzulufu na kuweza kuafikia malengo yake. Sifa ya uhasi inatumika kuhalalisha mahusiano yasiyodumu ambapo wazulufu wamekatiza mahusiano na mara nyingi kwa sababu zisizo na mashiko.

Mahusiano ya wazulufu huambatanishwa na kutodumu kwayo. Huwa ni kwa manufaa tu. Hili laweza kuelezea mahusiano ambayo ni chipuka na yasiyotabirika  na mahusiano yanayosababisha mimba zisizopangwa na uavyaji wa mimba. Katika utafiti, ingawa ni bayana kuwa mvuto wa macho huwa daraja ya kwanza ya kuvutia na kutaka kuzua uhusiano, sio sababu tosha ya kuvunja uhusiano. Katika utafiti neno hasi linalorejelea urembo ni "*past*". Katika lugha ya Kiingereza "Past" ni dhana ya wakati uliopita au hata zaidi hurejelea kuaga. Huu ni ufafanuzi ambao ukitumika miongoni mwa wazulufu unaashiria urembo usiovutia, usiopendeza. Hakuna la mno kuhusu anayerejelewa. Kutokana na kutodumu kwa mahusiano. Basi mzulufu hafai kushinikizwa kwa yaliyopita. Yaliyopita si ndwele, yagangwe yajayo.

### 4.4 Maneno yanayorejelea Mpenzi

Ikizingatiwa umuhimu wa ujinsia miongoni mwa wazaulufu, swala la mpenzi lilikuwa la kati katika mazungumzo ya wazulufu kuhusu ujinsia. Kategoria ya maneno yanayorejelea mada pana ya mpenzi yalijumuisha asilimia 18.55 ya maneno yote yaliyokusanywa (rejelea jedwali 2 uk 29). Mintarafu ya kategoria hii, maneno yanayowarejelea wazulufu wasichana yalishirikisha asilimia 68.12 ya maneno yote ilhali yale yanayotumika kuwarejelea wapenzi wavulana yalishirikisha asilimia 31.88 ya maneno yote kama ilivyo katika jedwali la 9 uk 78.

Tofauti hii yaweza kufafanuliwa kwa misingi ya kitamaduni ambapo wavulana huwaweka chamboni wasichana kwa maneno matamu kama ilivyo kwa msemo kuwa "*Maneno matamu humtoa nyoka pangoni*". Ugunduzi huu unafafanua ni kwa nini swala la ujinsia miongoni mwa wazulufu linajitokeza kama mchezo baina ya wavulana na wasichana. Katika utafiti huu, ilibainika kuwa maneno yanayorejelea mpenzi yaweza kugawika katika kategoria tano kama inavyobainika katika jedwali la 9.

| Kategoria | Kundi | Maneno | Idadi | Jumla (∑) | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| Hisi | MV | Bybz, boo, D.a, bae, swthrt, luv, chali/chally, hot stuff, darling,boy, secret heart, fisi, mshikaji | 14 | 30 | 55.5 |
| | MS | Babe/beb, sweety/swhrt, luv, bobo, hun/honey, kipusa, manzi, kasupuu, girl love, better half, kidosho, MYPT, chile, mafuta mafuta, Fisilet | 16 | | |
| Umiliki na Utukufu | MV | Prince charming, king governor, MCA, boy wangus, 4eva mine | 5 | 10 | 18.5 |
| | MS | First Lady, Governess, Her Majesty, my roses, Msupa wangu | 5 | | |
| Fedha | MV | Sponsor, private developer | 2 | 7 | 13 |
| | MS | Kagari, Shamba, Ploti, BMW, rangi ya thao | 5 | | |
| Ladha na Uzuri | MV | Honey pie | 1 | 5 | 9.3 |
| | MS | Honey pie, Honey comb, flower, sugar plum | 4 | | |
| Matunda | MV | | 0 | 2 | 3.7 |
| | MS | Watermelon, pumpkin | 2 | | |
| **JUMLA** | | | | **54** | **100%** |

Jedwali 9: Kategoria na Wingi idadi wa Maneno yanayomrejelea Mpenzi

Kutokana na jedwali la 9, mpenzi miongoni mwa wazulufu anafasirika kwa mikabala mitano mikuu kulingana na kategoria za maneno zilizoainishwa. Kila mkabala unakuza upeo fulani wa kimazungumzo na kuchangia taswira fulani ya jinsi wazulufu wanavyoelewa ujinsia wao. Kila mkabala unachanganuliwa na kufafanuliwa katika mjadala ufuatao.

Watafiti wengi, wametambulisha kuwa swala la mapenzi ni swala ambalo linajengwa kwa kiasi fulani na hisia za wahusika. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huu, madai hayo yanapata mashiko. Ilibainika kuwa wazulufu wanapozungumza kuhusu ujinsia, mada ya wapenzi hujitokeza. Kwa mujibu wa madhumuni ya kwanza, ilibainika kuwa wapenzi hurejelewa kupitia maneno yanayoegemea mguso wa moyo na hivyo kuibua hisia za kimapenzi. Kwa wazulufu wavulana, maneno kama vile "*bybz, d.a*, *bae*, *swthr*, *luv*, *darling* yalitumika sana. Ugunduzi huu unaelekeza kwa ukweli kuwa swala nzima lina mwegemeo wa kihisia. Watafiti wa mahusiano ya kimapenzi wanadai kuwa penzi ni hisia zinazowavuta watu pamoja. Licha ya hayo, utafiti huu unapiga hatua na kufasiri maneno ya kihisi yanayotumika.

Utanashati wa wazulufu wavulana unaporejelewa kwa maneno kama vile *hotstuff*, kunawiana na mkabala huu wa kihisi. Katika maelezo ya awali, neno *hotstuff* lilifasiriwa kama ule mvuto na

uzuri alio nao mtu. Mvuto na uzuri huu unazua hisia chanya kwa mhusika au wahusika na hivyo basi kuibua maneno ya mkabala wa kihisia. Kwa ambavyo mapenzi ni hisia, uwepo wa maneno ya kihisia si ajabu. La muhimu ni jinsi maneno husika yanavyokuza hisia chanya kumaanisha kuwa wapenzi hurejeleana kichanya. Ni maneno yanayoashiiria huba.

Mpenzi pia hurejelewa kwa mkabala wa umiliki na utukufu. Maneno yanayoashiria umiliki huwa yamebeba vimilikishi ama kwa Kiingereza, Kiswahili au hata lugha ya mtaani. Kuna matumizi ya maneno kama vile *boy wangus*, *4eva mine*, *msupa wangu* n.k. Hali hii inaashiria ile dhana ya mhusika kutaka kumiliki mwenzake na kumfanya kuwa chombo chake. Pia, neno kama *4eva* (forever) linaelekeza kwa ufasiri wa wazulufu kuhusu ujinsia. Swala la wawili kuwa katika mapenzi ni swala linalofaa kudumu. Huu ni ukinzani na jinsi wazulufu wengi walio katika mahaba wanavyotazamwa na ulimwengu. Wanajamii hawaamini na kimsingi hawatambui mahusiano hayo kuwa yanayoweza kudumu kwa muda mrefu. Itikadi kama hii ndiyo imewapelekea wanajamii kuyafasiri mahusiano ya wazulufu kama mahusiano chipuka na yasiyotabirika. Ingawa ni kweli kuwa idadi kubwa ya mahusiano haya hayadumu, kutokana na maneno haya ni muhimu kutambua nia njema waliyo nayo wazulufu.

Uelewa mwingine ni kuwa hata kama mahusiano haya hayatadumu, wazulufu wanaweza kujitetea kuwa tangu mwanzo walikuwa na nia nzuri. Aidha ni muhimu kutambua kuwa kimaumbile, wahusika katika swala la mapenzi wangependa kuwa ni wao tu katika maisha ya kimapenzi ya wenzao. Kutokana na hili wazulufu wanataka au wanadhihirisha ile hamu ya kumiliki. Mbali na hayo ni namna mojawapo ya kumpa mtu utambulisho na heshima miongoni mwa wahusika. Katika mkabala huu kuna matumizi ya maneno yanaoambatana na utukufu. Licha ya kuwa hali hii inashadidia uwepo wa maneno yanayoashiria urembo na utanashati, mpenzi anaporejelewa kwa maneno ya aina hii ni zaidi ya urembo au utanashati. Haya ni maneno yanayojenga uwepo wa kategoria ya tatu ya fedha. Pia yanazua upendelevu wa aina fulani kwa sababu ya hadhi.

Kwa misingi ya hadhi, miongoni mwa wazulufu wavulana kuna maneno kama vile: *king/mfalme*, *prince charming* na *governor*. Kwa wazulufu wasichana, kuna maneno kama vile, *angel*, *Her Excellency*, *malkia/queen* na *malaika*. Haya ni maneno ambayo kijamii yanabeba hadhi ya juu. Kuna mshabaha mkubwa baina ya maneno yanayotumiwa na wavulana na yale yanayotumiwa na wasichana. Neno *king* litaambatana na *queen*. La muhimu hapa ni kuwa hamna ule mgao wa

kimamlaka. Wazulufu wanayatumia maneno haya hivi ili kuonyesha nafasi na hadhi ya mpenzi katika maisha yao. Licha ya kuwa jamii inakashifu mapenzi katika miaka ya wazulufu, wazulufu wenyewe wamebainisha kuwa, ni swala la kati katika kujitambua kwao. Hii ndiyo sababu wana maneno matamu na mazuri ambayo kwa kiwango kikubwa yanahalalisha mahusiano yao. Ni maneno ambayo yakitumika hadharani na katika miktadha mbali mbali yanakubalika kwa wepesi.

Kutokana na katiba ya sasa nchini Kenya, kumekuwepo na watawala wa majimbo ambao wanaamua mkondo wa jimbo husika. Inabainika wazulufu hawapitwi na yanayojiri kwa wakati uliopo maishani mwao. Wamechukua sifa za watawala hao na kuwapa wapenzi wao. Gavana kwa mfano ndiye mkuu wa jimbo. Jimbo hapa linachukuliwa kama roho ya msichana na inamilikiwa na kutawaliwa na mvulana mpenziwe. Kwa upande ule mwingine, malkia ndiye mmiliki wa ufalme hivi kwamba roho ya mpenzi mvulana inachukuliwa kama himaya ya malkia. Kila mmoja wa wazulufu hawa aliye na mpenzi ana nafasi yake inayoambatana na majukumu mahususi. Kutokana na ufafanuzi huu ni dhahiri kuwa majukumu ya kila mmoja wao ni bayana kama ilivyo nafasi zao katika uhusiano wa kimapenzi. Swala hili linaweka wazi mgogoro unaobainika miongoni mwa kizazi hiki kuhusu mapenzi ambapo licha ya wasichana kurejelewa kwa majina hayo ya kitukufu wanataka kuchukua nafasi ya majina ya wavulana. Hii yaweza kufafanua kuvunjika kwa jamii za kisasa.

Mpenzi hurejelewa kwa kutumia maneno yanayoambatana na fedha. Kutokana na matumizi ya maneno ya kitukufu ambayo pia yanaambatana na nyadhifa na hadhi fulani katika ulimwengu halisi, wazulufu hutumia maneno yaliyo na ukuruba na fedha. Kwa wazulufu wavulana kulikuwa na maneno kama vile "*Sponsor*" na "*Private Developer*" ilhali kwa wazulufu wasichana kulikuwa na maneno kama vile *kagari/BMW*, *ploti/shamba* n,k. Neno "*Sponsor*" ni neno linaloashiria mfadhili. Basi wazulufu vijana hutazamwa kama wafadhili. Kuna mahusiano mengi tu katika jamii ambayo kiini na lengo lake ni ufadhili. Ingawa kuna kina mama ambao wanawafadhili wavulana, kijamii, kaida humtaka mwanamume kuwa mfadhili. Wazulufu wamechukua hali hii na kuingiza katika mazungumzo yao kuhusu ujinsia. Inabainika kuwa fedha ni muhimu na sharti mwanamume kutetea na kuilinda himaya yake kwa kuweza kugharimia yanayoambatana na mapenzi.

Hali hii inakubaliana na tafiti za wengine kuwa swala la mapenzi ni swala lililo na gharama ya kifedha. Uwezo wa kufadhili unampa mhusika mamlaka na uwezo dhidi ya mfadhiliwa.

Ikizingatiwa mahusiano ya kijamii baina ya wavulana na wasichana, mwanamume anamfadhili mwanamke na hivyo kuwa na mamlaka dhidi yake. Hii ni hali iliyokuwa bayana ambapo wavulana walielezea uhitaji wao wa kuwa na fedha ili kuwaridhisha wapenzi wao kwa kuwanunulia zawadi anuwai. Ni ishara ya mvulana kujiweza.

Pamoja na utumizi wa neno *sponsor*, kulikuwepo matumizi ya neno "*Private Developer*". Kwanza neno hili katika mkutadha wa taifa la Kenya linaibua mihemuko hasi na huambatanishwa na uporaji wa ardhi. Ni neno ambalo limekopwa ambapo kumekuwa na vuta ni kuvute kuhusu ardhi fulani. Ingawa si katika matilaba ya utafiti huu kulenga vuta ni kuvute iliyopo, ni muhimu kutaja kuwa kizazi cha wazulufu na kile cha wazazi kipo katika vuta ni kuvute hii. Wazazi wanadai wazulufu hawajakomaa kukabiliana na maswala ya mapenzi ilhali wazulufu wanaliona swala hilo kama haki yao. Kutokana na mtazamo huu, mvulana huenda akarejelewa kama "*private developer*" kuashiria kuwa amenyakua binti wa mtu. Aidha wazulufu wenyewe huenda wakawa wanang'ang'ania "*shamba*/*ploti* (binti fulani) moja kwa wakati mmoja.

Wasichana wazulufu hurejelewa kama *ploti/ shamba*, *kagari na BMW*. Nchini Kenya, ardhi ni uwekezaji ulio na riba kubwa. Thamani ya shamba au ploti ni ya juu sana. Aidha kuipata ploti au shamba si kazi rahisi. Muhimu katika utafiti huu ni hayo maswala mawili: thamani na riba. Thamani ya msichana inategemea mvuto wake kwa mvulana kutokana na urembo wake. Basi msichana atathaminiwa sana na mvulana iwapo katika macho ya mvulana anapendeza. Msichana anapokuwa mpenzi wa mvulana mahususi, riba yake inakuwa ni ya juu na huenda wavulana wengine wakajaribu kuzua uhusiano naye na ndiposa kuna dhana ya fedha. Iwapo mapenzi si ya dhati kama ilivyo kwa kiwango kikubwa katika ulimwengu wa wazulufu kwa sasa, basi huenda msichana akawa na mdhamini au wadhamini. Kwa hali kuwa hivi, wazulufu walio katika mahusiano ya aina hiyo, wanayahalalisha kwa ambavyo si vibaya kumdhamini mtu.

Jukumu la mvulana kumrai msichana awe mpenziwe linalinganishwa na ununuzi wa ploti au shamba. Iwapo uzuri na ubora wa ploti unaridhisha, hatua ya ununuzi huanza. La muhimu kutokana na ufasiri huu kuwa mapenzi baina ya wazulufu sio swala la ghafla. Kuna hatua kadhaa zinazopitiwa ili kuweza kufanya maamuzi ya kuwa wapenzi. Baada ya hatua hizi na pindi tu mvulana amekubaliwa anaweza kumiliki na hapo thamani yake na ya msichana huwa imepanda. Mbali na umiliki huu mvulana anapata uhuru na kibali cha kuendeleza miradi yake apendavyo.

Hapo ndipo kuliko na uhusiano wa *private developer* kumrejelea mvulana, na neno la kulima shamba au kuendeleza miradi kurejelea tendo la kujamiana.

Ni muhimu namna ambavyo wazulufu wanavyohalalisha matendo yao. Kupitia matumizi ya maneno ya aina hii, haina budi jamii kukubali kuwa kuna makubaliano baina ya wazulufu na wana haki ya matendo yao. Aidha ikizingatia utumizi wa neno mradi, iwapo tokeo la mradi fulani si chanya ama ilivyotarajiwa, wahusika kwenye mradi huo waweza kuamua cha kufanya. Kwa mujibu huu, iwapo binti atashika mimba kutokana na shamba kulimwa (tendo ambalo kwa wazulufu ni halali) ana hiari ya kuavya mimba hiyo. Kwa mkabala huu aidha inabainika kuna utumizi wa neno *kagari* kwanza kuonyesha nafasi ya msichana na pia kuibua hisi za aina fulani. Umiliki wa gari ni swala ambalo humpa mtu hadhi na heshima kiasi katika jamii. Aidha katika maswala la mapenzi huwa ni kivutio kikubwa kitumiwacho kumnasa mhusika katika pita pita za mahusiano ya kimapenzi. Maswala haya mawili (heshima/ hadhi na utumizi kama chambo) ni muhimu katika utafiti huu. Kuheshimika katika jamii huimarisha staha ya mtu.

Kwa wazulufu kuwa na mpenzi au katika mapenzi ni swala ambalo humfanya mmoja kuheshimiwa na wenzake na hapo kukuza utambulisho chanya wake na kuimarisha staha yake kama mtu binafsi kama ilivyo katika nukuu hii ya kikundi kiini:

**Dondoo 11: <u>Tunukuzi kutoka Kikundi Kiini Shule C</u>**

> MS003C: For me naona kuwa **single ni ujinga s**ometimes coz **kuwa single ni kujikazia maisha** na hiyo si poa lazima uexperience love. There is nothing wrong in girls having boyfriends. After all isn't it true that all First Ladies are wives.............. **<u>(Tzm Kiambatisho H Uk. 159)</u>**

Hali ya gari kutumika kama chambo si swala geni katika jamii pana. Wazulufu wanaitambua na wanaitekeleza. Utumizi wa neno hili katika mazungumzo ya wazulufu hususan kwa misingi ya viambishi vya udogo unadhihirisha sifa ya kimbembelezi. Wavulana wanalitumia kuonyesha uthamini wao kwa mhusika. Ni neno la kimahabuba. Katika utafiti huu, hizo ni fasiri zinazofanikisha uelewa wa wazulufu kuhusu ujinsia. Kwanza binti sharti abembelezwe kwa maneno matamu, thamani yake lazima iwe wazi na lazima kuwe na mguso wa kihisia.

Uwepo wa maneno kama vile: *Honey comb* (kwa wavulana) na *Sugar Plum, My Roses* miongoni mwa maneno mengine (kwa wasichana) ni ithibati kuwa wazulufu hurejelea wapenzi kwa mkabala wa maneno yanayoegemea ladha na uzuri. Mkabala huu ni muhimu katika kupata fasiri za

wazulufu kuhusu swala la ujinsia. Ladha kwa kiwango kikubwa huchangia katika mvuto wa kitu. Katika matumizi ya kawaida ladha nzuri/tamu hukifanya kitu kupendeza. Vingi vinavyopendwa huwa vimepewa ladha nzuri. Uzuri wa kitu au jambo waweza kutokana na ladha yake. Basi kuna muingiliano wa maswala haya mawili.

Katika ulimwengu wa wazulufu, wapenzi wamelinganishwa na vilivyo na ladha nzuri na pia vina uzuri wake. Hali hii inahalalisha wazulufu kuwa na wapenzi katika miaka yao. Ikizingatiwa neno kama vile *Honey Comb*, asali ni tamu na pia ni dawa hususan kwa mafua na tumbo. Wazulufu wanaitumia dhana hii kuashiria kuwa mapenzi yana utamu wake. Kuwa na mpenzi ni kama kuwa na tiba. Mawazo kama haya yanahalalisha swala la mapenzi miongoni mwa wazulufu. Neno *Sugar Plum* ni mwambatano wa maneno mawili sukari (sugar) na plamu kwa maana ya tunda kama zambarau. Maneno haya mawili yaweza kutumika kisitiari kuashiria kuvutia (sukari) na kitu bora (plamu).

Maana za kistiari zinaafiki zaidi muktadha wa mazungumzo ya wazulufu kuhusu ujinsia. Ikizingatiwa kuwa neno hili (sugar plum) linatumiwa kuwarejelea wasichana, maana ya kisitiari ni bayana. Kwanza ni hali ya kuvutia. Lazima binti awe na mnato machoni mwa mvulana. Kitu kinachovutia ni kitu bora katika mtazamo wa macho na ndiposa kinapendeza. Sifa hizi zikiunganishwa kwa pamoja, zinazua ari ya wazulufu kutafutana mapenzi. Muhimu zaidi ni ugunduzi kuwa kuna thamani kubwa kwa binti kuwa “kitu bora” na kitu hicho kiweze kuvutia. Utambuzi huu unafunua ufasiri wa wazulufu kuhusu ni nani atakayerejelewa kiumbo kwa maneno hasi na yaliyochanya. Inabainika kuwa hata kama wazazi wanapinga mahusiano baina ya wazulufu kwa kudai kuwa vitamu huua, wazulufu wenyewe hawaoni lolote baya. Wanahalalisha mahusiano hayo kwa kuwepo na maneno yanayokubalika. Maneno ya kila siku. Mitazamo hii tofauti inazua upinzani baina ya mtazamo wa wazazi na wazulufu kuhusu ujinsia na kuzua peo anuwai za ushughulikiaji wa swala nzima la ujinsia.

Utumizi wa neno *My Roses* unaelekeza kwa umiliki na uzuri. Maua hudhaminiwa sana katika swala nzima la mapenzi na ndiposa wazulufu wanawarejelea wapenzi wao kama maua. Maua ya waridi huwa na uturi mzuri. Aidha ni ishara ya mapenzi. Mbali na hayo maua huwa na uzuri wa kipekee na hutumika kupamba sherehe mbali mbali na hata kuwepo katika sehemu za mapokezi. Inabainika kuwa wavulana wangependa wasichana kuwa na uzuri fulani. Uzuri huu unakuza dhana

awali za kuvutia na kitu bora. Hata hivyo ni muhimu kuweka wazi kuwa, maua huwa na uhitaji wa uangalifu wa makini. Uhitaji huu wa utunzaji unaoanishwa na wasichana. Ni jukumu la kijana kuweza kumuangalia mpenziwe kwa makini huku akishughulikia mahitaji yake yote.

Mbali na hayo, inabainika kuwa wavulana wanafaa kuwa shupavu na wastahimilivu. Hali hii inakuza ule mtazamo wa jamii kuwa wanawake ni viumbe dhaifu wanaohitaji kutunzwa na kulindwa. Wanaume nao wanahitajika kutoa ulinzi huo na kustahimili utesi wa maisha. Fasiri hii inakuzwa na urejeleo wa wavulana kwa maneno kama vile *Sponsors* na *Private developers*. Labda urejelezi huu unakuza itikadi ya wavulana kukua katika mazingira ambapo wanawaona wasichana kama mali. Ndiposa labda wakiwafadhili wanawahitaji wawatumikie na kuwatekelezea majukumu maalum. Isipokuwa hivi kunazuka ubishi na kutofahamiana.

Kuambatana na ufafanuzi huo, ni bayana kuwa wavulana katika jamii wangali wanashikilia mamlaka dhidi ya wasichana. Huu ni mkabala ulio na umuhimu katika mazungumzo ya ujinsia miongoni mwa wazulufu kwa ambavyo ufasiri na uelewekaji wa ujinsia miongoni mwao umeegemea vyakula na matendo ya kula. Ni mkabala ambao umeshamiri kuanzia namna ambavyo wazulufu wanarejelea sehemu zilizo na uhusiano na ujinsia, urejeleaji wa umbo na mpenzi kwa jumla. Mkabala huu unawafaa wazulufu kwa namna kadhaa. Kwanza kuna sitiari ya chakula. Pili chakula ni muhimu katika maisha ya binadamu. Kizazi cha wazulufu basi kinahitaji chakula ili kujiimarisha na kukua. Tatu kwamba mtu amekula chakula au amefanya bidii kutafuta chakula ni swala ambalo halizui utata katika jamii. Mwisho ni kwamba wazulufu wanatumia dhana hii kama mkakati wa kiuzungumzi kuhalalisha vitendo vyao vinavyohusiana na ujinsia. Kunazo tafiti nyingi kuhusu uhusiano uliopo baina ya chakula na ujinsia (Bill, 1994; Braun na Kitzinger, 2001; Crumpacker, 2006; Farquhar, 2002; Probyn, 2000). Utafiti huu unaongeza ujuzi na kuchangia tafiti hizo.

Miongoni mwa baadhi ya jamii za Kikenya, tendo la kujamiana hurejelewa kitasfida kama “kula mtu”. Miongoni mwa wazulufu, kulinganisha tendo la kujamiana na kula chakula, ni sitiari inayoibua fahiwa ya kawaida kwa ambavyo matendo yote mawili yafaa kufurahiwa na yanayozua hamu. Bali na hayo si leksia za kuudhi na zinamwezesha mtumizi lugha kuzingatia miiko katika mazungumzo na kuonyesha kuwa kilichofanyika ni tukio tu la kawaida kama kula chakula. Kupitia sitiari hii wanachokifanya wazulufu ni kuhalalisha matendo yao kwa ambavyo kila mwanajamii

amewahi kuhisi njaa. Basi sitiari hii inakubalika zaidi. La muhimu katika sitiari hii, ni usawiri wa ukuzaji wa mzulufu msichana kama kitu cha kuliwa (kumfanya chombo) na mvulana kwa ajili ya manufaa ya mvulana binafsi.

Kutokana na utafiti ni wasichana pekee wanaorejelewa kwa mkabala huu wa kuliwa. Urejelezi unaoimarishwa na uwepo wa leksia zinazorejelea aina za matunda kama vile *pumpkin*, *tunguja* na *tikitimaji*. Hivi ni vyakula vinavyodaiwa kuwa na manufaa kwa mwili. Na kwa ambavyo vyakula hivi vina manufaa kwa mwili wa mwanadamu, basi mvulana hana budi kuvila. Ikizingatiwa tikiti maji, ni tunda lililo na maji mengi na hukata kiu. Wazulufu wanafasiri hali hii kama haja yao ya kukata kiu cha mapenzi. Haya ni manufaa yanayofaa kumfaidi mvulana. Urejelezi huu unakuza tu mvuto wa msichana kama chombo. Zaidi ya hayo, matunda hayo huwa na umbo maalum ambalo linatumika kurejelea umbo la msichana. Umbo hili huzua mvuto fulani kwa mvulana na kutokana na mvuto huu uhusiano huzuliwa.

Utumizi wa leksia ya chakula miongoni mwa wazulufu mintarafu ya utafiti huu unazua maswala muhimu katika uwasilishaji wa ujinsia. Kwanza leksia hizo zinaambatanishwa na matunda yanayopatikana nchini Kenya na vile vile matunda yanayoagizwa kutoka mataifa mengine. Leksia za vyakula visivyotambulika na kufahamika na wazulufu hazitumiki. Uhalisia huu unaweka wazi kuwa hata kama chakula kirejelewa hakiliwi sana, sharti kiwe kinafahamika na wazulufu. Isipokuwa hivyo basi sitiari haitakubalika miongoni mwa wazulufu.

Mintarafu ya mahusiano ya ujinsia miongoni mwa wazulufu, taswira hii inakuza mahusiano ya kiujinsia yanayokubaliwa tofauti na mahusiano mengine kama yale ya jinsia moja. leksia zinazoambatana na kundi maalum waweza kuelekeza uvutivu kwa kundi husika. Sitiari hizi zinazua umoja ulio muhimu katika kudumisha makundi ya wazulufu. Aidha kuna swala la uelewa wa sifa za kimaumbile za chakula husika. Hili ni jambo la kati katika kuelewa uhusiano wa karibu uliopo baina ya chakula, sehemu ya mwili na tendo lenyewe la kujamiana baina ya wazulufu. Hii ni sifa muhimu ya chakula kama sitiari nzuri katika swala kuu la ujinsia (Crumpacker, 2006) na (Parasecoli, 2007). Kulingana na ufafanuzi huo basi, miongoni mwa wazulufu, vyakula vilivyo na sifa ya urefu na udhabiti kama vile muwa vinatumika kurejelea dhakari ilhali vyakula vioevu kama vile, nyanya na tikiti maji vinatumika kwa wasichana. Mtazamo huu kinzani kuhusu wazulufu wasichana na miili yao unaweka bayana hofu yao katika swala la ujinsia. Inabainika kuwa jinsia

ya kike pekee inatambulika kama namna pekee inayokubalika ya kuridhisha ashiki za mvulana. Uhalisia huu ni sawia na maelezo  kuhusu uwili wa ujinsia unaoshutumu na kulaaani uzinzi wa wazulufu wasichana na kutukuza ushujaa na umahiri wa wavulana  (Olsen na Gould, 2008; Frank, 2007). Kuenziwa na kuenziana kwa wavulana kunajengeka katika uzinzi na uwezo wao wa kujamiana na kutungisha wasichana wengi. Kwa msingi huu, inabainika kuwa ujinsia wa mzulufu msichana ni kama bidhaa yenye thamani kubwa na ambayo bila kuwepo, mvulana hawezi kuinuka na kutambulika katika jamii.

Katika kuelewa ufasiri wa ujinsia miongoni mwa wazulufu ni muhimu kutambua ubaguzi kwa misingi ya maneno unaojitokeza katika urejeleaji wao. Ni wasichana pekee waliopewa majina ya vyakula. Wao ndio wanaofaa kuliwa. Wavulana wanafaidi kutokana na vyakula hivi. Huu ni mkakati wa ziada wa wazulufu kuhalalisha kujamiana kwao kwa mapema. Ikizingatiwa ubaguzi huu, wasichana wanaeleweka kama wahasiriwa wa nafasi waliopewa na jamii pana. Labda hii ndio sababu hata wakichangia katika kudhulumiwa wangali wanaonewa huruma. Aidha labda ndiposa wanahalalisha wao kufadhiliwa na wazulufu wenzao licha ya kwamba wao pia wana nafasi na uwezo wa kuwasaidia wavulana. Kinachobainika ni jinsi itikadi ya jamii pana inayokuzwa hata na dini kuwa mwanamume ndiye mwenye kumshughulikia mwanamke kimahitaji, inavyokita na kuimarishwa hata miongoni mwa wazulufu.

### 4.5  Maneno yanaorejelea hali ya kuwa wapenzi/katika mapenzi

Kwa mujibu wa maneno yanayorejelea hali ya wazulufu kuwa katika mapenzi, kategoria sita kama ilivyo katika jedwali lifutalo

| **Kategoria** | **Mifano** |
|---|---|
| Uhitaji | Was thirsty for you |
| Utwaaji | You stole my heart |
| Uhudumu | Utumishi kwa Uma/ wote |
| Utegemezi | You are my breath of fresh Air |
| Ufanisi | Tujenge jamii, Maendeleo |
| Thamani | Amemfia, Princess treatment |

Jedwali 10:Kategoria za Maneno yanayoashiria kuwa na Mpenzi

Kuwa katika mapenzi kunarejelewa kama uhitaji. Hali hii inabainika kwa kuwepo kauli kama "Was thirsty for you". Kauli hii haifasiriki tu kisemantiki bali ina maana za kipragmatiki. Kwa mujibu wa jinsi wazulufu wanavyorejelea dhana za umbo na wapenzi, kulikuwa na maneno kama vile "*mango juice*", "*german juice*" n.k. Mbali na kuashiria utamu na ladha, hivi ni vinywaji. Ili mzulufu avitumie sharti awe na hamu ambayo hapa inafasirika kama kiu ambacho katika muktadha wa mazungumzo ya wazulufu kuhusu ujinsia, ni haja ya kuwa na mpenzi na ashiki zao za kimapenzi. Kauli hii yaweza kufasirika kuwili; kwanza ni kuhalalisha sababu zao kuwa na wapenzi licha ya wao kuwa katika shule.

Itikadi na imani za wazazi (ambao wana ushawishi mkuu kuhusu vitendo vya wazulufu) ni kuwa wazulufu katika miaka hii wanafaa kuzingatia zaidi elimu. Wengi hata huwasuta wazulufu walio na wapenzi na kuwafasiri kama watu wanaopapia maswala ya utu uzima ambayo watakuwa na nafasi tosha ya kushiriki. Wazazi wananukuu bibilia kwamba kila jambo lina wakati wake mahususi. Ili kuepuka usutaji, wazulufu, wanafasiri haja yao ya kuwa katika mapenzi kama kiu na iwapo mtu ana kiu hana budi kukata kiu hicho. Pili kauli hii inatumika kuhalalisha ushiriki wao wa kujamiana. Iwapo ataulizwa yawezekana na tena kwa urahisi sana kudai kuwa alikuwa na kiu. Aidha inahalalisha ashiki zao ambazo wanadai ni haki zao. Mzulufu awe mvulana au msichana yawezekana kufafanua sababu zake za kushiriki au kutaka kujamiana kwa misingi ya kuwa na kiu. Zaidi iwapo binti anarejelewa kama "german Juice" hana budi kunywewa na mvulana ambapo wote watakuwa wametekeleza jukumu la kutendeana wema.

Kuwa na mpenzi au kuwa katika mapenzi hufasirika miongoni mwa wazulufu kama utwaaji. Hali hii inajitokeza kwa kuwepo maneno kama "*You stole my heart*" (yaani mhusika ameuteka moyo wa mwenzake). Kauli hii inamsawiri mzulufu kama mtu ambaye hana uthibiti wa kinachofanyika. Mwivi mara nyingi anaposhambulia, mhasiriwa huwa hana la kufanya. Kwa mujibu wa kauli hii, wazulufu wanajiondolea lawama la kuwa katika mapenzi. Aidha kila mmoja wao anamlaumu mwenzake. Ni muhimu kutaja kuwa, mara nyingi, uhusiano wa kimapenzi huanzwa kwa maneno yanayoibua na kukuza hisia. Basi wazulufu kutokana na umbo la wahusika, wanapovutiwa na wenzao wanahamu ya kutaka kuzua uhusiano (kiu) na katika kutimiza hamu hiyo, hata kama ataridhia kwa hiari yake, yale maneno yatakuwa yamemteka na hivyo basi kudai kuwa mwenzake "*stole his/her heart*". Taswira inayojitokeza hapa ni kwamba mzulufu hakupanga wala kukusudia kujipata katika lindi la mapenzi na labda hata katika kushiriki mapenzi. Yeye ni mhasiriwa wa hali

kamilifu ya maisha. Hatua ambayo lazima aipitie na hivyo basi hana la kufanya ila kukubali. Inabainika kuwa kimaksudi, wazulufu wanajisawiri kama wanyonge ambao wanajipata katika utesi wa hatua ya ukuaji. Huu ni ukinzani kwa ambavyo wenyewe wanajiona kukomaa na basi wanahitaji kuwa na uwezo wa kukabilian na hali halisi za maisha yao.

Kuwa katika mapenzi hufasirika kama utumishi na ufanisi. Mtazamo huu unatokana na uwepo wa kauli kama vile *utumishi kwa uma/wote*. Kauli hii inaungwa mkono na kauli za kurejelea dhana ya kujamiana kama hile "*Service to Humanity*". Wazulufu wanafasiri hamu yao ya kuwa katika mapenzi kama uhitaji na jukumu. Kwa ambavyo ni wanajamii, hawana budi kutimiza wajibu huu kwa kutoa huduma zao. Kwa kuongeza dhana ya umma na au watu, wanahalalisha uwepo wa wapenzi wengi kwa ambavyo hawajakitwa au kuweka mipaka ya ni nani watamhudumia na ni nani hawatamhudumia. Hii ni mikakati ya utafutaji wa nafasi zao katika jamii. Aidha wanapinga kauli za kiitikadi kuwa mja anastahili kuwa na mpenzi mmoja. Wanaona hali hiyo kama ubaguzi.ikiwa hivi ili dhana ya tenda wema pamoja na mama huruma haitakuwa na mashiko ilhali haya ni maneno wanayojitambulisha kwayo. Ufasiri huu unaelezwa kwa kuwepo mtazamo wa ufanisi ambapo wazulufu walikuwa na kauli kama vile "*tujenge jamii*" na "*maendeleo*". Dhana ya kujenga jamii yaweza kuelezewa kama hali ya kuongeza kizazi au ambapo wanaanzisha uhusiano na basi badala ya kutazamwa kama mtu mmoja wanatazamwa kama wawili. Kitu kinapoongezeka, huwa inafasirika kama maendeleo. Wazulufu basi wanapokuwa katika mapenzi ni kama wameendelea.

Kuwa na mpenzi hufasiriwa pia kwa mkabala wa kithamani. Mkabala huu unaungwa mkono na uwepo wa maneno kama vile: "*nimekukufia* na *princess treatment*". Maneno haya yanarejelea umuhimu unaotiliwa jambo linalozungumziwa. Kwa maana ya kawaida, ili mtu amfie mtu sharti huyu mtu awe na thamani ya juu. Ili mtu ampe mwingine princess treatment lazima mtu huyo awe na thamani ya juu kwake. Maneno haya yanafafanua sababu za wazulufu kupatikana katika vilabu na sehemu za kujifurahishia pamoja na anasa kwa ambavyo kwa uwezo wao hii ni hali ya kumpa mwenzake *princess treatment*.

### 4.6 Hitimisho

Sura hii imeweka wazi kategoria za leksia kiuamilifu miongoni mwa wazulufu katika uwasilishaji wa ujinsia. Kategoria tatu zimebainishwa ni zina sifa ya muingiliano cheshi wa matukio ya kila

siku. Kupitia leksia husika wazulufu huumba au upya au kukoleza ujinsia na utambulisho wao wazulufu kama kundi mahususi katika jamii. Kama walivyodai Jorgensen na Philips (2002) na Fairclough (2003); uwasilishaji wa ujinsia miongoni mwa wazulufu ni namna ambayo kwayo maneno na kauli za usemi zinazotumika zinaumba maana na kuchangia utambulisho, mahusiano ya kijamii na mifumo ya maarifa miongoni mwa wazulufu. La muhimu zaidi ni jinsi uwasilishaji huu hutenda kazi katika ruwaza tofauti, yaani, viwango mbali mbali vya ufahamu na maisha ya kijamii ili kuumba maarifa na uelewa wa ujinsia wa wazulufu.

Uamilifu wa maneno katika uwasilishi wa ujinsia miongoni mwa wazulufu imebainika kuwa husukumwa na kutawaliwa na haja ya wao kuwa tofauti na kwa wakati uo huo kustahilika kuwa. Matokeo ya utafiti huu yanakubaliana na dhana ya usi-lugha kama ilivyopendekezwa na Halliday (1985) ambayo inayoashiria kaida zilizobuniwa dhidi ya taratibu za jamii. Katika utafiti huu, hali hii onezi na chochezi ya lugha ya wazulufu imejitokeza bayana hususan kwa kuangazia kategoria za maneno, kama walivyobainisha wataalamu Gonzalez na Anna-Brita (2011) na inaambatana sana na mabadiliko ya kijamii. Kategoria bainifu za maneno yanayotumiwa na wazulufu zimeshadidia ukweli kuwa jinsia ya kiume huumba ujinsia wao kwa kiwango kikubwa kwa misingi ya mkabala wa kimwili kimahususi kwa kurejelea, vifaa, ushindani, ushari na mafanikio. Kwa wazulufu wasichana, ujinsia wao unaumbika zaidi kwa mkabala wa kujithibiti, kujihini na kujizuia.

Kutokana na tathmini za utafiti huu, uwasilishaji wa ujinsia miongoni mwa wazulufu unakuza na kudumisha ubaguzi kwa misingi ya kijinsia. Kulingana na hili, ashiki na ujinsia wa wazulufu unakubalika katika jamii kama swala la kawaida na wakati uo huo kudhibiti ashiki na ujinsia wa wasichana hali ambayo inalingana na tafiti za awali kama vile utafiti wa Tolman na McClelland (2011). Ubaguzi huu unakuzwa na uwili wa kirejelezi na matumizi ya maneno mahususi hususan kwa misingi ya uchanya na uhasi wa maneno husika. Kategoria zilizoibuka zimeweka wazi jinsi wazulufu wanavyozungumzia na kufasiri ujinsia wao na kudumisha ubabe-dume katika kutafuta utambulisho wao kama wazulufu.

Katika kuumba ujinsia, wazulufu hutumia maneno ya kitasfida na kistiari. Kama walivyodai Egan na Hawkes (2008) na Kokkola (2013), sitiari ni amali ya kiisimu ya kujieleza na pia tukio la kitendaji katika mazungumzo ya ujinsia miongoni mwa wazulufu nchini Kenya. Tasfida na sitiari

hizi si mbinu tu za lugha au sifa mojawapo ya lugha ya wazulufu bali pia ni utendaji wa kiitikadi ulio na nafasi muhimu katika uwasilishaji wa ujinsia miongoni mwa wazulufu katika shule za upili nchini Kenya. Mbinu hii ya matumizi lugha huwasaidia wazulufu katika kutumia maneno hayo kuumba peo zao na kufasiri ujinsia. Kwa kufanya hivi sifa za lugha ya wazulufu ni sehemu muhimu katika kuumba na kuamua mkondo wa ulimwengu wa kijamii kama alivyodai Andrew (2012). Sitiari na tasfida zilizojitokeza zina uhusiano wa karibu na mazingira ya kawaida ya wazulufu. Sitiari na tasfida hizi mbali na kuhakikisha kuwa wazulufu wanazingatia mipaka ya matumizi lugha kama wanajamii, inawarahisishia uzungumzi wao kwa ambavyo wanaweza kusema yasiyosemeka hadharani. Swala la ujinsia na maswala yanayohusiana na ujinsia huthibitiwa na miiko. Basi kama wanajamii, sharti wazulufu wabaini namna yao ya kuzungumzia swala hilo. Aidha, Sitiari hizi zinatumika kuhalalisha na kukawaidisha matendo ya wazulufu yanayohusiana na ujinsia. Kwa kurejelea kujamiana kama tendo la kula, huku ni kulinganisha matendo mawili ambayo kimsingi yana manufaa katika maisha ya mwanadamu. Chakula ni muhimu maishani na basi mwanadamu akiwa na njaa hana budi kula.

## SURA YA TANO

## PEO NA MIKAKATI YA KIMAZUNGUMZO KATIKA UUMBAJI WA UJINSIA MIONGONI MWA WAZULUFU

### 5.1 Utangulizi

Sura hii inazamia ufafanuzi wa madhumuni ya pili na tatu ya utafiti- peo na mikakati ya kimazungumzo katika uwasilishaji wa ujinsia miongoni mwa wazulufu. Mintarafu hiyo, sura imegawika katika sehemu mbili kuu. Sehemu ya kwanza inalenga ubainishaji na ufafanuzi wa peo za kimazungumzo. Sehemu ya pili inaangazia mikakati ya kimazungumzo inayotokana na peo mahususi zilizoainishwa.

### 5.2 Peo za Kimazungumzo

Peo ni njia ya mkato ya utambuzi ambayo watumizi lugha hutumia kuweka wazi habari tata katika mazungumzo au mijadala yao. Peo huwasaidia watumizi lugha kufasiri ulimwengu wao na kuuwasilisha kwa wengine. Humsaidia mtumizi lugha kupanga matukio tata katika makundi yenye muwala na ya kueleweka. Kwa kutathmini uwasilishaji wa ujinsia miongoni mwa wazulufu, utafiti huu umefanikiwa katika kuweka wazi peo bainifu na ruwaza za kuzua peo hizo. Katika sehemu hii, mjadala wa ufafanuzi wa peo bainifu unaendelezwa. Uainishaji wa Kelly (2007) pamoja na Kaufman, Michael na Deborah (2003) ulitwaliwa kuibuka na msingi wa peo za kimazungumzo.

#### 5.2.1 Upeo wa Udharura

Upeo huu unazungukia mazungumzo ya ujinsia na swala la kujamiana miongoni mwa wazulufu kama jambo ambalo ni la kupendeza na lililo muhimu. Aidha linazua raha ya aina yake :

**<u>Dondoo 12: Tunukuzi kutoka Kikundi Kiini Shule A</u>**

MS020: In my opinion it is so normal with high schoolers wote tumeharibika and you see, maboi unaidemand sana. By the way Kama hutakuwa umemuonjesha tunda katika mwezi wa kwanza boy atakutema kama ugali moto” Mvulana anakulike kulingana na utamu na raha unayompa. You start unaona kama umekua unamature ushaskia mtu msee akiongelelea hiyo hutaki kuachwa nyuma we unataka tu umove vile world inamove not according to na morals zako vile zinasema. **<u>(Tzm Kiambatisho J Uk. 179)</u>**

**<u>Dondoo 13: Tunukuzi kutoka Kikundi Kiini Shule C</u>**

MS001C: Siku hizi ni hard sana kupata vajo. So me naweza taka yeyote tu. Ukisikiliza mnapochapiana stori za wasee utasikia ooh my friend is having sex and she is fine and why not me? Today everyone is doing it. Its the in-thing. My friend always tells me of how good it is.....how sweet it

is..... when will i know these things? Ni vibaya nikiwa mkarimu? I need some experience. **(Tzm Kiambatisho H Uk. 163)**

**Dondoo 14: Tunukuzi kutoka Kikundi Kiini Shule B**

"Hii mambo ya kufunga......., wengi tumefisia na kama jamaa hajawahi onja utamu...yaani kutumia kalamu yake---mmmm---ee en unaelewa--- yeye ni mshamba. Fala. He is not a man enough."manze gari ni testing. Utajua vipi fimbo yako iko chonjo? Tunda likiiva linaliwa mara that that otherwise lita.....(FGD SCH B) **(Tzm Kiambatisho I Uk. 169)**

Kama ilivyo katika nukuu hizo za vikundi viini, upeo huu wa udharura unatokana na uhitaji maalum ambao wazulufu wanauumba kimaksudi. Nukuu mbili za kwanza zinatokana na washiriki wasichana. Wanaumba udharura kutokana na haja ya wao kutoachwa na wapenzi wao wavulana- "Kama hutakuwa umemuonjesha tunda katika mwezi wa kwanza boy atakutema kama ugali moto.

Katika nukuu ya pili, binti mhusika amesawiri hali ambayo ni ya dharura- haja yake ya kutaka kushiriki utamu anaoelezewa na wenzake. Kwa hili, utafiti huu unaafikiana na ugunduzi wa Lesko (2001) kuwa wazulufu wana mwegemeo mkubwa kwa wenza wao. Inabainika kama ilivyo katika nukuu hiyo kuwa wazulufu hawajaepukana na hadaa za wenza na kuwa wanachama wa utamaduni wa wenza unaowajamiisha katika kaida zao. Katika nukuu ya tatu, mvulana mhusika anaumba taswira ya ushamba na unyimivu kwa kuwa bikira. Si swala la kuonewa fahari.

Kutokana na nukuu hizo inabainika kuwa wazulufu wanatumia peo ndogo zinazotokana na maneno ya kushiriki ngono, maneno yanayorejelea ladha, ukarimu na yale yanayorejelea chakula. Kwa mujibu wa maneno ya kujamiana, wazulufu hutumia maneno kama vile *kujackpo*t na *kukwachua*, *kupanda mbegu/kudunga* na *kutumia mbegu*, *kuhacth* na *kuzulu shamba la mfalme*. Maneno haya yanajenga na kukuza upeo huu wa udharura. Mvuto wa kushinda kwa mfano katika shindano la bahati nasibu (*rejelea Sportpesa, Betway, Pambazuka National Lottery nchini Kenya*) humshinikiza mshiriki kuwekeza fedha zake kwa upesi asifungiwe nje na makataa. Aidha, ili mshiriki katika shindano la bahati nasibu aweze kushinda, sharti ashiriki shindano.

Kimsingi kushiriki shindano huwa ni swala ambalo huibua hisia za kufurahisha na husababisha udharura wa kutaka kushiriki ili kushinda taji lililopo. Iwapo mchezaji atashinda, atatunukiwa na kufurahiwa na wenzake. Kushiriki kwa shindano katika muktadha wa utafiti huu

kunaambatanishwa na wazulufu kushiriki tendo la kujamiana. Upeo huu wa udharura ni maarufu miongoni mwa wavulana ambao wangependa kuthibitisha ubabedume wao kwa mujibu wa itikadi za kijamii ambapo wanafaa kuwa na uzoefu fulani. Aidha inaashiria uhodari wao. Ni bayana basi kuwa upeo huu unachukulia kuwa iwapo mvulana angali bikira, hana uzoefu na ndiposa anarejelewa kama *mshamba*. Ikizingatiwa huu ni wakati ambapo wazulufu wanatafuta mahali pao katika jamii, mvulana hangependa kutambulishwa kwa sifa za ushamba. Basi kutokana na hali hii anaridhia kuupoteza ubikira wake haraka iwezekanavyo.

Kutokana na upeo huu ujinsia wa wazulufu unasawiriwa kama mchezo unaoshirikishwa katika mahusiano yao kwa minajili ya ashiki na ridhaa. Taswira inayojengwa na upeo huu ni ya mtu ambaye amekomaa na hivyo basi kukuza ufasiri wa upeo huu. Uwepo wa maneno kama vile *kupanda, kudunga* na *kutumia mbegu* ni maneno yanayojenga na kuimarisha udharura wa kujamiana. Uelewa wa ujinsia wa wazulufu unafasirika kwa misingi ya kijamii na kidini kwa mujibu wa maneno haya. Kwa msingi wa kijamii, wazulufu wanajenga picha pana ya shamba ambapo mkulima sharti aandae shamba, apande, apalilie na hatimaye avune ili kuweza kukimu kizazi. Maneno haya yanakuza na kudumisha ile dhana ya umuhimu inayojibainisha katika nukuuu za vikundi viini. Basi kwa wazulufu ni muhimu kushiriki upanzi (kujamiana) ili kukimu (kuendeleza) kizazi. Uelewa wao wa kujamiana katika ujinsia ni kuwa ni swala muhimu. Upeo huu unatumika kuhalalisha matendo yao ya ujinsia. Ni muhimu kwa mkulima yeyote kupanda.

Aidha upeo huu unakuza dhana ya kimsingi ya upeo huu ya udharura ambapo mbegu (kiume/kike) zikikaa sana hazitakuwa na manufaa kwa ambavyo zitakuwa zimeharibika. Aidha shamba likiwa tayari na halitumiwi halitakuwa na manufaa yoyote. Kwa mujibu wa upeo huu, inabainika kuwa mvulana ndiye mkulima na msichana ndiye shamba na hapo kujenga, kukuza na kudumisha itikadi ya kimamlaka inayokuzwa katika jamii. Ni majuzi tu katika taifa la Kenya ambapo katiba imeipa jinsia ya kike nafasi kamili ya kumiliki ardhi. Katika jamii za Kiafrika na hususan nchini Kenya ambapo utafiti huu ulifanyika, kumiliki shamba ni ishara ya hadhi katika jamii. Vivyo hivyo, mvulana kumiliki au kuwa na mpenzi huenda kukaoanishwa na hadhi hii hususan miongoni mwa mahirimu.

Wingi au ukubwa wa shamba ni kitambulisho muhimu. Vivyo hivyo kwa mzulufu kuwa na mpenzi ni kitambulisho muhimu kinachompa hadhi katika jamii. Kuafikia hadhi hii, ni hali inayompa

mhusika ari na dharura ya kujitambulisha. Baada ya shamba kumilikiwa sharti kuwe na ithibati ya kuwa kuna kazi inayofanyika shambani humo. Hali hii inazua udharura wa kutaka kutumia shamba. Shamba nalo sharti lithibitishe kuwa kuna mavuno. Hali hii ndiyo inayopelekea uwepo wa mimba za mapema na ambazo wazulufu wengi hawazijali/hawazionei aibu. Ni kana kwamba ni ishara ya uwezo wa kuendeleza jamii na pia kuwa mhusika ana uzoefu. Shamba lina rutuba.

Kwa msingi wa kidini, wazulufu wamekopa, kutumia na kuhalalisha maneno mahususi yanayotumika kanisani. Katika makanisa ya Kikenya, usemi wa "*kupanda mbegu*" unatumiwa sana. Asili ya usemi huu imedokezwa katika kitabu kitakatifu ambapo kuna fumbo la mpanzi ambapo mpanzi anashauriwa kupanda mbugu zake katika shamba lililo na rutuba. Ingawa usemi huu umetumiwa na wahubiri kuwapunja waumini kwa misingi ya matoleo, usemi huu una ushawishi mkubwa. Mbali na hayo, wazulufu wameiga hali hii ya kupunjana kwa kupanda mbegu na kuweka wazi shamba kwa minajili ya upanzi. Hili linakuzwa na uwepo wa maneno yanayorejelea ukarimu kama vile *kupeana* (*pewa*), *kutenda* na *kutendewa* wema.

Wavulana ndio wanaopewa na hivyo basi huwa wameomba kuashiria kuwa wametendewa wema nao wakatenda wema. Maneno haya yanakuza upeo huu kwa ambavyo iwapo mtu ana uhitaji, kuna dharura ya kumsaidia na kusaidia ni muhimu katika maisha ya kila siku. Taswira inayojengeka kutokana na haya ni kuwa mvulana ana uhitaji (ashiki) ambao unamsababishia haja fulani na ambayo haina budi kutimizwa. Msichana naye ana uhitaji wa kugundua utamu na uzuri na kupata tajiriba. Kinachojitokeza hapa ni kule kuambatana kwa vitendo viwili vinavyozua ari ya udharura: kushiriki shindano na au kuwa na mbegu ambazo zinahitaji kupandwa. Maneno haya ya kitasfida yanahalalisha swala la kujamiana.

Kwa kuegemea hali ya kutenda na kutendewa wema, maneno haya yanatokana na ule usemi wa *"Tenda wema nenda zako"*. Kutokana na kiini cha upeo huu cha umuhimu, yeyote (mvulana au msichana) aweza kutenda au kutendewa wema. La mno katika maelezo ya maneno haya ni kule kutotarajia au kutoajibikia matokeo ya kutenda wema. Hali hii yaweza kulinganishwa na omba omba ambao huwepo katika barabara ambapo wasamaria wema huwatendea wema na kwenda zao. Nao wazulufu hufasiri tendo la kujamiana kama kutenda wema. Msichana ametendewa wema kwa kupewa mbegu ilhali mvulana ametenda wema kwa kupanda mbegu. Aidha mvulana ametendewa

wema kwa kupewa mahali pa kupanda mbegu naye msichana ametenda wema kwa kupeana shamba.

Swala la ni nani mwenye mamlaka linadhihirika hapa ambapo mwanamke anachukuliwa kama kifaa cha kutumiwa hali ambayo inajengwa na utofauti wa jinsi sehemu za ujinsia za wavulana na wasichana zinavyorejelewa. Nafasi ya msichana ingali duni. Upeo huu aidha waweza kuelezwa kwa kuegemea maneno yanayorejelea utamu/ladha. Iwapo kitu fulani ni kitamu, huvutia zaidi na huibua hamu ya haraka ya kutaka aidha kuonja au kukila. Hii ni hali ya udharura. Akilini mwa wazulufu na kutokana na wayasemayo, itikadi ya utamu imekuzwa na hivyo basi kuna udharura miongoni mwao wa kutaka kuonja na kuushiriki utamu huu. Matumizi ya maneno kama vile *asali*, *sugar plum* na kadhalika yanakuza fasiri hii na uelewa wa upeo wa udharura. Ni vigumu kutokuwa na hamu ya kuonja au kuila asali. Ugumu huu unatumika na wazulufu kutaka kuhalalisha sababu za wao kujamiana. Wanatoa taswira ya wao hawana la kufanya kwa ambavyo hamu ya kuonja au kula ni hamu ambayo haipo katika upeo wa uwezo wao. Ni kana kwamba wao ni wahasiriwa tu wa hamu hiyo na hivyo basi hawafai kulaumiwa.

Kwa upande ule mwingine, neno kula linatumika kitasfida kukuza upeo huu kuashiria tendo la kujamiana. Ilibainika ni wavulana ambao hula (mamlaka) na ndiposa wanawarejelea wapenzio kwa maneno kama vile *halua* ambayo ikishanunuliwa sharti iliwe kutokana na wepesi wake wa kuyeyuka. Mbali na hayo vinywaji kama vile sharubati havidumu sana na hivyo basi kuna udharura wa kuvitumia kabla ya vitu hivyo kuharibika. Swala hili linakuzwa na maneno yote yanayorejelea vyakula. Kutokana na maelezo ya upeo huu wa udharura, kushiriki tendo la kujamiana hueleweka kama tendo linalofurahiwa na lililo muhimu katika utambulisho wa wazulufu kama viumbe wanaosakwa, wanaotambuliwa na wengine kama wanaohitajika na kupendeka ili kupata hadhi ya kijamii.

Kulingana na Carpenter (2005), asili ya usawiri wa ujinsia kama waa kwa wanaume ni ubabedume wa kitamaduni, ambapo wanaume wanatarajiwa kuwa wajuzi na walio na tajiriba ya ngono Utumizi wa upeo huu ni bayana katika mazungumzo ya wazulufu ambapo wazulufu wanatambua na kukumbatia ujinsia wa wasichana kama hali inayowapa mamlaka. Hata hivyo, ni bayana kuwa upeo huu unawapa wavulana mamlaka kwa ambavyo hakuna ukosoaji wa kuhusu upendeleo wa kiume unaoendelea na kuwaona wasichana kama chombo. Wazulufu wanashadidia hali hii kwa

kuwasawiri wasichana kama vifaa. Upeo huu unawasilisha kujamiana kwa wazulufu kama hali ya kawaida na inayotarajiwa. Upeo huu unawathibitishia wazulufu kuwa hisia za kimapenzi ni sehemu ya utambulisho wao na kwamba kuashiria hamu zao za ashiki katika ujinsia ni swala muhimu. Imebainika kuwa kwa mujibu wa upeo huu kama inavyodhihirika katika ujinsia wa kuumeni hisia za kimapenzi za wavulana, zinakolezwa na kufasirika kama hisia za kawaida ikilinganishwa na hisia za kimapenzi za wasichana. Ugunduzi huu unalingana na ugunduzi wa Fine na McClelland (2006); Tolman (2005). Kulingana na mwanasoshiolojia Plummer (2003a), kushiriki ngono ni amali ya kuafikia na kuimarisha uume, basi upeo huu unahalalisha dhana za ashiki zinazokawaidisha na kuhalalisha vitendo vya kijinsia baina ya wazulufu.

**<u>Dondoo 15: Tunukuzi kutoka Kikundi Kiini Shule B</u>**

> MV020: Me siwezi tambua kaa ni vajo au sio vajo. Mwenye tu amekuja mwenye tu nimempenda ndio naoa si lazima ukuwe vajo juu obvious huwezi pata virgo. Wasee, si kila mtu anabonga kuhusu sex esp afta midi. Chali anakueleza alivyosikia utamu na wewe hata huna copy. Huwezi hata changia unakaa fala sana. Nauliza, Mafeelings humpanda mtu so mnataka ado? Why Ni vibaya nikiwa mkarimu? I need some experience kama chali na experience hii lazima niwe nimefinya manzi. **<u>(Tzm Kiambatisho I Uk. 170)</u>**

Kutokana na nukuu hii, udharura wa kupoteza ubikira unadhihirika. Kwanza kuna shinikizo linalotokana na kutaka kugundua uzuri unaozungumziwa na wenzao. Kauli hizi zinaambatana na kauli za tafiti nyingine kule Uholanzi ambapo wasichana wanajihisi kuwa katika njia panda kutokana na shinikizo la mahirimu la kujamiana na upande ule mwingine kutoshiriki. Uwili huu unaoana na ugunduzi kuwa jinsia ya kike kwa kiwango kikubwa hutambua ubikira wao kama "zawadi" ambayo yafaa kutwaliwa tu na mpenziwe (Carpenter, 2005). Kufasirika kwa ubikira hivi kunakuza upeo wa kujihini. Peo hizi zinakuza ile hali ya njia panda na uwili.

### 5.2.2 Upeo wa kujihini

Upeo huu unatawaliwa, kujengwa na kukuzwa na maneno yote ya kitasfida yanayorejelea usafi, udhalilishaji, utegemezi na maneno mahususi yanayoangazia sehemu za ujinsia kama kifaa ama gari. Upeo huu hutazama ujinsia na tendo la kujamiana kama tendo la uadilifu au ukosefu wa maadili (Kelly, 2007). Upeo huu umejengeka katika imani na mitazamo ya watu. Katika utafiti huu, ilibainika kuwa wazulufu hutumia mkakati wa uzungumzi wa "sisi" na "wao" ambapo kundi la "sisi" hujifasiri kichanya likijilinganisha na kundi la "wao". Ni kutokana na mgao wa aina hii amabapo kulizuka maneno yanayorejelea wazulufu ambao hawajashiriki tendo la ndoa kama walio

safi. Upeo huu unashirikisha mada za usafi na hadhi ya kutovunja ubikira na hatari za kimwili, kifikra na kijamii za kujamiana pamoja na matokeo hasi ya kujamiana.

Kwa misingi ya matokeo ya utafiti huu, waliozingatia maadili ya kujihini walitunukiwa maneno kama vile *Holy Jo, Mtoto, Mtoto/mtoi wa Pastor/pasi,priest, Mtakatifu, Priest/Pastor/bishop/Pope, Mtoto, Vajo, Holy Jo, Mary Mother of Jesus, Nun/Sister.* Maneno haya yanajenga upeo huu kutokana na misingi yake katika dini. Kimsingi hawa huchukuliwa kuwa watu walio na usafi wa kiwango fulani. Basi kutojamiana kunasawiriwa kama hali adilifu na kuzua dhana ya uchafu ambapo aliyeshiriki husawiriwa kama mtu asiye na maadili na hivyo basi ni mchafu. Kwa kuangazia maneno kama vile mtoto na mtoi, dhana ya kujini ni bayana kulingana na taswira iliyo akilini. Neno mtoto linaweka wazi upeo wa kitu ambacho hakina ujuzi au utaalamu, kina

Kwa kurejelea maneno ya udhalilishaji inabainika kuwa wazulufu licha ya kuwa na maneno chanya kwa walio bikira, kujihini hujitokeza kama swala ambalo limepitiwa na wakati. Ubikira kulingana na upeo huu hauthaminiwi na kushiriki ngono ni hali muhimu katika "ushindani" wa kijinsia ambapo wasichana wazulufu wanaonekana kuwa washiriki. Hali hii inakuza upeo wa udharura ambapo mzulufu angependa kuupoteza ubikira wake haraka iwezekanavyo. Wavulana ambao hawajajamiana hurejelewa kama *m(wa)shamba*, *outdated*, *fala*, *hustler*, *Mlalia masikio*. Maneno haya hukuza upeo wa kujihini kwa namna hasi. Neno "*ushamba*" katika muktadha wa taifa la Kenya ni ishara ya kutopevuka. Dhana hii inapata mashiko kwa kuwepo meneno ambatani kama vile *mlalia masikio*. Inaelekea kuwa kujihini hususan miongoni mwa wavulana sio swala la kuonewa fahari hali ambayo inakuza umuhimu wa kujamiana na kukuza upeo wa udharura. Iligunduliwa kuwa, kuwa bikira hakuimarishi usharifu wa mzulufu.

**<u>Dondoo 16: Tunukuzi kutoka Kikundi Kiini Shule A</u>**

> MS018: I agree with her it is impossible coz hata ukiskia hao watu wako in relationships wakiongelea kuhusu utaona tu at some point kuna part wanafika wanaplan about how to do it. Hii mambo ya kufunga, kuwa mchoyo na kujifanya nun ma msee wa CU ni pretence tu. Mtu anajifaaanya. Ni kuwa <u>m-hypo</u>. By the way in this school unaeza hesabu mavajo. Wengi tumepeana. Tumefunguliwa na kama hujawahi kaguliwa ulicho nacho yaani kuingiwa mmmm---ee en unaelewa----- wewe ni mchoyo, desperate. Nani hapa hajawahi ombwa? Sote ila tu labda may be hukupeana coz of fear. **<u>(Tzm Kiambatisho J Uk. 183)</u>**

Inabainika kuwa baadhi ya wazulufu wanafasiri hali ya kujihini kama unyanyapaa na hivyo basi unafaa kuvunjwa mapema na haraka iwezekanavyo. Kwa wazulufu wasichana kuna maneno kama vile *desperate, mama pima* na mengine. Kwa mujibu wa uelewa wa wazulufu, licha ya manufaa yanayotokana na kutojamiana, utumizi wa maneno kama haya unasababisha udharura, haja na hamu ya kutaka kuvunja ubikira ili kupata utambulisho chanya miongoni mwa wazulufu. Neno mama pima ni neno linalotumika katika muktadha wa sokoni nchini Kenya hususan katika vibanda ambapo mnunuzi hupimiwa anachotaka kununua. Wazulufu wanatumia maneno kama haya ili kuimarisha na kujitetea kwa nini wanashiriki ngono za mapema. Jina ni muhimu kwa mtu na jinsi arejelewavyo mtu huathiri pakubwa maamuzi na matendo yake. Hata hivyo inabainika kuwa wale ambao wameshiriki aidha wanarejelewa kwa maneno hasi: *tastless*, *poko*, *malaya* n.k. hali hii inakuza haja ya binti kusalia bikira. Aidha inabainika ni jukumu la msichana kuwa mwangalifu.

**Dondoo 17: Tunukuzi kutoka Kikundi Kiini Shule A**

> MS014: Me I prefer the pregnancy part coz these days unaweza kaenda these days you just do away with it and it's over as in with the pregnancy you can go and abort but with the HIV and STI there is no way we are going to come out of that. Ingawa hakuna lolote baya na girls having boyfriends, ni jukumu langu kujijua.....am still in school na kama nitakuwa capital D, mvulana atakitoa na kuniacha kwenye mataa. So you will just have to drop out of school and you know... "Mahitaji ya uzazi ni kibao- chakula, nguo, hospitali nitatoa wapi. Wazazi nao they can even disown you. Utaenda wapi? Aibu kutoka kwa marafiki. Dunia itakucheka. If i accidentally get pregnant i will just have an abortion. Hii ni kama kutema mate au kikohozi. I better die nikitema kuliko kuchekwa na mabeshete kuwa sijui kujipanga. **(Tzm Kiambatisho J Uk. 184)**

Inabainika kutokana na nukuu hiyo, kuwa waa unaotokana na ujauzito waweza kumfanya binti akataka kusalia bikira. Upeo huu unaweka wazi upeo wa kushughulikia hali ya ujauzito ikitokea. Kwa wazulufu, kuavya mimba ni kama kutema mate au kutoa kikohozi. Taswira pana inayotokea hapa ni kuwa ujauzito ambao haukupangiwa ni kama kikohozi ambacho mja hakai nacho na ni jambo la kawaida. Kwanza wazulufu wasichana wanahalalisha haja ya wao kuwa katika uhusiano kwa ambavyo hakuna kosa lolote na ni hitaji la kimsingi la mwanadamu. Katika kuhalalisha hilo, mzulufu anatambua jukumu lake la kujilinda kutokana na hatari za kupeana tunda. Ugunduzi huu ni sawia na ugunduzi wa Alexander na Terri (2003), Jackson na Cram (2003), Sakaluk, Todd, Milhausen, na Lachowsky (2014), Sakaluk na Milhausen (2012) na Wiederman (2005) waliotambulisha jukumu hili kama jukumu mahususi la msichana. Kulingana na nukuu hiyo, mvulana amesawiriwa kama mtu ambaye atamwacha mwenzake kwenye mataa na kutoajibika. Ili

kuepukana na kuachwa kwenye mataa, inamlazimu msichana "kujipanga". Baadhi ya wavulana hata hivyo walikiri wangeweza kukubali matokeo na hapo kuzua tofauti za kijinsia katika mikakati ya kushughulikia mimba za mapema:

**<u>Dondoo 18: Tunukuzi kutoka Kikundi Kiini Shule B</u>**

> Kwanza aisee nitajisikia fiti sana. I am a man bwana na nafeel proud. Imagine ninakaphotocopy kamine mahali. Nilipanda mbegu na ikaota. Sikutupa mbegu: I feel like a hero. A real man". Tutanego kama atakaa na mtoto ama mimi ndio nitakaa na mtoto juu unajua tukifika hiyo decision ya kuhave sex tupate mtoi obvious nilikuwa naitake it serious na yeye kabisa. So kaa saa hizi point yangu ni hii akiweza pata ball na ilikuwa ni willing kabisa sa nilikuwa nataka **kumtafuna** akapata ball tuseme hatukujiprotect vizuuuri sa hapo ndio pahali penye itabidi umeambia paro afanye kenye atafanya. **<u>(Tzm Kiambatisho I Uk. 167)</u>**

Kwa mujibu wa nukuu hiyo, usharifu wa mvulana ni ya juu. Inabainika wao hawazingatii sana kitakachosemwa kihasi bali ithibati ya kwamba yeye amethibitisha kuwa ni mwanamume. Hali hii ni muhimu katika kuumba utambulisho wa vijana wazulufu. Wao wanajionea fahari ilhali wasichana wanaibuka na hisi za aibu na kuwa wachafu. Kauli hii inawiana na kauli za Sprecher, Barbee, na Schwartz (1995), Sprecher na Regan (1996), Lindisfarne (1994); Schwartz na Laws (1977) waliodai kuwa mahirimu wa kiume huhimiza wanachama wake katika ushindani wa mahusiano na kushabikia mafanikio. Hii ni tofauti na makundi ya mahirimu wasichana ambao hawatambui kufungwa bao au hata hali ya kuwa na wapenzi wengi kama mafanikio kwa wenzao. Utambuzi unaotokana na upeo huu unaweka wazi uhalisia wa maisha uliopo kuwa, hata kama kuna mabadiliko ya kijamii kuhusu ujinsia, sheria zinambana binti kuliko zinavyombana mvulana. Wasichana wenyewe kama ilivyo kwa jamii wanajiona kama "*loosers*" na hivyo wanalazimika kujihini na kutokuwa na marafiki wengi wanaoshiriki nao ujinsia. Kwa upande wa pili, wavulana wanashangiliwa na kupewa uhuru pamoja na kushinikizwa kujibaini.

Aidha, upeo wa kujihini unafasirika kimaadili kuwili: namna chanya na namna hasi. Kwanza kwa wazulufu wawe wavulana au wasichana kuwa bikira ni ishara ya usafi. Hali hii imekuzwa na mafunzo ya kidini na matarajio ya wanajamii. Kwa makundi yote mawili kuna maneno chanya yanayoashiria hali hii. Licha ya misukosuko ya mpito wa wakati na ujio wa usasa ambapo kujihini hakuthaminiwi sana, imetambulika kuwa kungali na maneno chanya ya walio bikira. Wanalinganishwa na *utakatifu*, *Maria mama wa kanisa*, *Askofu*, *Kadinali* hata *Papa*. Taswira itokanayo na utumizi wa maneno haya ni ya watu walio na ushawishi na wanaoenziwa sana katika

jamii. Utumizi wa maneno haya basi unakuza upeo wa kujihini ikizingatiwa kuwa wazulufu wanatafuta utanbulisho wao na basi kurejelewa kichanya kwa maneno hayo yanayoibua staha katika jamii kunaimarisha usharifu wa mzulufu.

Ikirejelewa neno *Maria mama wa Kanisa*, swala la maadili ya imani ni bayana. Aidha kwa wanaoshiriki Imani ya Kikatoliki huyu ni mtu aliyetawazwa na kupewa mamlaka ya kuwa mama wa Mkombozi. Ana staha na hadhi kuu. Basi binti ambaye ni bikira anachukuliwa kuwa na hadhi, mtu aliye na msimamo na ambaye hajakengeuka. Kwa msingi wa upeo huu, wazulufu inabainika wanaweka mgao kwa kuamua kuzua kategoria za maamuzi "mazuri" na "mabaya". Kwa kuumba ubikira kama uakisi wa mtu binafsi ni sifa ya jinsi tabia na matendo ya msichana husababisha maamuzi na hukumu ya kijamii kuhusu utu na tabia yake. Mtazamo huu unajenga taswira ya kujihini kama hali iliyo na manufaa. Iwapo jamii haitamsuta mhusika atakuwa amefaidi kimawazo na kwa msingi huu usharifu wake unaimarika. Ikizingatiwa kuwa wazulufu wapo katika jamii, ni bayana kutambua umuhimu wanaoambatisha kwa jinsi wanajamii wanavyowarejelea.

Kuwa bikira miongoni mwa wazulufu kunatazamwa kama hali iliyopitwa na wakati (`it's practically not in fashion to be a virgin leo no matter what the society says and thinks. It doesn't feel cool`*)*. Kutokana na kauli hiyo, ni bayana kuwa ngono inafasirika na wazulufu kama hali '*cool*', na hivyo basi walio bikira au wanaojihini wanakejeliwa. Ni *washamba*, *wanaogopa sweet life* kama wavulana wanavyowarejelea. Kutokana na hili wengi wanashiriki ngono ili kukubalika katika jamii ya wazulufu. Kwa mujibu wa wazulufu, kuvunja ubikira ni hatua ambayo kwayo wazulufu wanaingizwa katika kundi la wajuzi, wasawa, *expert* na *pro*.

**Dondoo 19: Tunukuzi kutoka Kikundi Kiini Shule A**

> MS020: Si hali ya kujivunia kuwa bikira. Singependa. Huna lolote linalokujumuisha na wenzako..... Huna ujuzi wowote wa maisha. Wanafunzi wa umri wako asilimia 90 na kwenda juu, wakati wa sasa wanapeana. Wana hata namna za kujikinga na ikiwa mbaya wanatema. It's practically not in fashion to be a virgin leo.It doesn't feel cool. So kulingana nami a virgin is not valued at this age and people do not want to be virgins because boys want people who have tried things people who have tried this and that but I think later in life people realize that being a virgin was actually better but saa hizi students think not being a virgin is the best thing. Its being insyc. Cool. **(Tzm Kiambatisho J Uk. 196)**

Utambuzi kuwa wavulana ambao wana ufahamu na ujuzi wa kujamiana wanatambuliwa kama magwiji lakini hakuna neno chanya la msichana ni ubayana wa namna mbili/viwango viwili vya

taswira ya ubikira katika jamii. Inaelekea wavulana wanasifiwa ilhali wasichana wanadunishwa na kupewa hadhi ya chini. Kutokana na maneno yaliyotumika, utofauti huu unakuzwa na kuendelezwa katika jamii ya wazulufu na jinsia zote mbili. Wasichana wanawaita wenzao *poko* kama wavulana wanavyowaita. Kutokana na hili, wasichana kwa kujua au kutojua wanalazimika kuchukua nafasi ya kuamua dira ya mahusiano yao. Upeo huu unazua dhana ya sifa na mtazamo wa wazulufu unaowasilishwa kama tahmini chanya na hasi kuakisi mtu binafsi kama anavyotazamwa na wengine. Maamuzi ya kushiriki ngono au kutoshiriki ngono kimsingi inadhihirika huambatana na utata wa kimaadili na kimaamuzi unaosababisha mtazamo wa chema na kibaya. ingawa mtanziko na utata huu unaathiriwa na nguvu za nje, maamuzi yanaonekana ishara ya maadili ambayo wazulufu wanayo na kama vipimo vya ukuaji wao binafsi.

### 5.2.3 Upeo wa Mamlaka

Upeo huu humfaa mtu katika kuamua ni mamlaka yepi yaliyo halali na yale ambayo yanaweza kukuza nafasi yake. Kuelewa na kupambanua upeo huu na jinsi unavyotumika na wazuluufu ni vema kuangazia mamlaka na udhibiti walio nao wavulana. Kwanza udhibiti wa kiwango cha kwanza ni udhibiti wa akili yaani imani za wasichana na udhibiti wa vitendo vyao kwa misingi ya imani hadaifu. Ili kuakisi udhibiti huu, wavulana kwanza lazima watimize masharti ya kibinafsi na kijamii ili kuweza kuwashawishi wengine. Kwa mujibu wa utafiti huu, peo za mamlaka zilijibainisha kupitia maneno yanaoyohusiana na uzani, vifaa, stakabadhi, taasisi, umashuhuri, thamani, utukufu na weledi.

Tasfida zilizobainika katika maneno ya wazulufu zinasisitiza utumikizi au utenda kazi kuliko maadili. Upeo huu unaegemea jinsi tendo hutekelezwa zaidi ya dhana za utu na kijamii. Kwa kuegemea dhana ya vifaa, wavulana ilibainika kuwa wana mamlaka dhidi ya wasichana. Kwa kuangazia urejelezi wa sehemu za ujinsia, sehemu za uume zilirejelewa kwa maneno kama vile *nyundo, fimbo ya nyayo*, *transformer*, *booster* na mengine. Hii ni mifano inayoashiria mamlaka walio nayo wavulana kwa wasichana. Katika historia ya Kenya, Raisi wa pili wa taifa alitumia fimbo kama ishara ya mamlaka yake. Katika hafla zote rasmi alikuwa na fimbo hiyo. Aidha wakati wa wimbo wa taifa aliinyosha juu. Kwa mujibu wa utafiti huu, hii inaashiria udhabiti wa sehemu hii katika kutekeleza wajibu wake. Aidha inaweka bayana taswira ya sehemu hiyo ambapo mvulana amepatwa na ashiki.

Kama walivyodai Kaufman, Michael, & Deborah (2003) kuwa "Peo ni njia za mkato ambazo watu hutumia kufahamu na kuelewa habari tata. Huwasaidia wanadamu kuufasiri ulimwengu unaowazunguka na kuuwakilisha kwa wengine". Mintarafu ya maelezo haya na kwa mujibu wa upeo wa mamlaka, wazulufu wanatumia njia ya mkato ya vifaa ambavyo vinaweza kurejelewa hadharani ili kuumba hali ya ashiki kuwa zimemshika mvulana. Kwa wepesi wanawakilisha swala hili kwa wenzao pasi kukiuka kaida za kimazungumzo katika jamii.

Hali hii inaambatana na utumizi wa maneno mengine kama vile *kuchapwa miti*. Maneno haya yanaashiria kuwa ni mvulana aliye na mti na mti huo unatumika kumchapa msichana. Haya ni maneno ya kitasfida yanayoashiria tendo la ndoa. Kawaida anayemchapa mwingine huwa na mamlaka juu yake. Hali hii inawasawiri wasichana kama watu hafifu. Kukuza hili, sehemu za uke zimerejerelewa kama milango. Hali hii inaakisi zaidi utumikizi wa sehemu hiyo kama kitu kinachoweza kufungwa au kufunguliwa. Inaweza kudaiwa kuwa kutokana na mmiliki kuamua kufunga au kufungua ana mamlaka dhidi ya anayetaka kuingia na ataingia tu iwapo ataruhusiwa.

Hata hivyo, upeo huu unamkuza msichana kama mpokezi tu ambaye kazi yake ni kufungua mlango, mtu anaingia na kutoka. Maneno mengi wanayoyatumia katika uwasilishaji wa ujinsia yanazungukia wanchowatendea wazulufu wasichana. Wazulufu wasichana wanachukuliwa kama vifaa vya kutosheleza ashiki za kingono za wavulana. Ni vifaa ambavyo sharti vitumiwe lakini vizisikike. Huu ni unyanyasaji na ni mtazamo wa kimsingi unaoshikiliwa na jamii kuhusu jinsia ya kike. Wazulufu wanajipata ndani ya unyanyasaji huo. Matokeo haya yanakubaliana na madai ya Armstrong, Hamilton na Seeley (2014), Andrew (2012), Attwood (2006) na Bell (2012) kuwa miili ya wanawake wakiwemo wasichana wazulufu husawiriwa kitamaduni kama watendwa (passively) wasionyesha hisia na kudunishwa. Wasichana wazulufu wanaokinai mtazamo huu na kukataa hadaa za wavulana wanakejeliwa kama utafiti huu ulivyogundua katika nukuu hii ya mazungumzo katika mojawapo wa vikundi viini:

**<u>Dondoo 20: Tunukuzi kutoka Kikundi Kiini Shule C</u>**

> *MV001C:* Haya wacha niongee kulingana na group ya wasee wengi kusema ukweli wasichana kuna kitu moja mnajidanganyaga wacha nikuambie ukatae sex ulose chali unaona? Kitu ya kwanza inakuaga hivyo. unajua sikia vile inaendaga yaani kaa punda ilikataa na nyama, ngozi na maziwa cheki saa vile inapigwa viboko, unaona? So dem usijifanye punda tafadhali. Unakataa chali wa kwanza juu ametaka sex na wewe utakataa wa kwanza. Age imeadvance na unaona unakataa sex juu unaona chali atakulose na maybe uko 30 years. Chali anatakaga kitu inaitwa road test (kicheko). Wacha nigonge nyoka kwa kichwa sasa lazima chali before akuoe lazima alale na wewe ndio afeel

> game yako iko aje unaona? Vile game yako iko kwa bed unaweza mlekaje unaona? So ni chali alale na wewe ndio ajue huyu amequalify kuwa wife material game yake iko aje unaona? So madem acheni kujidanganya eti kuwa pure. Kuwa pure uzeeke kwenu. **(Tzm Kiambatisho H Uk. 162)**

Mbali na hayo ikilinganishwa na kifaa kama *bazuka* au *transfoma*, hivyo ni vifaa ambavyo vinampa mvulana mamlaka zaidi. Maelezo zaidi ya upeo huu kwa mujibu wa tasfida zinazotumika ni kwa misingi ya ukawaida wa vifaa ambavyo vimetumika kurejelea sehemu hizo. Wazulufu wanatumia vifaa vya kawaida kuhalalisha matendo yao. Inabainika ni vifaa vinavyorejelewa au vinavyozungumziwa wakati mwingi na kwa ukawaida mkubwa. Kwa misingi hiyo, inafasirika kuwa ni tendo la kawaida kumfungulia mtu mlango. Ni heshima kubwa inayotunukiwa mtu au hata aliye na mamlaka. Walinzi wa watu mashuhuri huwafungulia milango kwenye magari yanayowabeba. Mlango ule haufunguliwi mtu yeyote. Na ikizingatiwa mahusiano ya kimapenzi ni heshima kumfungulia mtu mlango. Wazulufu wanatumia hali ya kufunga na kufungua mlango kitasfida kuashiria uhalali wa wao kujamiana. Ni jambo la kawaida na la kila siku. Ugunduzi huu unaweza kufafanua ni kwa nini ngono za mapema zimekithiri kutokana na uhalisia wa kuwa hakuna lolote baya katika kumfungulia mja mlango. Ingawa inabainika mfunguzi wa mlango huenda akawa na mamlaka, kimatumizi anayeingia ndiye mwenye mamlaka zaidi.

Ufunguzi wa mlango unaambatana na upeo mdogo wa *kasri* ambapo tendo la kujamiana hurejelewa kama kuzuru shamba au kasri ya mfalme. Mvulana ndiye anayezuru. Ndiye anaingia kwenye kasiri. Ndiye mfalme. Kwa kuwepo maneno kama haya upeo huu unakuza dhana ya mamlaka ya mvulana dhidi ya msichana. Kasiri hata likiwa zuri vipi, hupata umaarufu kutokana na mfalme anayeishi pale. Basi msichana anachukuliwa tu kama bawabu mlinda kasiri (mlango) ambapo mfalme akitaka kuzuru sharti afunguliwe mlango. Mfalme ndiye mmiliki wa shamba. Yeye ndiye anayelima. Binti ni shamba tu. Inabainika kuwa msichana analinganishwa na shamba ambalo sharti limilikiwe. Mmiliki ana uhuru wa kuamua cha kufanya na shamba hilo.

Taswira inayojitokeza inakuzwa na utumizi wa maneno kama vile *kusoma kitabu* ambayo kimsingi ni fumbo. Wazulufu wanafumba tendo la kujamiana. Ili kitabu kisomwe sharti kifunguliwe hali inayoambatana na ufunguzi wa mlango. Kitabu hata kikiwepo, lazima anayetaka kukisoma akifungue. Hapa dhana hii inatumika kuashiria maandalizi ambayo wazulufu wanayafanya ili kujamiana. Upeo huu unakuzwa kwa kuwepo maneno yanayorejelea sehemu za ujinsia kama stakabadhi. Wazulufu wanatumia maneno kama vile katiba kimafumbo kusitiri matendo yao.

Katiba ni sheria zinazotawala taifa fulani na kiongozi awaye yeyote yule hukiri na kuapa kuilinda katiba hiyo. Aidha humpa mwongozo wa atakavyotawala. Utumizi wa mamlaka kama haya unakuza mkakati wa kimazungumzo wa mamlaka ambapo wazulufu wanaweza kutetea matendo yao kwa kurejelea katiba. Ni iyo hiyo katiba inayowapa haki za kibinadamu. Aidha hakuna kosa lolote kusoma katiba ili kuelewa jinsi taifa linavyostahili kuongozwa na kutambua haki za mhusika kama mwananchi. Wazulufu wanatumia upeo huu na mkakati huu kuhalalisha vitendo vyao kwa ambavyo swala la kusoma ni swala la kawaida sana. Aidha ili mtu awe mtu katika jamii lazima awe na maarifa. Maarifa haya huibuka kutokana na tajriba. Tajiriba ya mapenzi inapatikana kutokana na kuzuru shamba hivyo basi mja anaweza kulima na kupata mavuno.

Kwa kuzingatia maneno yanayorejelea weledi, ni bayana kuwa wavulana wana mamlaka kuliko wasichana. Hali hii inaambatana na ufafanuzi wa Kaufman, Michael na Deborah (2003) kuwa upeo wa mamlaka husaidia wahusika kutambua mamlaka yaliyo halali pamoja na aina za mamlaka ambazo zinaweza kuendeleza nafasi ya mtu kama vile nguvu, rasilimali na ujuzi. Inabainika kuwa wazulufu wanarejelewa kwa maneno kama vile *striker*, *player*, *pro* na *expert* (Ujuzi na nguvu fulani). Maneno haya kwa pamoja humpa mtu mamlaka dhidi ya wengine. Inabainika kuwa wazulufu wanauumba upeo huu na kuutumia kuhalalisha ubinafsi, kushawishi umma, na kuelekeza kwa upendelevu wa matokeo fulani mahususi. Ni uhalisia wa kijamii kuwa wengi hupenda au hutaka kuoanishwa na walio na ujuzi fulani katika shughuli mbali mbali. Wazulufu hujitambulisha na wanasoka watajika, magari ya kifahari au hata watu maarufu.

Kwa kutumia maneno yanaoyokuza upeo huu wa mamlaka na kuyaegemeza kwenye umaarufu katika michezo, wazulufu wanafasiri swala nzima la ujinsia kama mchezo au spoti ya aina fulani. Kwa misingi ya ufasiri wa ujinsia kama spoti, wachezaji ambao wana ushawishi mkubwa hata kwenye klabu ni washambulizi. Hawa huwa na jukumu la kufunga mabao. Ndiposa mvulana akifunga bao (amempachika binti mimba), yeye ni maarufu, anaenziwa na wenzake. Katika hali za michezo hiki ndicho kilele cha mchezaji. Ingawa neno *player* ni neno hasi likionekana, kwa wazulufu ni neno chanya. Kwamba mhusika anaweza kumcheza au kuwacheza wapenzi wenzake. Ana uwezo wa kuwa na wapenzi wengi kwa wakati mmoja. Anayemiliki sifa hii hususan kwa wavulana ana mamlaka zaidi. Kwa mujibu wa hili, wazulufu wanahalalisha hali ya mtu mmoja kuwa na wapenzi wengi kwa wakati mmoja. Hii ni hali inayoungwa na kauli kama vile hakuna

jogoo wa mwera mmoja au chakula kile kile huchosha na kabla uamue chakula ukipendacho huna budi kuonja vyakula vingi.

**Dondoo 21: Tunukuzi kutoka Kikundi Kiini Shule C**

> MV001C: So unapata maswali zingine for example boy anakuuliza ukiweza pata girlfriend mmoja ama in future ukiweza oa unaweza kuwa faithful kwa bibi mmoja? Kwanza answer ni **No, yeah because wanasemaga hakuna jogoo ya kuku moja unaona**? (kicheko)**Huwezi kula chakula moja every now and then na ukose kulose appetite. So you have to change the diet.** Of course boys huwa wanaongea mambo mengi kama watakuambia shape ya madem; dem mnono huwa anakuaga aje, dem mkonde mrefu huwa anakaaga aje unaona? A man must not eat only vegetable. In the Bible Solomon alikuwa vipi? Si alikuwa na wengi? Unaona? **(Tzm Kiambatisho H Uk. 157)**

Kauli hii inaungwa mkono na sehemu ya dondoo la 3 kiambatisho H uk 156: So lazima udanganye madem uwaingize box wakishaingia kwa box yako ujifunze na wao vile game itakuwa inachezwa ndio sometimes in future ukiingia kwa game bibi yako atakuwa anashindwa na huyu alifunzwa na nani unaona?

Kulikuwa na urejelezi wa kimamlaka ambapo wazulufu waliwataja watu maarufu kama vile Suleimani kwenye Bibilia. Basi kwa mujibu wa upeo huu mvulana ana mamlaka na si vibaya kwake kuwa na wapenzi wengi. Kwa msichana dhana ya uhafifu inajitokeza. Bado amefungwa kwenye minyororo ya utamaduni. Kitamaduni, ni swala baya na la ukosefu wa maadili kwa binti kuwa na wapenzi wawili au hata zaidi kwa wakati mmoja. Hali hii inafafanua kwa nini uweledi wa msichana haufasiriki kwa misingi ya idadi ya wapenzi au mara alizojamiana hali inayomkosesha mamlaka akilinganishwa na mvulana. Kama ilidhihirika katika utafiti huu, hakuna maneno chanya yanayomrejelea msichana ambaye ana ujuzi wa ujinsia.

Maneno ya kiutukufu kama vile *prince*, *gavana*, *mfalme*, *malkia*, *his/her excellency*, *malaika* pamoja na maneno ya thamani kama vile *future*, *potential* na *past* ni maneno yanayojenga upeo huu. Maneno haya yanaibua dhana ya ni nani aliye na ushawishi na yanakuza dhana ya mamlaka kwa misingi ya jinsia. Mfalme ana mamlaka kuliko malkia na ndiposa malkia hufungua mlango mfalme ajapo. Aidha mfalme anapotaka kulima shamba sharti shamba liwe tayari. Basi hali ya msichana kuchukuliwa kama mshiriki tendi inatokana na maelezo ya ni nani aliye na mamlaka zaidi ya mwingine. Kwa kuangazia neno malaika, ni bayana kuwa malaika wana mamlaka kuliko viumbe walio chini yao. Kwa misingi hii basi, mvulana anachukuliwa kuwa na mamlaka zaidi na ndiposa ana uhuru wa hata kuwa na wapenzi wengi. La muhimu ni jinsi ambavyo jinsia moja huweza kutumia upeo huu kwa manufaa ya kibinafsi.

Kulingana na utafiti huu, ni bayana kuwa dhana ya wavulana kujinufaisha kwa njia za kilaghai hakuhusishi tu mamlaka bali pia utawala ambapo wanatumia nafasi zao vibaya. Kulingana na van Djik (2005; 2006) hadaa huashiria utumikizi wa ushawishi usio halali kwa njia ya usemi. Hili ni swala linalojidhihirisha katika mazungumzo ya ujinsia baina ya wazulufu. Inabainika kuwa wavulana ni kama walaghai wanaowahandaa wasichana kuamini na kutenda/kutekeleza matendo ambayo ni kwa manufaa ya wavulana. Ugunduzi huu unaambatana na ugunduzi wa watalamu wengine kama vile Blackledge (2005), Chouliaraki (2005), Martín na van Djik (1997) katika tafiti zao za usemi na uhalalishaji wa maswala mengine katika jamii kama vile vita.

Kwa misingi ya utafiti huu upeo huu wa mamlaka unatumika kushawishi na vile vile kuhandaa. Maelezo haya yanaafikiana na tafiti za O'Keefe (2002) Dillard na Shen (2012) kuhusu ushawishi. Inabainika wazulufu wavulana wanawashawishi wenzao wa kike kuwafungulia mlango kwa kuwaita maneno matamu na kuambatanisha na usemi wa kutenda wema ambapo kwa pamoja watakuwa wametendeana wema. Utumizi wa usemi huu unahalalisha mahusiano hayo na kuwaondolea wazulufu lawama. Upeo huu unaungwa mkono na dhana za utu uzima ambapo wazulufu wanadai kuwa wamekuwa watu wazima walio na haki zao pamoja na uwezo wa kujiamulia maishani.

Dhana nyingine ni ile ya maadili na uamuzi wa wazulufu katika kushughulikia shinikizo la kujamiiana na shughuli nyingine za ngono. Dhana hii kama ilivyobainika inasisitiza mtanziko na utata wa kichaguzi walio nao kama nafasi ya kufanya maamuzi sahihi ya kibinafsi na hapo kuashiria ukuaji wao. Wanaofaidi zaidi ni wavulana na hapo kuweka wazi tofauti iliyopo baina ya hadaa na ushawishi. Katika ushawishi unaodhihirika hapa, wazulufu wanaridhia na wako huru kuamini na kutenda wapendavyo iwe wanakubaliana au hawakubaliani na kauli za mshawishi. Hata hivyo ni muhimu kuangazia jinsi upeo huu unavyochagiza hadaa zaidi ya ushawishi. Katika kuhadaa, wanaohadaiwa hupewa nafasi na jukumu duni: ni waathiriwa wa hadaa. Uhasi huu katika upeo huu ni mbinu waitumiayo wavulana dhidi ya wasichana ambao kutokana na kushawishiwa wanakosa kuelewa bayana nia halisi na au kutambua matokeo halisi ya imani na vitendo vya wavulana. Hili hutokea ambapo wasichana hawana namna bayana ya kustahimili hadaa za vijana.

Katika utafiti huu, ilibainika wavulana wamekuza ubabe dume wao (Taga, 2003); (Petersen, 2003) na (Morrell & Swart, 2005). Aidha wasichana wamesawiriwa kama wahusika wasio na uwezo. Mbali na hayo wamepewa majina yenye staha katika jamii. Kwa msingi huu utafti huu unatambua masharti ya kijamii kwa mujibu wa uwanachama katika kundi mahususi, weledi au ujuzi pamoja na amali zinazoashiria uwezo wa makundi na wanachama wavyo. Wavulana basi wanawahadaa wasichana kwa misingi ya upeo wa mamlaka kupitia nafasi waliopewa na jamii na mamlaka yao. Hata hivyo, si kwamba wasichana hawawezi kuwahadaa wavulana, hili hata hivyo halitokani na nafasi yao lakini kama namna ya  uasi kwa misingi ya tabia za kibinafsi. Matokeo ya utafiti huu yamebainisha kuwa wazulufu wanautumia upeo huu kuhalalisha matendo yao ya kushiriki ngono za mapema. Matumizi ya upeo huu yanaakisi na kuweka bayana mamlaka aliyo nayo mvulana dhidi  ya msichana na kuumba taswira kuu ya: mvulana kama mshiriki tendi anayemsaka binti, anayetafuta uhusiano wa kimapenzi na anayetafuta ukubalifu wa msichana ingawa msichana anashiriki mahusiano haya ili tu kudumisha uhusiano wa kihisia na wa kimapenzi.

Utambuzi wa uwepo wa upeo huu na utumizi wake katika mazungumzo ya wazulufu ni dhihirisho la majukumu ya jadi ya kijinsia na mila kuhusu mapenzi ambapo yalielezewa kwa njia ya maandishi na hadithi ambazo zilisisitiza uongozi wa kiume na utendaji wa kijinsia usiosawa. Uongozi wa kiume ni maonyesho ya mamlaka au nguvu ambazo wavulana wanazo dhidi ya wasichana, wakati utendaji wa kijinsia unaohusisha jinsia unaibusha dhana ya kawaida ya uume na uke. Wakati uume unahusishwa na nguvu za kimwili, uthibiti wa kihisia, ulinzi wa mwanamke, na kutozingatia maadili, uke unahusishwa na mazingira magumu ya udhaifu wa kihisia, udhaifu wa kimwili, haja ya kuwalea wengine, na tabia ya kukomaa zaidi na uzingatiifu wa maadili.

### 5.2.4 Upeo wa Uanishaji na Utambulisho

Upeo huu hutawaliwa na mazungumzo yanayowasawiri washiriki katika mawasiliano kama washiriki wanaojiainisha au kujitambulisha kama washiriki walio na sifa mahususi zinazotakana na mtazamo wa mtu binafsi na uhusiano na kundi. Vile vile washiriki huwatazama wengine kama walio na sifa fulani mahususi zilizo karibu na au zinazohusiana na mawazoganda. Sifa hizo zaweza kuwa hasi au chanya. Lengo la upeo huu kimsingi huwa ni kudhoofisha uhalali wa wengine na nafasi yao. Mbali na hayo upeo huu huwa muhimu katika kukuza dhana ya mkakati wa uzungumzaji wa “sisi” na “wao”.

Katika utafiti huu, iligunduliwa kwamba wazulufu waweza kujitambulisha au hutambuliwa kama *player*(*s*), *striker*, *holy jo*, *pasi*, *kadinali*, *mshamba*, *fala prince charming*, *chick*, *mtoto*, "*momo"*, *gari kubwa 1* na *8 GB* n.k. Kwa misingi ya utambulisho huu, uainishaji unajitokeza bayana. Ambao hawajashiriki tendo la ndoa hurejelewa na walioshiriki kama *fala* na *washamba*. Uanishaji na utambulisho huu unanuiwa kudidimisha umuhimu wa ubikira. Kuwa bikira ni swala linalofaa kuonewa fahari na hivyo basi waliovunja ubikira wao wanataka kukweza hali yao ili isionekane kama hali mbaya kutokana na misuto ya kijamii na madhara yanayoweza kutokea. Kwa upande ule mwingine, ambao ni bikira wanajiona au wanatambulishwa kama *holy jo*, *mtoto, pasta*, *mama wa kanisa* n.k. Linalojitokeza bayana ni ule mgao wa "sisi" na "wao" ambao kila kundi linajotambulisha kwa kujianisha kwa kuwa na sifa fulani.

Kwa mujibu wa maelezo ya upeo huu, sifa zaweza kuwa chanya au hasi kutegemea uhusika katika kundi fulani. Ili kuwasawiri waliovunja ubikira kama *striker* (utambulisho) lazima kuwe na sifa chanya kama vile uwezo wa kufunga mabao na kwa wepesi. Ni mhusika anayetambua nafasi kwa haraka na kuitumia. Kutokana na hili ambao hawajavunja ubikira wanatambulishwa kama *washamba*, *mafala*, *walalia masikio* na *mabwege*. Haya ni majina hasi na yanayoambatana na sifa ya kukosa kupevuka, ukosefu wa weledi na hawawezi kutegemewa. Kwa upande wao wenyewe wanajiona na kujitambulisha kama *mapasta*, *watakatifu*, *makasisi* na kuwarejelea wenzao waliovunja ubikira kama *poko*, *mtaka yote fisi*, *vulture* na kadhalika. Hapa walio mabikira wanajiainisha kama watu walio na usafi na waliozingatia maadili na hivyo basi wenzao wamepotoka kimaadili na ndiposa wamerejelewa kwa maneno hasi.

Upeo huu wa uanishaji na utambulisho unakuzwa na uwepo wa maneno mengine kama vile *mtoto*. Mtoto ni mtu tegemezi. Mara nyingi hajiamulii la kufanya. Hizi ni sifa zinazooanishwa na walio bikira. Fasiri ni kwamba wangali katika himaya ya wakuu wao na hivyo basi hawawezi kujiamulia. Aidha hawajatambua haki zao. Ikizingatiwa ufafanuzi wa sifa ya uanishaji katika upeo wa utambulisho kuwa lengo la upeo wa uainishaji ni kudunisha au kushusha uhalali na kuzua ukosefu wa kuaminika, hali hii ni dhahiri katika upeo huu. Watoto hawaaminiki sana. Aidha hawana tajriba kuu maishani inayoweza kurejelewa. Kwa wazulufu basi, wanawaona hawa ambao wanaogopa *sweet life*- (dhana inayokuza ushiriki wa tendo la ndoa kama tendo tamu) kama watoto na ndiposa hawawezi kuwa wataalamu au wajuzi kwa ambavyo wataalamu lazima wawe na sifa, weledi na ujuzi fulani. Kutokana na sifa kama hizo (weledi, ujuzi) waliovunja ubikira wanaaminika.

Upeo huu unafungua ufasiri wa wazulufu kuhusu kujamiana. Kuna wanaotazama hali hii kama ukosefu wa maadili na ndiposa kuna kundi la *watakatifu* na *maholy jo* na kuna wale wanaoona hali hii kama ni hali ya kawaida na ambayo mzulufu yeyote asiye na ujuzi wa tendo hilo ni *mshamba*. Maana za kisemantiki zinazohusiana na uteuzi na utumizi wa maneno kama haya inabainika umechukua ruwaza mahususi. Yaani wana kundi fulani pamoja na wanachama wanajitambulisha kwa namna chanya. Kwa upande ule mwingine wale wengine (wasio wanachama wa kundi husika) hutambuliwa kwa namna hasi. Katika utafiti huu ugunduzi huu unaingiliana na nadharia za maingiliano ya makundi, nadharia za mawazoganda na utambuzi wa kijamii (Fiske na Taylor, 1991; Hamilton, 1991; Semin na Fiedler, 1992; Turner na Giles, 1981; Wodak, 1989).

Miongoni mwa wazulufu upeo huu unafasirika kwa kuchukulia kuwa uwakilishi wao wa makundi haya unakuzwa na kudumishwa na msingi wa mielekeo na itikadi zimazoathiri tathmini yao na hivyo kuathiri uteuzi na utumizi wa maneno mahususi. Hali hii ni bayana katika maneno ambayo ni nomino yanayotumika kueleza au kurejelea uwanachama katika makundi tofauti na sifa zao mahususi. Mabikira wavulana kwa wasichana wanahusishwa na sifa za kitoto, uaminifu, utakatifu, dini, kutokuwa wakarimu na kutokuwa na ujuzi wa maisha. Hata hivyo mgao huu si sawa inapozingatiwa wavulana wasio bikira na wasichana wasio bikira. Wavulana bikira wanahusishwa na ujuzi ilhali wasichana wanarejelewa kwa maneno hasi. Utambulisho wao ni hasi (*poko, malaya, mtaro, tasteless*). Kupitia upeo huu mkakati wa uzungumzi wa uwasilishi chanya wa mtu binafsi na uwasilishi hasi wa wengine ambao kama walivyodai wataalamu kama vile van Djik (2006) ni namna bayana ya kuashiria miundo ya itikadi kimazungumzo.

Kutokana na mkakati huu kuna utumizi na upendeleo wa kundi la mhusika na kulihusisha na mazuri na mtazamo hasi kwa wanachama wa kundi la nje. Kulingana na nomino zote kama vile *mshamba* na *exper*t pamoja *na door mat* ukwezaji wa dhana ya “sisi” na “wao” ni bayana. Hili ni swala muhimu kwa wazulufu katika kuweka wazi utambulisho wao kama wanachama wa kundi mahususi katika jamii. Kwa mujibu wa utambulisho huu, ni bayana kuwa mvulana bikira kila wakati atabeba mzigo wa kuwa mshamba na hivyo kukuza ari ya upeo wa udharura ambapo anataka kuupoteza ubikira wake ili apate utambulisho wa kundi husika na kuwa “*mtu kusema*, *pro* ama *player*” ambao ni utambulisho chanya kwa kundi hilo. Yaani kundi la wasio bikira hususan wavulana wanahusishwa na *ujuzi, weledi, kutoogopa sweet life,* matendo chanya kama vile *kutenda wema, huduma kwa jamii* matendo yanayozua hali chanya kama vile *kushibisha* na *kuscore*.

Katika uchambuzi wa upeo huu, wasichana wanakabiliwa na hali ya kimazungumzo iliyo na mvutano na utata. Ni mazungumzo ya ujinsia yanayowasawiri wasichana kama viumbe wanaotawaliwa na hisi na ambao maslahi yao ya kimsingi ni kutafuta na kudumisha mahusiano yanayokubalika katika jamii kukubaliana na tabia za kiume.

**<u>Dondoo 22: Tunukuzi kutoka Kikundi Kiini Shule A</u>**

> MS018: Ok I think it's a virgin who is more valued coz nakumbuka tukiwa ryma tulikuwa tunaambiwa eti when you grow up your husband will be happy to open the envelope first so a virgin is more valued. Lakini kwa machali ni zi. Chali virgin atakufungua vipi? Surprisingly we girls tungependa sexually experienced boys. Maboi wanapokukatia wanakusweet talk na kudai kuwa they will accept a non-virgin. Uongo! Hii ni kwa relationship ya kupass time lakini mresh wanataka kutake home kwa maparo they want manzi mclean ambaye hajachunwa au kufunguliwa. But the same boiz wanataka uwape. Wanaomba sana! How do you remain a vajo? **<u>(Tzm Kiambatisho J Uk. 196)</u>**

**<u>Dondoo 23: Tunukuzi kutoka Kikundi Kiini Shule C</u>**

> MS004: Kwangu inaanza na salamu, hug the more unaendelea ndio unataka kusikia yenye iko huko mbele inarudi hug halafu kiss halafu hapo unajua vile utaopeleka Nitasurvive vipi bila my boyfriend. Umesikia wamesema usipowapa utazeekea kwenu. So I agree to him akiniomba. Ninampee tu. Najua promises zake nyingi ni za uwongo but nikoattached kwake sana. It is impossible for me to refuse him. **<u>(Tzm Kiambatisho I Uk. 162)</u>**

Kuhitimisha sehemu hii ya peo za kimazungumzo, matokeo ya utafiti yamedhihihirisha kuwa, wazulufu hutumia peo nne za kimsingi katika uwasilishi wa ujinsia wao. Hizo ndizo peo zinazochuja mtazamo wao kwa swala pana la ujinsia. Peo hizi hutambulika kupitia peo andamizi ambazo zinafasirika kupitia leksia wanazozitumia wazulufu kuzungumzia maswala yanayohusiana na ujinsia. Maelezo na ufafanuzi wa kila upeo umeegemezwa kwa maneno mahususi na imebainika kuwa baadhi ya peo zinategemeana na baadhi ya leksia zaweza kutumika kuimarisha na kukoleza zaidi ya upeo mmoja. Basi kutokana na peo hizi, wazulufu wanazua mikakatia anuwai ya jinsi ya kukabiliana na ujinsia wao na yanayoweza kutokana na matendo ya kiujinsia. Sehemu ya 5.3 hapa chini inatathmini kwa kina mikakati iliyoibuka katika uwasilishaji wa ujinsia miongoni mwa wazulufu.

### 5.3 Mikakati ya Kimazungumzo

Mfumo wa kichanganuzi uliotumika katika kutalii lengo hili la utafiti ulikuwa wa van Djik (2006). Katika mfumo huo, van Djik anafafanua mikakati 27 ya kiitikadi ambapo kuna makundi mawili: usafidi na uaibishaji. Ugavi huu ni muhimu katika kutekeleza mkakati wa msingi wa 'usawiri

chanya wa mtu binafsi na usawiri hasi wa wengine. Mgao wa usawiri chanya kama anavyoeleza van Dijk ni tukio la kiitikadi ambalo hutumiwa kujisawiri kuwa bora zaidi kuliko wengine; ule wa pili ni usawiri wa wengine kama duni au dhaifu. Hushusha hadhi na heshima. Mintarafu ya maelezo haya mikakati saba ya kimazungumzo ilidhihirika katika mazungumzo ya wazulufu kuhusu ujinsia.

### 5.3.1 Mkakati wa Ukinai

Mkakati huu unafafanua njia ambayo kwayo msemaji husema au huwasilisha kimazungumzo kitu chanya kwanza, na kisha anakataa au kukinai kwa kutumia neno fulani kama vile *lakini*, *ila* na kadhalika kama ilivyobainishwa katika tafiti za van Djik (2006a; 2006b) na Van Leeuwen (2007). Lengo la mtumizi lugha kufanya hivi huwa ni kudumisha mtazamo wake (van Djik (2006a).Wazungumzaji hutumia mkakati huu kama usawiri chanya wa uhalalishaji wa kibinafsi na usawiri hasi wa wengine. Katika utathmini wa mazungumzo ya wazulufu kuhusu ujinsia, mkakati huu ulijitokeza bayana

**<u>Dondoo 24: Tunukuzi kutoka Kikundi Kiini Shule B</u>**

> Mwenyewe sina lolote baya kwa mavajo lakini jo si ni ushamba.
>
> **<u>(Tzm Kiambatisho I Uk.)</u>**

Katika nukuu hii, mzulufu mhusika anadai kwanza kuwa yeye hana lolote au hisia zozote hasi kwa walio bikira. Huu ni usemi chanya ambao unatekeleza jukumu la kimazungumzo la kudumisha tahayuri. Hili ni dhahiri kwa ambavyo baada ya kauli hiyo, msemaji anafuatiliza mazungumzo na maneno hasi: *lakini jo si ni ushamba!* Kupitia maneno hayo, msemaji anakoleza mtazamo wake kuwa kwa wazulufu kuwa mabikira ni swala lililopitwa na wakati na kulilinganisha na mja kuwa mshamba. Kichanganuzi, hizi ni pande mbili zinazokinzana na ndiposa mkakati wa ukinai unadhihirika. Msemaji kwanza amedai hana lolote baya kwa walio mabikira lakini kwa wakati uo huo anawaona kuwa washamba. Mkakati huu unaungwa mkono na uwepo wa nukuu nyingine:

**<u>Dondoo 25: Tunukuzi kutoka Kikundi Kiini Shule B</u>**

> MV001: Kitu iko hii kitu enyewe ni opportunity imejileta hii ndiyo **opportunity we ukiiget nice for you. Yaani ukijikuta umejikuta mtu amekuletea.** Siku hizi msee aweza kuwa very appealing, attractive na kadhalika, **<u>but</u>** kama hajafinya/ hajaingiwa….that attractiveness is of no use and value. **<u>(Tzm Kiambatisho I Uk. 175)</u>**

Katika nukuu hii, kuna utumizi wa neno la Kiingereza *but*. Msemaji kwanza anakubali kuwa anayerejelewa anavutia na kupendeza hali ambayo ni chanya na ya kati hususan miongoni mwa wazulufu. Licha ya hali hiyo chanya, msemaji anaambatanisha na hali hasi ambapo anawadunisha mabikira kwa kudai kuwa huo uzuri wao hauna thamani na kuzidisha kwa kudai kuwa wao ni kujifanya tu. Mkakati huu unakuza upeo wa udharura ambapo mzulufu kheri apoteze ubikira wake na kusali kutambulika kuwa na uzuri na kuvutia na kwa pamoja ule upeo wa uainishaji unajitokeza

**<u>Dondoo 26: Tunukuzi kutoka Kikundi Kiini Shule A</u>**

> MS013: Niko na support mbili sasa hii kitu ya protection mostly wasee wengi madem wengi hawawezi kuafford kubuy contraceptive pills then ukisema utumie hii condom maboy wengi husema hawataki kula sweet na karatasi dem saa zingine anagive in tu. We as girls do everything we can, but these boys ni mafisi, walaghai….we are a hopless lot. **<u>(Tzm Kiambatisho J Uk. 185)</u>**

### 5.3.2 Mkakati wa Urejelezi ya Mamlaka

Wasemaji wengi hutaja na kurejelea mamlaka ili kuunga mkono tetesi zao. Kawaida mamlaka rejelewa huwa ni mashirika au watu wenye hadhi fulani katika jamii, au ambao ni wataalamu wa kawaida au viongozi wa maadili. Mashirika ya kimataifa (kama vile Umoja wa Mataifa), wasomi, waandishi wa habari, kanisa au mahakama mara nyingi wana jukumu hilo. Wazungumzaji kutegemea mwelekeo wao hurejelea mamlaka tofauti. La kimsingi katika mkakati huu ni kuwa sharti mamlaka rejelewa au tajwa yawe na ukubalifu katika jamii. Katika utafiti huu mamlaka ya kibinafsi yalibainika. Kwa mujibu wa Van Leeuwen (2007), mamlaka ya kibinafsi hupewa mtu kwa sababu ya hadhi yao au wajibu wao katika taasisi husika. Kulingana na mamlaka haya jibu la ni kwa nini hujibiwa kupitia kauli teule kwa ambavyo anayerejelewa ana mamlaka. Kwa mujibu wa ushawishi na mamlaka aliyonayo anayerejelewa, mkakati mamlaka unadhihirika.

**<u>Dondoo 27: Tunukuzi kutoka Kikundi Kiini Shule C</u>**

> There is nothing wrong in girls having boyfriends. After all isn't it true that all First Ladies are wives to husbands who are Presidents? In fact wasichana wote yafaa wawe na maboyfies. Till I had a boyfriend, my friends used to tease me for not having one. **<u>(Tzm Kiambatisho H Uk. 160)</u>**

Kutokana na nukuu hiyo, urejelezi wa *First Lady* unaweka wazi mamlaka ambayo kila mke wa rais huwa nayo. Kimsingi hata huwa ametawazwa jina la heshima kama vile Mama wa Taifa, Her Excellency na kadhalika. Kutokana na mamlaka aliyonayo, huwa ni kivutio kikubwa kwa wengi hivi kwamba, wazulufu wanamtumia kuweza kuhalalisha sababu zao za kutaka kuwa na mahusiano ya kimapenzi. Aidha wanataja rais. Kimsingi rais huwa na mamlaka na usemi katika

taifa analoliongoza. Kutokana na hili, huweza kuwa na ushawishi mkuu. Mbali na urejelezi huo, msemaji katika nukuu hii ametumia mkakati wa idadi ambapo amerai kuwa haina budi wasichana wote kuwa na wapenzi. Kwa kuingiza mkakati huu katika mkakati wa mamlaka ni hali ya kushadida kauli zake na kuongeza umuhimu wa wahusika kuwa na wapenzi. Mamlaka haya yana ukuruba sana na mamlaka ya watu mashuhuri ambapo wahusika hufuata na kuiga mifano ya watu wa aina hiyo ama walio na usemi katika jamii. Mama wa taifa ni mtu wa kuigwa kama walivyo wabunge, magavana na wengine walio mashuhuri katika jamii.

### 5.3.3 Mkakati wa Uainishaji

Kutokana na saikolojia ya kijamii, watu huwaainisha wengine, kama ilivyo miongoni mwa wazulufu. Mkakati huu ni mahususi hasa wakati wengine wanarejelewa katika swala husika. Uanishaji na kategoria kama walivyodai Bowker na Star (2000), ni migao iliyobuniwa kijamii inayowaweka watu wanaochukuliwa kuwa na sifa sawa. Kategoria hizi ni muhimu katika udumishaji na ukuzaji wa mahusiano ya kijamii. Miongoni wa wazulufu, wahusika wanajiainisha na kuwaainisha wenzao kama makundi shindani kutokana na mitazamo na imani zao. Kwa mujibu huu na kama walivyogundua Hannan, Polos na Carroll (2007); Navis na Glynn (2010) katika utafiti wao wa taasisi za mauzo, makundi au kategoria, huibuka na uanachama hubadilika kulingana na matarajio na mpito wa wakati pamoja na hali iliyopo. Baadhi hudumu ilhali mengine hupotea kabisa hali ambayo inaambatana na walivyogundua Durand & Paolella (2013) pamoja na Kennedy & Fiss (2013) katika utafiti wao wa makundi ya mauzo na bidhaa.

Wasomi wa maswala ya kategoria wameshikilia kuwa lugha inayotumiwa kurejelea kategoria fulani huakisi kategoria hiyo na kusisitiza umuhimu wa maneno tumikizi (Kahl na Grodal, 2016). Kwa mujibu wa utafiti huu, ilibainika kuwa kuna maneno mahususi ambayo wazulufu hutumia kuweka wazi migao baina yao. Maneno ya kuwadharau wasio mabikira (fisi, poko, mshamba, fala, *used paper*, mtaro n.k) yanaweka wazi ubayana wa sisi na wao kwa ambavyo walio mabikira wanasawiriwa au kujisawiri kama *maholy jo, pasta, bishop, mtakatifu, mama kanisa, hail holy Mary mother of God* n.k. Utafiti huu unarai kuwa pasi kuelewa jinsi uainishaji huu (sisi na wao) unavyojitokeza miongoni mwa wazulufu na kuwa na umuhimu au maana miongoni mwao, haiwezekani kueleweka jinsi ugavi huu unakuwa muhimu na wenye wiano na matendo yao. Huo ndio mchango mkuu wa mkakati huu ambapo wazulufu wameweka wazi mgao wa “sisi” na “wao” katika mazungumzo yao kuhusu ujinsia.

Ni muhimu kutaja kuwa hii ni hatua muhimu ya utambulisho ambapo katika miaka ya wazulufu utambulisho ni swala muhimu. Walio mabikira wanawaona wenzao waliopoteza ubikira kama watovu wa maadili kwa kusisitiza wema na maadili yao na sababu za wao kuenziwa katika jamii huku wakiweka kwenye uwazi utovu wa kimaadili wa wenzao na hivyo basi kutokuwa na sababu zozote za wao kuenziwa katika jamii. Hata hivyo, waliopoteza ubikira wao wanajitambulisha kama watu waliopevuka (*wajuzi*, *maexpert*, *mapro*, *mtu kusema*, *m-swa* n.k) na kwa kufanya hivyo wanasisitiza sifa za ujuzi na weledi wao wa kimaisha na kudunisha wenzao kwa kuwasawiri kama wasiojuwa na ndiposa wanawaita mafala, walalia masikio na washamba n.k Ni katika uainishaji wa aina hii ambapo mijadala dhahiri huibuka kila upande ukujaribu kutetea msimamo wake. Aidha kupitia uanishaji wa aina hii, usawiri na uelewa wa taswira za kiakili za kila kila kundi kuhusu ujinsia zinabainika

### 5.3.4 Mkakati wa kitasfida

Tasfida ni mkakati wa kisemantiki wa kimazungumzo unaolenga kupunguza makali, kuepusha uzuaji wa hisia hasi, maoni mabaya kuhusu swala husika. Kimsingi ni utumizi wa neno au kirai cha maneno ambacho kinakubalika zaidi mahali pa neno au kirai ambacho kinachukuliwa kuwa cha kuudhi kimazungumzo au kisichopendeza kwa mpokezi (Gomaa na Shi, 2012). Tasfida ni sehemu muhimu ya lugha na imekita mizizi sana kiasi cha kutumika kila siku hata pasi matarajio (Linfoot-Ham, 2005; Warren, 1992). Aidha uhitaji wa tasfida unatokana na msukumo wa kijamii na kihisia kwa ambavyo hufanikisha mazungumzo juu ya maswala nyeti katika jamii ujinsia ukiwemo.

Tasfida kama mkakati wa lugha imetambuliwa kuwa ni sehemu muhimu ya itikadi na itikadi huanza kwa kutaja au kwa majina. Katika utafiti wa jinsi wazulufu wanavyozungumzia swala la ujinsia, ilibainika kuwa mazungumzo yao yamesheheni tasfida nying kuanzia urejelezi wa sehemu, urembo na utanashati, ubikira na hali ya kutokuwa bikira. Basi tasfida kama mkakati wa kimazungumzo miongoni mwa wazulufu inaelekea hutimiza lengo la unyenyekevu kwa kutumia maneno yanayokubalika kijamii baadala ya maneno wazi tu ambayo kijamii huenda yaibue hisia za utovu wa nidhamu za kimazungumzo. Ni mkakati bayana wa unyenyekevu na wa kiitikadi kama alivyodai van Djik (2011) wa kusitiri ukweli na hupunguza aibu za kijamii ili kumkinga mzulufu. Hali hii inafikiwa kupitia utumizi wa maneno yasiyo na makali na maneno yasiyo dhahiri au yakini.

Ujinsia miongoni mwa wazulufu ni uwanja mmojawapo ambapo utumizi wa tasfida umekita mizizi kama ilivyobainika katika utafiti huu. Hali hii inatokana na mahitaji ya wazulufu ya kutaka kujitambulisha kama kundi bayana na kuficha ukweli kupitia tasfida. Kutokana na tasfida zilizobainika, ni bayana kuwa maeneo tofauti tofauti pamoja na wazungumzaji mbali mbali watakuwa na tofauti za kimila, kiitikadi, kitamaduni ambazo zinaakisi ujanibishaji wa lugha kama sifa mojawapo ya tasfida. Sifa hii ni bainifu inapoangaziwa tofauti za kitasfida miongoni mwa wazulufu kwa misingi ya kijinsia. Wavulana wana tasfida zao ilhali wasichana wana tasfida zao. Kwa pamoja hurejelea hali mbali mbali zinazohusiana na ujinsia kwa maneno tofauti. Aidha tasfida hubadilika.

Tasfida huambatana na mpito wa wakati. Maneno wayatumiayo wazulufu huashiria unyumbufu wa lugha, swala ambalo ni muhimu katika kuashira uhai wa lugha. Mbali na hayo sifa ya ubadilifu wa maneno ni bayana. Ubadilifu wa maneno  kimsingi ni namna mwafaka ya kupunguza makali ya maneno yanayochukuliwa kuwa makali na ya kuudhi katika muktadha fulani. Katika utafiti huu, mkutadha wa kimazungumzo ulikuwa ni mazungumzo kuhusu ujinsia miongoni mwa wazulufu. Kijamii maswala yanayozungumziwa mengine ni mwiko na hivyo basi wazulufu hawana budi kuibuka na namna yao mahususi ya kuyazungumzia. Ili kutimiza hili, wanatumia tasfida ambapo tasfida tumikizi zinatimiza uhitaji wa hamu ya kuepuka maneno miiko yanayoweza kuathiri kaida za kijamii na kuafiki masharti ya mazungumzo nyenyekevu. Tasfida chanya zinakuza na kufanya kirejelewa kupata hadhi na kuwa muhimu zaidi kuliko ilivyo.

Kutokana na utafiti huu, inabainika kuwa tasfida chanya zinashirikisha majina chanya yanayokuza nafsi na hadhi ya wahusika. Mbali na hayo, baadhi yazo zinaakisi uwili wa kimazungumzo/ urejeleaji. Tasfida hasi hushusha hadhi. Kimsingi hufidia au kusawazisha ukali wa maneno ya kimwiko na kuondoa katika mazungumzo yote ambayo watumizi lugha hawapendi au hawangetaka kuzungumzia moja kwa moja.

Kwa mujibu wa maelezo hayo, yaweza kudaiwa kuwa lengo kuu la utumizi wa tasfida katika mazungumzo ya wazulufu ni kuafikia unyenyekevu. Kama walivyodai wataalamu wa kimazungumzo, unyenyekevu huwa na nafasi muhimu katika mawasiliano ya kibinadamu swala ambalo ni dhahiri katika mazungumzo ya wazulufu. Ni muhimu kwa ambavyo hudumisha mawasiliano na kutawala tabia za kimazungumzo baina ya wahusika kwa kuwashinikiza

kuzingatia hisia za wengine. Uzingatiifu huu huzua ngazi za maridhiano na kuimarisha mahusiano na mawasiliano ya kibinadamu. Makakati huu wa kitasfida umeweka wazi jinsi wazulufu wanavyoridhia kuwasiliana miongoni mwao.

Tasfida husika kama vile kutafuna na kumega, kupanda, kuzuru shamba, kulima na kunyunyizia maji zinatumika kuhakikisha unyeneyekevu kuwili wa kimazungumzo. Yaani namna chanya inayoelekeza katika udumishaji wa tahayuri na staha ya kijamii ya washiriki na namna hasi inayohusishwa na uhuru wa kimatendo na uhuru kutokana na masharti katika mawasiliano. Ugunduzi huu umeambatana na maelezo ya nadharia ya tahayuri, iliyoasisiwa na Goffman (2005). Katika nadharia hiyo kama ilivyotambuliwa katika utafiti huu, dhana ya tahayuri inahusishwa na tahayuri ya kibinafsi ambayo washiriki katika muktadha wa kimazungumzo wanajizolea.

Kwa mujibu wa uwili wa unyenyekevu, tahayuri hujidhihirisha kuwili: tahayuri chanya inayotambulishwa na haja ya mtu kutazamwa kichanya katika muktadha wa kijamii na tahayuri hasi inayohusishwa na haja ya mshiriki kutofunwa na masharti. Yaani kuwa huru. Tasfida, hutekeleza yote haya: kwanza katika kutimiza uhitaji wa mzungumzaji wa kupunguza makali na uwezekano wa kuwepo mgogoro wa kijamii /ukosefu wa mapatano baina ya wanajamii unaoweza kushusha hadhi ya mzungumzaji na pili huweka dhahiri namna ya kupunguza tishio la mshiriki katika mazungumzo kutawala mazungumzo.

### 5.3.5 Mkakati wa Kisitiari

Utumizi wa sitiari ni uhalisia wa maisha ya kijamii hususan baina ya vijana (Underhill, 2010). Sitiari ni kauli ya kufafanua hali/kitu kwa sifa zake na kwa njia fiche. Humfaidi mtumizi lugha katika kuelewa kitu/hali moja kwa misingi ya kitu kingine. Huumba na kuunda mtazamo wa mtumizi lugha pamoja na ulewa na hivyo kusababisha muundo msingi ambao kwao tajriba zake hufasirika na kupewa maana. Ni mbinu ya lugha inayozua uhusiano usio wa moja kwa moja baina ya vitu, watu, na hali mbali mbali maishani (Underhill, 2010). Hudhihirisha uwezo wa lugha kama swala ambalo halibani bali humwezesha mtumizi lugha kuumba, kuumbua na kuumba tena dhana mbali mbali. Mintarafu ya maelezo haya, ufasiri wa ujinsia miongoni mwa wazulufu inabainika huathiriwa na sitiari wazitumiazo na hivyo kuaathiri maamuzi yao kuhusu ujinsia. Kwa kuangazia leksia zilizoibuka katika uwasilishi wa ujinsia miongoni mwa wazulufu, mkakati wa sitiari ni

bayana. Kujamiana baina ya wazulufu kunawakilishwa na sitiari pana ya utumikizi wa kitu kwa ajili ya manufaa na uanisi wa ujinsia.

Kutokana na utafiti, maneno mengi yaliyotumika na wazulufu ni ya kisitiari yanayokuzwa na kuimarishwa na ule mkakati wa kitasfida. Wazulufu wanaporejelea sehemu zao za ujinsia, wanatumia sitiari kama vile *Fimbo ya Nyayo, transfoma, kalamu, support document, milango, kitabu, katiba na kadhalika*. Sitiari hizi zinaonyesha msisitizo wa wazulufu katika utumizi, utenda kazi na kazi ya kifaa mahususi. Kwa uwepo wa maneno hayo, sehemu za mwili wa mzulufu na swala nzima la kujamiana liaakilishwa kwa misingi ya kifaa, matumizi na manufaa yacho badala ya sifa nyingine kama vile uzuri. Kwanza sitiari hii inamsawiri mzulufu kama kifaa.

Kwa msingi wa maneno hayo utekelezwaji wa matendo ya ujinsia na utumikizi wa vifaa husika na rejelewa unakuzwa zaidi ya tathmini za kijamii na kimaadili za mzulufu binafsi katika swala nzima la ujinsia wake. Leksia hizi zinabainisha na kukoleza umuhimu wa kimatumizi wa kifaa husika. Sitiari hizi ni muhimu katika kuelewa ulimwengu wa ujinsia wa wazulufu kwa ambavyo zina sifa mahususi; sifa ambazo zinaweka wazi kwanza, tofauti za kijinsia baina ya wazulufu, kubaini nani mwenye mamlaka na kukuza utenda kazi wa ujinsia. Sitiari hizi zinakuza dhana ya mvulana kumtawala msichana na kushadidia athari hasi kwa nguvu ya ujinsia wa mzulufu msichana, ufanywaji chombo na kutawaliwa. Kwa wazulufu wavulana, dhakari imerejelewa kisitiari kwa vifaa ambavyo vina uwezo mkubwa. Ni kama zana za kivita. Mbali na haya ni ithibati ya ubabe dume wa wavulana na pia jinsi hata wao wanavyoweza kuwa chombo cha kutumiwa.

Kuna sitiari pana inayohusiana na vyakula. Sitiari hii bali na kukuza mkakati wa kitasfida, inaweka wazi kuwa wasichana ni watu ambao kwao wavulana wanafaa kufaidi. Wao ni vyakula vya kuliwa na wavulana. Kwa mujibu huu, wao ni washiriki tendwa ilhali wavulana ni washiriki tendi. Hali hii inaambatana na mtazamo wa kitamaduni ambapo wavulana wanashinikizwa kuwa tendi hali inayojidhihirisha hata katika maneno mengine kama vile *striker* na *mlaji* na sitiari zinazorejelea vifaa. Kwa mujibu wa chakula, chakula kinatumika kama sitiari onekevu kuashiria tendo la kujamiana kupitia tendo la “kula” neno ambalo pia ni la kitasfida. Kula huku kunazua dhana ya raha. Vyakula rejelewa vinaashiria ashiki na unyegereshi pamoja na utamanifu (*halua, sharubati, lips nyanya*), majaribu au ushawishi na uamshaji wa hisia pamoja na utimilifu na ukamilifu wa ulaji.

Kwa mujibu wa wazulufu, chakula kinahusishwa na ngono kwa ambavyo, chakula pamoja na kushiriki ngono ni "bidhaa" zilizo muhimu kwa ajili ya maisha na undelezi wa kizazi. Inabainika kuwa sitiari hii ya chakula inahusishwa zaidi na wasichana kutokana na hali duni wanayopewa. Wao ni vyakula vya wavulana mbali na kuhusishwa na jukumu lao kitamaduni la ulezi (Parasecoli, 2007). Ingawa kumeibuka wasichana wasio wa kuaminika, kimsingi chakula kinachoandaliwa na binti hukubalika na uaminika zaidi. Uelewa wa sitiari hii kwa mkabala huu, unakuza mgao wa majukumu kitamaduni na kukoleza nafasi ya jinsia ya kike katika jamii. Mbali na hayo, miongoni mwa wazulufu, chakula kinamithilishwa na ujinsia na hivyo basi chaweza kuwa hatari kikiwa mikononi mwa mhusika asiyeaminika hali ambayo inaafikiana na ugunduzi wa Olsen na Gould (2008).

Mbali na hayo, wazulufu wanahusisha na kulinganisha ujinsia na chakula kiisimu ambapo bidhaa za vyakula vinalinganishwa na sehemu za mwili pamoja na kuashiria hamu, ashiki, tamaa, kiu na njaa ya kujamiana kama ilivyo kwa ulaji. Wazulufu kwa msingi wa taswira hii wanabainisha kuwa kujamiana ni swala ambalo kimsingi linafaa kuzua na kuwa la raha. Udokezi wa ladha na mguso unashadidia hali hii ambapo baina ya wazulufu, kujamiana hakuna budi kuvutia hisi. Haina budi kuwa na ladha nzuri "sweet life". Ingawa yaweza kuashiria kuwa wazulufu walioshiriki ngono wameshushwa hadhi na kuwa chakula au kuwa chombo au kifaa, dhana nyingine ni kuwa chakula, halua, nyanya, matunda, miwa na ndizi ni vyakula tamu na kuvila kunafaa kuzua raha ya aina yake kutokana na utamu wavyo na vivyo hivyo kujamiana kunafaa kuibua raha. Wazulufi kwa mkabala huu, inaeleweka kwa nini wanachukuliwa kama kizazi hatarishi. Wanaangazia zaidi raha na utamu wa ujinsia na kushusha nafasi ya madhara yanayoweza kutokea kutokana na vitendo vya wazulufu kujamiana.

Sitiari hii ya chakula pamoja na tasfida ya ulaji inakuza hali ya kukawaidisha vitendo vya wazulufu. Sehemu za siri za wazulufu kwa kutumia sitiari ya chakula hazifungwi katika usiri na ufiche baina ya wazulufu. Dhana hii ya kufanya swala la ujinsia pamoja na kushiriki ngono kuwa la kawaida kunaungwa mkono na sitiari ya mlango ambao kufunga na kufungua mlango ni mkakati wa wazulufu wa kuratibisha tabia zao za kiujinsia, kuumba kama swala la kawaida na la kila siku hususan swala kuu la kuvunja ubikira. Kifaa ni cha kutumiwa na chakula ni cha kuliwa.

**Dondoo 28: Tunukuzi kutoka Kikundi Kiini Shule C**

> MV001C: So unapata maswali zingine for example boy anakuuliza ukiweza pata girlfriend mmoja ama in future ukiweza oa unaweza kuwa faithful kwa bibi mmoja? Kwanza answer ni No, yeah because wanasemaga hakuna jogoo ya kuku moja unaona? **(Tzm Kiambatisho H Uk. 156)**

Dondoo hizi zinathibitisha uwepo wa sitiari na utumizi wa sitiari hii unaashiria kuwa kwa wazulufu, swala la ujinsia, kujamiana na marafiki wapenzi hi hali ya kawaida sana miongoni mwao ambapo washiriki wanaweza kubadilisha wapenzi kama chakula, mavazi ama tairi la akiba. Mbali na hayo, sitiari hizi ni za kitumizi na zinatumika kukawaidisha na kuhalalisha kujamiana na swala la mzulufu kuwa na wapenzi zaidi ya mmoja. Mtazamo huu unakuzwa na kutaka kuonyesha jinsi ni hali isiyo ya kawaida kwa mwanafunzi kuwa na sare seti moja au mtu kuwa na jozi moja tu la viatu au hata dereva kuendesha gari bila tairi la akiba. Hali hii inashadidiwa na dhana pana ya mja anayeshiriki chakula aina moja tu na kuna uwezekano wa yeye kuchoshwa na chakula hicho au hata kupatwa na utapia mlo.

Sitiari hiyo ya chakula miongoni mwa wazulufu pia inatosheleza kigezo cha sitiari bora ya chakula kama kibadala cha ujinsia. Imebainika kuwa kama alivyobaini Crumpacker (2006), sitiari nzuri sharti ibebe sifa za kiumbo zinazolingana na sehemu ya mwili au tendo linalorejelewa (kujamiana). Kwa kurejelea vyakula vyote vilivyotajwa, sifa hizo no bayana hususan kwa misingi ya umbo, ugumu na uthabiti wa sehemu rejelewa (Parasecoli, 2007). Baina ya wazulufu vyakula vilivyothabiti na virefu kama vile muwa na ndizi vinatumika kisitiari kuwasilisha dhakari ilhali matunda yenye uoevu yanatumiwa kurejelea uke. Ufafanuzi huu waweza kutumiwa kuamsha haja ya wasichana kujiamini na kuchukua mamlaka yao kwa ambavyo, utumizi wa vyakula hivyo unawasawiri wasichana kama amali ya kipekee na inayokubalika ya kutosheleza ashiki za wavulana (Olsen na Gould, 2008).

Dhana ya raha katika kujamiana inakuzwa na maelezo ya jinsi ya kula vyakula kama vile halua, ndizi na muwa. Kimsingi vyakula hivi huliwa baada ya kuambuliwa. Kula vyakula hivi pamoja na karatasi na maganda yake si kawaida. Uhalisia huu unakoleza kauli ya kuwa wazulufu hushiriki hali hatarishi (kiafya, kitabia na kimitindo). Uteuzi na utumizi wa sitiari hii ya kula chakula unabainisha na kusisitiza mtazamo wao (wazulufu) wa jinsi kujamiana kunafaa kuwa tendo la kuzua furaha na raha kwa kushiriki tendo hili kwa kutumia kingi ni hali isiyo ya kawaida. Dhahiri sitiari kama hizi zinauwezo wa kuimarisha mtazamo na upeo wa kuanisi na kuhalalisha ngono za

mapema na baina ya wapenzi wengi kama swala la kawaida katika ukuzaji wa utambulisho wao wa ujinsia.

Kuhitimisha, wazulufu ulimwenguni kote imegunduliwa kuwa wanashiriki ngono mapema. Mkakati huu wa kisitiari umepiga hatua na kuonyesha jinsi wazulufu kama kundi mahususi katika jamii hutumia lugha kijamii na kimuktadha kuwasilisha ujinsia wao. Utumizi wa sitiari ni sifa kuu katika uwasilishaji wa ujinsia miongoni mwa wazulufu. Sitiari ibuka zinakoleza uwezo wa lugha na unyumbufu wake katika utekelezaji wa shughuli mbali mbali za mwanadamu. Wazulufu wanatumia lugha kibunifu kusawiri uelewa na kuumba ujinisa wao kama kundi maalum katika jamii. Wazulufu katika taasisi za elimu zilizoshirikishwa katika utafiti wanatumia mkakati wa kisitiari kuhalalisha ujinsia na matendo yao yanayotokana na mahusiano yao ya ujinsia. Aidha wanatumia mkakati huo kwa kukuza sitiari mahususi zinazokuza na kuimarisha amali yao ya lugha pamoja na kukuza na kuendeleza umoja na uanachama wao kama wazulufu.

Sitiari ya vifaa na chakula imebainisha kuwa miongoni mwa wazulufu, haitumiki tu kuashiria tofauti za kijinsia lakini pia yaweza kutumika kuashiria sifa mbali mbali za ujinsia. Kwa kutumia zana za kivita, wavulana wanasawiriwa kama wahusika wanaoweza kusababisha maafa na au pia kulinda na ni wahusika hai/tendi ilhali wazulufu wasichana ni waathiriwa wa uharibifu au maafa ya wavulana hivi kwamba wao ni hoi na wapo kwa minajili ya manufaa ya wavulana. Uhalisia wa uwepo wapenzi zaidi ya mmoja baina ya wazulufu ni swala la kawaida kama iliyobainishwa katika dondo hili:

**<u>Dondoo 29: Tunukuzi kutoka Kikundi Kiini Shule B</u>**

> MV019: As in you sleep with all of them. Kuhave sex. Shuleni tunakula chakula kadhaa.Hotelini the menu is varied. Kwenye buffet unasample na kuonja onja. Cheki si lazima gari iwe na spare wheel?--- Normally hata sisi wanafunzi we just don’t have one set of uniform. Nina uhakika hata wewe (pointing at the moderator) you have viatu pair nyingi na huwa unabadilisha upendavyo. Lazima usample madem kadhaa. Ama ni vipi?

**<u>(Tzm Kiambatisho I Uk. 167)</u>**

Wazulufu hawaegemei tu mkabala wa matokeo hasi ya ujinsia bali pia wanaegemea mkabala wa uanisi unaoibushwa na mahusiano ya ujinsia miongoni mwao. Basi licha ya mikakati ya wazazi ya kutaka kubana uwepo wa uanisi wa kingono, sitiari zinazoibuka kwa wazulufu zinaonyesha kuwa wao kama kundi la wanajamii wanafahamu jukumu la utashi wa kujamiana.

### 5.3.6 Mkakati wa Kitakwimu

Kwa mujibu wa mkakati huu, ushahidi mkubwa katika mazungumzo huwa ni kwa ajili ya kukuza kuaminika kwa kisemwacho kupitia takwimu au utumizi wa idadi na asilimia zinazoashiria utoupendelevu. Nambari na takwimu kimsingi ndio namna bayana zaidi za kuashiria kishawishi uhalali wa swala fulani. Katika mazungumzo ya wazulufu kuhusu ujinsia, ilibainika kuwa wazulufu hutumia mkakati huu kwa kurejelea idadi kamilifu na idadi zisizo kamilifu. Kwa upande wa idadi kamilifu, ilibainika kuna matumizi ya asilimia kama inavyojitokeza katika nukuu hii:

**<u>Dondoo 30: Tunukuzi kutoka Kikundi Kiini Shule A</u>**

> Si hali ya kujivunia kuwa bikira. Singependa. Huna lolote linalokujumuisha na wenzako..... wanafunzi wa umri wako, **asilimia 90 na kwenda juu**, wakati wa sasa......... **<u>(Tzm Kiambatisho J Uk. 195)</u>**

Kwa upande wa idadi zisizo bayana kuna utumizi wa maneno jumulishi kama inavyobainika katika nukuu hii:

**<u>Dondoo 31: Tunukuzi kutoka Kikundi Kiini Shule B</u>**

> MV013: **According to situation vile iko kuget dem vajo inakuwa ni ngori Today everyone is doing it. Its the in-thing.**
>
> **<u>(Tzm Kiambatisho I Uk. 168)</u>**

**<u>Dondoo 32: Tunukuzi kutoka Kikundi Kiini Shule A</u>**

**MS020: In my opinion it is so normal with high schoolers wote tumeharibika and you see, maboi unaidemand sana.** **<u>(Tzm Kiambatisho J Uk. 177)</u>**

Kama ilivyo katika nukuu hizo, wazulufu wahusika wanatumia mkakati huu kujaribu kahalalisha mtazamo wao. Kwa ambavyo jamii imewakita katika mipaka ya kiumri ili kuweza kujamiana, kwa unyenyekevu wao wanakinzana na jamii kupitia mkakati huu. Ni rahisi kwa mtumizi lugha kusawiri picha ya kila mtu anafanya hivi na vile na hivyo basi inakuwa kama ndiyo hali ya kawaida. Wale ambao hawapo katika kundi lile wanachukuliwa kama wanaoasi. Asilimia 90 ni takwimu ya juu ambayo ikitajwa inaweza kuaminika na kukubalika kwa wepesi zaidi na hivyo basi kuhalalisha matendo ya wazulufu. Kwa kutumia idadi isiyobainifu, wazulufu wanakuza uwezo wao wa kuyafanya matendo yao kuwa ya kawaida na kukubalika. Idadi isiyobainifu kiisimu ni idadi ambayo mhusika mtumizi hawezi kuajibishwa. Ni idadi inayoweza kuuliziwa maswali na kupata jawabu. Wazulufu wanaposema “everyone” si bayana ni kina nani wanaorejelewa kama wote . kwa kufanya hivi, wazulufu hawawezi kuwajibishwa kwa walilolisema. Hata hivyo, umuhimu mkuu wa mkakati huu ni kuweza kuhalalisha na kufanya swala fulani kuwa la kawaida.

### 5.3.7 Mkakati wa kupiga chuku

Kupiga chuku ni mkakati wa kisemantiki wa kukuza maana. Kwa mujibu huu na kulingana na mtazamo mpana wa mazungumzo ya wazulufu kuhusu ujinsia, tukio la kujisawiri kichanya na kuwasawiri wengine kihasi ni bayana. Upigaji chuku huu hata hivyo katika mazungumzo ya wazulufu umekolezwa kwa sitiari mahususi. Kwa mujibu wa Van Leeuwen (2007) hali hii hujitokeza kwa misingi ya mamlaka, utathmini wa kimaadili na uhalalishaji. Utumizi wa mamlaka kama upigaji chuku kama inavyojitokeza katika utafiti huu, ni kuwa uhalalishaji wa matendo ya wazulufu unaafikiwa kupitia watu mashuhuri ambao wana ushawishi mkuu katika jamii.

**Dondoo 33: Tunukuzi kutoka Kikundi Kiini Shule B**

> MS003C: **For me naona kuwa single ni ujinga s**ometimes coz **kuwa single ni kujikazia maisha** na hiyo si poa lazima uexperience love. **There is nothing wrong in girls having boyfriends. After all isn't it true that all First Ladies are wives to husbands who r Presidents?** **(Tzm Kiambatisho H Uk. 159)**

Katika nukuu hiyo, dhana ya kupiga chuku kwa kuwarejelea wake wa maraisi ni bayana. Kupiga chuku huku hata kunaimarishwa zaidi na utumizi wa swali. Ni bayana kuwa kila "First Lady huwa ni mke wa rais. Basi kwa kutumia mtu mashuhuri hivi, ni namna ya wazulufu kuazimu kuonyesha umuhimu wao katika jamii, kuhalalisha matendo yao kama wanajamii na kujiondolea lawama kutokana na matendo yao. Kulingana na kategoria ya msingi wa utathmini wa kimaadili, kuna urejelezi wa maadili mahususi katika jamii. Uhalalishaji kulingana na utafiti huu ni ngazi ya wazulufu ya kurejelea malengo, majukumu na kazi za kidesturi zilizotaasisishwa na kwa ujuzi ambao jamii imeumba ili kujitosheleza na uidhibati wa kitambuzi ambao upo au umejaribiwa katika desturi nyingine. Ugunduzi huu unaweka wazi uhalisia wa mithopoea katika mazungumzo ya wazulufu (masimulizi ambayo matokeo yake hutunuku tabia fulani kama tabia zinazokubalika na zinazopendeka na nyingine kukataliwa kama zisizokubalika).

## 5.4 Hitimisho

Sura hii imejengeka katika dhumuni la pili na la tatu la utafiti. Kwa mujibu wa madhumuni , sura hii imefafanua peo na mikakati ya kimazungumzo katika uumbaji wa ujinsia. Utafiti ulitambulisha kuwa wazulufu hutumia peo nne kuu (udharura, kujihini, mamlaka na uainishaji). Kwa mujibu wa mikakati, mikakati saba ya kimazungumzo iliyobainika imefafanuliwa.

# SURA YA SITA

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 6.1 Utangulizi

Katika sura hii, kama namna ya kuhitimisha tasnifu, dhana tafitiwa na zinazojibainisha katika sura tangulizi zinaangaziwa. Msomaji anaelekezwa kimuhtasari kwa madhumuni na matokeo ya utafiti na hatimaye kuwekewa wazi sehemu muhimu za utafiti wa baadaye. Sehemu ya 6.2, ni muhtasari wa matokeo kwa kurejelea maswali ya utafiti. Sehemu ya 6.3 ni hitimisho na inalenga athari za ugunduzi mintarafu ya maswali hayo kwa ufasiri na uelewa wa ujinsia miongoni mwa wazulufu na kwa jamii pana kwa misingi ya sera. Sehemu ya 6.4 inaweka bayana mapendekezo ya utafiti wa baadaye.

## 6.2 Muhtasari wa Matokeo Muhimu

Sura ya kwanza inatanguliza kwa madai kuwa lugha ni kiingilio muhimu maishani mwa jamii yoyote ile. Hata hivyo, ilikisiwa kuwa haijulikani jinsi lugha waitumiayo wazulufu kuhusu ujinsia huathiri maamuzi na matendo yao kuhusu kushiriki au kutoshiriki kujamiana. Basi utafiti huu ulitathmini sifa za lugha waitumiayo wazulufu kama malighafi ya kuumba na kuuwasilisha ujinsia wao. Kuafikia hilo, ililazimu kutahmini leksia katika mazungumzo wa ujinsia. Leksia hizo ziliweka bayana peo za kimazungumzo; peo ambazo ni msingi wa mikakati inayotumiwa na wazulufu.

Utafiti umethibitisha kama alivyodai Eyo (2016) kuwa, lugha ni sehemu mojawapo ya dhana zinazochangia katika mkusanyiko wa kisemiotiki ambao wazulufu huumba na kujipata. Kama kundi mahususi wazulufu wametambuliwa kuwa na mtindo wao wa kimavazi, muziki, michezo mitindo ya kukatika, tambiko na ulimwengu mzima unaobeba dhana na fikra zao na kufanyiza ulimwengu wao. Katika tasnifu hii imeonyeshwa jinsi wazulufu katika taasisi za elimu nchini Kenya wanavyotumia lugha kwa namna yao katika uwasilishaji wa ujinsia. Lugha hiyo ina sifa mahususi.

Kuhusu leksia tumikizi katika uwasilishaji wa ujinsia miongoni mwa wazulufu, ilibainika kuwa keksia wanazozitumia wazulufu ni za kitasfida na zimepigwa chuku. Leksia hizo zaweza kuwekwa katika kategoria nne kuu kiuamilifu. Kategoria hizi ni pamoja na:

a) Kategoria ya maneno yanayorejelea ubikira na matokeo ya kujamiana ambapo kulikuwa na hali mbili. Yaani kuwa bikira na kutokuwa bikira. Ilibainika kuwa kuwa bikira na kutokuwa bikira hufasirika kuwili kwa namna chanya na hasi kwa kuumba taswira ya usafi, udhalilishaji, weledi, uchoyo na ukarimu. Taswira ya bahati na bahati nasibu, spoti, ukarimu na upishi ndizo fasiri zinazotokana na matokeo ya wazulufu kujamiana.
b) Kategoria ya maneno yanayoashiria maumbile ambapo kulikuwa na vikategoria vidogo vidogo ifuatavyo:
    i) Maneno yanaoakisi sehemu za ujinsia. Iligunduliwa kuwa katika maneno haya kuna usafidi wa uzani, kifaa, chakula, stakabadhi na taasisi.
    ii) Maneno ya kiumbo ambapo kuna tasfida za umbo la nje, umashuhuri na chombo.
    iii) Maneno yanayolenga urembo na utanashati na ikabainika kuwa maneno haya yanagawika kwa misingi ya maneno ya kibembelezi, utukufu, ladha na utegemezi.
c) Kategoria ya maneno ya kumrejelea mzulufu mpenzi. Katika kategoria hii kulikuwepo maneno ya kihisi, umiliki na utukufu, fedha, ladha na uzuri pamoja na matunda.
d) Kategoria ya maneno ya hali ya mzulufu kuwa katika mapenzi. Maneno yaliyobainika katika kategoria hii ni virai vya maneno (si neno moja moja). Virai hivi vilichukua sifa za uhitaji, utwaaji, utegemezi, ufanisi na thamani. Katika kategoria hii, ilibainika kuwa swala la ujinsia halikuathiri jinsi hali ilivyorejelewa kwani hakuna hali ya uana katika kuwa katika mapenzi.

Kuhusu lengo la pili na la tatu la utafiti huu, baada ya kugundua kuwa mazungumzo ya wazulufu kuhusu ujinsia huakisi leksia bainifu na nyumbufu, utafiti uligundua kuwa zipo peo bayana za kimazungumzo zinazotawala ufasiri na uelewa wa wazulufu kuhusu ujinsia. Peo nne kuu za kimsingi zilibainika ambazo zilikuzwa na peo jenzi au saidizi kutokana na utasfida wa maneno yaliyotumika. Peo hizi za kimsingi ni pamoja na:

a) Upeo wa udharura. Huu ni upeo unaoufasiri ubikira na swala nzima la kutokuwa bikira kama jambo la dharura. Upeo huu unakuzwa na peo ndogo zinazotokana na leksia zinazorejelea chakula, uzuri/ utamu na ladha, ujuzi/weledi na ushamba, ukulima/upanzi, aibu na uhitaji.

b) Upeo wa kujihini ambao unaegemea maadili ya kijamii. Upeo huu unakuzwa na peo ndogo za usafi/uadilifu, waa na aibu, weledi, utegemezi unafiki na ufunguzi. Aidha zipo peo ndogo za vifaa na vitu vilivyotumiwa.
c) Upeo wa mamlaka. Upeo huu unaegemea ni nani anayeshikilia dira na mwelekeo wa mahusiano ya kijinsia miongoni mwa wazulufu. Upeo huu unathibitiwa na peo ndogo za vifaa, utukufu na hadhi, taasisi, ufahari, ushindi na stakabadhi.
d) Upeo wa uanishaji na utambulisho. Upeo huu ulikuwa muhimu katika swala nzima na usharifu wa mzulufu. Wazulufu katika awamu hii ya maisha yao wanasaka mahali na nafasi yao katika jamii. Upeo huu ulikuzwa na peo ndogo za wanyama na sifa zao, umashuhuri na ugwiji, maumbile, sifa na mamlaka.

Kwa mujibu wa mikakati ya mazungumzo, imetambuliwa kuwa, mazungumzo ya wazulufu kuhusu ujinsia yanatawaliwa na mikakati saba muhimu kama ifuatavyo:
a) Mkakati wa ukinai ambapo msemaji husema au huwasilisha kimazungumzo kitu chanya kwanza, na kisha anakataa au kukinai kwa kutumia neno fulani kama vile *lakini, ila* nia ikiwa ni kudumisha nafasi yake chanya.
b) Mkakati wa mamlaka ambapo mtumizi lugha hurejelea watu mashuhuri au walio mamlakani ili kuweza kuyapa ayasemayo mashiko. Lengo kuu la mkakati huu kama ilivyobainika huwa ni kuhalalisha jambo husika.
c) Mkakati wa uainishaji ambapo wazulufu kwa kujua au pasi kujua kama ilivyo katika jamii pana hujiweka katika makundi au kujitambua kama wanachama wa kundi fulani. Mintarafu ya utafiti huu kuhusu ujinsia, ilibainika mgao wazi wa “sisi” na “wao” kuhusu kuwa bikira na kutokuwa bikira. Kulikuwa na uchanya na uhasi wa kiuainishi. Walio bikira wanawaona wasio bikira kwa namna hasi. Ni wakosefu wa maadili. Waliovunja ubikira nao wanawaona waliobikira kama wanafiki, wachoyo, washamba na wasio na weledi wa maisha. Ni waoga.
d) Mkakati wa kitasfida. Mkakati huu ni muhimu katika kutimiza kaida za kijamii katika mawasiliano na kudumisha kanuni za unyenyekevu katika mawasiliano. Aidha udumishaji wa tahayuri. Hutumika kupunguza ukali wa yasiyosemeka au kutamkika hadharani swala linalompa mzulufu nafasi ya kuzungumzia maswala nyeti katika jamii. Aidha mkakati huu unatumika kwa ajili ya kuwatawala kwa hila wahusika.

e) Mkakati wa kisitiari unaouumba na kuunda mtazamo wa mtumizi lugha pamoja na uelewa wake na hivyo kusababisha muundo msingi ambao kwao tajriba zake hufasirika na kupewa maana. Ufasiri wa ujinsia miongoni mwa wazulufu imebainika huathiriwa na stiari wazitumiazo na hivyo kuaathiri maamuzi yao kuhusu ujinsia.
f) Mkakati wa kitakwimu unaotumika kwa ajili ya kukuza kuaminika kwa kisemwacho kupitia takwimu au utumizi wa idadi bainifu na idadi jumlishi pamoja na asilimia zinazoashiria utekelezwaji au ushiriki na uhusika katika swala rejelewa. Huu mkakati kama ilivyo kwa mkakati wa mamlaka, hutumika ili kuweza kuhalalisha jambo. Hii ni hali muhimu kwa wazulufu ili kuonyesha kuwa matendo yao ya kijinsia yapo katika upeo wa yanayokubalika.
g) Mkakati wa kupiga chuku ambao ni mkakati wa kisemantiki unaokoleza maana na hukuzwa na mikakati mingine kama vile mkakati wa kistiari na kitasfida. Huu ni mkakati maarufu katika urejelezi wa matokeo, kuwa na kutokuwa bikira.

**6.3 Hitimisho.**

Utafiti huu ni awamu ndogo tu katika hatua ya uelewa wa wazulufu. Hatua hii ya kitafiti imebainisha utajiri wa kiisimu wa wazulufu kama amali ya usemi na uchanganuzi usemi.Tasnifu hii imeonyesha kuwa uchanganuzi wa uumbaji wa ujinsia miongoni mwa wazulufu waweza kuzua matokeo ya aina yake ambayo yanakubaliana na tafiti nyingine zilizo na uhusiano na swala la wazulufu na ujinsia. Uamilifu wa leksia ibuka, peo na mikakati ya uzungumzi inaashiria uhalisia wa ujinsia baina ya wazulufu ambapo kuna mwelekeo mpana katika utenda au uamilifu wa ujinsia, ubidhaaishaji, utawala na mvutano wa kimamlaka baina ya wazulufu kwa misingi ya ujinsia wao. Kwa kuhalalisha matendo na tabia zao za ujinsia kupitia mikakati mbali mbali ya uzungumzi, wazulufu wanauona ujinsia wao, tabia na matendo ibuka kama swala la kawaida lililo muhimu katika utambulisho na ukuaji wao.

Kimsingi inabainika kuwa wazulufu wanafasiri na kuelewa ujinsia wao kama swala la kawaida na ambalo sharti wakabiliane nalo kama kundi mahususi la kijamii. Ubikira, ambao ni muhimu katika swala nzima la ujinsia miongoni mwa wazulufu unafasirika kama swala la aibu linalomfanya mhusika mvulana kuonekana kama mshamba asiye na ujuzi wowote. Ni hali ambayo mzulufu mvulana anafaa kuiondokea haraka iwezekanavyo. Kutokuwa bikira kunabainishwa kama weledi na utambuzi wa utamu wa maisha. Inabainika basi kuwa hii ni daraja ambayo inamvusha mzulufu

mvulana kutoka ulimwengu wa kutojua hadi ule wa kujua. Kwa mzulufu msichana, hana lake kwani atatamanika akiwa bikira. Akivunja ubikira wake anafedheheshwa kama mwanamke mkoo. Ukinzani huu na uwili wa kirejelezi wa swala moja ni hali inayochangia katika mtanziko wa wazulufu kuhusu ujinsia.

Wazulufu wanatumia peo anuwai kuumba ujinsia wao. Peo hizi zinakolezwa na mikakati ya kimazungumzo ambayo kwa kina kirefu inatumika kuhalalisha na kukawaidisha matendo ya kiujinsia ya wazulufu. Hii ni hali inayofafanua basi kwa nini kuna kukithiri kwa mimba zisizopangwa, ongezeko la uavyaji mimba, kutokamilisha masomo, magonjwa ya zinaa miongoni mwa wazulufu. Kwa hali hii, sharti wanasera, watambue mchango wa lugha waitumiayo wazulufu katika kubuni mikakati mwafaka ya kukabiliana na hali hii. Wanasera na taasisi husika hazina budi kushirikisha lugha ya wazulufu katika miongozo yao ili kuwapa wazulufu nafasi ya kujitambulisha na miongozo kama hiyo na kuiona kama yao.

Ithibati ya matokeo katika utafiti huu yaelekeza katika utambuzi kuwa lugha na sifa za lugha ya wazulufu ni amali muhimu katika kufumbua uelewa wa ujinsia miongoni mwa wazulufu kiisimu swala linaloweza kuchangia kichanya kwa wanaohusika na ushauri na unasihi wa wazulufu. Washauri hawa waweza kuelekezwa namna ya kutathmini na kutumia uelewa wa wazulufu wa ujinsia miongoni mwao kuimarisha mafunzo yao. Kwa mfano imebainika katika utafiti huu uwepo wa sitiari nyingi zinazorejelea vifaa na vyakula na uamilifu wavyo hali inayoathiri usawiri wa ujinsia miongoni mwa wazulufu. Washauri hawa waweza kutumia na kutathmini sitiari hizo ili kubaini iwapo zinazua uchanya na uhasi wa uumbaji wa ujinsia na tabia na matendo ya ujinsia miongoni mwa wazulufu.

Dhana ya ufedheheshaji wa mwanamke mkoo “slut shaming” ilikuwa dhana muhimu iliyojitokeza katika utafiti huu. Dhana hii yaweza kuwa kigezo muhimu cha kutambua athari ya lugha waitumiayo wazulufu kwa wenzao. Dhana hii yaweza kutumiwa kuumbua ujinsia hasi unaotokana na itakadi za wazulufu na hivyo kuweza kuepuka tabia hatarishi na kila mzulufu kuchukua mamlaka yake ambapo watu watakuwa na usawa utakaokuza mahusiano bora ya kijinsia.

Utafiti wa tasnifu hii umefanikiwa katika kujaribu kuelewa lugha ya wazulufu katika uwasilishaji wa ujinsia. Aidha umejaribu kuonyesha uhusiano uliopo baina ya leksia wazitumiazo wazulufu na

peo zinazoibuka pamoja na mikakati ya kimazungumzo wanayotumia kuhalalisha matendo yao yanayohusiana na ujinsia.

**6.4 Mapendekezo**

Utafiti huu ni hatua ya mwanzo tu katika uelewa wa ulimwengu wa wazulufu kupitia uchanganuzi wa lugha wanayoitumia kuzungumzia swala la ujinsia. Mazungumzo yao ni amali kuu katika kuelewa ufasiri wao wa ujinsia na kupata uangavu wa sababu za mwelekeo wa maamuzi na matendo yao. Kwa hili, mtafiti anapendekeza yafuatayo:

i) Wanaobuni sera hawana budi kushirikisha lugha ya wazulufu katika uundaji wa sera zao.
ii) Fasiri za ubikira na kutokuwa bikira miongoni mwa wazulufu sharti zizingatiwe iwapo jamii pana itataka kujua, kuelewa na kutatua tatizo la mimba zisizopangwa, uavyaji mimba na mahusiano ya kingono ya mapema miongoni mwa wazulufu.
iii) Uwili wa urejelezi wa swala nzima la wazulufu ni hali ya kuzingatiwa.

Kuhusu utafiti wa baadaye, inapendekezwa kuwe na:

a) Utafiti wa utakaolenga kuchunguza iwapo athari za utamaduni na mila zinachangia katika uumbaji wa ujinsia miongoni mwa wazulufu.
b) Utafiti utakaochunguza nafasi ya vyombo vya habari na mifumo mipya ya mawasiliano katika uumbaji wa ujinsia wa wazulufu
c) Utafiti wa kuchanganua miundo na maumbo ya maneno yanayotumika na wazulufu kuzungumzia na kuumba ujinsia wao.
d) Utafiti wa muundo wa mazungumzo baina ya wazulufu kuhusu ujinsia

## MAREJELEO


Aggleton, P., & Warwick, I. (1997). Young People, Sexuality, HIV and AIDS Education. Kwenye Sherr, L. *AIDS and Adolesescents.* Netherlands: Harwood Academic Publishers.

Albert, D., & Steinberg, L. (2011). "Judgment and Decision Making in Adolescence". *Journal of Research on Adolescence. 21 (1)*, 211- 224.

Alexander, M. G., & Terri, D. F. (2003). "Truth and Consequences: Using the Bogus Pipeline to Examine Sex Differences in Self- reported Sexuality.". *Journal of of Sex Research 40 (1)*, 27-35.

Andrew, P. (2012). *The Social Construction of Age: Adult Foreign Language Learners.* Bristol: Multilingual Matters.

Armstrong, E. A., Hamilton, L. T., & Seeley, J. L. (2014). "Good Girls": Gender, Social Class and Slut Discourse on Campus. *Social Psychology Quarterly 77 (2)*, 100-122.

Arnett, J. J. (2007). "Emerging Adulthood: What Is It, and What Is It Good For?". *Child Development Perspectives. 1 (2)*, 68-73.

Attwood, F. (2006). “Sexed Up: Theorizing the Sexualisation of Culture. *Sexualities 9 (1)*, 77-94.

Aubrey, J. S. (2004). Sex and Punishment: An Examination of Sexual Consequences and the Sexual Double Standard in Teen Programming. *Sex Roles 50 (7–8)*, 505- 514.

Avusabo-Asere, K., Bankole, A., & Kumi-kyereme, A. (2008). *Views of Adults on Adolescents Sexual and Reproductive Health: Qualitative Evidence from Ghana.* New York: Guttmamacher Institute.

Barber, N. (1995). The evolutionary psychology of physical attractiveness: Sexual selection and human morphology. *Ethology and Sociobiology*, 395–424.

Bearman, P. S., & Brückner, H. (2001). Promising the Future: Virginity Pledges and First Intercourse. *African Journal of Sexuality 106 (4)*, 859-912.

Beck, R. (2015). Sheng: An Urban Variety of Swahiili in Kenya. Kwenye N. Nico, & H. Andrea, *Youth Language Practices in Africa and Beyond* (kur. 51-80). Mouton: De Gruyter.

Becker, B. E., & Luthar, S. S. (2007). Peer-perceived admiration and social preference: Contextual correlates of positive peer regard among suburban and urban adolescents. *Journal of Research on Adolescence 17*, 117-144.

Beguy, D., Kabiru, C. W., Nderu, E. N., & Ngware, M. W. (2009). Inconsistencies in Self Reporting of Sexual Activity among Young People in Nairobi, Kenya. *Journal of Adolescent Health 45,*, 595-601.

Bell, S. (2012). Young People and Sexual Agency in Rural Uganda. *Culture, Health and Sexuality 14 (3)*, 283-296.

Berndt, T. J., & Savin-Williams, R. C. (1993). Peer relations and friendships. Kwenye Tolan, H. *Handbook of clinical research and practice with adolescents* (kur. 203 – 219). Oxford, UK: Wiley.

Bill, M. C. (1994). Refusal to Eat and Drink: A Metaphor for ‘Safe Sex’ in Tsonga Folktales. *African Languages and Cultures 7 1),* 49-77.

Blackledge, A. (2005). *Discourse and Power in a Multilingual World.* Amsterdam/Philadelphia, PA: John Benjamins.

Boislard, M., & Zimmer-Gembeck, M. (2012). *Adolescent Sexual Behavior: Current Knowledge, Challenges and Implications for Research and Policy. In: Colombus F., editor. Sexuality: Perspectives, Role and Issues in Society.* . New York. NOVA Publishers.

Bordini, G. S., & Sperb, T. ( 2013). Sexual double standard: A review of the literature between 2001 and 2010. *Sexuality and Culture 17*, 686–704.

Bouchey, H. A., & Furman, W. (2003). Dating and romantic experiences in adolescence. Kwenye &. M. G. R. Adams, *The Blackwell handbook of adolescence* (kur. 313 – 329). Oxford, UK: Black Publishers.

Bowker, G. C., & Star, S. L. (2000). *Sorting things out.* Cambridge, MA: The MIT Press.

Boyatzis, C. J., Baloff, P., & Durieux, C. (1998). Effects of perceived attractiveness and academic success on early adolescent peer popularity. *Journal of Genetic Psychology 159*, 337-344.

Braun, M. F., & Bryan, A. (2006). Female waist-to-hip and male waist-to-shoulder ratios as determinants of romantic partner desirability. *Journal of Social and Personal Relationships 23,* 805-819.

Braun, V., & Kitzinger, C. (2001). “Snatch,” “Hole,” or “Honey-Pot”? Semantic Categories and the Problem of Nonspecificity in Female Genital Slang. *The Journal of Sex Research 38 (2),* 146- 158.

Breines, J., Crocker, J., & Garcia, J. (2008). Self-objectification and well-being in women’s daily lives. . *Personality and Social Psychology Bulletin, 34,* , 583-598.

Brody, G. H., Murry, V. M., Gerrard, M., Gibbons, F., McNair, L., Brown, A., & al, e. (2006). The strong African American families program: Prevention of youths’ high-risk behavior and a test of a model of change. *Journal of Family Psychology 20(1),* 1-11.

Brown, B. B., Feiring, C., & Furman, W. (1999). Missing the Lobe Boat: Why Researchers have Shied away from Adolescent Romance. Kwenye Furman, W., Brown, B. B., & Feirings, C. *The Development of Romantic Relationships in Adolescence* (kur. 1-16). New York: Cambridge University Press.

Brown, J. (2002). Mass media influences on sexuality. *Journal of Sex Research 39 (1),* 42–45.

Brubaker, R., & Cooper, F. (2000). Beyond 'Identity. *Theory and Society 29,* 1-47.

Bucholtz, M., & Skapoulli, E. (2009). Youth Language at the Intersection: From Migration to Globalization. *Pragmatics 19(1),* 1-16.

Buss, D. M., Shackelford, T. K., Kirkpatrick, L. A., & Larsen, R. J. (2001). A half-century of mate preferences: The cultural evolution of values. *Journal of Marriage and Family 63*, 491-503.

Buss, D., & Schmitt, D. (1993). Sexual strategies theory: an evolutionary perspective on human mating. *Psychological Review 100*, 204- 232.

Buunk, B. P., Dijkstra, P., Fetchenhauer, D., & Kenrick, D. T. (2002). Age and gender differences in mate selection criteria for various involvement levels . *Personal Relationships 9*, 271-278.

Cameron, D., & Kulick, D. (2003). *Language and Sexuality*. Cambridge: Cambridge University press.

Caron, F., Godin, G., Otis, J., & Lambert, L. (2004). Evaluation of a Theoretically Based AIDS/STD Peer Education Program on Postponing Sexual Intercourse and on Condom Use Among Adolescents Attending High School. *Health Education Research Journal, 19*, 185-197.

Carpenter, L. M. (2005). *Virginity lost: An intimate portrait of first sexual experiences.* New York: NYU Press.

Cense, M. (2014). Sexual Discourses and Strategies among Minority Youth in the Netherlands. *Culture, Health and Sexuality 16*, 835-849.

Centres for Disease Control and Prevention. (2009). *Youth risk behavior surveillance-United States.* New York: CDC.

Chomba, E. N. (2005). *Usawiri wa Mwanamke Katika Methali za Kikuyu*. Unpublished M.A Thesis. Egerton University. Njoro, Kenya.

Chouliaraki, L. (2005). Introduction: The soft power of war – legitimacy and community in Iraq war discourses. *Journal of Language and Politics 4 (1)*, 1-10.

Cleland, J., & Ali, M. M. (2006). Sexual Abstinence, Contraception and Condom Use by Young African Women: A Secondary Analysis of Survey Data. *Lancet 368*, 1788-1793.

Connolly, J., Furman, W., & Konarksi, R. (2000). The roles peers in the emergence of heterosexual romantic relationships in Adolescence. *Child Development, 17*, 1395 – 1408.

Côté, J. E. (2006). Emerging adulthood as an institutionalized moratorium: Risks and benefits to Identity Formation. Kwenye J. J. Arnett & J. L. Tanner (Eds.), *Emerging adults in America: Coming* (kur. 85-116). Washington, DC: American Psychological Association.

Crawford, M., & Popp, D. (2003). Sexual double standards: A review and methodological critique of two decades of research. *Journal of Sex Research 40*, 13–26.

Crumpacker, B. (2006). *The Sex Life of Food: When Body and Soul Meet to Eat.* . New York: St. Martin's Griffin.

Cunningham, S. J., & Russell, P. A. (2004). The influence of gender roles on evolved mate preferences. *Sexualties, Evolution, and Gender 6 (2-3)*, 131-150. .

Dennison, R., & Russell, S. T. (2005). Positive Perspectives on Adolescent Sexuality: Contributions of the National Longitudinal Study of Adolescent Health. *Sexuality Research and Social Policy 2 (4)*, 54-59.

DiCenso, A., Borthwick, V. W., Busca, C., Creatura, C., Holmez, J. A., & Kalagian, W. F. (2001). Completing the Picture: Adolescent Talk about what's Missing in Sexual Health Services. *Canadian Journal of Public Health; 92*, 35-38.

DiClemente, R., Crittenden, C., Rose, E., Sales, J., Wingood, G., Crosby, R., & al, e. (2008). Psychosocial predictors of HIV-associated sexual behaviors and the efficacy of prevention interventions in adolescent at-risk for HIV infection: What works and what doesn't work? *Psychosomatic Medicine 70 (5)*, 598–605.

Dillard, J. P., & Shen, L. (2012). *Handbook of Persuasion: Developments in Theory and Practice.* Thousand Oaks: SAGE.

Dittus, P., Miller, K. S., Kotchick, B. A., & Forehand, R. (2004). Why parents matter!: The conceptual basis for a community-based HIV prevention program for the parents of African American youth. *Journal of Child and Family Studies 13(1)*, 5-20.

Dixon-Muller, R. (2008). How young is "too young?" Comparative Perspectives on Adolescent Sexual, Marital and Reproductive Transitions. *Studies in Family Planning 39,*, 247-262.

Dixon-Muller, R. (2009). Starting Young: Sexual Initiation and HIV Prevention in Early Adolescence. *Aids and Behaviour 13,*, 100-109.

Dixson, B. J., Vasey, P. L., Sagata, K., Sibanda, N., Linklater, W. L., & Dixson, A. F. (2010). Men's preferences for women's breast morphology in New Zealand, Samoa, and Papua New Guinea. *Archives of Sexual Behavior.*

Durand, R., & Paolella, L. (2013). Category stretching: Reorienting research on categories in strategy, entrepreneurship, and organization theory. *Journal of Management Studies 50 (6)* , 1100-1123.

Eagly, A., Ashmore, R., Makhijani, M., & Longo, L. ( 1991). What is beautiful is good, but . . .: A meta-analytic review of research on the physical attractiveness stereotype. *Psychological Bulletin 110*, 109–128.

Eastwick, P. W., Eagly, A. H., Finkel, E. J., & Johnson, S. E. (2011). Implicit and explicit preferences for physical attractiveness in a romantic partner: A double dissociation in predictive validity. *Journal of Personality and Social Psychology 101 (5)*, 993- 1011.

Eaton, L., Flisher, A., & Aaro, E. L. (2003). Unsafe sexual behaviour in South African youth. *Social Science and Medicine 56*, 149- 165.

Egan, R. D., & Hawkes, G. L. (2008). Endangered girls and incendiary objects: Unpacking the discourse on sexualization. , 291-311. *Sexuality & Culture 12*, 291-311.

Emanatian, M. (1996). Metaphors of Lust and Sex in Chigga. *Ethos 24 (2)*, 195-236.

England, P., & Bearak, J. (2014). The sexual double standard and gender differences in attitudes toward casual sex among US university students. *Demographic Research 30*, 1327–1338.

Entman, R. M. (2004). Framing: Toward Clarification of a Fractured Paradigm. *Journal of Communication 43 (4)*, 51-80.

Epstein, D., & Johnson, R. (1998). *Schooling Sexualities.* Milton Keynes: Open University Press.

Eyal, K., & Kunkel, D. (2008). The effects of sex in television drama shows on emerging adults' sexual attitudes and moral judgements. *Journal of Broadcasting & Electronic Media 52*, 161-181.

Eyo, M. (2016). The Dynamics of Youth Language in Africa: An Introduction. *Sociolinguistic Studies 10 (1&2)*, 1-14.

Fairclough, N. (2001). Critical Discourse Analysis as a Method in Social Science Research. Kwenye R. Wodak, & Meyer, M. *Methods of Critical Discourse Analysis.* London: Sage.

Fairclough, N. (2003). *Analysing Discourse: Textual Analysis for Social Research.* London: Routledge.

Fan, J., Dai, W., Liu, F., & Wu, J. (2005). Visual perception of male body attractiveness. *Biological Sciences*, 219- 226.

Farquhar, J. (2002). *Appetites: Food and Sex in Post-Socialist China.* Durham and London: Duke University press.

Feingold, A. (1992b). Good looking people are not what we think. *Psychological Bulletin, 111,*, 304-341.

Fergus, S., Zimmerman, M. A., & Caldwel, C. (2007). Growth Trajectories of Sexual Risk Behaviour in Adolescence and Young Adults. *American Journal of Public Health. 97*, 1096-1101.

Fine, M., & McClelland, S. I. (2006). Sexuality education and the discourse of desire: Still missing after all these years. *Harvard Educational Review Journal 76*, 297–338.

Finer, L. (2010). Unintended Pregnancy among US Adolescents: Accounting for Sexual Activity. *Journal Of Adolescent Health; 47*, 312-314.

Finkel, E. J., & Eastwick, P. W. (2008). Sex differences in mate preferences revisited: Do people know what they initially desire in a romantic partner? *Journal of Personality and Social Psychology 94 (2)*, 245–264.

Fiske, S., & Taylor, S. (1991). *Social Cognition. (Second edition).* New York: McGraw-Hill.

Flood, M. (2008). Men, sex, and homosociality: How bonds between men shape their sexual relations with women. *Men and Masculinities 10*, 339-359.

Forhan, S. F., Gottleib, S., Sternberg, M. R., Xu, F., Datta, D., McQuillan, G. M., & Markowitz, L. (2009). Prevalence of Sexually Transmitted Infections among Female Adolescents aged 14-19 in the United States. *Pediatrics, 124*, 1505-1512.

Forrest, S. (2000). "Big and tough": Boys' learning about sexuality and manhood. *Sexual and Relationship Therapy 15*, 246-261.

Frank, K. (2007). Female Agency and Oppression in Caribbean Bacchanalian Culture: Soca, Carnival, and Dancehall. *Women's Studies Quarterly 35 (1/2)*, 172- 190.

Frederick, D. A., & Haselton, M. G. (2007). Why is muscularity sexy? Tests of the fitness indicator hypothesis. *Personality and Social Psychology Bulletin 33*, 1167-1183.

French, D. C., & Dishion, T. J. (2003). Predictors of early initiation of sexual intercourse among high-risk adolescents. *Journal of Early Adolescence, 23*, 295-315.

Furman, W., & Shaffer, L. (2003). The Role of Romantic Relationships in Adolescent Development. Kwenye P. Florsheim, *Adolescent Romantic Relations and Sexual Behavior: Theory, Research and Practical Implications* (kur. 3-22). Mahwah, NJ7: Lawrence Erlbaum Associates.

Furnham, A., & Swami, V. (2007). Perceptions of female buttocks and breast size in profile. *Social Behavior and Personality 35*, 1-8.

Galliher, R. V., Rostosky, S. S., Welsh, D. P., & Kawaguchi, M. C. (1999). Power and psychological well-being in late adolescent romantic relationships. *Sex Roles 40*, 689- 710.

Galvan, A., Hare, T., Voss, H., Glover, G., & Casey, B. J. (2007). Risk Taking and Adolescent Brain: Who is at Risk. *International Journal of Developmental Science 10*, F8-F14.

Goff, J. L. (1990). Sexual confusion among certain college males. *Journal of Adolescence, 25,* 599 – 614.

Goffman, E. (1974). *Frame Analysis: An Essay on the Organization of Experience.* New York: Harper and Row.

Goffman, E. (2005). *Interaction Ritual: Essays in Face to Face Behavior (rev Ed).* New Brunswick USA and London UK: AldineTransaction.

Gomaa, Y. A., & Shi, Y. (2012). *The Linguistics of Euphemism: A Diachronic Study of Euphemism Formation. University of Florida, USA.* Florida: University of Florida, USA.

Gonzalez, F., & Anna-Brita, S. (2011). Expressive Devices in the Language of English and Spanish Speaking Youth. *Revista Alicantina de Estudios Ingleses 24*, 235-256.

Greenfield, P. M. (2003). Online discourse in a teen chat room: New codes and new modes of coherence in a Visual Medium. *Journal of Applied Developmental Psychology, 24*, 713 – 738.

Gueguen, N. (2007). Women’s bust size and men’s courtship solicitation. *Body Image,* 386-390.

Gupta, N., & Mahy, M. (2003). Sexual Initiation Among Adolescent Girls and Boys: Trends and Differentials in Sub-Saharan Africa. *Archives of Sexual Behaviour*, 41-53.

Halliday, M. A. (1985). *An Introduction to Functional Grammar.* London: Edward Arnold.

Halstead, J. M., & Reiss, M. (2003). *Values in Sex Education.* London: Routledge.

Hamilton, D. (. (1991). *Cognitive Processes in Stereotyping and Intergroup Behavior1981.* Hillsdale, Mass: Erlbaum.

Hannan, M. T., Polos, L., & Carroll, G. R. (2007). *Logics of organization theory: Audiences codes and ecologies.* Oxford: Princeton University Press.

Hargreaves, D. A., & Tiggemann, M. (2003). Female ―thin ideal media images and boys attitudes towards girls. *Sex Roles 49 (9-10)*, 539-544.

Harper, B., & Tiggemann, M. (2008). The effect of thin ideal media images on women's self-objectification, mood, and body image. . *Sex Roles,*, 649-657.

Hatfield, E., & Sprecher, S. (1995). Men's and women's preferences in marital partners in the United States, Russia, and Japan. *Journal of Cross-Cultural Psychology 44 (3)*, 728-750.

Helleve, A., Flisher, A. J., Onya, H., Koma, W., & Klepp, K. (2011). Can any Teacher Teach Sexuality and HIV/AIDS? Perspectives of South African Life Orientation Teachers. *Sex Education Journal, 11*, 13-26.

Herring, S. (2000). *Gender differences in CMC: Findings and implications.* The CPSR Newsletter.

Hess, A. (January 2014). *Pacific Standard.* Imechukuliwa toka Pacific Standard web site: https://psmag.com/social-justice/women-arent-welcome-internet-72170

Holland, D., & Eisenhart, M. (1990). *Educated in romance: Women, achievement and college.* Chicago: University of Chicago Press.

Holland, J., Ramazazanoglu, C., Scott, S., Sharpe, S., & Thomoson, R. (1991). *Pressure, Resistance, Empowerment: Young Women and the Negotiation of Safe Sex.* London: The Tufnell Press.

Hong, D. S. (1998). Variables related to formation and development of dating relationships. *Korean Journal of Social and Personality Psychology 12 (2)*, 199-266.

Izugbara, C. (2004). Notions of sex, sexuality and relationships among adolescent boys in rural southeastern Nigeria". *Sex Education: Sexuality, Society and Learning, vol. 4*, pp. 63–79,.

Izugbara, C. (2005). The socio-cultural context of adolescents' notions of sex and sexuality in rural south-eastern Nigeria,". *Sexualities, vol. 8, no. 5,*, 600-617.

Jackson, L. A., Hunter, J. E., & Hodge, C. N. (1995). Physical attractiveness and intellectual competence: A meta-analytic review. *Social Psychology Quarterly 58*, 108–122.

Jackson, S. M., & Cram, F. (2003). Disrupting the sexual double standard: Young women's talk about heterosexuality. *British Journal of Social Psychology 42*, 113- 127.

Jekielek, S., & Brown, B. (2005). *The Transition to Adulthood: Characteristics of Young Adults ages 18-24 in America.* Balitimore: Child Trends, MD.

Jorgensen, W. M., & Philips, L. (2002). *Discourse Analysis as Theory and Methods.* London: SAGE.

Kabiru, C. W., & Ezeh, A. (2007). Factors Associated with Sexual Abstinence among Adolescents in Four Sub- Saharan African Countries. *African Journal of Reproductive Health*, 111-132.

Kahl, S. J., & Grodal, S. (2016). Discursive strategies and radical technological change: Multi level discourse analysis of the early computer (1947-1958). *Strategic Management Journal, 37(1), ,* 149-166.

Kar, S., Choudhury, A., & Singh, A. (2015). Understanding Normal Development of Adolescent Sexuality: A Bumpy Ride. *Journal of Human Reproductive Sciences, 8(2),*, 70-74.

Kaufman, S., Michael, E., & Deborah, S. (2003). *"Frames, Framing and Reframing." Beyond Intractability.* Boulder: University of Colorado.

Kelly, M. F. (August Thursday, 2007). Discursive Framing of Teenage Sexuality: Virginity Loss on "Teen Drama" Television Programs. *Journal of Sex Research*, 479-489. Imechukuliwa toka American Sociological Association: http://www.allacademic.com/metal/p

Kennedy, M. T., & Fiss, P. C. (2013). An ontological turn in categories research: From standards of legitimacy to evidence of actuality. . *Journal of Management Studies 50 (6)*, 1138-1154.

Kirby, D. (2008). The Impact of Abstinence and Comprehensive Sex and STD/HIV Education Programs on Adolescent Sexual Behavior. *Sexuality Research and Social Policy, 5*, 18-27.

KNBS. (August Friday, 2011). *knbs.or.ke.* Imechukuliwa toka datarequest@knbs.or.ke: http://www.prb.org/Publications/Articles/2008/kenya.aspx

KNBS, MOH, NACC, KMRI, NCPD, DHS, & ICF. (December Monday, 2014). *Kenya Demographic and Health Survey 2014.* Rockville Maryland, USA: USAID. Imechukuliwa toka ttp://dhsprogram.com/pubs/pdf/FR308/FR308.pdf.

Kokkola, L. (2013). *Fictions of adolescent carnality: Sexy sinners and delinquent deviants.* Philadelphia : John Benjamins.

Kotchik, B., Shaffer, A., Forehand, R., & Miller, K. (2001). Adolescent Sexual Risk Behaviour: A Multi-System Perspective. *Clinical Psychology Review, 21*, 493-519.

Kroger, J. (2003). Identity development during adolescence. . Kwenye G. R. Berzonsky, *Blackwell handbook of adolescence* (kur. 205-226). Malden, MA: Blackwell.

Kundanis, R. M. (2003). *Childreen, teens, famileies and mass media: The Millennial Generation.* Mahwah, NJ: Lawrence Erlbaum Associates.

Kunkel, D., Cope, K., Farinola, W., Biely, E., Rollin, E., & Donnerstein, E. (2000). Sexual Messages on Entertainment Tv in the USA. *Children in the new Media Landscape*, 155-158.

Kunkel, D., Eyal, K., Finnerty, K., Biely, E., & Donnerstein, E. (2005). *Sex on TV 4.* Menlo Park, CA: Henry J. Kaiser Family Foundation.

Kunkel, D., Farrar, K., Eyal, K., Biely, E., Donnerstein, E., & V., R. (2007). Sexual socialization messages in entertainment television: Comparing content trends 1997-2002. *Media Psychology 9*, 595–622.

Kurzban, R., & Weeden, J. (2005). Hurry Date: Mate preferences in action. *Evolution and Human Behavior, 26(3),*, 227–244.

Lakshmi, P. V., Gupta, N., & Kumar, R. (2007). Psychosocial Predictors of Adolescent Sexual Behaviour. *Indian Journal of Pediatrics*, 923-926.

